

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Ishirini na Mbili – Tarehe 4 Mei, 2021

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na Mkutano wetu wa Tatu, leo ni Kikao cha Ishirini na mbili.

Katibu!

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO - K.n.y. MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI A KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha

2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Husna Sekiboko kwa niaba ya Kamati.

Katibu!

NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Swali letu la kwanza leo tunaanza na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, swali hilo litaulizwa na Mheshimiwa Hassan Selemani Mtenga Mbunge wa Mtwara Mjini. Mheshimiwa Mtenga tafadhalii uliza swali lako.

Na. 179

**Kujenga Barabara za Lami-Kata za Manispaa ya
Mtwara Mikindani**

MHE. HASSAN S. MTENGA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara za Iami katika Kata za Ufukoni, Magomeni na shangani Manispaa ya Mtwara Mikindani.

SPIKA: Majibu ya swali lako, Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde tafadhalii majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA
SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Selemani Mtenga Mbunge wa Jimbo la Mtwara Mjini kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kujenga mundombini ya barabara nakufanya matengenezo katika Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani ambapo katika mwaka wa fedha 2017/2018 kupitia Miradi ya Uendelezaji Miji yaani *Tanzania Strategic Cities Projects* Serikali ili jenga barabara za lami zeny urefu wa kilomita 4.53 katika Kata ya Shangani Manispaa Mtwara Mikindani kwa gharama ya shilingi bilioni 7.09. Aidha, katika mwaka wa fedha 2019/2020 kupitiafedha za Mfuko wa Barabara Serikali imejenga barabara za lami zeny urefu wa kilomita 0.85 katika Kata ya Shangani kwa gharama ya shilingi milioni 232.98. Vilevile, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali imetenga shilingi milioni 117.38 kwa ajili ya ujenzi wa barabara za lami zeny urefu wa kilomita 0.55 kwa kiwango cha lami katika mtaa wa Maduka Makubwa ambapo mkandarasi anaendelea na ujenzi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21 barabara zeny urefu wa kilomita 22.37 zimefanyiwa matengenezo na kilomita 1.3 zinaendelea na matengenezo kwa gharama ya shilingi milioni 74.19 katika Kata za Ufukoni na Magomeni. Serikali inatambua ukuaji wa haraka wa Mji wa Mtwara naitaendelea kuupa kipaumbele cha barabara za lami na mifereji ya maji ya mvua kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Mtwara Mjini, nimekuona swali la nyongeza.

MHE. HASSAN S. MTENGA: Mheshimiwa Spika, kwanza nitoe shukurani kwa majibu, lakini nataka niseme kwa mradi ambao unazungumzwa wa *TACTIC* mradi huu nadhani ulishapangiwa fedha, lakini mpaka sasa hivi jinsi ninavyozungumza kuhusu Kata ya Magomeni na Ufukoni bado hali ni mbaya. Je, Serikali ni lini ujenzi wa barabara hizi utakua tayari?

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili ni lini miundombini ya mifereji ambayo tulikua tunaizungumza toka mwanzo Serikali itakua tayari kuweza kuboresha mifereji

ambayo sasa hivi mara kwa mara kunapatikana mafuriko makubwa na wananchi inatokea hali sinto fahamu kwenye majumba ya watu na wengine kupoteza maisha. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI tafadhalii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ametaka kufahamu ni lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ambazo ameziainisha zilizopo katika mradi wa *TACTIC* kwa kifupi ni kwamba mradi wa *TACTIC* bado katika hatua za mwisho za makubaliano na mahafikiano na Serikali ili zianze kutekezwa.

Kwa hiyo, Mbunge nikuhakikishie kabisa kwamba mara baada ya huu mradi kuwa umekamilika na Serikali kumaliza hatua zote, barabara hizo ambazo umeziainisha zitaanza kujengwa kwa sababu ziko katika mradi wa *TACTIC*.

Mheshimiwa Spika, vile vile, katika sehumu ya ule mradi wa *TACTIC* mionganii mwa *component* ambazo ziko ndani yake ni pamoja na ujenzi wa mifereji kwa hiyo, mradi huu utakapokua umefikia hatua za mwisho na ninaamini Serikali ipo katika mazungumzo na ninahuhakika kabisa mara itakavyokamilia basi barabara zako pamoja na mifereji ya wananchi wa Mtwara Mjini itajengwa kama ambavyo imeainishwa katika huo mradi ahsante sana.

SPIKA: Mheshimiwa Aida Khenani nimekuona uliza swali la nyongeza.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru changamoto iliyopo Mtwara ya barabara inafanana sana na changamoto Nkasi. Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano alituahidi wana Nkasi kipande cha barabara kutoka Chala mpaka Mpalamawe, ningependa kupata *commitment* ya Serikali kwa kuwa ahadi zote zinakua recorded ni lini ahadi hiyo itatekelezwa.

SPIKA: Ni lini ahadi hiyo itatekelezwa Mheshimiwa Naibu Waziri, David Silinde majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ametaka kujua tu ni lini ahadi ya Mheshimiwa Hayati Rais ama niseme ahadi zote za viongozi ni kwamba sasa hivi Ofisi ya Rais, TAMISEMI ipo katika hatua ya mwisho tunakusanya na kuandaa mpango wa namna ya kutekeleza ahadi zote za viongozi na nikuhakikishie tu kwamba kuanzia mwaka wa fedha ujao tutaanza kutenga pole pole fedha kwa ajili ya kuhakikisha zile ahadi zote ambazo viongozi wakuu walikua wamezitoa zinaanza kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, na kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Sita ni Serikali makini na imeshazungumza hadharani kwamba kazi inaendelea yale yote yaliyozungumzwa tutayaendeleza kuhakikisha kwamba tunawahudumia wananchi wetu vizuri. Kwa hiyo, waambie wananchi wa Nkasi Kaskazini kwamba zile ahadi zilizoaidiwa Serikali itazitekeleza kwa vitendo ahsante.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Utumishi na Utawala Bora, swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mheshimiwa Shangazi uliza swali lako tafadhali.

Na. 180

Rushwa katika Mchezo wa Soka

MHE. RASHID A. SHANGAZI aliuliza:-

Vitendo vya rushwa vimekithiri sana katika mchezo wa soka hapa nchini.

Je, ni kwa kiasi gani Serikali inakabiliana na kudhibiti hali hiyo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Deogratius Ndejembii, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora tafadhalli.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwepo kwa vitendo vya rushwa katika sekta ya michezo hususan mchezo wa soka hali inayoathiri maendeleo ya mchezo huu kwa ujumla, lakini pia kuikosesha Serikali mapato.

Mheshimiwa Spika, Serikali kuititia *TAKUKURU*'imekuwa ikitabili ana na vitendo vya rushwa kwenye mchezo wa soka kwa kufanya uchambuzi wa mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya viingilio katika mechi za mpira wa miguu. Matokeo ya uchambuzi huo yaliwezesha kubaini kwamba kuna mianya ya rushwa kwenye eneo hili ambapo baada ya kubana mianya hiyo mapato yaliongezeka hadi kufikia shilingi milioni 206 kwa watu 50,233 waliokata tiketi katika mechi iliyochewza kwenye Uwanja wa Taifa mwezi Machi, 2019 ukilinganisha na mapato ya shilingi milioni 122 kwa watu 47,499 waliokata tiketi kwa mechi iliyochewza Januari, 2019 kwenye uwanja huo.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa sekta ya michezo nchini, mwaka 2016 *TAKUKURU* iliunda Timu Maalum ya Uchunguzi kufuatilia na kuchunguza vitendo vya rushwa katika michezo ambapo kesi tatu zimefunguliwa mahakamani na tuhuma saba zinaendelea kuchunguzwa. Aidha, semina zimetolewa kwa makundi mbalimbali ikiwemo Chama cha Makocha wa Mpira wa Miguu (*TAFCA*), Waamuzi na Makamisaa wanaotumika katika michezo ya Ligi Kuu na Ligi Daraja la Kwanza pamoja na kufanya vikao na viongozi

wa Chama cha Mpira wa Miguu (*TFF*) kuhusu kuweka mikakati ya pamoja kuelimisha umma kupitia soka.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuwataka *TFF*, wasimamizi wa soka na viwanja vya michezo waruhusu na kushirikiana na TAKUKURU kuweka matangazo ya kukemea rushwa kwenye soka na michezo kwa ujumla.

SPIKA: Mheshimiwa Shangazi, swali la nyongeza.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali ambayo yanaonesha mwanga wa kupambana na rushwa katika michezo, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, je, ni hatua gani zimechukuliwa kwa watu ambao wamebainika kujihusisha na vitendo vya rushwa katika michezo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, ni mkakati gani Serikali itatumia kuboresha mifumo ya uuzaaji tiketi na kukusanya mapato, lakini pia kuziba mianya ili kuongeza mapato zaidi katika sekta hii ya michezo?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Deo Ndejembii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua mbalimbali katika kuhakikisha kudhibiti mianya ya rushwa katika soka nchini, lakini vilevile imekuwa ikichukulia hatua watuhumiwa waliokutwa na hatia katika kujishughulisha na masuala ya rushwa. Ikumbukwe kwamba mwaka 2017 kuna watuhumiwa ambao walifikishwa mahakamani na kukutwa na hatia na hatimaye kulipishwa faini.

Mheshimiwa Spika, vilevile, mwaka 2018 kuna kesi moja ambayo ilikuwa ni maarufu sana hapa nchini, ambapo kuna mtuhumiwa alikutwa na hatia ya kula shilingi milioni 90

za Chama cha Mpira wa Miguu nchini *TFF* na yeye vilevile, alifunguliwa mashitaka ikiwemo ya uhujumu uchumi, lakini na baadaye kuweza kulipa fedha hizo kuzirudisha katika *TFF*. Kwa hiyo, tutaendelea kushughulika na watuhumiwa wa aina hii.

Mheshimiwa Spika, nikijibu swalii la pili la Mheshimiwa Shangazi, ili kuziba mianya sote tunafahamu kwamba sasa tunaenda kwenye ulimwengu wa teknolojia, hivyo basi, niwaase wenzetu wa *TFF* na timu za mipira za miguu kwamba sasa waende katika kuachana na tiketi zile za vitini vyaa kuchana na waweze kwenda kwenye *electronic ticket*, hii itasaidia sana upungufu na upotevu wa mapato, itaongeza mapato kwa timu zao, lakini vilevile kwa *TFF*.

Mheshimiwa Spika, vilevile niwaagize kwasababu *e-government (eGA)* ipo chini ya Ofisi yetu niwaagize hapa mbele ya Bunge lako Tukufu washirikiane na wenzetu wa *TFF* ili kuweka mfumo bora wa kukata tiketi za kuingia katika michezo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema katika hii *trend* tulioiona mwaka 2019 ya mwezi Januari kupata shilingi milioni 122 na mwezi Machi, mechi zote hizi zilikuwa ni za timu ya mpira ya Simba; kwa hiyo, kumeonekana kukiwa na timu ya Simba inacheza uwanja unajaa sana, lakini bado mapato yanakuwa hafifu, ukilinganisha na timu nydingine ambayo ni kubwa Afrika Mashariki na Kati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

SPIKA: Waheshimiwa muwe mnasikiliza majibu ya Mheshimiwa Waziri, kuna timu zikicheza uwanja unajaa sana. Swalii la nyongeza nimekuona Mheshimiwa Mbunge wa Kinondoni, Mheshimiwa Tarimba. (*Makofii/Kicheko*)

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swalii la nyongeza na hili linahusu rushwa. *Weekend* iliyopita timu ya *Prisons* ilicheza na mabigwa wa kihistoria *Young Africans* kule Katavi na katika

mchezo ule baada ya kumalizika na mabigwa hawa kupata ushindi kiongozi wa *Prisons* alisimama na kusema kwamba na amenukuliwa katika vyombo vyahabari kwamba timu yake ilikua iko katika kuhongwa shilingi milioni 40 ili iweze kuachia mchezo ule.

Je, Serikali haioni sasa kwamba taarifa kama hizi ndizo za kuanzia kufanya kazi na kuwahoji watu kama hawa ili tuweze kupata ukweli? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya swali hilo Naibu Waziri Mheshimiwa Deo Ndejembii.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Spika, kumekuwa na tabia ya viongozi wa timu mbalimbali hapa nchini hasa wanapofungwa na *Young Africans* kwa halali kabisa, kutoa kauli za kwamba waliogwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ifike wakati sasa viongozi wa timu hizi na timu hizi na Watanzania kwa ujumla kwamba wakubali kwamba *Young Africans*, Yanga moja ndio timu bigwa hapa Tanzania na tibu bora hapa Afrika, kwa hiyo, wanapofungwa wakubaliane na matokeo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Jamani mechili iko Jumamosi, Jumatatu tutakutana uwanja huu huu hapa.

Mheshimiwa Festo Sanga Mbunge wa Makete swali la mwisho la nyongeza. Kuna majibu ya nyongeza oh! Mheshimiwa Waziri wa Michezo tafadhalii.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri Deo Ndejembii kwa kujibu maswali vizuri, hongera sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Waheshimiwa Wabunge, ningependa kuwahakikishia kwamba Serikali

kupitia Wizara ya Michezo ninayoiongoza tunapambana na rushwa kwenye michezo kwa nguvu zote na tunashirikiana na vyombo vya Ulinzi na Usalaam kuhakikisha tunaweka mazingira wezeshi ya michezo nchini kukua bila kuwepo na mazingira ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningependa kuwapa uhakika Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watanzania kwamba Serikali hii haitafumbia macho timu au mshirika yoyote katika michezo ambaye anatumia rushwa ili kuweza kujipatia ushindi ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Baada ya majibu hayo Mheshimiwa Festo bado unaswali la nyongeza, umeridhika ahsante sana.

Tuendelee Waheshimiwa, Jumamosi itaamua tu, nani anatoa rushwa na nini, tuko Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Wazee na Watoto, Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko.

Na. 181

Serikali Kuwawezesha Wanawake Wajasiriamali

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO aliuliza:-

Je, Serikali inatumia njia gani kuwawezesha wanawake wajasiriamali kupata mafunzo ya ujasiriamali, uandaaji wa maandiko ya miradi na kuwaunganisha na taasisi za kifedha ili wapate mikopo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Naibu Waziri Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba

kujibu swalii la Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uwezeshaji wanawake kiuchumi ni suala muhimu katika kufikia usawa wa kijinsia na kupunguza umaskini wa kipato katika jamii. Serikali imeweeka kipaumbele katika kuwawezesha wanawake kiuchumi kama mkakati wa kufikia usawa wa kijinsia katika nyanja zote.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika kuwawezesha wanawake kiuchumi na kuwaunganisha na taasisi za mikopo inaratibu makongamano ya kiuchumi ya wanawake wajasiriamali ambapo kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2019/2020 hadi sasa Serikali imeweza makongamano matano (moja katika kila mkoa) katika mikoa mitano (5) ya Arusha, Dodoma, Singida, Ruvuma na Mbeya kati ya makongamano 26 ya mikoa iliyopangwa.

Mheshimiwa Spika, katika makongamano haya elimu ya matumizi ya teknolojia rahisi na sahihi katika uzalishaji, kuanzisha na kujunga na vikundi vya kiuchumi pamoja na umuhimu wa kuzingatia viwango vya ubora wa bidhaa zinazozalishwa ili kukidhi matakwa ya kisheria na masoko inatolewa. Aidha, makongamano haya yamewafikia takribani jumla ya wanawake 2,768 kati ya 1,500 waliolengwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na *SIDO*, *TBS*, *TMDA*, *BRELA* na Halmashauri imeendelea kuwajengea uwezo wanawake wajasiriamali hapa nchini katika stadi mbalimbali za ujasiriamali ikiwa ni pamoja na namna ya uboreshaji wa huduma na bidhaa zinazozalishwa na wanawake na uandaaji wa maandiko ya miradi. Katika kipindi cha mwaka 2019/2020 jumla wanawake 3,424 walifikiwa kati ya 5,000 waliolengwa.

SPIKA: Mheshimiwa Husna, swalii la nyongeza.

MHE. HUSNA J. SEKIBOKO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza, akina mama wa Mkoa wa Tanga ni watafutaji na wachapakazi, wamejiunda kwenye vikundi lakini wanakosa tija kwa kukosa elimu ya kuandaa maandiko ya miradi na namna ambavyo wanaweza kuunganishwa kwenye taasisi za fedha ili waweze kupata mikopo. Je, ni lini Serikali italeta makongamano hayo ambayo Serikali imeyafanya katika mikoa mingine kwenye Mkoa wa Tanga ili akina mama hawa na wenyewe waweze kupata ujuzi huo kwa ajili ya kuendeleza shughuli za ujasiliamali?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, elimu ni kitu endelevu; makongamano pekee yanaweza yasikidhi ile haja ya akina mama wa Mkoa wa Tanga. Je, ni kwa namna gani sasa Serikali inajipanga kuimarisha Ofisi za Maendeleo ya Jamii kwenye Halmashauri zetu ili ziweze kutoa elimu hii ya uandishi wa maandiko ya miradi pamoja na kuwasaldia akina mama na taasisi za kifedha badala ya kutegemea zile za Halmashauri peke yake?

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Husna Sekiboko. Majibu ya maswali hayo, lini makongamano Tanga na kuna mpango gani wa kuimarisha Ofisi za Maendeleo ya Jamii.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Husna, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi, hadi sasa Serikali imeshafanya makongamano katika mikoa mitano kati ya mikoa 26 nchini. Katika mikoa hiyo 26 Tanga ni mkoaa mmojawapo kati ya mikoa 21 ambayo hajapata mafunzo hadi sasa. Tunategemea kupata rasilimali fedha na baada ya kupata rasilimali fedha hizo tutafanya makongamano hayo katika mikoa iliyobaki. Nimuombe tu Mheshimiwa Husna awe mstahamilivu kwa hili, Serikali tumeshajipanga kuendesha makongamano hayo wakati wowote tutakapopata fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili Mheshimiwa Husna amesema vipi tutawezesha halmashauri ili wanawake waweze kupata elimu. Serikali imeshaanza kuweza halmashauri nichini na katika mwaka 2000 imeandaa miongozo ya utoaji mikopo kwa ajili ya vikundi mbalimbali nya wanawake ikiwemo kuwapatia elimu ya ujasiliamali na mafunzo ya uendeshaji wa biashara kabla na baada ya kupata mikopo. Hata hivyo, mwongozo huo umeambatanishwa na mfano rahisi wa andiko la miradi ulioandikwa na Maafisa Maendeleo ya Jamii katika kutoa elimu kuhusu namna ya kuandaa andiko hilo.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Husna kwa kuwapigania wanawake wa mkoa wake ili waweze kupata elimu ya kiuchumi kwa ajili ya kuondoa umaskini.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis, nakupongeza sana. Mheshimiwa Mwanaidi huyu bibi yake ni katika wale wabibi wa Mapinduzi. Huyu bibi nilikuwa naye kwenye Bunge la mwaka 2000 - 2005 akiitwa Bi. Mwanaidi, tulikaa Pamoja kitihiki na kitihiki Msekwa kule. Kwa hiyo, hongera sana mjukuu wetu. (*Makofu/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tuelekee Wizara ya Kilimo na swali la Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza.

Na. 182

Kilimo cha Umwagiliaji kwa Mikoa Muhimu Nchini

MHE. AGNESTA L. KAIZA aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji katika Mikoa ya Kigoma, Mwanza, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma na Morogoro ili kuongeza mazao ya kilimo yatakayosafirishwa kuititia *SGR*?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri Kilimo Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea kutekeleza na kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji katika mikoa inayopitiwa na reli ya kisasa ya mwendokasi kuanzia Mkoa wa Pwani na kufanya kutathmini maeneo yote yenye sifa ya kufanya uzalishaji kwa kutumia njia ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 na 2020/2021 eneo linalomwagiliwa limeongezeka hadi kufikia hekta 695,045 na hivyo kufikia asilimia 58 ya lengo la kufikia hekta millioni 1.2 ifikapo 2025. Ongezeko hilo limetokana na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu za umwagiliaji za *Kilangali Seed Farm* (Kilosa) kupitia mradi wa *ERPP* na akimu 13 za *SSIDP* kupitia mradi wa *SSIDP*. Serikali inakamilisha ujenzi wa awali kwa skimu za umwagiliaji katika Mikoa ya Shinyanga, Tabora, Kigoma, Singida, Morogoro, Dodoma na Kagera. Aidha, Serikali itaendelea na ukamilishaji wa skimu hizo hili ziweze kutumiwa ipasavyo na wakulima.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inakamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa Mradi mkubwa wa Umwagiliaji katika Mkoa wa Kigoma wenyewe hekta 3,000 ambapo ujenzi wa mradi huo wa Luiche unatarajiwaa kuanza katika mwaka wa fedha 2021/2022.

Aidha, miradi mingine ya umwagiliaji inayopitiwa na reli ya *SGR* itakayoteklezwa katika mwaka wa fedha 2021 ni pamoja na Skimu za Ngomai (Kongwa), Idudumo (Tabora) na Msufini pamoja na Shamba la Mbegu la Msimba (Morogoro).

SPIKA: Swali la nyongeza Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, tafadhalii

MHE. AGNESTA L. KAIZA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, Tume ya Umwagiliaji imekuwa ikipata shida kubwa sana ya bajeti ili kuweza kuteleza majukumu yake yanayohusiana na skimu za umwagiliaji. Je, Serikali ina mkakati gani endelevu wa kuhakikisha Tume hii ya Umwagiliaji nchini inapata bajeti endelevu na si ya kusuasua kama ilivyo sasa?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, soko la ndani pekee haliwezi kuwanufaisha wakulima wa mazao katika skimu ya umwagiliaji. Je, Serikali ina mpango gani madhubuti wa kuhakikisha mazao haya sasa yanayopatikana kwenye hizi skimu za umwagiliaji yanapata masoko nje ya nchi kuliko ilivyo sasa?

Mheshimiwa Spika, nakushuru sana.

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Agnesta, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kumekuwa na upungufu wa rasilimali fedha katika maeneo mbalimbali lakini mkakati ambaeo Serikali unao na hili lilikuwa ni agizo la Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan alilolitoa mwaka jana akiwa Makamu wa Rais katika Mkoa wa Simiyu ni kuzifanya *subsector* zilizoko ndani ya sekta ya kilimo kuijidesha. Wizara ya Kilimo hatua ya kwanza ambayo tumechukua na Bunge hili likituidhinishia bajeti, katika mwaka wa fedha ujao tunaanzisha kitu tunaita *Irrigation Development Fund* (Mfuko wa Kuendeleza Umwagiliaji).

Mheshimiwa Spika, suala la ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji ni wajibu wa Serikali. Serikali inaenda kujenga

miundombinu ya umwagiliaji kwenye mashamba ya wananchi wa kawaida. Hivi karibuni tumefanya mradi kwenye skimu tano kwa zaidi ya dola milioni 22 katika Mkoa wa Morogoro, tunatengeneza utaratibu ambao umo kwenye sheria kwamba tunapowekeza katika eneo la umwagiliaji kunakuwa kuna kuzzungusha zile fedha ili zirudi katika Mfuko na ziweze kutumika katika eneo lingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo katika bajeti ijayo mtaona tunaanzisha Mfuko wa Umwagiliaji ambao utakuwa *sustainable* na *revolving* ambao utawezesha sekta ya umwagiliaji kuwa na uhakika wa fedha. Tunawashukuru wenzetu wa Wizara ya Fedha wameturuhusu *part of that fund* ziweze kuwa *retained* na Mfuko na hazitaenda katika Mfuko Mkuu wa Hazina ili tuwe na uhakika wa kuweza kujidesha.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili katika eneo la umwagiliaji badala ya miradi mingi kuendesha katika mfumo ambao tumekuwa tukiendesha sasa hivi, tunafanya miradi mipya kuanzia mwaka kesho kwa kutumia mfumo wa *design and build* na kutumia *force account* kama tunavyojenga shule, zahanati na vituo vya afya katika Halmashauri. Pia tutaiwezesha Tume ya Umwagiliaji kwa kuipatia vifaa ili iweze kufanya miradi yenyewe moja kwa moja badala ya kutegemea njia zingine. Kwa hiyo, hii nadhani itatusaidia sana kupunguza gharama za miradi lakini kuifanya Tume kuwa na uhakika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu soko la mazao, siyo tu mazao yanayotokana na skimu za umwagiliaji, dhana yetu ya umwagiliaji mara nyingi tunaitazama katika mpunga tu, kila ukimsikiliza Mbunge au mtu ye yeyote anaitazama dhana ya umwagiliaji katika suala la mpunga. Sisi tunafanya jitihada ya kufungua masoko ya mazao yote, sasa hivi tunatumia Balozi zetu na hasa mazao ya nafaka, tunaanza *communication* na nchi ambazo zina masoko tuweze kujenga *bonded warehouses* kulekule ili wafanyabishara wetu waweze kupeleka mazao na kuyauzia sokoni badala ya kumsubiri mnunuzi atoke Kongo kuja Dar es Salaam au kuja Tanzania kununua. Kwa hiyo, hii ni njia nyingine ambayo

tunaitumia, tunaamini kwa kutumia Mabalozi; kupunguza ukiritimba katika biashara ya mazao; kufungua mipaka; kupunguza gharama za biashara na kuongeza tija mazao yetu yatapata masoko ya uhakika.

SPIKA: Mheshimiwa Fatuma Toufiq nimekuona, swali fupi la nyongeza.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuiliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika eneo la Zuzu, Jiji la Dodoma kuna bonde kubwa sana ambalo linafaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Je, Serikali haioni umefikia wakati wa kuweka miundombinu katika bonde hili la Zuzu ili kusudi kuendeleza kilimo cha umwagiliaji?

SPIKA: Majibu mafupi Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, tafadhalii. Zuzu pale kwa Mheshimiwa Mizengo Pinda.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mama Toufiq, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, siyo tu eneo la Zuzu, Wizara ya Kilimo tutatumia *potential area* zote ambazo tunaweza kwanza kukusanya maji kwa ajili ya mabwawa ambayo yana gharama nafuu, lakini maeneo yote ambayo yana mabonde na yanatatusaidia katika eneo la umwagiliaji na hasa hii mikoa ya kati ambayo ina ukame lakini ina mvua za kipindi kifupi lakini nyngi.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Zuzu na maeneo mengine yote ambayo ni *potential* katika Mkoa wa Dodoma na mikoa mingine tutaiweka katika mipango na tutaifanyia kazi.

SPIKA: Ahsante sana, wananchi wa Ngomai kule Kongwa Mheshimiwa Waziri ameellezea jinsi ambavyo Serikali ina mpango wa kuweka skimu kubwa ya umwagiliaji kule, kwa hiyo waendelee kuijandaa.

Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga uliza swali lako.

Na. 183

Kuwa na Sera na Mitaala Shirikishi Kati ya Zanzibar na Tanzania Bara kwa Elimu Msingi na Sekondari

MHE. NAJMA MURTAZA GIGA aliuliza:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwa na Sera na Mitaala shirikishi ili kuwa na msingi wa aina moja kuanzia elimu ya maandalizi, elimu msingi na sekondari kati ya Tanzania Bara na Zanzibar ili kuongeza ufaulu zaidi kwa upande wa Zanzibar?

SPIKA: Majibu ya swali hili, Naibu Waziri Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Omari Juma Kipanga, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Mbunge, naomba kuchukua fursa hii kuwatakia heri wanafunzi wetu wote wa kidato cha sita walioanza mitihani yao siku ya jana ambayo itaendelea mpaka tarehe 25. Tuna watahiniwa wa kidato cha sita 81,343 katika vituo 808 kote nchini. Sambamba na hao vilevile tuna watahiniwa 6,973 wa vyuo vya ualimu ambao nao vilevile wanafanya mitihani yao katika vyuo 75 nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikishirikiana vizuri na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika masuala mbalimbali ikiwemo

suala la elimu hususan katika utekelezaji wa mitaala na kutoa elimu bora kwa watoto wa Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sera na Mitaala shirikishi baina ya pande mbili za Muungano, Taasisi ya Elimu Tanzania (*TET*) hushirikiana na Taasisi ya Elimu Zanzibar (*TEZ*) katika masuala mbalimbali yahusuyo utekelezaji wa mitaala. Ushirikiano huu hutoa fursa mbalimbali ikiwemo mijadala kuhusu utekelezaji wa mitaala na jinsi ya kukabiliana na changamoto mbalimbali zitokanazo na ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi. Aidha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inafanya mapitio ya Sera ya Elimu ili kuweka uwiano wa miaka kwa Elimu ya Msingi baina ya Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara. Hivyo, nitoe rai kwa Watanzania wote kutumia nafasi hii ili kutoa maoni yao kuhusu mfumo huo. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Najma swalii la nyongeza, tafadhali.

MHE. NAJMA MURTAZA GIGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na nashukuru Serikali kwa hatua iliyofikia katika kurekebisha masuala ya sera na mitaala kwa pande mbilli za Muungano, hata hivyo na maswali mawili madogo sana ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza, muda mrefu sana Baraza la Mitihani lilikuwa likiwasiliana moja kwa moja na vituo vya mitihani vya Zanzibar na mara nyingi Wizara ya Elimu bila kuwa na taarifa. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuunda chombo maalumu cha kisheria ambacho kinatambulika ili kuweza kuunganisha Wizara ya Elimu ya Muungano na Wizara ya Elimu ya Zanzibar?

Mheshimiwa Spika swalii langu la pili ni kuhusu elimu ya juu, katika Bunge la Kumi na Moja niliuliza na nikaambiwa linafanyiwa kazi kuhusu vyuo vikuu huria ambapo vilevile vyuo ambavyo vinatumika hapa na kutambulika na *NACTE* wale watu ambao wamefanya mitihani kupitia vyuo hivyo wanakubalika kufanya kazi Tanzania Bara na pia

wanatambulika kwamba wamesoma na vyeti vyao vinatambulika lakini kwa Zanzibar havitambuliki. Je, suala hili limeflikia wapi? Ahsante.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Giga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Baraza la Mitihani Tanzania (*NECTA*) ni Taasisi ya Muungano ambayo inaendesha mitihani hapa nchini. Baraza la Mitihani lina muundo wa namna ya kuendesha shughuli zake; tunakuwa na Kamati za Mitihani ngazi ya Taifa, Mikoa na Wilaya. Kamati hizi ndizo ambazo zinafanya ule mtiririko wa mawasiliano na mahusiano katika uendeshaji wa shughuli za Baraza la Mitihani. Kwa hiyo, kimsingi vyombo viro, kwa kutumia Kamati hizi; ndizo ambazo zinaratibu pamoja na kuendesha mitihani kote nchini ikiwemo Tanzania Bara na Tanzania Visiwani.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Mitihani lina watumishi kule Zanzibar na vilevile tuna ofisi pale Zanzibar katika jengo lile la Shirika la Bima Zanzibar. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba Baraza la Mitihani limejipanga vizuri na namna bora ya mawasiliano pamoja na *co-ordination* ni kama hivyo nilivyooleza.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la pili, kwamba kuna vyuo ambavyo havitambuliwi na *NACTE*; naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba vyuo vyote vya elimu ya kati ambavyo vinahusika na masuala haya ya *NACTE* vimesajiliwa na *NACTE* na orodha ya vyuo hivyo ipo kwenye website.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namqomba tu Mheshimiwa Mbunge labda tuweze kukaa na kuangalia kuna changamoto zifi kule Zanzibar ambapo labda kuna vyuo

ambavyo havijapata usajili ili tuweze kujua kitu gani cha kufanya. Nakushukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana. Kwa sababu ya muda, naomba tuendelee. Kuanzia sasa sitaweka swali la nyongeza kwa sababu ya dakika ambazo ziko pale, ni chache sana.

Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima, Mbunge wa Kawe, uliza swali lako.

Na. 184

Kurasimisha Makazi ya Wananchi – Jimbo la Kawe

MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itakuja na mpango maalum wa kurasimisha makazi ya wananchi wa Mabwepande, Nakasangwe, Chasimba, Chatembo, Chachui, Ndumbwi na Jogoo ili kumaliza migogoro ya ardhi na kuiongezea mapato Serikali?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Askofu Josephat Gwajima, Mbunge wa Kawe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza Programu ya Urasimishaji wa Makazi ya Wananchi Nchini ikiwa ni pamoa na maeneo ya Nyakasangwe, Mabwepande na upangaji na upimaji wa maeneo ya Chasimba, Chatembo na Chachui, kadri ya matakwa ya kisheria. Pia, Halmashauri

kwa kushirikiana na Kampuni ya Upangaji ya *Afro Map Limited*, imeandaa michoro nane ya urasimishaji katika eneo la Nyakasangwe yenye jumla ya viwanja 9,472 ambapo viwanja 7,790 upimaji umekamilika na taratibu za umilikishaji zinaendelea kwa wananchi waliokamilisha malipo.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Mabwepande, Serikali kwa kushirikiana na Kampuni ya Upangaji ya *Mosaic Company Limited* imeandaa michoro saba ya urasimishaji yenye jumla ya viwanja 1,431. Viwanja hivyo viko katika hatua mbalimbali za upimaji na umilikishaji.

Aidha, katika maeneo ya Chasimba na Chachui (Mtaa wa Bashaya) na Chatembo (Mtaa wa Wazo), Serikali imepanga na kupima jumla ya viwanja 4,098 ili kutatua mgogoro uliodumu kwa muda mrefu kati ya wananchi na wamiliki wa Kiwanda cha Saruji cha Wazo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maeneo ya Mtaa wa Ndumbwi, Serikali inashirikiana na Kampuni ya Upangaji ya *Urban Vision* pamoja na Kampuni ya Upimaji ya *AG Sun Land Consult* kufanya urasimishaji katika maeneo ya Ndumbwi ambapo kazi ya kuandaa michoro saba ya mipangomiji yenye jumla ya viwanja 956 imekamilika.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni itaendelea na utekelezaji wa Mpango wa Urasimishaji wa maeneo ya Mtaa wa Jogoo katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022. Umilikishwaji wa viwanja vipatavyo 15,957 katika maeneo yote yaliyotajwa kutawezesha wananchi kuwa na milki salama, kupunguza migogoro na kupanua wigo wa makusanyo ya Serikali yatokanayo na sekta ya ardhi.

SPIKA: Mheshimiwa Askofu Gwajima ameridhika.
(*Kicheko*)

MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, napenda kuuliza:-

Mheshimiwa Spika, huko Nyakasangwe ambapo kule nyuma kumetokea mauaji kwa sababu ya matatizo ya ardhi. Je, ni lini sasa Waziri atakwenda pamoja nami huko ili tushughulike kuweka mambo ya wananchi sawa? Ahsante sana.

SPIKA: Majibu kwa kifupi, safari ya kaka na dada kuelekea Nyakasangwe.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, napenda nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge, Askofu Gwajima, kwamba tutapanga wakati wowote tuweze kwenda kwa sababu sasa tuko kwenye bajeti, lakini tutapata fursa nzuri ya kwenda kwenye eneo alilolitaja.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Nishati, swali la Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza.

Na. 185

Hitaji la Umeme Vijiji 127 Vilivyobaki vya Mkoa wa Songwe

MHE. JULIANA D. SHONZA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika vijiji 127 vilivyobaki vya Mkoa wa Songwe?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Naibu Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Byabato Stephen Lujwahuka tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Songwe una jumla ya vijiji 307 ambapo kati ya hivyo, vijiji 180 tayari vimeapatiwa

umeme na vijiji 127 bado havijapatiwa umeme. Nia ya Serikali ni kuvipatia umeme vijiji vyote visivyo na umeme kabla ya mwisho wa mwaka 2022.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TANESCO* na Wakala wa Nishati Vijiji (REA) inaendelea kupeleka umeme katika vijiji vyote ambavyo havijafikiwa na umeme Tanzania Bara. Vijiji 127 vilivyobaki katika Mkoa wa Songwe vitapatiwa umeme kupitia utekelezaji wa Mradi wa Kusambaza Umeme Vijiji Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili ambapo utekelezaji wake ulianza mwezi Machi, 2021 na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2022.

Mheshimiwa Spika, kazi za mradi kwa Mkoa wa Songwe zinajumuisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 1,065.4, msongo wa kilovoti 0.4 urefu wa kilomita 120, ufungaji wa transfoma 120 za 50kVA, pamoja na kuwaunganishia umeme wateja wa awali 2,640. Gharama ya mradi huu ni takriban shilingi bilioni 38.7.

SPIKA: Mheshimiwa Juliana Shonza, swali la nyongeza.

MHE. JULIANA D. SHONZA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini vilevile kwa *commitment* ambayo ameitoa kwa wananchi wa Mkoa wa Songwe. Nataka nitoe tu ushauri kwamba katika kutekeleza mkakati huo, wasisahau taasisi muhimu, hususan shule za *boarding*, kwa sababu katika Mkoa wa Songwe, shule nydingi sana za *boarding* zinakabiliwa na changamoto ya kutokuwepo kwa umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba niulize swali langu moja la nyongeza. Utakubaliana nami kwamba upatikanaji wa umeme wa uhakika ni *aspect* muhimu sana katika kukuza uchumi wa eneo husika; nasi wananchi wa Mkoa wa Songwe tunakabiliwa na changamoto kubwa sana ya kukatika katika kwa umeme mara kwa mara; na hii imekuwa ni changamoto kubwa hususan katika ile miji mikubwa ya kibashara kwa

maana ya Miji ya Mlowo, Tunduma kule kwa Mheshimiwa David Silinde na Vwawa:- (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka kujua kwamba je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kwenda ama kutuma wataalam wake katika Mkoa wa Songwe ili kuweza kubaini changamoto hiyo na kuipatia ufumbuzi? Ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Kalemani, majibu ya maswali hayo tafadhalii.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri katika swalii msingi la Mheshimiwa Shonza. Kwanza, ni kweli zipo taasisi nyingi ambazo kimsingi zinahitaji kupatiwa umeme, hasa huu wa Programu ya REA; na tumeainisha taasisi zote ziliwemo shule za msingi, sekondari na vituo vya afya, na tumetoa maelekezo kwa wakandarasi kuzingatia kipaumbele cha kupeleka umeme kwenye taasisi za Umma kama kipaumbele. Kwa hiyo, naomba nitoe msisitizo kwa wakandarasi kuzingatia hilo. Pili, nawaomba Wakurugenzi na Wenyeviti wa Halmashauri kutenga fedha kidogo angalau kulipia kupelekea taasisi za Umma umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika swalii la pili ambalo ni la uimara wa umeme katika Mkoa wa Songwe. Nampongeza sana Mheshimiwa Shonza na Wabunge wa Songwe kwa ujumla kwa kufuatilia masuala ya umeme katika mkoa wao. Ni kweli Mkoa wa Songwe unapata umeme kutoka lyunga iliyoko Mbeya, na ni takribani kilometra 70 kutoka kwenye kituo cha kupoozea umeme.

Mheshimiwa Spika, tumechukua hatua mbili madhubuti, na niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa Songwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hatua ya kwanza, tumejenga njia ya kusafirisha umeme kwa dharura kwa kuipusha kukatika kwa umeme katika Mkoa mzima wa Songwe kwa kujenga

laini ya kilometra 70 kutoka Iyunga mpaka Mlowo; na tumeanza hivyo toka Januari na mradi unakamilika Mei mwaka 2021. Tumetenga shilingi bilioni 2.4 ambazo ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, maeneo yatakayopelekewa umeme ni Mlowo, Tunduma, Vwawa yenyewe pamoja na Momba; na tutagawa laini *specific* kwa kazi hiyo. Kwa hiyo, kuazia mwezi Mei mwaka huu, maeneo ya Songwe yatapata umeme wa uhakika. Ahsante sana. (*Makofî*)

SPIKA: Mheshimiwa Stella Ikupa, nilikuona. Swali fupi la nyongeza.

MHE. STELLA I. ALEX: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Tatizo ambalo lipo katika Mkoa wa Songwe linafanana kabisa na tatizo ambalo liko katika Mkoa wa Dar es Salaam kwenye baadhi ya maeneo, na hasa katika Jimbo la Ukonga kwenye baadhi ya Mitaa ya Kata za Msongola, Chanika, Zingiziwa na Buyuni:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inasema nini kwa habari ya kuhakikisha kwamba Mkoa wa Dar es Salaam unapata umeme?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Nishati.

WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Dar es Salaam una mahitaji makubwa sana ya umeme, ingawa Dar es Salaam tuna jumla ya Megawati 572 zinazotumika kwa Dar es Salaam, lakini mahitaji yanaongezeka kila leo. Tumejenga *dedicated line* ya kutoka Kinyerezi kupita Gongo la Mboto kwenda mpaka Ukonga – Pugu mpaka Dondwe kule Chanika Zingiziwa kwa ajili ya kupelekea umeme wananchi wa huko.

Mheshimiwa Spika, tumewapatia mkandarasi wa *peri-urban* atakayepeleka umeme katika maeneo ya Bomba Mbili, Majohé, Mvuti, Songambele pamoja na Zingiziwa

mpaka Kisasa, mpaka Magerezani kule Dondwe ndani. Kwa hiyo, wananchi wa Dar es Salaam watapata umeme, na ni ndani ya miezi sita utaratibu utakamilika na wananchi kupata umeme wa uhakika.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo. Bado tuko Wizara ya Nishati. Sasa tunaelekea Meatu kwa Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya.

Na. 186

Hitaji la Umeme Katika Kata ya Meatu

MHE. LEAH J. KOMANYA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Kata za Mwamalole, Mbushi, Mwamanongu, Imalaseko, Mwamanimba, Mwabuzo na Kimali ili wananchi waweze kufaidika na huduma hiyo na kuchochea maendeleo katika Kata hizo?

SPIKA: Swali hili muhimu sana Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. Kata saba ndani ya Wilaya ya Meatu hazina umeme kabisa.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kuititia Mradi Kabambe wa kupeleka umeme vijiini unaosimamiwa na Wakala wa Nishati Vijiini (*REA*) inaendelea kupeleka umeme katika kata na viji viyote ambavyo havijafikiwa na umeme Tanzania Bara zikiwemo Kata za Mwamamole, Mwamanimba, Mwabuzo, Imalaseko, Mwamanongu, Mbushi na Kimali. Kata hizi pamoja na viji vyake vyote vya Meatu vinatarajiwa kufikishiwa umeme ifikapo mwezi Desemba, 2022.

Mheshimiwa Spika, kazi za mradi katika Wilaya ya Meatu zinajumuisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometra 555.90, msongo wa kilovoti 0.4 urefu wa kilomita 48, ufungaji wa transfoma 48 za 50kVA, pamoja na kuwaunganishia umeme wateja wa awali 1,056. Gharama ya mradi huu ni takriban shilingi bilioni 22.6.

SPIKA: Mheshimiwa Leah Komanya.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Pia namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuongeza vijiji tisa ambavyo viliachwa katika mzunguko wa pili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika Mzunguko wa Pili wa REA Awamu ya Tatu, Serikali imetenga wigo mdogo wa kusambaza umeme katika vijiji ambao ni kilometra moja.

Je, Serikali haionti namna ya kuongeza wigo kutokana na mtawanyiko wa jinsi vijiji vyetu vilivyo? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kukatika katika kwa umeme katika Jimbo la Meatu na Mkoa wa Simiyu kwa ujumla kumeathiri utekelezaji wa shughuli za maendeleo za wananchi: Je, ni lini kituo cha kupoozea umeme kitakamilika katika Mkoa wa Simiyu?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika upelekaji wa umeme kwenye maeneo yetu hatuwezi kufika katika maeneo yote kwa wakati mmoja. Ni kweli kwamba wigo uliopo hautoshelezi mahitaji tuliyokuwa nayo kwa sababu mahitaji ni makubwa kuzidi uwezo tuliokuwa nao.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi kwamba mara kwa mara tumekuwa tukiongeza wigo kwa maana ya kupanua *scope* ya kazi ambayo

tunakuwa tumempa mkandarasi kulingana na mahitaji ya eneo husika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Leah, ambaye amekuwa mfuatiliaji mzuri sana wa masuala ya umeme ya Jimbo lake, kwamba tutakapokwenda katika utekelezaji, tutaongeza wigo kama ambavyo tayari tumeongeza wigo wa vijiji tisa ambavyo Mheshimiwa Waziri amevitaja hapo kuhakikisha kwamba tunawafikia wananchi wote kuwapelekea umeme.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili; ni kweli Mkao wa Simiyu unapokea umeme kutoka maeneo matatu; Mwanza, Shinyanga (Ibadakuli) na Bunda. Umeme huo unakuwa siyo wa uhakika kwa sababu unasafiri umbali mrefu. Hivyo Serikali imechukuwa jitihada za kuamua kujenga kituo cha kupooza umeme pale Imalilo katika Mkao wa Simiyu ambacho kitagharimu takribani shilingi bilioni 75 na ujenzi wa *transmission line* ya kilometra 109 kutoka Ibadakuli (Shinyanga) mpaka pale Imalilo.

Mheshimiwa Spika, kituo hiki tayari kilizinduliwa na Mheshimiwa Waziri. Ujenzi wake ulizinduliwa tarehe 3 Machi, kwa kuweka jiwe la msingi na tunatarajia kwamba mwezi Julai tutakuwa tayari tumekamilisha taratibu za manunuza na kufikia mwishoni mwa mwaka ujao Desemba, kituo hicho kitakuwa kimekamilika chenye kuweza kusafirisha msongo wa kilovoti 220.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mkao wa Simiyu utakuwa una uhakika wa umeme kwa sababu umeme mkubwa utakuwa unapoozwa pale na kusambazwa katika maeneo yote ya Mkao wa Simiyu na hivyo tatizo la kukatika katika kwa umeme litakwisha. (*Makofii*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara Ujenzi na Uchukuzi, swali la Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela.

Na. 187

Ujenzi wa Barabara ya Mpakani – Mtawanya – Nanyumbu

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya mpakani kutoka Mtawanya kwenda Nanyumbu kuititia Mpilipili – Mapili – Chikoropola – Lichele – Lupaso hadi Lipumburu?

SPIKA: Majibu ya swali hilo la watu wa Lulindi, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa *Engineer Godfrey Kasekenya Msongwe*.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimwa Issa Ally Mchungahela, Mbunge wa Lulindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Mpilipili – Mapili – Chikoropora – Lichele – Lupaso hadi Lipumburu ni sehemu ya barabara ya ulinzi ya Mtwara – Madimba – Tangazo – Mahurunga – Kitaya – Namikupa hadi Mitemaupinde yenye urefu wa kilometra 365.5. Sehemu ya barabara hii yenye urefu wa kilometra 258.0 imeshafunguliwa na inaendelea kufanyiwa matengenezo ya kila mwaka na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*). Aidha, Serikali imekuwa ikitenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuendelea kuifungua barabara hii kwa sehemu iliyobaki yenye urefu wa kilometra 107.3.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) unaendelea kuiboresha barabara hii kwa kuhakikisha inapitika majira yote ya mwaka ambapo jumla ya kilometra 10.8 zimejengwa kwa kiwango cha lami katika maeneo korofa ya milima ya Mtawanya, Kilimahewa, Mdenganamadi, Mnongodi na Dinyeke. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Mchungahela, Mbunge wa Lulindi, swali la nyongeza.

MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA: Mheshimiwa Spika, naomba nijenge maswali yangu kuititia kwenye hoja tatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii ni muhimu sana kwa ajili ya ulinzi wa nchi hii; pia barabara hii ni muhimu sana kwa usafirishaji wa mazao ya ufuta na korosho katika kata zilizopo pembezoni mwa Mkoa wa Mtwara; barabara hii ni muhimu vile vile kwa usafirishaji wa ufuta na korosho kutoka katika maeneo ya nchi jirani ambayo mazao hayo hayana masoko kule:-

(i) Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami? (*Makofii*)

(ii) Je, Serikali ina *commitment* gani kwamba barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami na lini?

SPIKA: Ahsante sana. Majibu ya maswali hayo, unaweza ukayaunganisha Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhalii. Barabara ya lami katika barabara hiyo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE): Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Issa Ally Mchungahela yote mawili kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, naomba tu nitoe taarifa kwamba barabara hii ni barabara ambayo inafunguliwa. Kwa hiyo awamu ya kwanza ni kuifungua barabara hii yenye urefu wa kilometra 365 na ikishafunguliwa ndipo utaratibu wa kuijenga kwa kiwango cha lami utaanza kufanyika.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetambua umuhimu wa barabara hii, kwanza ni barabara ambayo ni muhimu sana kwa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, lakini pia ni barabara muhimu sana kwani ikishafunguliwa itafungua uchumi na itaboresha maisha ya wananchi wengi ambaa wanaishi katika kata ambazo amezitaja.

Mheshimiwa Spika, barabara hii inatoka Mtwara hadi Ruvuma na ni barabara ambayo inaambaaambaa na Mto Ruvuma. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya hatua ya kujenga barabara hii kwa kiwango cha changarawe, hatua za ujenzi kwa kiwango cha lami zitafuata kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Jerry Silaa, bado tuko Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.

Na. 188

**Ujenzi wa Barabara Inayounganisha Jimbo la
Ukonga na la Mbagala**

MHE. JERRY W. SILAA aliuliza:-

Je ni lini Serikali itajenga barabara inayounganisha Jimbo la Ukonga na Mbagala kwa mkupuo badala ya kujenga kilometra moja kila mwaka ili kuondoa kero ya usafiri kwa wakazi wa Majimbo hayo?

SPIKA: Majibu ya Swali hilo, Mheshimiwa Mwita Mwaikwabe Waitara, Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA
M. WAITARA) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jerry William Silaa, Mbunge wa Jimbo la Ukonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa bajeti, kuanzia mwaka 2000 Serikali imekuwa ikijenga barabara hii ya Chanika - Mbande inayounganisha Jimbo la Ukonga na Mbagala kwa kiwango cha lami kwa awamu. Hadi sasa jumla ya kilometra 14.34 kati ya kilometra 19.29 sawa na asilimia 74.5 zimejengwa na kukamilika kwa kiwango cha lami. Aidha,

kilometra 4.95 zilizosalia zitaendelea kujengwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Jerry Silaa.

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Spika, pamoja na salamu za shukrani na pongezi kwa Mheshimiwa Waitara kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi na shukurani zetu kwa Mheshimiwa Rais kwa kumpa nafasi hii, tunaamini swali hili angeweza kulijibu bila hata kusoma, kwa nasaba yake na Jimbo la Ukonga. Naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza, kwa kuwa Jimbo la Ukonga na Jimbo la Mbagala ndiyo majimbo pekee kwenye Mkoa wa Dar es Salaam ambayo hayaunganishwi na barabara ya lami; na barabara hii ni barabara muhimu sana kwa wananchi wa Kata ya Chanika, Msongola kujunga na Jimbo la Mbagala.

Naomba *commitment* ya Serikali kipande hiki kidogo kilichobaki cha kilometra 4.95 ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, kwa kuwa mazingira ya Jimbo la Ukonga yanafafana na Jimbo la Mbeya Mjini, ni lini Serikali itapanua barabara ya *TANZAM* inayotoka Dar es Salaam kuelekea Tunduma, kipande cha Uyole – Tunduma kilometra 104, na kipande cha Uyole – Igawa kilometra 116. Barabara hii inasomeka ukurasa wa 66 wa llani yetu ya Uchaguzi yenye kurasa 303. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo na hasa swalii la pili linahitaji majibu maalum kabisa. (*Makofii/Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jerry William Silaa, Mbunge wa Ukonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ili ni swali la kihistoria, Waswahili wanasema mtoto mpe mchawi akulelee. Ni kweli kwamba barabara ya Mbagala – Mbande naifahamu na Mheshimiwa Jerry pamoja na Mheshimiwa Chaurembo Mbunge wa Mbagala, nilipoteuliwa kuwa Naibu Waziri katika eneo hili suala la kwanza, hata hawakunisalimia, walitaja barabara hii na kwa sababu ya umuhimu wake. Barabara hii ikijengwa vizuri kiwango cha lami wananchi wanaweza wakatoka Ukonga wakaenda Mbagala wakaenda Kusini au Kusini anakuja Dodoma haina sababu ya kupitia mjini kuepuka foleni anaweza akapita eneo hili.

Mheshimiwa Spika, nimekwishaongea na *Chief wa TANROAD Engineer* Mfugale, kwamba walikuwa wametenga fedha vipande vipande vyta matengenezo mbalimbali katika eneo hili. Kuanzia mwezi Julai mwaka mpya wa fedha 2021/2022 Mheshimiwa Jerry na Mheshimiwa Chaurembo barabara hii kilometra 4.9 zitaanza kujengwa kwa kiwango cha lami ili watu waweze kupata huduma katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, wiki iliyopita Mheshimiwa Naibu Spika alikalia kitu hapo ulipokaa, akatoa malalamiko kwamba eneo lake daraja lilivunjika tangu 2019 na mpaka leo anapozungumza na asubuhi amenikumbusha mkandarasi hayupo *site* na nilitoa maelekezo hapa kwamba mkandarasi aende *site* wafanye kazi ya dharura ili kuwa na uunganisho katika eneo hilo ili watu wapite.

Mheshimiwa Spika, leo nazungumza habari ya barabara. La kwanza, kabla leo jua halijazama nipate maelezo kwa nini mkandarasi hajawa *site* katika eneo lile, daraja lile halijatengenezwa tangu 2019 mpaka leo. La pili, kwa kibali chako na kibali cha Mheshimiwa Waziri Mkuu *weekend* ijayo nitaenda Mbeya kutembelea barabara hii pamoja na daraja nione kama kweli mkandarasi hayupo *site*, baada ya hapo tutaongea vizuri. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Swali la mwisho kwa siku ya leo litaelekea Wizara ya Maji na litaulizwa na Mheshimiwa Reuben Nhamanilo Kwagilwa, Mbunge wa Handeni Mjini.

Na. 189

Utekelezaji wa Mradi wa Maji Handeni

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya ujenzi wa mradi mkubwa wa maji *Handeni Trunk Main (HTM)*?

SPIKA: Majibu ya swali hilo. Mheshimiwa Naibu Waziri Maji *Engineer Maryprisca Mahundi*, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Reuben Kwagilwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipata mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya India kupitia Benki ya *Exim*, jumla ya Dola za Marekani milioni 500 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika miji 28 nchini ukiwemo Mradi wa Maji wa Kitaifa Handeni (*Handeni Trunk Main*) utakaohudumia vijiji 84 katika Wilaya ya Handeni pamoja na Miji Midogo ya Mkata, Komkonga, Kabuku, Michungwani, Segera pamoja na Mji wa Handeni.

Mheshimiwa Spika, taratibu za kupatikana kwa wakandarasi watakaotekeliza mradi huu zimekamilika na unatarajiwu kuanza wakati wowote katika mwaka wa fedha 2020/2021 na ujenzi wa mradi umepangwa kutekelezwa miezi 24.

SPIKA: Mheshimiwa Reuben Kwagilwa Mbunge wa Handeni Mjini, swali lako nyongeza.

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Ndani ya Mkutano huu wa Tatu Serikali ilikuja hapa ikatoa majibu kwamba mradi huu wa *HTM* utaanza mwezi wa Aprili.

Wananchi wamekuwa wakiniuliza mara kwa mara mwezi Aprili umepita na mradi haujaanza. Sasa kwenye majibu ya Serikali wanadai kwamba mradi utaanza kabla ya mwaka huu wa fedha kuisha. Mwaka wa fedha unaisha mwezi mmoja mbele, naomba njue ni lini hasa mradi huu utaanza kwa ajili ya wananchi wa Jimbo la Handeni? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, wananchi wa Jimbo la Handeni tuna dhiki kubwa ya maji na tumekuwa tukinywa maji kwenye mabwawa kwa miaka mingi lakini mabwawa haya pia yamebebwa na mvua katika misimu iliyopita. Bwawa la Kwimkambala pale Kwendyamba, Kumkole pale Mabanda pamoja na Bwana la Mandela pale Kwenjugo; yote haya yamebebwa na mvua.

Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati wa mabwawa haya ili wananchi angalau tuendelee kunywa maji tukisubiria Mradi huu wa *HTM*. (*Makofii*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Aweso, anataka ni lini?

WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru lakini nimponeze Naibu wangu kwa namna anavyojibu maswali. Kubwa nimponeze sana kaka yangu Reuben amekuwa amefuatilia mradi huu mkubwa wa miji 28.

Mheshimiwa Spika, kesho nimewaalika Wabunge wote wanaohusiana na mradi huu wa miji 28 tuwape *commitment* na uelekeo mzima wa mradi huu. Kwa hiyo nimwombe sana kesho katika kikao ambacho tutakachokaa tutatoa commitment ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kubwa tunatambua kabisa kwa eneo la Handeni palitokea mafuriko yale mabawa yalikwenda na maji, Mheshimiwa Mbunge kwa udharura huo na sisi tuna pesa za dharura, naomba saa saba tukutane tuone namna ya kuweza kusaidia wananchi wake waweweze kupata huduma ya maji. (*Makofii*)

SPIKA: Tatizo la maji ni kubwa, tunajua Wizara ya Maji mnajitahidi sana lakini Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mwigulu tunahangaika na tatizo la maji hapa ambalo Mheshimiwa Waziri wa Maji anahangaika nalo sana na Naibu wake. Hata hivyo, kama ambavyo huwa tunasema mara kwa mara kwamba Wizara ya Fedha na nyinyi tunahitaji huko mbele maelezo kidogo. Kwa mfano, kuna fedha zilitolewa na Serikali ya Misri kwa ajili ya visima virefu 30 miaka miwili na hii ni *grant free*, miaka miwili zimekwama Wizara ya Fedha. Hii mikwamo hebu nenda kaikwamue huko na kama unakwama sana basi tujulishe tuelewe ili tusiwe tunawasumbua. Pale tunapokuwa tumesaidiwa na tuna shida kubwa namna hii yaani tatizo ni nini? Ahsante sana. (*Makof!*)

Sasa ni wakati wa kuwatambulisha wageni walioko Bungeni. Naanza na Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt. Lenard Akwilapo, karibu sana Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu pamoja na Wakuu wa Vitengo na Taasisi Mbalimbali na Maafisa wa Wizara ya Elimu. (*Makof!*)

Wageni wanne wa Mheshimiwa Priscus Tarimo ambaao ni Wadau wa Utalii kutoka Moshi, Mkoani Kilimanjaro wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa ZARA Tours, ndugu Zainabu Anselm. Karibuni sana popote pale mlipo ZARA Tours. (*Makof!*)

Wageni sita wa Mheshimiwa Salma Kikwete, ambaao ni watoto wake kutoka Taasisi ya Wanawake wa Maendeleo (WAMA) pia ni wawakilishi na viongozi wa vijana ambaao wamenufaika na taasisi hiyo wakiongozwa na ndugu Mohamed Pwimu. Karibu sana wapo pale, hongereni sana, mazao ya kazi za mikono ya Mama Salma, Mwenyezi Mungu atakubariki sana katika kazi hiyo. Ahsante sana. (*Makof!*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambaao ni Waratibu wa Mradi wa Haki Elimu kutoka Jijini Dar es Salaam ndugu Godfrey Bonaventure na ndugu Makumba Mwemezi, wale kule. Ahsante sana. (*Makof!*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Florent Kyombo, ambao ni wapiga kura wake kutoka Bukoba Mkoani Kagera ambao ni ndugu Fred Kanyika, ndugu Sadati Mnyasa na ndugu Michael Miraji. Karibuni sana. (*Makofî*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Oliver Semuguruka, ambao ndugu zake kutoka Bukoba Mkoani Kagera wakiongozwa na ndugu Almasoud Kalumuna. Karibuni sana wa kutoka Kagera kule. (*Makofî*).

Wageni wanne wa Mheshimiwa Jonas Zeeland, ambao ni Madiwani toka Wilaya ya Mvomero Mkoani Morogoro wakiongozwa na Frank Mwananziche. Madiwani toka Mvomero karibuni sana. (*Makofî*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, ambao ni wana maombi kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na ndugu Godson Mushi, wapo kule, karibu sana, sana. (*Makofî*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Innocent Bilakwate, ambao ni wana maombi kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na ndugu Neema Ngomoka, nadhani ni hawa hawa. (*Makofî*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Pauline Gekul, Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, hawa ni wana maombi wanaoongozwa na Amochiche Kita, karibuni sana pia. (*Makofî*)

Pia, tuna wanamaombi wageni wa Mheshimiwa Atupele Mwakibete, kutoka hapa Dodoma wakiongozwa na Mchungaji Obadia Chitalia, karibuni sana. (*Makofî*)

Mtaona wanamaombi wamekuwa wakialikwa kuja na ni jambo jema, waendelee katuombea, waliombee Taifa letu, mumwombee Rais wetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, ni muhimu sana kuwa na Taifa lenye kumuamini Mungu.

Pia kuna wanamaombi wageni wa Mheshimiwa Christine Ishengoma, Ritha Kabati pia na wana maombi wengine na watumishi. Karibuni. (*Makof*)

Mheshimiwa Janejelly Ntate ana watumishi wa Mungu kutoka mikoa mbalimbali wakiongoza na Hakimu Mbago, karibuni sana. (*Makof*)

Wageni kumi wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao pia ni wanamaombi kutoka Mikoa ya Dodoma, Morogoro, Mbeya na mahali pengine, karibuni sana, leo kwa kweli tumebarikiwa kuwa na wanamaombi wengi sana. (*Makof*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Irene Ndyamkama ambao ni wanamaombi pia wakiongozwa na Happy Nuru. Karibuni sana. (*Makof*)

Wageni kumi na tano wa Mheshimiwa Abubakar Asenga, Mheshimiwa Asia Alamga na Mheshimiwa Ng'wasi Kamani kutoka Taasisi ya Tanzania *Youth Vision Association* Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Mwenyekiti wao ndugu Abdallah Lugome, wale pale, karibuni sana. (*Makof*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Noah Lemburis ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimboni Arumeru wakiongozwa na Proches Ndau, wale kule toka Arumeru. Karibuni sana. (*Makof*)

Wageni thelathini na nne wa Mheshimiwa Hassan Kungu ambao ni timu ya mpira wa miguu ya Namungo FC, hiyo ni Namungo FC, hongereni sana, sana. Waheshimiwa makofi hayatoshi kwa Namungo hayo, hongereni sana, mmetubebea, mmetupa sifa kubwa, mmeanza vizuri, ni timu yenye kutia matumaini. Endeleeni sana kujitahidi katika mpira, lakini kama mmekuja kucheza na Dodoma Jiji, endapo hicho ndicho kilichowaleta mijipange, kwa sababu Dodoma Jiji ni baba lao. (*Makof/ Kicheko*)

Mwisho siyo kwa umuhimu, tunaye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa Mheshimiwa White Zuberi

karibu sana. Lakini pia Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa Dkt. Omary Nkullo. (*Makof*)

Kipekee kwa mara ya kwanza toka niwe Mbunge kwa miaka ishirini Madiwani wa Kongwa hawajawahi kufika Bungeni hapa, lakini leo kwa mara ya kwanza Baraza la Madiwani la Kongwa lipo hapa mjengoni.

Naomba Madiwani wa Kongwa msimame wote. Karibuni sana, sana, Waheshimiwa Madiwani. Hiyo ndiyo timu ya ushindi, hiyo ndiyo timu ya ushindi ya Mheshimiwa Spika. (*Makofi/ Kicheko*)

Katika mara tano ambayo nimeshinda Kongwa mara mbili nimeshinda bila kupingwa nikiwa na timu hii. Hongereni na karibuni sana ndugu zangu, ingawaje ndiyo mnafika kwa mara ya kwanza lakini hamjachelewa, karibuni sana, nimefarijiwa sana kwa kuja kwenu. (*Makofi/ Kicheko*).

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Spika, jambo la dharura.

SPIKA: Kanuni?

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 54.

SPIKA: Kanuni ya 54, ngoja niifungue, tusomee hiyo Kanuni kwanza. Haya endelea.

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Spika...

SPIKA: Tusomee Kanuni kwanza, mwenye kitabu ampe, hicho hapo unaazimwa. (*Kicheko*)

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Spika, nasimama kwa Kanuni ya 54, kuahirisha Shughuli za Bunge ili kujadili jambo la dharura. Baada ya muda maswali kuisha 54(1): *"Mbunge ye yote anaweza kutoa hoja ya Shughuli za Bunge kama zilivyoonyeshwa kwenye Orodha ya Shughuli ziahirishwe*

ili Bunge lijadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa umma." (Kicheko)

SPIKA: Nakuruhusu sasa.

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Spika, wote mnafahamu kwamba na tumeona kwenye vyombo mbalimbali vya habari kwamba zipo mvua zinaendelea kunyesha kwenye maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Mvua hizi zimeleta madhara makubwa sana kwenye miundombinu ya barabara, yapo maeneo mengi na Waheshimiwa Wabunge hapa ni mashahidi; kule Malinyi barabara zimekatika na mawasiliano yamekatika, kule Kyela barabara zimekatika na mafuriko yametokea.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mbeya Mjini napo kuna matatizo makubwa, Jimbo la Kilombero kwa Assenga mmeona akipiga magoti, lakin na Jimbo la Ukonga maeneo ya Majohi, Bombambili, Kivule, Ulongoni barabara hazipitiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naleta kwako jambo hili la dharura ili shughuli za Bunge kama itakupendeza zisimame ili jambo hili liwekwe kwenye orodha ya shughuli za Bunge, tuweze kufanya mjadala, kuona Serikali ina mpango gani wa kuwanusuru wananchi. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Nasoma tena Kanuni subirini. Kanuni inasema, maana tunajifunza Wabunge wengi bado wageni jamani.

Baada ya muda wa maswali kuisha, yuko sahihi Mbunge mpaka sasa. Mbunge ye yeyote anaweza kutoa hoja na Mbunge hajatoa hoja ikaungwa mkono kwa hiyo, jambo lake halichukuliwi. Tuendelee kujifunza jamani kanuni hizo.

Katibu.

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI

HOJA ZA SERIKALI

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA ELIMU,
SAYANSI NA TEKNOLOJIA KWA MWAKA WA
FEDHA 2021/2022**

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Profesa Ndalichako nakukaribisha uendelee na shughuli ahsante sana. (*Kicheko/Makofi*)

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa kunipa nafasi ya kuweza kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane, tumsikilize Waziri.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema na kuniwezesha kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu, kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha, 2020/2021 umekuwa ni mwaka wenye majonzi makubwa katika nchi yetu. Tumeondokewa na mpendwa wetu kiongozi wetu

shupavu mchapakazi na mzaledo Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia tumeondokewa na Mheshimiwa Benjamin William Mkapa aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tumeondokewa na Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Balozi John William Kijazi aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu pia limewapoteza Waheshimiwa Wabunge wawili, Mheshimiwa Martha Umbula aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Manyara na Mheshimiwa Atashasta Nditiye aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Muhammadi. Tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuapishwa kuwa Rais wa Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nampongeza pia, kwa hotuba aliyoitoa tarehe 22 Aprili, 2021 katika Bunge lako Tukufu ambayo imetoa dira na mwelekeo wa Serikali yake. Kwa heshima na unyenyekevu mkubwa natoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunteua kuendelea kusimamia Wizara hii, naahidi kuwa nitatekeleza majukumu yangu kwa weledi na uadilifu wa hali ya juu. Naomba Mwenyezi Mungu anisaidie.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Phillip Isdor Mpango kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kwa kuaminiwa tena kushika wadhifa huo. Napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, naomba nikupongeze wewe Mheshimiwa Job Yustino Ndugai, Spika wa Bunge letu Tukufu na Naibu Spika Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu kwa kuchaguliwa tena kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa awamu nyingine.

Mheshimiwa Spika, kuchaguliwa kwenu tena kuongoza Bunge hili kunaonesha ni jinsi gani mlitekeleza kwa weledi majukumu yenu katika Bunge la 11, tunawaombea Mwenyezi Mungu awape hekima na busara muendelee kutuongeza vyema.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezeki wa Kamati ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Makamu Mwenyezeki na Wajumbe wote wa kamati kwa kuchambua na kuishauri Wizara kuhusu Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwapongeza Mawaziri wenzangu na Manaibu Mawaziri wote walioteuliwa kuongoza Wizara mbalimbali. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa Wabunge wa Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hongereni sana Waheshimiwa Wabunge wote, naahidi kuwapa ushirikiano wa dhati nami naomba ushirikiano wenu ili kwa pamoja tuboreshe elimu katika nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naishukuru kwa dhati familia yangu kwa kuendelea kunipa ushirikiano na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa utulivu. Aidha, kwa namna ya pekee kabisa nawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Kasulu Mjini, kwa kunichagua kwa kura za kishindo na kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitumie nafasi hii kuwataki heri watahiniwa 81,343 wa Kidato cha Sita na 6,973 wa Ualimu walioanza mitihani yao jana tarehe 3 Mei, 2021. Mwenyezi Mungu awape utulivu ili wafanye mitihani yao vizuri

kwani naamini kuwa, walimu wamefanya kazi nzuri ya kuwaandaa kitaaluma na kimaadili.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba nitoe taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya utekelezaji wa bajeti, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha shilingi 1,348,563,375,000 kwa ajili ya Fungu 46. shilingi 491,049,151,000 zilikuwa ni za Matumizi ya Kawaida na shilingi 857,514,224,000 zilikuwa ni za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, kupitia Tume ya *UNESCO* Fungu Na. 18 Bunge liliidhinisha kiasi cha shilingi 2,239,181,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na mishahara ya watumishi wa Tume.

Mheshimiwa Spika, Ukusanyaji wa maduhuli, wizara ilitarajia kukusanya shilingi 555,651,650,346.52 hadi kufikia Aprili, Wizara ilikuwa imekusanya shilingi 339,128,392,104.16 ambayo ni sawa na asilimia 16 ya makadirio. Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi 434,737,497,950.09 kwa ajili ya Matumizi ya kawaida sawa na asilimia 88.5 ya fedha zilizoidhinisha. Aidha, kupitia Tume ya *UNESCO* Fungu Na. 18 Wizara ilipokea kiasi cha Shilingi 1,515,856,166.60 sawa na asilimia 60 ya fedha iliyoidhinishwa. Kwa upande wa miradi ya maendeleo, hadi kufikia Aprili 2021, Wizara ilikuwa imepokea shilingi 634,622,139,494.67 sawa na asilimia 74 ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya utekelezaji wa majukumu, sasa naomba nitoe taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kama ilivyoainishwa katika ukurasa wa 7 hadi 22 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, Uendeshaji wa Elimu msingi, Sekondari na Vyuo vya Walimu, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Serikali imechapa na kusambaza vitabu vya kiada nakala 4,905,586, kiongozi cha mwalimu nakala 268,000 na mihutasari nakala 365,368 kwa masomo yote ya darasa la

sita na la saba. Aidha, Serikali imewezesha udhibiti ubora wa shule kufanya tathmini kwa shule za awali na msingi 2,755 na imefanya ufuatilaji na tathmini katika vituo vya walimu 269.

Mheshimiwa Spika, Programu ya lipa kulingana na matokeo, kupitia programu hii Serikali imejenga ofisi 55 za udhibiti ubora wa shule, inaendelea na ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Mfano hapa Dodoma inayogharimu kiasi cha shilingi bilioni 17, imewezesha ujenzi wa shule mpya 44 kwa gharama ya shilingi bilioni 28 kwa lengo la kuongeza fursa za elimu. Na pia, imewezesha ujenzi wa vyumba vya madarasa 3,283 matundu ya vyoo 5,383, mabweni 112, nyumba za walimu 32 pamoja na miundombinu mingine ya elimu ambapo kiasi cha shilingi bilioni 83.59 kimetumika. Pia, kupitia mradi huu tumewezesha ukarabati katika vyuo vya ualimu 9 na ujenzi wa vyuo vya walimu vya Dakawa, Muhonda na Sumbawanga.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi na uendelezaji wa elimu maalum, Serikali imetoa mafunzo kazini kwa walimu 1,076 wa shule za msingi na sekondari wanaofundisha wanafunzi viziwi, wasioona, wenyе ulemavu wa akili na wenyе usonji. Imenunua vishikwabi 402 katika shule 38 ili kuimarisha ufundishaji wa lugha ya alama. Pia imenunua viti mwendo 536 kwa ajili ya wanafunzi wenyе ulemavu wa viungo na imesambaza vifaa vya kielimu na saidizi 33,458 kwa wanafunzi wenyе mahitaji maalum katika shule za msingi 1,260 na sekondari 45.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa kuimarisha mafunzo ya elimu ya ualimu. Kupitia mradi huu, Serikali imewezesha mafunzo ya lugha ya alama kwa walimu wa sekondari 269 kutoka shule 24 na imewezesha mafunzo ya *TEHAMA* kwa wakufunzi 396 wa Vyuo vya Ualimu vya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa ukarabati wa Vyuo vya Ualimu, Serikali imekamilisha ujenzi na ukarabati wa miundo mbinu katika Chuo cha Ualimu Shinyanga, imekamilisha ujenzi wa bwalo katika Chuo cha Ualimu Mpuguso, imekamilisha

ukarabati wa mabweni, vyoo vya wanachuo na nyumba za watumishi katika Chuo cha Ualimu Ndala na inaendelea na kukamilisha ujenzi wa miundo mbinu katika Chuo cha Ualimu Kitangali.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi na uendelezaji wa elimu ya juu, Serikali inatambua umuhimu wa elimu ya juu kama nyenzo muhimu ya maendeleo katika nchi yetu. Katika Mwaka wa Fedha, 2020/2021 Serikali imefadhlili mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa watumishi 909 katika Taasisi za Elimu ya Juu. Aidha, Vyuo Vikuu vimetekeleza miradi 404 ya utafiti, vimechapisha jumla ya machapisho 620 katika nyanja mbalimbali na vimeendelea kudahili wanafunzi pamoja na kutoa ushauri kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi na uendelezaji wa elimu ya ufunzi, Serikali imeendelea na uanzishwaji wa vituo vya umahiri katika nyanja ya teknolojia ya habari na mawasiliano, usafiri wa anga, nishati jadidifu na mazao ya ngozi. Imeandaa mitaala mipya 54 inayohusu mafunzo kwa vitendo, imetoa mafunzo ya muda mfupi ya fani mbalimbali kwa washiriki 10,499 katika Vyuo vya Maendeleo vya wananchi 54.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa elimu wa kukuza ujuzi na stadi za kazi, Serikali imetoa mafunzo kwa watumishi 1,177 ili kuimarisha utendaji wao. Imeendelea na ujenzi wa Vyuo vya VETA katika wilaya 29, imewezesha uanzishwaji wa programu 80 za mafunzo zinazoendana na vipaumbele vya mkakati wa Kitaifa wa kuendeleza ujuzi ambapo vijana 29,047 wamenufaika na programu hizo. Pia imewezesha mafunzo kwa vitendo kwa wahandisi wahitimu 500 katika miradi mikubwa ya ujenzi wa Kitaifa, ikiwemo ujenzi wa reli ya kisasa, bwawa la kufua umeme la Mwalimu Nyerere na Daraja la juu la Kijazi. Aidha, mradi huu umewezesha ukarabati wa maktaba za mikoa 7 na ujenzi wa shule maalum ya viziwi ya Lukuledi, Masasi.

Mheshimiwa Spika, Uimarishaji na uendelezaji wa sayansi, teknolojia na ubunifu. Katika kuratibu na kuendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu, Serikali inawaendeleza

wabunifu 130 waliopatikana katika mashindano ya Kitaifa ya sayansi, teknolojia na ubunifu ya Mwaka 2019 na Mwaka 2020. Na imetambua na kuhakiki teknolojia mpya 79 na hivyo, kufanya teknolojia zilizozalishwa na kutambuliwa nchini kufikia 310 hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, shughuli zilizofanywa na Taasisi, Mamlaka na Wakala zilizochini ya elimu. Wizara imeendelea na kuratibu majukumu ya Taasisi, Mamlaka na Wakala zilizochini yake, kazi zilizofanyika kwa kila Taasisi zimebainishwa kuanzia ukurasa wa 23 hadi ukurasa wa 68 wa kitabu cha hotuba. Kutokana na muda nitaeleza tu baadhi ya shughuli.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo kimetoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi 60 shahada za awali 50 na umahiri 10 ambapo asilimia ya wanufalika ni wanafunzi wa kike. Chuo kinaendelea na mradi wa ujenzi wa kituo cha wanafunzi na kimekarabati hosteli za wanafunzi, kumbi za mihadhara, nyumba za wahadhiri na miundo mbinu ya maji safi na maji taka.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, chuo kimeanza kutoa mafunzo katika kampasi mpya ya Mizengo Pinda, Katavi katika fani za kilimo, utalii, mifugo na misitu ambapo wanafunzi 105 wamedahiliwa. Chuo kimeendelea kutoa elimu na ushauri kwa washiriki 1,280 kupitia vituo atamizi vyta mafunzo, mashamba darasa na semina na kinaendelea na ujenzi wa jengo la maabara mtambuka lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 3,200 kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, chuo kinaendelea na ujenzi wa kituo cha umahiri cha magonjwa ya moyo na mishipa katika kampasi ya Mloganzila ambapo ujenzi umefikia asilimia 75.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Ardhi, Chuo Kikuu cha Ardhi kimepata mradi wenye thamani ya Euro 300,000 ambayo ni sawa na shilingi za Kitanzania 837,450,000 wa kujenga uwezo katika elimu, utafiti, ubunifu na huduma kwa

jamii katika miji inayokuwa haraka. Pia Chuo kimekamilisha ujenzi wa jengo la ardhi, *Wing B* lenye ofisi 42, vyumba nya madarasa na vyumba nya mikutano.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Mzumbe, chuo kimekamilisha ujenzi wa hosteli zenyne uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,024 katika kampasi kuu Morogoro. Vilevile, kimekamilisha ujenzi wa jengo jipya la madarasa na kumbi za mihadhara zenyne uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu Dodoma, Chuo Kikuu cha Dodoma kimeboresha miundo mbinu ikiwa ni pamoja na kufunga viti vipyta 600 katika ukumbi wa Chimwaga na kukarabati mabweni 20 katika Ndaki ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı Stadi. Mamlaka imedahili wanafunzi 357,850 wakiwemo wanafunzi 807 wenye ulemavu. Pia imetoa mafunzo kwa wajasiriamali 282 katika sekta isiyo rasmi.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, taasisi imeendelea kuimarisha upatikanaji wa elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 imesajili wanafunzi 9,939 wa mpango wa elimu changamani na imefanya utafiti juu ya hali ya kisomo nchini.

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia, Mbeya, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya kimedahili wanafunzi 140 katika programu za mafunzo ya ualimu wa ufundı katika ngazi ya Stashahada, Shahada na Uzamili na kinaendelea na ubunifu na utafiti katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, taasisi imeanzisha kituo atamizi cha teknolojia kwa ajili ya kuwajengea uwezo wahandisi na wana sayansi katika kuandaa vifaa tiba na imeendelea na kazi za utafiti na ubunifu.

Mheshimiwa Spika, Tathmini ya utoaji wa elimu na mafunzo, Serikali imeendelea kuziwezesha taasisi zenye majukumu ya kutathmini ubora na mafunzo ya utoaji wa elimu nchini kufanya kazi hizo. Shughuli zilizofanyika kwa kila taasisi zimebainishwa kwa kina kuanzia ukurasa wa 50 hadi 56 wa kitabu. Nitaeleza kwa kifupi shughuli chache.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania, Tume ya Vyuo Vikuu imekagua vyuo vikuu 19 kwa lengo la kuhakiki ubora wake na imefanya tathmini na kutoa ithibati ya mitaala 153 iliyowasilishwa na vyuo vikuu nchini. Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu limetoa mafunzo kuhusu mitaala inayozingatia umahiri kwa wakufunzi 806 na imehakiki mitaala 118 ilioandaliwa na vyuo vya ufundu.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Elimu ya Tanzania. Kwa kutambua umuhimu wa kutoa elimu bora kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum, imechapa na kusambaza nakala 2,000 za mwongozo wa utekelezaji wa mtaala wa elimu ya sekondari kwa wanafunzi viziwi na wenye baki ya usikivu. Lakini pia, imechapa na kusambaza nakala 4,100 za vitabu vya kiada vya breli vya sekondari kwa ajili ya wanafunzi wasioona.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Elimu Tanzania, Kupitia Mamlaka Serikali imewezesha ujenzi wa madarasa 180, nyumba za walimu 100 na matundu ya vyoo 360. Pia, imeboresha miundo mbini ya kufundishia na kujifunzia katika Chuo cha Karume cha Sayansi na Teknolojia kilichoko Zanzibar kwa gharama ya shilingi milioni 300.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu, Wakala umetoa mafunzo ya udhibiti ubora wa shule wa ndani kwa wakuu wa shule za msingi 8,800, maafisa elimu taaluma msingi pamoja na wadhibiti ubora wa shule wa wilaya.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu imetoa mikopo kwa wanafunzi 149,398. Aidha, hadi kufikia

mwezi Machi, 2021 Bodi ilikuwa imekusanya marejesho ya Shilingi bilioni 139.2 kati ya bilioni 194.1 zilizokuwa zimepangwa.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Huduma za Maktaba, Bodi imewezesha upatikanaji wa jumla ya vitabu 432,499, magazeti 3,246 na majorida 13. Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia. Tume inaendelea na ufadhili na usimamizi wa miradi 173 ya utafiti na ubunifu inayotekelawa kupitia taasisi mbalimbali za utafiti na maendeleo na taasisi za elimu ya juu.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Nguvu za Atomiki. Tume inaendelea na upimaji wa viwango vya mionzi na ukaguzi wa vituo ambavyo vinamiliki na kutumia vyanzo vya mionzi. Aidha, imeendelea na ujenzi wa maabara changamano awamu ya pili inayogharamu kiasi cha shilingi bilioni 10.4 ambapo ujenzi umefikia asilimia 73.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuelekeza utekelezaji wa shughuli zilizopita, sasa naomba nieleze mpango wa bajeti Fungu 46 kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Maandalizi ya Mpango wa Bajeti yamezingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Ilani ya Chama cha Mapinduzi na hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan aliyotoa tarehe 22 Aprili, 2021 mbele ya Bunge lako Tukufu.

Aidha, michango ya Waheshimiwa Wabunge katika hotuba ya Waziri Mkuu na hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI pia imezingitiwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara itatoa kipaumbele katika kuimarisha elimu kwa kuzingatia maoni na ushauri wa wadau wa elimu. Vilevile, Wizara itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi kama yalivyoainishwa katika Haki Idhini ya mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya kipaumbele. Vipaumbele vya Wizara ya Elimu vitakuwa kama ifuatavyo:-

(i) Mapitio ya Sera na Sheria ya Elimu. Serikali itafanya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 kwa lengo la kuhakikisha kuwa inakidhi mahitaji ya sasa. Aidha, Serikali itafanya mapitio ya Sheria ya Elimu ya mwaka 1978 ili kuhakikisha inaendana na mazingira ya sasa.

(ii) Uimarishaji wa mafunzo yanayojenga ujuzi. Serikali itaweka msisitizo zaidi katika ufundishaji wa masomo ya ufundi kwa kuimarisha mafunzo kwa vitendo katika shule za sekondari za ufundi zilizopo ambazo ni lyunga, Ifunda, Tanga, Bwiru Wavulana, Musoma, Chato, Mwadui, Moshi na Mtwara. Vilevile, Serikali itaimarisha ufundishaji wa masomo yanayowajengea wanafunzi ujuzi katika shule za msingi na shule za sekondari. Masomo hayo ni pamoja na kilimo, ufundi, stadi za kazi, michezo na biashara.

(iii) Tathmini na mapitio ya elimu. Serikali itafanya ufuatiliaji wa kina wa mitaala inayotumika kwa sasa ili kuhakikisha kuwa viwango na vigezo vilivyowekwa vinazingatiwa kikamilifu katika ufundishwaji na ufundishaji. Vigezo hivyo ni pamoja na uwepo wa walimu kulingana na idadi ya wanafunzi, vitabu na mazingira fanisi ya kujifunzia. Pia Serikali itaanza kufanya mapitio ya mitaala katika ngazi zote za elimu ili kuhakikisha kuwa elimu na mafunzo yanayotolewa katika nchi yetu yanajikita katika kujenga ujuzi na kuzingatia mahitaji ya soko la ajira.

(iv) Tozo za mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Katika kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoyatoka katika Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani tarehe 1 Mei, 2021 Mkoani Mwanza, Serikali itaondoa tozo ya asilimia sita ya kulinda thamani ya fedha katika urejeshaji wa mikopo kuanzia tarehe 1 Julai, 2021.

Vilevile Serikali inaiagiza Bodi ya Wakurugenzi wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kuondoa pia tozo ya adhabu ya asilimia 10 ya mikopo ambayo inatozwa kwa wanufaika wanaochelewa kulipa mikopo hiyo kuanzia tarehe 1 Julai, 2021. (*Makof*)

(v) Bodi ya Kitaalam ya Walimu. Serikali itafanya kazi maoni na ushauri wa wadau wa elimu kuhusu utekelezaji wa Sheria ya mwaka 2018 iliyounda Bodi ya Kitaalam ya Walimu. Aidha, Serikali itazingatia pia maoni na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo waliiyoyatoa katika majadiliano na Wizara yaliyofanyika tarehe 28 Aprili, 2021 kuhusu Kanuni za Bodi ya Kitaalam ya Walimu. Vilevile maelekezo ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Bodi ya Kitaalam ya Walimu aliyyoyatoa katika maadhimisho ya siku ya Wafanyakazi Duniani yatazingatiwa kikamilifu. Kwa hiyo, niwatoe hofu walimu wenzangu kwamba Serikali ipo makini, Serikali hii ni Sikivu, tutakaa kwenye meza ya majadiliano na tutafikia muafaka hakuna jambo litakaloharibika.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya msingi ya Wizara. Wizara Itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi kuititia idara, vitengo na taasisi kama ilivyofafanuliwa kuanzia Uk. 72 – 115.

Mheshimiwa Spika, elimu ya juu. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Idara na Taasisi za Elimu ya Juu zitaendelea na majukumu yake ya kudahili, kufundisha, kutoa huduma kwa jamii na kufanya tafiti. Aidha, ili kutoa fursa zaidi za kujinga na elimu ya juu kwa wanafunzi amba wanatoka katika familia zenye kipato kidogo, Serikali imeongeza bajeti ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kutoka shilingi bilioni 464 mwaka 2020/2021 hadi shilingi bilioni 500 katika mwaka wa fedha 2021/2022. Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Serikali pia itaanza kutekeleza mradi wa kuendeleza elimu ya juu kwa maendeleo ya uchumi. Kiasi cha shilingi bilioni 40.6 zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha ukarabati wa miundombinu katika taasisi 23 na kuwajengea uwezo wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*). Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali itaendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu na itendelea kuibua, kutambua na kuendeleza ubunifu, ugunduzi na teknolojia zilizoibuliwa nchini na itaendelea

kutumia matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia katika sekta mbalimbali za kijamii na kiuchumi. Majukumu mengine ya taasisi yatakayotekelezwa ni kama yalivyoainishwa katika kitabu cha bajeti. Pia, Wizara itaendelea kusimamia miradi ambayo imemeanishwa katika Ukurasa wa 115 – 124 ya kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya *UNESCO*. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Tume ya Taifa ya *UNESCO* itasimamia utekelezaji wa program na miradi iliyopitishwa katika mpango wa kimataifa *UNESCO* na itashiriki kwa niaba ya Serikali katika kupanga, kutekeleza na kutathmini shughuli za *UNESCO*.

Mheshimiwa Spika, shukrani. Napenda kutambua mchango mkubwa wa viongozi wenzangu katika kutekeleza na kufanikisha majukumu ya Wizara. Kipekee kabisa namshukuru Mheshimiwa Omari Juma Kipanga, Mbunge wa Mafia, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ushirikiano mkubwa anaonipa katika kusimamia Wizara hii. Hakika nimepata Naibu Waziri Jembe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aidha, namshukuru Katibu Mkuu, Dkt. Leonard Akwilapo, Naibu Makatibu Wakuu Profesa James Mdoe na Profesa Carolyne Nombo, Wakurugenzi, Wakuu wa Idara na Vitengo na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ushirikiano wao katika kusimamia na kwa kutekeleza kwa weledi majukumu ya Wizara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi, watumishi wa Wizara na taasisi zake, walimu, wakufunzi wahadhiri, wanafunzi na wadau wote elimu kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa. Aidha, napenda kutoa shukrani za dhati kwa wamiliki wa shule, vyuo na taasisi binafsi kwa mchango mkubwa sana wanaotoa katika sekta ya elimu hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru washirika wa maendeleo na wadau wa elimu waliochangia utekelezaji wa mipango ya elimu, naomba kuwatambua baadhi yao

kama ifuatavyo: Serikali ya Canada, China, Finland, Hungary, India, Italia, Korea ya Kusini, Marekani, Misri, Netherland, Norway, Sweden, Ufaransa, Uswisi, Uingereza, Ujeruman na Uhlanzi pamoja na washirika wote kama ilivyoainishwa kwenye kitabu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuyashukuru mashirika ya kimataifa na ya kitaifa yaliyochangia kufanikisha programu na Miradi ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo ni pamoja na Benki ya Dunia, Ofisi ya Uingereza na Jumuiya ya Madola ya Maendeleo, Shirika la Kimataifa la Ushirikiano katika Elimu, GPE, mfuko wa kuendeleza ubunifu, Umoja wa Nchi za Ulaya, Benki ya Maendeleo ya Afrika, British Council, Jumuiya ya Madola, *SIDA, UNICEF UNDP, KOICA, USAID, JAICA* na *UNESCO*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha. Ili kuwezesha Wizara kutekeleza wa malengo kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh.1,384,414,801,000.00 kwa mchanganuo ufuatao: Sh.480,474,878,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya kawaida ya Wizara ambapo shilingi 447,214,694,000.00 ni kwa ajili ya Mishahara na shilingi 33,260,184,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo; na shilingi 903,939,923,000.00 zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo shilingi 706,639,923,000.00 ni fedha za ndani na shilingi 197,300,000,000.00 fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Tume ya Taifa ya *UNESCO* Fungu Na. 18, Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 2,679,073,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 1,146,780,000 ni za Mishahra na Matumizi shilingi 1,532,293,000.00 ni za Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kuitisha Makadirio ya Bajeti ya Mafungu yote mawili Fungu Na.46 na Fungu Na.18 yenye jumla ya shilingi 1,387,093,774,000.00.

Mheshimiwa Spika, napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe kwa kusimamia mjadala huu na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
MHESHIMIWA PROF. JOYCE LAZARO NDALICHAKO (MB)
AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA
MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2021/22 - KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

A. UTANGULIZI

- 1. Mheshimiwa Spika**, kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii iliyochambua makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu, likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2020/21. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/22.
- 2. Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema, kuniwezesha kuendelea kutimiza majukumu yangu na kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2021/22.

- 3. Mheshimiwa Spika**, mwaka wa fedha 2020/21 umekuwa ni mwaka wenye majonzi makubwa katika nchi yetu. Tumeondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyefariki tarehe 17 Machi, 2021; Pia tumeondokewa na Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyefariki tarehe 24 Julai, 2020; Mheshimiwa Maalim

Seif Sharif Hamad aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar aliyefariki tarehe 17 Februari, 2021; na Balozi John William Herbert Kijazi aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi aliyefariki tarehe 17 Februari, 2021.

4. Mheshimiwa Spika, Vile vile Bunge lako Tukufu limewapoteza Waheshimiwa Wabunge wawili: Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum CCM – Mkoa wa Manyara aliyefariki tarehe 21 Januari, 2021; na Mheshimiwa Atashasta Justus Nditiye Mbunge wa Jimbo la Muhamwe aliyefariki tarehe 12 Februari, 2021. Nitumie fursa hii kutoa pole kwa ndugu, jamaa na Watanzania wote kwa kuondokewa na Viongozi wetu; tunaomba Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

5. Mheshimiwa Spika, nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuapishwa na kuwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akiwa Mwanamke wa Kwanza kuwa Rais wa nchi yetu. Nampongeza pia kwa Hotuba aliyoitoa tarehe 22 Aprili, 2021 katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo imetoa dira na mwelekeo wa Serikali yake. Vilevile, natoa shukrani za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini na kunitfea kuendelea kusimamia Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Naahidi kuwa nitatekeleza majukumu yangu kwa weledi na uadilifu wa hali ya juu. Naomba Mwenyezi Mungu anisaidie niweze kukidhi matarajio ya Mheshimiwa Rais na Watanzania kwa ujumla.

6. Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Phillip Isdor Mpango kwa kuteuliwa na kuthibitishwa na Bunge lako Tukufu kwa kura zote kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nimpongeze Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) kwa uongozi wake makini. Nampongeza pia kwa miongozo anayoitoa na ufuatiliaji anaofanya katika kuhakikisha kuwa malengo ya Serikali yanatekelezwa kwa ufanisi mkubwa.

7. Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Nampongeza kwa kazi nzuri anayoendelea kuifanya. Vile vile nampongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mheshimiwa Hemedy Suleiman Abdullah kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

8. Mheshimiwa Spika, naomba nikupongeze kwa dhati wewe mwenyewe Mheshimiwa Job Yustino Ndugai na Naibu Spika Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa awamu nyingine. Kuchaguliwa kwenu ni matokeo ya umahiri mliouonesha katika kutekeleza majukumu yenu katika Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

9. Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo (Mb), Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Aloyce John Kamamba (Mb), na Wajumbe wote wa Kamati kwa kuchambua na kuishauri Wizara kuhusu Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa mwaka 2021/22. Kamati hii ni makini sana na imekuwa ikitoa maoni na ushauri wenye lengo la kuhakikisha tunaendelea kuboresha elimu ili kutoa wahitimu wenye ujuzi unaokidhi mahiataji ya sasa.

10. Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza Mawaziri na Manaibu Mawaziri wote walioteuliwa kuongoza Wizara mbalimbali. Nawaahidi kutoa ushirikiano wa hali ya juu katika kuhakikisha tunatoa huduma na kuleta maendeleo kwa taifa letu hasa katika Sekta ya Elimu hapa nchini.

11. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hii ni Hotuba yangu ya kwanza kwenye Bunge hili la 12 napenda pia kuwapongeza waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa na kuteuliwa kwao kuwa Wabunge wa Bunge la 12 la Jamhuri ya

Muongano wa Tanzania. Hongereni sana na naomba ushirikiano wenu katika kuiendeleza Sekta hii muhimu ya Elimu.

12. Mheshimiwa Spika, naishukuru kwa dhati familia yangu kwa kuendelea kunipa ushirikiano na kuniwezesha kutekeleza majukumu ya ujenzi wa Taifa kupitia Sekta ya Elimu.

13. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba nitoe taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2020/21 na Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/22.

B. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2020/21

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI

14. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21 Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha **Shilingi 1,348,563,375,000.00** kwa ajili ya Fungu 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambapo **Shilingi 491,049,151,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 857,514,224,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO - Fungu 18 Bunge liliidhinisha kiasi cha **Shilingi 2,239,181,000.00** ambapo **Shilingi 1,532,293,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 706,888,000.00** kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Tume.

Ukusanyaji wa Maduhuli

15. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21, Wizara kupitia Fungu 46 ilitarajia kukusanya maduhuli yenye thamani ya **Shilingi 555,651,650,346.52** ambapo kiasi cha **Shilingi 15,459,750,000.00** kilipangwa kukusanya na Idara na Vitengo na **Shilingi 540,191,900,346.52** kilipangwa kukusanya na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Vyanzo vya maduhuli haya ni kutokana na ada, ushauri elekezi, ukaguzi wa shule na utoaji wa huduma mbalimbali.

16. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili 2021, Wizara ilikuwa imekusanya **Shilingi 339,128,992,104.16** sawa na asilimia **61** ya makadirio ambapo **Shilingi 6,050,266,699.80** zimekusanya na Idara na Vitengo na **Shilingi 333,078,725,404.36** zimekusanya na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

Matumizi ya Kawaida

17. Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili 2021, Wizara ilikuwa imepokea Jumla ya **Shilingi 434,737,497,950.09** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kupitia Fungu 46, ambazo ni sawa na asilimia **88.5** ya fedha za Matumizi ya Kawaida zilizoidhinishwa. Aidha, kupitia Tume ya UNESCO – Fungu 18 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 1,515,856,166.60** sawa na asilimia **68** ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Miradi ya Maendeleo

18. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya maendeleo hadi kufikia Aprili 2021, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 634,622,139,494.67** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambazo ni sawa na asilimia **74** ya bajeti iliyotengwa. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 397,496,012,792.52** ni fedha za ndani na **Shilingi 237,126,126,702.15** ni fedha za nje.

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA

19. Mheshimiwa Spika, sasa naomba nitoe taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Fungu 46 na Fungu 18 katika mwaka wa fedha 2020/21.

Uendelezaji wa Elimumsingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu

20. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha Elimu ya Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu ambapo katika mwaka wa fedha 2020/21 imetekeliza yafuatayo:

(i) imewezesha mafunzo kwa walimu 174 wa shule za sekondari yaliyohusu utoaji wa ushauri na unasihi kwa wanafunzi kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kuimarisha stadi za utoaji wa huduma za malezi na unasihi shulen;

(ii) imekamilisha Mwongozo wa Malezi, Unasihi na Ulinzi wa Mtoto kwa Shule na Vyuo vya Ualimu. Mwongozo huo utawasaidia walimu wanaishi kuwa na fasili sahihi ya huduma katika Shule na Vyuo na kukuza stadi za kutoa huduma, kuzipima na kuzitathmini. Mwongozo huo unapatikana katika tovuti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; na

(iii) imeandaa Mwongozo wa Utoaji wa Huduma ya Chakula na Lishe Shuleni. Mwongozo huo utawezesha utolewaji wa huduma ya chakula shuleni katika viwango stahiki na hatimaye kuboresha mahudhurio ya wanafunzi.

21. Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia **Mradi wa Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni** (School Water, Sanitation and Hygiene – SWASH), katika mwaka wa fedha 2020/21 imetekeleza yafuatayo:

(i) imeendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa matundu ya vyoo, miundombinu ya maji na vifaa vya kunawia mikono katika Shule za Msingi 602 ambapo shule 380 zimekamilisha ujenzi na shule 222 zipo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji wa miundombinu hiyo; na

(ii) imewezesha ununuzi wa gari moja kwa ajili ya kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mradi.

22. Mheshimiwa Spika, Serikali kuitia **Mradi wa Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Sekondari – SEQUIP** katika mwaka wa fedha 2020/21, imetekeleza yafuatayo:

(i) imeandaa Nyaraka ya uendeshaji wa mradi (Programme Operation Manual) na Andiko la Tathmini ya Mradi (Project Appraisal Document) pamoja na andiko la Makubaliano ya Kifedha (Financial Agreement) ambapo nyaraka hizo zitatoa mwongozo wa utekelezaji wa mradi; na

(ii) imedurusu mihtasari na moduli za Elimu Nje ya Mfumo Rasmi kwa hatua ya kwanza kwa Kidato cha I na II na hatua ya pili kwa Kidato cha III na IV kwa masomo saba (7) ya English, Kiswahili, Geography, History, Civics, Biology na Mathematics.

Mihtasari hiyo itawezesha utoaji Elimu kwa Njia Mbadala (Alternative Education Pathway - AEP) na kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu.

23. Mheshimiwa Spika, Serikali **kupitia Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) - Kuimarisha Ufundishaji na Ujifunzaji kwa Elimu ya Awali na Msingi (GPE - LANES II)**, katika mwaka wa fedha 2020/21 imetekeleza yafuatayo:

- (i) imekamilisha uchapaji wa vitabu 46,830 vya uchambuzi wa matokeo ya upimaji wa darasa la pili 2019 (PIRA -STNA). Aidha, inaendelea na uchapaji wa vitabu 304,897 vya uchambuzi wa matokeo ya upimaji wa darasa la nne, 2020 (PIRA - SFNA) na vitabu 249,020 vya uchambuzi wa matokeo ya mtihani wa kumaliza Elimu ya Msingi 2020 (PIRA - PSLE);
- (ii) imechapa na kusambaza vitabu vya kiada 4,905,586, Kiongozi cha Mwalimu 268,000 na mihtasari 365,368 kwa masomo yote ya Darasa la VI na VII. Aidha, inaendelea na uchapaji wa vitabu vya kiada 14,650,531;
- (iii) imeandaa moduli 10 za mafunzo endelevu kazini kwa walimu wa Shule za Msingi (Darasa V - VII), wawezeshaji wa MEMKWA, na walimu wa Elimu Maalum ikijumuisha moduli tatu (3) kwa kila kundi ambazo ni: Moduli ya Ufundishaji na Ujifunzaji; Upimaji na Tathmini; na Stadi za Maisha pamoja na moduli moja (1) ya mbinu za mawasiliano kwa Lugha ya Kiingereza;
- (iv) imewezesha ukamilishaji wa vitini vya Miongozo ya Mafunzo ya Uthibiti Ubora wa Shule wa Ndani na kutoa mafunzo kwa wawezeshaji (TOT) 445 ikijumuisha Maafisa Taaluma wa Wilaya 184, Viongozi 20 kutoka Makao Makuu ya WyEST na OR - TAMISEMI, Maafisa 70 kutoka ADEM na Wathibiti Ubora wa Shule 183. Wawezeshaji hawa walitoa mafunzo kwa Walimu Wakuu 8,091 sawa na asilimia 99.74 ya Walimu Wakuu 8,112 waliokuwa kwenye mpango wa mafunzo awamu ya kwanza;

(v) imewezesha Wathibiti Ubora wa Shule kufanya Tathmini ya Jumla kwa Shule za Awali na Msingi 2,755 ambazo ni sawa na asilimia 101 ya Shule 2,726 zilizolengwa kufanyiwa tathmini ya ubora wa elimu nchini katika mwaka wa fedha 2020/21;

(vi) imefanya ufuutiliaji na tathmini katika Vituo vya Walimu (TRCs) 269 sawa na asilimia 87 ya vituo 308 vilivyokuwa katika mpango. Ufuutiliaji ulibaini kuwa asilimia 54 ya vituo vilikuwa vinafanya kazi ya kuendesha mafunzo kwa walimu katika kipindi cha miaka mitatu ya nyuma. Aidha, vituo hivyo vilionekana kuwa na mahitaji makubwa ya miundombinu pamoja na vitendea kazi ikiwemo mifumo ya TEHAMA ili kusaidia vituo hivyo kuwa sehemu sahihi kwa walimu kuijendeleza kitaaluma na kitaalam; na

(vii) imeandaa rasimu ya Mwongozo wa Uendeshaji wa Vituo vya Wallimu (Teachers Resources Centers – TRCs) kwa ajili ya Waratibu wa Vituo ili kuendana na Mpango wa Kitaifa wa Mafunzo Endelevu kazini.

24. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kuitia **Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Sekta ya Elimu - EP4R**) imeendelea kuboresha miundombinu ya shule, Ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule na Vyuo vya Ualimu kama ifuatavyo:

(i) imejenga Ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule 55 kwa lengo la kusogeza huduma kwa wateja na kuimarisha mazingira ya utendaji kazi ambapo ujenzi upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji;

(ii) imewezesha ujenzi wa hosteli, bwalo la chakula na mifumo ya maji katika Chuo Kikuu cha Mzumbe kwa lengo la kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji;

(iii) inaendelea na ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Mfano Dodoma ambapo ujenzi huo unatarajia kukamilika mwezi Februari, 2022. Kukamilika kwa ujenzi wa shule hiyo kutawezesha ufundishaji na ujifunzaji fanisi kutokana na

kuwepo kwa mahitaji muhimu na hivyo kuhamasisha shule nyingine na jamii kujifunza umuhimu wa utoshelevu wa mahitaji katika kujifunza;

(iv) imewezesha ujenzi wa shule mpya 19 (Msingi 11 na Sekondari 8) kwa awamu ya kwanza na shule 25 (Msingi 9 na Sekondari 16) kwa awamu ya pili kwa lengo la kuongeza fursa za upatikanaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari na kupunguza msongamo wa wanafunzi unaotokana na utekelezaji wa Sera ya Elimu Bila Malipo;

(v) imewezesha ujenzi wa vyumba vya madarasa 3,283, matundu ya vyoo 5,383, mabweni 112, nyumba za watumishi 32 (2 in 1), mabwalo sita (6), majengo ya utawala matano (5) na maabara 12 katika shule 1,714 (Msingi 998 na Sekondari 716) zilizopo katika Halmashauri 184 kwa lengo la kuimarishe mazingira ya ufundishajli na ujifunzaji; na

(vi) imekarabati Vyuo vya Ualimu tisa (9) vya Monduli, Mamire, Singachini, Bustani, Bunda, Mtwara (U), Mtwara (K), Katoke na Vikindu ambapo ukarabati upo katika hatua mbalimbali. Aidha, imewezesha ujenzi wa Vyuo vya Ualimu vitatu (3) vya Dakawa, Mhonda na Sumbawanga pamoja na ukarabati wa nyumba za wakufunzi katika Vyuo vya Ualimu 18. Kukamilika kwa ujenzi na ukarabati kutaimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

Ithibati na Usajili wa Shule na Vyuo vya Ualimu

25. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu la upatikanaji wa fursa ya Elimu na Mafunzo, Serikali imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imefuatilia na kutathmini shule 213 zilizosajiliwa kwa masharti na kubaini kuwa shule hizo zimefuata sheria, kanuni na taratibu za usajili wa shule ikiwa ni pamoja na kuongeza miundombinu ya vyumba vya madarasa, ofisi na matundu ya vyoo vya watumishi na wanafunzi;

- (ii) imesajili shule 433 zilizoomba na kukidhi vigezo vya usajili kwa lengo la kuongeza idadi ya wanafunzi wanaosajiliwa katika Shule za msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu;
- (iii) imechapa na kutoa jumla ya vyeti vya usajili wa shule 86 kwa lengo la kuwezesha shule kutambulika rasmi na kuendeshwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu;
- (iv) imekamilisha uandaaji wa mfumo wa kieletroniki wa Usajili wa Shule za Awali na Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu ambao utawezesha usajili kufanyika kwa ufanisi zaidi; na
- (v) imehuisha Mwongozo wa Uanzishaji na Usajili wa Shule za Awali, Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu ili kukidhi mahitaji ya sasa ya jamii.

Usimamizi na Uendelezaji wa Elimu Maalum

26. Mheshimiwa Spika, pamoja na kuendelea kuimarisha utekelezaji wa afua zenye kuhakikisha elimu yetu inakuwa jumuishi, Serikali imeendelea kutoa mafunzo yanayolenga kuboresha utoaji wa Elimu Maalum na Jumuishi kama ifuatavyo:

- (i) imetoa mafunzo kazini kwa walimu 1,076 wa shule za msingi na sekondari wanaofundisha wanafunzi viziwi, wasioona, wenyе ulemavu wa akili na wenyе usonji kuhusu matumizi ya Lugha ya Alama ya Tanzania, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, huduma ya utengamao na matumizi ya vifaa vya kuchapia maandishi ya Nukta Nundu (Braille) kwa wanafunzi wasioona;
- (ii) imehamasisha jamii kuhusu utambuzi wa mapema, uandikishaji na utoaji wa huduma za kielimu kwa wanafunzi wenyе mahitaji maalum katika ngazi zote za elimu. Lengo ni kuongeza ushiriki wa wazazi, walezi, jamii na wadau wa elimu katika kutoa elimu kwa usawa kwa watoto wenyе mahitaji maalum nchini; na

(iii) imehamasisha Walimu, Maafisa Elimu Maalum, Maafisa Afya na Ustawi 314 kuhusu namna bora ya kuwabaini watoto wenyewe mahitaji maalum wenyewe umri wa kuandikishwa shule.

27. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalum, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imenunua vishikwambi 402 kwa lengo la kuimarishe ujifunzaji wa Lugha ya Alama ya Tanzania katika Shule 38 (Msingi 15 na Sekondari 23). Vilevile, imenunua vitimwendoo 536 kwa ajili ya wanafunzi wenyewe ulemavu wa viungo waliopo shule ya msingi na sekondari ili kurahisisha ujifunzaji wa wanafunzi hao; na

(ii) imesambaza jumla ya vifaa vya kielimu na saidizi 33,458 kwa ajili ya Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalum katika shule 1,305 (msingi 1,260 na sekondari 45) kwa lengo la kuimarishe ufundishaji na ujifunzaji.

Kuimarishe Mafunzo ya Elimu ya Ualimu

28. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa walimu bora wanaandaliwa na wanakidhi mahitaji nchini Serikali imeendelea kuimarishe Elimu ya Ualimu na kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu nchini ambapo katika mwaka wa fedha 2020/21 imetekeleza yafuatayo:

(i) imedahili jumla ya wanachuo 7,046 (Wanawake: 3,529 Wanaume: 3,517) wa mwaka wa kwanza katika mafunzo ya Ualimu. Udhili wa wanachuo hao utaongeza idadi ya walimu tarajali kwa lengo la kukidhi mahitaji ya walimu nchini;

(ii) imeandaa miongozo ya Umahiri wa Walimu na Wakufunzi, Mafunzo ya Ualimu kwa Vitendo na Mwongozo wa Elimu ya Kujitegemea katika Vyuo vya Ualimu kwa lengo la kuboresha uendeshaji wa Mafunzo ya Ualimu nchini; na

(iii) imegharamia Mafunzo ya Ualimu kwa Vitendo (BTP) kwa wanachuo 15,576 wa Astashahada na Stashahada ili

kuwawezesha kufanya mazoezi ya kufundisha na hivyo kuimarisha ubora wa walimu.

29. Mheshimiwa Spika, Serikali kuititia **Mradi wa Kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu (Teacher Education Support Program – TESP)** imetekeleza yafuatayo:

- (i) imewezesha ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali 35 kwa uwiano wa Shilingi 25,000 kwa mwanachuo kwa lengo la kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji;
- (ii) inatekeleza Mkakati wa Usawa wa Kijinsia wa Elimu ya Ualimu ili kuimarisha usimamizi wa masuala ya jinsia katika ufundishaji na ujifunzaji katika Vyuo vya Ualimu;
- (iii) imewezesha mafunzo ya Lugha ya Alama kwa walimu wa sekondari 269 kutoka shule 24 zinazopokea wanafunzi viziwi kwa lengo la kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule za sekondari na Vyuo vya Ualimu; na
- (iv) imewezesha mafunzo ya TEHAMA awamu ya pili kwa wakufunzi 366 katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali 35 ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji.

30. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kuititia **Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu (Upgrading Teachers' Colleges - UTC)** imetekeleza kazi zifuatazo:

- (i) inaendelea kukamilisha ujenzi na ukarabati wa miundombini katika Chuo cha Ualimu Shinyanga (Lot 1) unaohusisha: Ujenzi wa Bweni la ghorofa moja (1); Jengo la ghorofa moja (1) kwa ajili ya nyumba za wafanyakazi na ukuta kuzunguka eneo la Chuo. Aidha, imekarabati nyumba mbili (2) za wafanyakazi na nyumba ya Mkuu wa Chuo;
- (ii) imekamilisha ujenzi wa Bwalo katika Chuo cha Ualimu Mpuguso (Lot 2). Aidha, inaendelea na ukamilishaji wa ujenzi

wa miundombinu mingine ikiwemo jengo la ghorofa lenye madarasa 16, maktaba, jengo la mihadhara na jengo la mikutano;

(iii) imekamilisha ukarabati wa mabweni, vyoo vya wanachuo na nyumba za watumishi katika Chuo cha Ualimu Ndala (Lot 2). Aidha, inaendelea na ujenzi (Lot 1) wa Mabweni mawili (2) ya ghorofa yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 304, ghorofa lenye vyumba 16 vya madarasa, jengo la mihadhara, jengo la maktaba na jengo la maabara; na

(iv) inaendelea kukamilisha ujenzi wa miundombinu katika Chuo cha Ualimu Kitangali (Lot 2) ambapo ujenzi huo unahusisha jengo la ghorofa lenye madarasa 16, maktaba, jengo la mihadhara na majengo mawili (2) ya ghorofa kwa ajili ya mabweni yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 304.

Kusimamia Ubora wa Elimu katika Shule na Vyuo vya Ualimu

31. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa taasisi zilizopata Ithibati na Usajili zinatoa elimu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu. Kutokana na azma hiyo, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imefanya tathmini ya jumla katika asasi 5,057 kati ya 6,020 (sawa na asilimia 84) zikiwemo shule za Awali na Msingi 4,286 kati ya lengo la 4,700, Sekondari 718 kati ya 1200 na Vyuo vya Ualimu 53 kati ya 120 ambapo shule zilizobainika kuwa na mapungufu zilipewa ushauri wa kitaalam na kitaaluma kwa ajili ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji;

(ii) imefanya ufuutiliaji wa ushauri uliotolewa katika asasi 569 zikiwemo: Shule za Awali na Msingi 490, Sekondari 74 na Vyuo vya Ualimu vitano (5) kati ya 870 zilizobainika kuwa na kiwango dhaifu na kisichoridhisha kutokana na matokeo ya tathmini ya jumla ya mwaka 2018/19 na 2019/20 kwa lengo la kutathmini hali ya utekelezaji wa ushauri na mapendekezo yaliyotolewa;

(iii) imesimamia ujenzi wa ofisi mpya 55 na ukarabati wa ofisi 31 za Uthibiti Ubora wa Shule zilizojengwa na kukarabatiwa kuititia Mradi EP4R; na

(iv) imefanya mafunzo ya usimamizi na uwajibikaji kwa Wathibiti Wakuu Ubora wa Shule 368 wakiwemo Wathibiti Wakuu Ubora wa Shule Kanda 11, Wathibiti Wakuu Ubora wa Shule Wilaya 173, Naibu Wathibiti Wakuu Kanda 11 na Naibu Wathibiti Wakuu Wilaya 173 kwa ajili ya kuimarisha utendaji kazi.

Usimamizi na Uendelezaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi

32. Mheshimiwa Spika, katika kusimamia na kuendeleza Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Serikali kuititia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21 imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imewezesha upatikanaji wa hati miliki katika Vyuo nane (8) vya Maendeleo ya Wananchi. Aidha, taratibu za upimaji na upatikanaji wa hati miliki unaendelea kwa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 46; na

(ii) inaendelea na uanzishwaji wa vituo vinne (4) vya umahiri katika nyanja za TEHAMA, mazao ya Ngozi, usafiri wa ang ana nishati jadidifu katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam katika Kampasi Kuu ya Dar es Salaam na Kampasi ya Mwanza, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji na Chuo cha Ufundi Arusha mtawalia kuititia Mradi wa Kujenga Ujuzi Afrika Mashariki (EASTRIP) kwa lengo la kuviongezea vyuo hivyo uwezo wa kutoa mafunzo kwa vitendo yanayoendana na mpango wa nchi na soko la ajira.

33. Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha uwezo wa kutoa mafunzo kwa vitendo katika taasisi nchini, Serikali kuititia **Mradi wa Kujenga Ujuzi Afrika Mashariki - East Africa for Transformation and Regional Integration Project (EASTRIP)** katika mwaka wa fedha 2020/21, imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imeandaa mitaala mipyä 54 inayohusu mafunzo kwa vitendo kwa lengo la kukidhi mahitaji ya soko la ajira na tayari imeanza kutumika katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam Kampasi Kuu ya Dar es Salaam na Kampasi ya Mwanza, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji na Chuo cha Ufundı Arusha; na

(ii) imenunua magari nane (8) na mabasi mawili (2) katika taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam Kampasi ya Dar es Salaam na Mwanza, Chuo cha Usafirishaji na Chuo cha Ufundı Arusha kwa lengo la kuwezesha utendaji kazi.

34. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ujuzi wa Elimu ya Ufundı na Mafunzo ya Ufundı Stadi nchini, Serikali kuititia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21 immeendelea kutoa mafunzo kwa makundi mbalimbali kama ifuatavyo:

(i) imewezesha mafunzo ya muda mrefu ya Ufundı Stadi kwa wanachuo 9,565 katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54 ili kuwapa ujuzi unaohitajika katika soko la ajira;

(ii) imetoa mafunzo ya muda mfupi ya fani mbalimbali kwa Washiriki 10,449 (Wanawake: 6,224 Wanaume: 4,225) katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54 ili kuwaongezea uwezo wa kutekeleza miradi ya maendeleo na shughuli katika maeneo wanayoishi; na

(iii) imewezesha mafunzo kwa wakufunzi 412 wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54 ili kuboresha ufundishaji kwa masafa na kwa kutumia mitaala inayoendana na soko la ajira.

35. Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha utoaji wa huduma za Elimu ya Ufundı na Mafunzo ya Ufundı Stadi nchini, Serikali kuititia **Mradi wa Elimu na Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi (Education and Skills for Productive Jobs – ESPJ)** katika mwaka wa fedha 2020/21 imetekeliza kazi zifuatazo:

- (i) imetoa mafunzo kwa watumishi 1,177 (Wanawake: 591, Wanaume: 586) kulingana na maeneo ya ubobezi na aina ya kazi wanazosimamia ili kuimarisha utendaji;
- (ii) imeendelea na ujenzi wa Vyuo vya VETA vya Wilaya 29 ambavyo ni; Kongwa, Kasulu, Ruangwa, Nyasa, Igunga, Bahi, Lushoto, Masasi, Iringa, Mbarali, Uvinza, Buhigwe, Kishapu, Longido, Mafia, Butiama, Ulanga, Korogwe, Mkinga, Chemba, Kilindi, Kwimba, Ukerewe, Ikungi, Monduli, Chunya, Uyui, Pangani na Rufiji ambapo ujenzi upo katika hatua mbalimbali;
- (iii) imewezesha uanzishwaji wa programu za mafunzo 80 ambazo zinaendana na vipaumbele vya Mkakati wa Kitaifa wa Kuendeleza Ujuzi ambavyo ni Kilimo-Biashara, Utalii na Ukarimu, Ujenzi, Uchukuzi, Nishati na TEHAMA. Aldha, viljana 29,047 wamenufaika na programu hizo kupitia Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF);
- (iv) imewezesha mafunzo kwa vitendo (uanagenzi) kwa wahandisi wahitimu 500 (Wanawake: 130, Wanaume: 370) katika miradi mikubwa ya ujenzi ya kitaifa ikiwemo Standard Gauge Railway (SGR) na Mwalimu Julius Nyerere Hydropower Project (MJNHP) na Ubungo Interchange Bridge kwa usimamizi wa Bodi ya Usajili wa Wahandisi nchini. Mafunzo hayo yanalenga kuwajengea uwezo wahitimu kuajiriwa na kujiajiri na hivyo kufikia lengo la Serikali la kukuza uchumi nchini;
- (v) imeendelea na ukarabati wa maktaba za Mikoa saba (7) ambazo ni; Tabora, Morogoro, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Rukwa na Iringa. Ukarabati huo umekamilika katika Mikoa ya Kagera, Iringa na Rukwa na Mikoa mingine ipo katika hatua za mwisho za ukamilishaji;
- (vi) imewezesha ujenzi wa Shule Maalumu ya Viziwi ya Lukuledi Masasi ili kuongeza fursa ya upatikanaji wa Elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum nchini ambapo ujenzi upo katika hatua ya ukamilishaji; na

(vii) imeendelea na ujenzi wa ofisi za NACTE katika Kanda tano (5) za Kaskazini, Ziwa, Nyanda za Juu Kusini, Kusini na Magharibi ili kusogezza huduma karibu na wananchi ambapo ujenzi umefikia asilimia 55.

36. Mheshimiwa Spika, Serikali inaandaa miongozo mbalimbali itakayotumika katika taasisi zinazotoa elimu ya ufundi ukiwemo Mwongozo wa ulinganifu wa Kitaaluma wa Kitaifa (National Qualification Framework); "TVET Curricula Development Manual"; "CBET Training Manual on CBET Curricula Development/Review, Delivery and Assessment"; na "Occupational Standards for EASTRIP TVET Priority Sectors (Energy, Leather Processing, Transport and ICT)". Miongozo hiyo ipo katika hatua mbalimbali za kupata maoni kutoka kwa wadau kwa lengo la kuboresha maudhui yatakayokidhi mahitaji ya soko la ajira.

Usimamizi na Uendelezaji wa Elimu ya Juu

37. Mheshimiwa Spika, katika usimamizi na uendelezaji wa Elimu ya Juu nchini kwa mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kuititia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imeratibu ufadhilli wa masomo kwa wanafunzi 134 kutoka nchi mbalimbali ikiwemo Morocco wanafunzi 26 (Wanawake 6), Hangaria 27 (Wanawake 6), Jumuiya ya Madola wanafunzi watano (5) (Shahada ya Umahiri watatu (3) na Uzamivu wawili (2) na China 76 (Wanawake 23) kuanzia ngazi ya Shahada ya Kwanza hadi Shahada ya Uzamivu;

(ii) imeratibu vikao vinne (4) vya Uongozi na Usimamizi (National Steering Committee) wa Vituo vya Umahiri vya Africa (African Centre of Excellence ACE II) katika Taasisi za Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela kwa lengo la kujadili utendaji wa pamoja na kuweka mikakati itakayowezesha vituo hivyo kuwa endelevu;

(iii) imeendelea kuratibu ufadhilli wa masomo kwa wanataluma 68 katika ngazi ya Shahada ya Umahiri wanne

4 (wanaume) na Shahada ya Uzamivu 64 (Wanawake 17) kutoka katika Vyuo Vikuu vya Umma katika fani za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi, Usanifu majengo, Hisabati na ICT; na

(iv) imefanya ufuatiliaji wa mahitaji ya Wanafunzi wenyewe Mahitaji Maalumu katika Vyuo Vikuu vya Umma na uchambuzi wa maombi unaendelea ili kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ununuvi wa vifaa saidizi kwa wanafunzi hao.

Usimamizi na Uendelezaji wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu

38. Mheshimiwa Spika, katika kuratibu na kusimamia uendelezaji wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu nchini, Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/21 kuitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imeendelea na kazi ya kuwaendeleza wabunifu 130 waliopatikana katika Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) ya mwaka 2019 na 2020 kwa kuboresha ubunifu wao ili ufikie hatua ya ubiasharishaji na kuwa fursa ya kiuchumi kwa wabunifu wenyewe na jamii kwa ujumla. Aidha, bunifu 26 kati ya 130 zinazoendeleza na Serikali zipo katika hatua ya kubiasharishwa na hivyo kutumika kutatua changamoto mbalimbali katika sekta za kilimo, maji, nishati, madini, afya na elimu;

(ii) imeratibu maandalizi ya Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2021 kwa lengo la kuibua, kutambua na kuendeleza wabunifu na wavumbuzi wachanga nchini. Jumla ya wabunifu 714 wamejitokeza kushiriki mashindano ya mwaka 2020/21 ambapo wabunifu mahiri takribani 70 wamepatikana na watashiriki kilele cha mashindano kitakachofanyika tarehe 6 – 11 Mei, 2021 katika Uwanja wa Jamhuri Jijini Dodoma. Wabunifu watatu kwa kila kundi watapewa tuzo mbalimbali;

(iii) imetambua na kuhakiki teknolojia mpya 79 na kufanya jumla ya teknolojia zilizozalishwa nchini na kutambuliwa hadi sasa kufikia 310. Lengo la utambuzi huo ni kuwa na kanzidata

ya kitaifa itakayorahisisha upatikanaji wa taarifa muhimu kuhusu teknolojia na bunifu nchini;

(iv) imefanya mafunzo kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii katika ngazi ya Mkoa kwa Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara kwa lengo la kuwajengea uwezo wa namna ya kuibua, kutambua na kuendeleza wabunifu na wavumbuzi wachanga nchini;

(v) imetambua matokeo ya tafiti na vifaa ya kufanyia utafiti katika Taasisi 154 za Utafiti na Maendeleo na Elimu ya Juu za umma kwa lengo la kuanisha matokeo ya utafiti hususan yale yenye manufaa ya moja kwa moja kwa jamii, pamoja na kubaini uwezo wa vifaa na wataalam katika Taasisi hizo;

(vi) imefanya ufuutilaji na tathmini ya miradi (10) ya utafiti inayofadhiliwa na Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani (IAEA) na kuratibiwa na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania katika Sekta za Maji, Afya, Kilimo na Mifugo na kubaini kuwa utekelezaji wa miradi hiyo unafanyika kulingana na makubaliano; na

(vii) imeshiriki Mkutano Mkuu wa 64 wa Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (IAEA) uliofanyika Vienna, Austria mwezi Septemba, 2020 ambapo ushiriki huo uliwezesha miradi mitatu ya utafiti katika sekta za afya, kilimo (food irradiator) na elimu (research reactor) kupata ufadhilli.

Usimamizi na Uendelezaji wa Rasilimali za Wizara

39. Mheshimiwa Spika, katika kusimamia na kuendeleza Rasilimaliwateru kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetekeliza kazi zifuatazo:

(i) imeandaa Muundo na Mgawanyo wa Majukumu ya Bodi ya Kitaalam ya Walimu pamoja na Miundo na Mgawanyo wa Majukumu ya Vyuo Vikuu na kuwasilisha Ofisi ya Rais Utumishi (OR – UTUMISHI);

- (ii) imekamilisha Muundo wa Uthibiti Ubora wa Shule ili kurahisisha usimamizi na uendelezaji wa watumishi kwa lengo la kuongeza ufanisi na uwajibikaji;
- (iii) imeandaa, kuchambua na kutoa vibali vyta ajira za kigeni kwa waombaji 184 waliokidhi vigezo katika maombi 185 yaliyowasilishwa kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma; na
- (iv) imefanya ukaguzi wa Ufanisi (Performamce Audit) katika Taasisi 13 zilizo chini ya Wizara kwa lengo la kubainisha hali halisi ya utendaji na utekelezaji wa kazi mbalimbali za taasisi ikilinganishwa na Sheria ya uanzishwaji wa Taasisi husika.

SHUGHULI ZILIZOFANYWA NA TAASISI, MAMLAKA NA WAKALA ZILIZO CHINI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21

40. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kuratibu majukumu ya Taasisi, Mamlaka na Wakala zilizo chini yake ili kuhakikisha nchi inazalisha rasilimaliwatu yenye weledi kwa kuzingatia mahitaji ya Mipango ya ndani ya nchi, Soko la Kitifa, Kikanda na Kimataifa. Kazi zilizofanyika kwa kila taasisi ni kama ifuatavyo:

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM)

41. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam imetekeliza kazi zifuatazo:

- (i) imedahili jumla ya wanafunzi 42,745 (Wanawake 19,633 Wanaume 23,112);
- (ii) imetoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi 60 (Shahada za Awali 50 na Umahiri 10) ambapo asilimia 50 ya wanufaika ni wanafunzi wa kike. Kati ya wanufaika hao asilimia 90 ni wanafunzi wanaosoma masomo ya sayansi;
- (iii) imefadhili wanafunzi watatu (3) wa shahada ya umahiri katika lugha ya kiswahili kutoka nchi za; Ghana, Rwanda na Uganda;

(iv) imefadhili wanataaluma 38 (Shahada za Uzamivu 21 na Shahada za Umahiri 17) kwa lengo la kuongeza idadi ya wahadhiri wenye sifa stahiki;

(v) imeongeza miradi mipyä ya utafiti 66 na hivyo kuwezesha chuo kuwa na jumla ya miradi 239 kutoka 173 ya awali. Miradi hiyo inahusisha: Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, TEHAMA na Maendeleo ya Viwanda; Elimu, Kilimo, Usalama wa Chakula na Afya; Utawala Bora, Sera za Viwanda na Uzalishaji na Matumizi Endelevu; Jinsia, Ukuzaji wa Utaalamu, Uandaaji na Utekelezaji wa Sera; Historia, Utamaduni, lugha, Uriithi na Utalii Endelevu; na Maliasili, Mazingira na Teknolojia; na Sheria na Maendeleo Jumuishi ya Taifa; na

(vi) imeongeza idadi ya machapisho ya chuo katika majarida ya kitaifa na kimataifa kutoka machapisho 1,048 hadi kufikia 1,172.

42. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21 Serikali imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imekamilisha usanifu na inaendelea na hatua za manunuzi ya kumpata mkandarasi atakayefanya upanuzi wa bweni la Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa ghorofa mbili zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,280 na hivyo kufanya bweni kuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 5,120;

(ii) imekamilisha utiaji saini mkataba na kukabidhi eneo la ujenzi kwa mkandarasi ili kuanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa Jengo la Shule Kuu ya Uchumi katika kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere. Jengo litakuwa na ukubwa wa ghorofa sita (6) zenye ofisi 50 za wafanyakazi, ofisi za kukaa wanafunzi 60 wa masomo ya uzamili, kumbi za mihadhara sita (6) zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 800, ukumbi wa mikutano wenye uwezo wa kuchukua watu 80; na sehemu ya huduma ya chakula yenye uwezo wa kuchukua watu 120;

(iii) inaendelea na mradi wa kituo cha wanafunzi ambacho tayari ujenzi wa ghorofa saba (7) umekamilika na kazi

zilizobaki ni ujenzi wa paa, nguzo za mapambo (decorative columns) na kuanza awamu ya umaliziaji na kufunga samani. Jengo hili litakapokamilika litatoa huduma za sehemu za kujisomea, huduma za kibenki, maduka, saluni za kike na kiume, sehemu za vinywaji, ukumbi wa burudani na wa kutumbuiza na ofisi ya Mlezi wa Wanafunzi; na

(iv) imekarabati hosteli za wanafunzi, kumbi za mihadhara, kituo cha polisi, nyumba za wahadhiri, miundombinu ya maji safi na majitaka, umeme, barabara na kuta za kuzuia udongo.

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA)

43. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imedahili jumla ya wanafunzi wapya 5,499 kati ya hao Astashahada wanafunzi 38 (Wanawake: 12, Wanaume: 26), Stashahada wanafunzi 249 (Wanawake: 106, Wanaume: 143) na Shahada za Awali 4,964 (Wanawake: 1,864 Wanaume: 3,100) na Shahada za Uzamili (Umahiri na Uzamivu) wanafunzi 248 (Wanawake: 97 Wanaume: 151);

(ii) imeanza kutoa mafunzo katika Kampasi mpya ya Mizengo Pinda - Katavi kwa ngazi ya Astashahada, Stashahada na Shahada katika nyanja za Kilimo, Utalii, Mifugo na Misitu ambapo wanafunzi 105 (Wanawake: 32, Wanaume: 73) wamesajiliwa;

(iii) imeendelea kuviongezea uwezo vitengo vya uzalishaji ikiwa ni pamoja na: Kitengo cha kuzalisha mikate; Kitengo cha daharia kilichopo katika Taasisi ya Elimu ya Kujiendeleza (Institute of Continuing Education - ICE); Kitengo cha Msitu wa Mafunzo Olmotonyi; na Kitengo cha Ng'ombe wa Maziwa na shamba la Katani lilitopo katika shamba la chuo na Maabara ya Udongo; na

(iv) imepima jumla ya sampuli 2,500 za udongo kutoka kwa wakulima kupitia Maabara ya Udongo kwa lengo la kuleta

tija katika kuzalisha mazao ya kilimo na kuweza kupunguza umaskini. Sampuli hizo ni kama ifuatavyo: udongo (1,678); maji (252); mbolea za viwandani (151); samadi (6); na mimea (413).

44. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo iliandaa na kushiriki katika Maonesho ya Nanenane Kanda ya Mashariki yaliyofanyika katika viwanja vya Mwalimu Nyerere Morogoro na maonesho ya kilimo ya kitaifa yaliyofanyika katika viwanja vya Nyakabindi, Bariadi - Mkoani Simiyu. Maonesho hayo yalilenga kutoa elimu kuhusu kilimo na ufugaji na yaliwafikia zaidi ya wadau 10,000. Katika maonesho ya kilimo ya kitaifa Simiyu, SUA ilishinda kombe na cheti cha mshindi wa kwanza katika kundi la Vyuo Vikuu na katika maonesho ya ukanda wa mashariki Morogoro, SUA ilipata cheti cha mshindi wa tatu katika kitengo cha mashirika ya umma.

45. Mheshimiwa Spika, katika kutoa elimu na kuendeleza Sekta ya Kilimo nchini, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imeendelea kutoa elimu na ushauri kwa washiriki 1,280 kupitia Vituo Atamizi vya Mafunzo ya Kilimo-Biashara, mashamba darasa na semina katika maeneo ya Manispaa ya Morogoro, Bahi, Kongwa, Mlali na Simiyu. Utoaji wa elimu na ushauri ulilenga kuongeza tija katika uzalishaji na hatimaye kupunguza umaskini mionganoni mwa washiriki; na

(ii) imeendesha semina kupitia washirika wa maendeleo kwa lengo la kuwashirikisha wadau wa ndani na nje ya chuo kutoa maoni kuhusu uundaji wa sera itakayotumika kuinua kilimo na mifugo nchini.

46. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kujenga na kukarabati miundombinu kama ifuatavyo:

(i) imejenga jengo la Maabara Mtambuka ambalo lina maabara nane (8) na madarasa nane (8) na lina uwezo wa kuchukua wanafunzi 3,200 kwa wakati mmoja. Jengo hilo

litajumuisha ofisi saba (7) zitakazo tumika na wafanyakazi 38, vyumba nya maandalizi 11 na stoo saba (7) za kuhifadhi kemikali;

(ii) imekarabati miundombinu mbalimbali ikiwemo madarasa, karakana, maabara, majengo ya Ndaki ya Tiba ya Wanyama ikiwemo Hospitali ya Taifa ya Rufaa ya Wanyama, Maktaba ya Taifa ya Kilimo ya Sokoine, mabweni ya wanafunzi na nyumba za wafanyakazi kwa lengo la kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia;

(iii) imekarabati majengo katika kampasi mpya ya Mizengo Pinda - Katavi ambapo ukarabati huo uliwezesha udahili wa wanafunzi kwa mwaka wa masomo 2020/21; na

(iv) imeboresha sehemu ya Makumbusho ya Mazao (Crop Museum) kwa kudumisha mazao yaliyopo na kupanda mazao mapya.

47. Mheshimiwa Spika, ili kuendana na mahitaji ya soko la ajira, Serikali imeongeza programu mpya za masomo 20 katika ngazi tofauti kama ifuatavyo: Shahada za Uzamili (12); Shahada za Awali (6); Stashahada (1); na Astashahada (1) ambapo baadhi ya programu hizo zimeanza kutolewa kwa wanafunzi kwa mwaka wa masomo 2020/21.

Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS)

48. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imeongeza udahili wa wanafunzi kutoka 4,051 kwa mwaka wa masomo 2019/20 hadi kufikia 4,200 kwa mwaka 2020/21 (Stashahada 373, Shahada ya kwanza 2,695 na Shahada ya Uzamili 1,132); na

(ii) imesajili jumla ya kozi 172 katika mfumo wa TEHAMA na kati ya kozi hizo kozi 81 zimetumika katika mwaka wa masomo wa 2020/21.

49. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha elimu inayotolewa inakuwa na ubora unaokidhi viwango na mahitaji ya soko la ajira Kitaifa, Kikanda na Kimataifa, Serikali kupitia MUHAS imetekeleza yafuatayo:

- (i) imeandaa jumla ya maandiko dhana ya tafiti 21 na kuwasilisha katika taasisi mbalimbali zinazoweza kufadhili tafiti hizo ambapo maandiko 16 katika hayo yalipata ufadhili kwa ajili ya kutekeleza tafiti husika; na
- (ii) imepata Mshauri Elekezi (Consultant) kwa ajili ya kutengeneza Andiko la Mpango wa Biashara la Kuanzisha Kliniki ya Uporoto (Uporoto Polyclinic) na yupo katika hatua za uandishi wa andiko hilo kwa kushirikiana na wataalamu wa MUHAS.

50. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kujenga na kukarabati miundombinu kama ifuatavyo:

- (i) inaendelea na ujenzi wa kituo cha umahiri wa magonjwa ya moyo na mishipa ya damu (Center of Excellence in Cardiovascular Sciences) katika kampasi ya Mloganzila ambapo ujenzi umekamilika kwa asilimia 75;
- (ii) imekarabati chumba cha kutolea huduma binafsi katika shule ya meno na taratibu za ununuzi wa vifaa vyta meno zinaendelea; na
- (iii) imekarabati hosteli za wanafunzi zilizopo barabara ya Chole - Dar es Salaam zenyewe uwezo wa kuchukua wanafunzi 550.

Chuo Kikuu Ardhi (ARU)

51. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu Ardhi imetekeleza kazi zifuatazo:

- (i) imedahili jumla ya wanafunzi 4,920 wakiwemo wa ngazi ya Shahada ya Kwanza 4,619 (Wanawake: 1,965 Wanaume:

2,654), Shahada ya Umahiri 226 (Wanawake: 68 Wanaume: 158) na Shahada ya Uzamivu 75 (Wanawake: 10 Wanaume: 65);

(ii) imechapisha jumla ya machapisho 59 katika majarida mbalimbali (peer reviewed journals) kwa lengo la kuongeza maarifa kwa jamii kuhusu usimamizi wa ardhi na mazingira, uboreshaji wa mazingira na usanifu majengo;

(iii) imetoa mafunzo kwa wakazi wa kata ya Goba, Wilaya ya Kinondoni Mkoa wa Dar es Salaam kuhusu ujenzi bora wa makazi ili kujikinga na athari zitokanazo na mabadiliko ya tabia nchi ambapo wananchi walielimishwa kuhusu viwango na kanuni za mipango miji na matumizi bora ya ardhi;

(iv) imepata mradi wa kujenga uwezo katika elimu, utafiti, ubunifu na huduma kwa jamii kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Hasselt cha Ubeligiji. Mradi unalenga kukuza mazingira jengwa (Built Environment) jumuishi na endelevu katika miji inayokua haraka (SDG 11 in Dar es Salaam) na utatekelezwa katika mkoa wa Dar es Salaam. Mradi huu unafadhiliwa na Shirika la VLIR - OUS la Ubeligiji kwa kiasi cha fedha Euro 300,000 kwa mwaka kwa kipindi cha miaka 10;

(v) imeendelea kufanya utafiti wa kubuni modeli ya urasimishaji makazi holela katika miji inayoibukia katika wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya ambapo takribani viwanja 70,000 vitapimwa. Mradi unalenga kutatua changamoto ya makazi holela na utapima kila kipande cha ardhi ya jumla (general land). Aidha, utekelezaji wa mradi huo utawezesha Serikali kupata mapato kutokana na ada za umilikishaji ardhi, tozo ya thamani ya ardhi wakati wa umilikishaji na kodi ya pango la ardhi; na

(vi) imeendelea kusimamia miradi ya tafiti 53 zinazolenga kutatua changamoto za kijamii hususan katika maeneo ya matumizi bora ya ardhi, utunzaji wa mazingira, kujikinga na maafa, usimamizi bora wa ardhi, makazi na ujenzi.

52. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Chuo Kikuu Ardhi imetoa ushauri wa kitaalamu kwa jamii kwenye miradi ya: Ujenzi wa kituo cha mabasi cha Kimataifa cha Magufuli Dar es Salaam; Shule ya mfano ya sekondari ya Dodoma (Dodoma Model Secondary School); na Ukabarati wa vyuo vya ualimu nchini (Kleruu, Mpwapwa, Kitangali, Mpuguso, Shinyanga na Ndala). Vilevile, imetoa ushauri wa kusanifu michoro ya jengo la maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) linalotarajiwa kujengwa jijini Dodoma; kusanifu michoro na kusimamia ujenzi wa majengo ya Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu Julius K. Nyerere cha Butiama, majengo ya hospitali za rufaa za Mwalimu Nyerere - Mara, Simiyu, Mtwara na Njombe; pamoja na majengo ya maabara za Tume ya Taifa ya Nguvu za Atomiki (TAEC) zinazotarijiwa kujengwa Dodoma, Mwanza na Dar es Salaam.

53. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, Serikali imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imekamilisha ujenzi wa Jengo la Ardhi (Land Building) 'wing B' lenye ofisi 42 zenyе uwezo wa kuchukua wafanyakazi 84 na vyumba vinne (4) vya madarasa vyenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 32 wa Shahada ya Uzamivu pamoja na vyumba vitatu (3) vya mikutano vyenye uwezo wa kuchukua watu 36 kwa kila chumba. Pia, inaendelea na ujenzi wa bweni la wanafunzi lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 592 ambapo hadi sasa sehemu ya jengo hilo lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 352 imekamilika pamoja na uwekaji wa samani. Vilevile, imefanya ukarabati wa mabweni ya wanafunzi, maabara, madarasa, ofisi za wafanyakazi, miundombinu ya TEHAMA, maji safi na majitaka pamoja na kuweka taa za barabarani.

54. Mheshimiwa Spika, ili kujenga uwezo wa chuo katika kutoa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa huduma kwa jamii, Serikali imeendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi wapatao 35; wakiwemo wa ngazi ya shahada ya Uzamivu 17 (Wanawake: 2 Wanaume: 15), ngazi ya Umahiri 15 (Wanawake: 6 Wanaume: 9) ngazi ya Shahada ya Awali

mmoja (mwanaume) na wa ngazi ya Stashahada wawili (mwanamke na mwanaume).

Chuo Kikuu Mzumbe

55. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Mzumbe imetekeleza kazi zifuatazo:

- (i) imedahili wanafunzi wapya 4,754 (Astashahada 455, Stashahada 379, Shahada ya Awali 3,304, Shahada ya Umahiri 603 na Shahada ya Uzamivu 13);
- (ii) imefadhlili masomo kwa watumishi 69 kwa ngazi ya Uzamili (Shahada ya Uzamivu 59 na Shahada ya Umahiri 10);
- (iii) imechapisha jumla ya machapisho 51 ya kitaaluma kwa lengo la kuwezesha jamii kupata maarifa;
- (iv) imeendelea kutekeleza miradi ya utafiti 29 katika maeneo ya utawala, uongozi na ujasiriamali; na
- (v) imekamilisha ujenzi wa majengo mapya manne (4) ya hosteli zenyе uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,024 katika Kampasi Kuu na taratibu za ununuzi wa samani unaendelea. Vilevile, imekamilisha ujenzi wa jengo jipya la madarasa na kumbi za mihadhara lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000.

Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM)

56. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Dodoma imetekeleza kazi zifuatazo:

- (i) imedahili jumla ya wanafunzi 9,713 ambapo Shahada ya Awali 9,033 na Shahada za Uzamili 680 (Uzamivu 114, Umahiri 545 na Stashahada ya Uzamili 21);

- (ii) imeanzisha progamu mpya tano (5) ambapo Shahada ya Awali moja (1), Shahada za Umahiri mbili (2) na katika Shahada ya Uzamivu mbili (2) ili kuwezesha chuo kuzalisha wahitimu wanaoendana na soko la ajira;
- (iii) imechapisha jumla ya machapisho 282 ambayo yalichapishwa katika majarida mbalimbali. Aidha, imeanzisha majarida manne (4) ya ndani kwa ajili ya tafiti;
- (iv) imefadhlili mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 141 na mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 296 kuanzia ngazi ya Astashahada hadi Shahada ya uzamili. Aidha, imewezesha mafunzo ya muda mfupi kwa viongozi 73 wa ngazi mbalimbali za uongozi; na
- (v) imeboresha mfumo wa usajili wa wanafunzi ambapo wanafunzi wote walisajiliwa kwa kutumia mfumo wa kielektroniki (Online Registration). Mfumo huu umepunguza gharama za usajili na kurahisisha zoezi la usajili na kuwawezesha wanafunzi kusajili popote walipo.

57. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kununua vitabu 828, vifaa vya maabara, TEHAMA na kufunga Kamera za Uoni (CCTV Camera) kwa ajili ya maeneo muhimu ya chuo kwa lengo la kuimarisha usalama. Aidha, imefunga viti vipyta 600 katika ukumbi wa Chmwaga na kukarabati mabweni 20 Ndaki ya Elimu.

Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU)

58. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kuititia Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi imetekeleza yafuatayo:

- (i) imedahili wanafunzi wapya 5,025 katika ngazi mbalimbali ambapo Astashahada ni wanafunzi 1,796 (Wanawake: 949 Wanaume: 847), Stashahada 1,070 (Wanawake: 559 Wanaume: 471), Shahada za Awali 2,052 (Wanawake: 948 Wanaume: 1,104) na Shahada za Uzamili 147 (Wanawake: 48 Wanaume: 99);

- (ii) imewezesha watumishi 69 (Wanataaluma 58 na Waendeshaji 11) kuhudhuria mafunzo katika ngazi mbalimbali kama ifuatavyo: Shahada ya Uzamivu (43); Shahada za Umahiri (20); Stashahada za Uzamili (2); Shahada za Awali (3); na Stashahada (1);
- (iii) imeandaa programu tano (5) za mafunzo ili kuongeza wigo wa udahili wa wanafunzi hususan katika fani za ushirika na biashara, huduma za kibenki, usimamizi wa fedha pamoja na ushirika wa mazao na masoko;
- (iv) imechapisha jumla ya machapisho 70 ya kitaaluma kwa lengo la kueneza matokeo ya tafiti kwa jamii; na
- (v) imeandaa mpango kazi wa tafiti tatu (3) za kimkakati kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika nchini kwa lengo la kusaldia jamii kutatua changamoto mbalimbali katika sekta ya ushirika.

59. Mheshimiwa Spika, ili kuwajengea uwezo wahadhiri na wanafunzi katika masuala ya kutatua matatizo ya kijamii kuititia TEHAMA pamoja na kuwawezesha wanafunzi kubaini fursa mbalimbali za ajira, Serikali kuititia Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi imetekeleza yafuatayo:

- (i) imeratibu upatikanaji wa miradi miwili ambayo ni "Sustainable Business and Employability through Active Pedagogy in HEI (SUSIE) Research Project" na "Social Innovations in GEO-ICT Education at Tanzanian HEIs for Improved Employability (GeolCT4e)"; na
- (ii) imeendelea na utekelezaji wa mradi wa kutoa mafunzo ya KilimoBiashara na Ujasiriamali (Skills Development Fund) kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kujajiri vijana 181 wa mwaka wa pili na wa tatu wa Shahada ya Awali ya uchumi wa biashara.

60. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha Elimu ya Ushirika inawafikia wadau mbalimbali nchini, Serikali kuititia Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi imetekeleza yafuatayo:

- (i) imeratibu mafunzo kuhusu elimu ya ushirika kupitia ofisi za Chuo za mikoani ambapo wanachama, viongozi na watendaji wa vyama mbalimbali nya ushirika 7,296 wamepatiwa mafunzo. Mafunzo hayo yatawawezesha washiriki kuongeza ufanisi wa usimamizi wa vyama nya ushirika;
- (ii) imetoea huduma za kijamii na ushauri kwa wanachama 3,130 katika vyama nya ushirika na vikundi mbalimbali nya maendeleo ili kuongeza ufanisi katika usimamizi na uendeshaji wa vyama nya ushirika; na
- (iii) imeandaa na kurusha vipindi nya redio kuhusu masuala ya ushirika ambapo jumla ya vipindi nya redio 36 vimerushwa kupitia TBC – Taifa na vipindi 15 kupitia redio za kijamii.

61. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi imekarabati kumbi nne (4) pamoja na vyumba 10 nya miadhara vyenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,308 kwa wakati mmoja pamoja na maabara ya kompyuta moja na nyumba 10 za makazi. Aidha, inaendelea na ujenzi wa ukumbi mmoja wa miadhara wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 400 kwa wakati mmoja.

Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT)

62. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu Huria cha Tanzania imetekeleza kazi zifuatazo:

- (i) imedahili wanafunzi 12,929 (Astashahada 3,831, Stashahada 2,596, Shahada ya Awali 3,895, Stashahada ya Uzamili 518, Shahada ya Umahiri 1,982, na Shahada ya Uzamivu 107);
- (ii) imeandaa kongamano lililowezesha uandaaji wa maandiko yatakayochapishwa katika toleo maalum la Jarida la Huria. Kongamano hilo lilifanyika kwa njia ya “Zoom” na lilivutia washiriki 22 kutoka katika taasisi zifuatazo; Saint Mary's

University of Minnesota - USA (4); Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (3); na wafanyakazi na wanafunzi wa shahada za uzamivu kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (15);

(iii) imeandaa Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Wanafunzi wa Shahada za Uzamili "Postgradute Management Information System" (PGMIS) unaopatikana kupitia tovuti ya chuo <https://pgmis.out.ac.tz>. Mfumo huo utawezesha wanafunzi kuwasilisha mapendeleko yao, kupokea maelekezo, ushauri wa wasimamizi na ufuatiliaji; na

(iv) imerekodi mihadhara ya video 204 kwa kozi 61 inayopatikana kwa njia ya mtandao (youtube) kwa jina la "ODL TV".

63. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya kufundishla na kujifunzia kwa kujenga vituo vitano (5) katika mikoa ya Geita, Manyara, Lindi, Simiyu na Kigoma ambapo ujenzi upo katika hatua mbalimbali. Aidha, imekarabati Mfumo wa Umeme katika Kituo cha Mkoa wa Mwanza pamoja na kukarabati vyoo katika Kituo cha Mbeya.

Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE)

64. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam kimetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imedahili wanafunzi 2,104 wa mwaka wa kwanza ambapo Shahada ya Awali ni 2,039 (Wanawake: 1,061 Wanaume: 978) na Shahada za Uzamili ni 65 (Wanawake: 30 na Wanaume: 35);

(ii) imeandaa mitaala miwili (2) ya Stashahada ya Uzamili ya Ushauri na Unasihi na Shahada ya Elimu Jamii katika Lugha ya Kitaalamu kwa lengo la kuongeza idadi ya wataalamu wa kada ya ushauri na unasihi;

(iii) imewezesha mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 36 (Wanataluma 29 na Waendeshaji 7) na mafunzo ya muda

mfupi kwa watumishi 80 kwa lengo la kuleta ufanisi na tija katika utekelezaji wa majukumu yao; na

(iv) imefanya tafiti 21 zikiwemo tafiti mpya 19 kwa lengo la kupata maarifa yatakayosaidia kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili jamii.

65. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, Serikali kupitia Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam imetekeleza Awamu ya Pili ya upanuzi wa jengo la Utawala ambapo nafasi 136 za ofisi zimepatikana. Vilevile, imekarabati vyumba vya madarasa, hosteli za wanafunzi na ofisi na kuweka samani zenyne uwezo wa kuchukua wanafunzi 216 katika hosteli za wanafunzi (NSSF Mtoni Kijichi).

66. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam kinatoa elimu bora na kwa usawa, Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imenunua kompyuta 20 pamoja na vifaa mbalimbali vya kufundishia na kujifunzia vya wanafunzi wenye mahitaji maalum ili kuwezesha utoaji wa elimu jumuishi na kutimiza azma ya Serikali ya kutoa elimu bora kwa wote; na

(ii) imenunua kompyuta 100 kwa ajili ya wanafunzi na watumishi na kuongeza ujazo wa intaneti kutoka Mbps 50 hadi Mbps 60 na hivyo kusaidia kuboresha upatikanaji wa huduma ya intaneti chuoni pamoja na kuwezesha chuo kutumia TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji.

Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE)

67. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa imetekeleza yafuatayo:

(i) imedahili jumla ya wanafunzi 6,399 ambapo kati yao Shahada ya Awali 6,378 na Shahada za Umahiri 21;

- (ii) imeanzisha programu moja (1) isiyo ya kielimu (B.Sc. Chemistry) ikiwa ni asilimia 17 ya lengo la programu sita (6). Aidha, programu tano (5) zipo katika hatua za uidhinishaji;
- (iii) imetoa machapisho 34 katika Nyanja za Insia na Sayansi za Jamii, Elimu na Sayansi;
- (iv) imeratibu semina moja (1) ya kitaaluma na kutekeleza miradi 21 ya utafiti na ushauri ili kuongeza wingi na ubora wa kazi za kitafiti na kiugunduzi;
- (v) imeratibu kongamano moja (1) la Kimataifa la Sayansi na Teknolojia kwa Maendeleo Endelevu. Kongamano hili liliwakusanya watafiti ambao waliwasilisha mada mbalimbali, lengo likiwa ni kutafuta majawabu ya changamoto za jamii na kubadilishana uzoefu na kuongeza wigo wa mashirikiano katika utafiti na maendeleo;
- (vi) iliendesha mafunzo kwa walimu 40 kutoka katika Wilaya za Mpwapwa, Kilosa na Iramba kwa lengo la kuwaongezea uwezo hivyo kuboresha elimu ya awali kwa watoto wa kitanzania; na
- (vii) imewezesha watumishi 88 kupata mafunzo ya muda mrefu katika ngazi za Shahada ya Kwanza na Uzamili ili kuongeza weledi na ufanisi katika utendaji kazi.

68. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, Serikali kuititia Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa imenunua vitabu 449, vifaa vya maabara, kompyuta na vifaa vya TEHAMA. Aidha, imekarabati miundombinu ya Chuo pamoja na kujenga jengo la maabara ya Kemia.

Chuo cha Ufundı Arusha (ATC)

69. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kuititia Chuo cha Ufundı Arusha imetekeliza kazi zifuatazo:

- (i) imedahili jumla ya wanafunzi 2,814 ambapo ngazi ya Stashahada (NTA Level 4) 1,350, Shahada (NTA Level 7) 311 na Mafunzo ya Ufundii Stadi (VET) 1,153;
- (ii) imetoa mafunzo kwa vitendo (industrial practical training) kwa wanafunzi 2,050; na
- (iii) imeanzisha mifumo saba (7) ya ndani ya uthibiti ubora ambayo itawezesha mwanafunzi kufuatilia maendeleo yake na chuo kufuatilia utaratibu unaotumika katika kutoa mafunzo na upimaji.

70. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kufanya utafiti wa matumizi bora ya maji katika kilimo cha mpunga kwa kushirikiana na Japan International Research Centre for Agricultural Sciences (JIRCAS) katika maeneo ya miradi ya Skimu za Mahande (Mto wa Mbu) na Lower Moshi (Kilimanjaro). Utafiti huo utawezesha kufanya kilimo cha mpunga hata katika maeneo yenye mvua chache na uhaba wa maji.

71. Mheshimiwa Spika, ili kutoa ushauri wa kitaalamu katika miradi ya maendeleo, Serikali kuitia Chuo cha Ufundii Arusha imetekeleza yafuatayo:

- (i) imesanifu na kusimamia miradi ya ujenzi katika: Vyuo vya VETA (Kasulu, Ruangwa, Kongwa na Nyasa); Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 31; Vyuo vya Ualimu 16; na Mradi wa stendi kuu ya mabasi ya Kahumo – Wilaya ya Chato - Geita;
- (ii) imepima udongo katika miradi ya: Upanuzi wa maji safi na majitaka katika Jiji la Arusha; Upanuzi wa uwanja wa ndege wa Arusha; Ujenzi wa ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Hai; Upanuzi wa Hospitali ya Wilaya ya Babati na Ujenzi wa Bwawa la Umwagiliaji Kivingo – Lushoto, Tanga;
- (iii) imepima lami katika miradi ya ukarabati wa barabara Bariadi – Slama A, Lamadi – Wigelekelo na Bariadi – Kisera pamoa na upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Arusha; na

(iv) imetekeleza miradi midogo kama vile usanifu na ufungaji wa taa za kuongozea magari barabarani, upimaji wa udongo kwa makampuni ya ujenzi na ujenzi wa nyumba za watu binafsi kwa wananchi wa kawaida katika Mkoa wa Arusha na mikoa ya jirani.

72. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Chuo cha Ufundu Arusha imeendelea kuboresha miundombinu kwa kutekeleza kazi zifuatazo:

(i) imejenga jengo la ghorofa tatu (3) kwa ajili ya madarasa, maabara na ofisi za walimu ambapo kukamilika kwa ujenzi huo kutaongeza udahili na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia;

(ii) imejenga tenki la kuhifadhia maji safi lenye uwezo wa kuhifadhi lita za ujazo 1,125,000 ambalo litapunguza changamoto ya upatikanaji wa maji safi kwa wanafunzi;

(iii) imenunua vifaa vya kufundishia mazoezi kwa vitendo katika idara nane (8) za kitaaluma ili kujenga weledi kwa wanafunzi wa fani za ufundu na uhandisi ambazo zinahitaji zaidi mazoezi kwa vitendo; na

(iv) imefanya usanifu na uandaaji wa michoro na makadirio, upimaji wa udongo (geotechnical investigations) kwa ajili ya ujenzi wa kliniki ya kisasa ya kutolea huduma za afya. Kliniki hiyo itahudumia wanafunzi, wafanyakazi na wananchi wa maeneo ya jirani.

Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere

73. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere imetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) imeongeza udahili wa wanafunzi ambapo hadi mwezi Machi, 2021 jumla ya waliodahiliwa ni 11,790 kati ya lengo la wanafunzi 9,389 kwa mwaka 2020/21. Ongezeko la wanafunzi 2,401 limechangiwa na kuboreshwa kwa mazingira ya

kufundishia na kujifunzia, kufunguliwa kwa Tawi jipya la Pemba na kuanzishwa kwa programu mpya ya shahada ya uzamili katika masomo ya Utawala na Rasilimaliwater;

(ii) imefanya tafiti 17 katika masuala ya Maendeleo ya Uchumi, Jamii, Jinsia, Elimu na Maadili ambazo zimechapishwa katika majarida mbalimbali ya kitaaluma ya ndani na nje ya nchi;

(iii) imegharamia mafunzo ya shahada ya uzamivu kwa watumishi 24 ili kuongeza umahiri wa Wahadhiri Waandamizi;

(iv) imeanza taratibu za ujenzi wa bweni la wanafunzi katika Kampasi ya Karume Zanzibar ambapo Mshauri Elekezi na Mkandarasi wamepatikana kwa ajili ya ujenzi wa mradi;

(v) imehuisha mitaala 29 ya chuo illi iendane na mahitaji ya soko na mingine ipo katika hatua za mapitio kwa ajili ya kupatiwa ithibati; na

(vi) imetoa mafunzo kwa wakutubi watatu (3) kuhusu kuingiza taarifa (vitabu na majarida) katika mfumo wa kielektroniki (KOHA) uliopo maktaba za Kampasi ya Kivukoni, Karume na Pemba.

Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA)

74. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kuititia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imedahili jumla ya wanafunzi 357,850 (Wanawake: 145,251 Wanaume: 212,599) sawa na asilimia 97 ya lengo la mwaka wa masomo 2020/21 la kudahili wanafunzi 370,000 ikiwa ni pamoja na wanafunzi 807 wenye ulemavu na wanafunzi 1,368 kutoka katika mazingira magumu;

(ii) imefanya maandalizi ya kuanzisha Kituo cha Uchapaji katika Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi Chang'ombe - Dar es Salaam;

(iii) imekamilisha andiko la mfumo wa kuwezesha kutoa taarifa za soko la ajira kupitia mtandao; na

(iv) imetekeleza mpango wa kukuza ujuzi viwandani katika viwanda vidogo 26 vya kusindika mbegu za alizeti katika Manispaa ya Singida chini ya uratibu wa Jumuiya ya SIMUSOPA. Mpango huo unatarajiwa kuwanufaisha wananchi 100 wanaojishughulisha na usindikaji wa mbegu za Alizeti katika Manispaa ya Singida.

75. Mheshimiwa Spika, katika kutoa mafunzo kazini na kuwajengea uwezo watumishi pamoja na kukuza ujuzi nchini, Serikali kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis Stadi (VETA), katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21, imetekeleza yafuatayo:

(i) imeweza masomo ya muda mrefu kwa watumishi 51 ili kuongeza ufanisi wa kazi;

(ii) imetoa mafunzo ya Elimu Masafa (ODL) kwa wakufunzi 25 na walimu 60 kutoka vyuo vya Ufundis Stadi na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ikiwa ni majaribio ya awali ya mafunzo ya ualimu kwa njia ya Elimu Masafa;

(iii) imetoa mafunzo kwa wajasiriamali 282 wa Sekta Isiyo Rasmi kupitia programu ya Intergrated Training for Enterpreneurship Promotion (INTEP) kwa lengo la kuboresha uwezo wao wa kuendesha shughuli za uzalishaji na kuboresha hali zao kiuchumi; na

(iv) imeendelea kuelimisha umma kuhusu shughuli za Mamlaka kupitia vyombo mbalimbali vya habari, ikiwemo kipindi cha Ujuzi ni Maisha kinachorushwa na Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) pamoja na makala mbalimbali kupitia redio na mitandao ya kijamii, programu za kuhabarisha jamii, ushiriki katika maonesho na kufanikisha mawasiliano ya kidigitali.

76. Mheshimiwa Spika, ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Vyuo vya Ufundis Stadi, Serikali imeendelea

na ujenzi wa chuo cha Ufundu Stadi na Huduma cha mkoa wa Kagera. Aidha, Serikali imekamilisha ujenzi wa karakana nne (4) katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo:

- (i) karakana ya kisasa ya zana za kilimo (modern agro-mechanics workshop) katika Chuo cha Ufundu Stadi cha Arusha (Oljoro);
- (ii) karakana ya teknolojia ya ubunifu wa mitindo na ushonaji nguo katika Mkoa wa Lindi;
- (iii) karakana ya ufundu wa majokofu na viyoyozi, ufundu bomba, uchomeleaji na vyuma, na uashi katika Chuo cha VETA cha Mkoa wa Lindi; na
- (iv) karakana ya matengenezo ya breki za magari (side slip and brake tester) katika Chuo cha VETA cha Mkoa wa Lindi.

Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)

77. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi ili kuhakikisha kuwa vijana na watu wazima wengi wanapata stadi, ujuzi na maarifa stahiki. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kuititia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima imetekeleza yafuatayo:

- (i) imedahili jumla ya wanafunzi wapya 4,766 (Astashahada 165, Stashahada 4,510 na Shahada 91) kwa mwaka wa masomo 2020/21;
- (ii) imesajili jumla ya wanafunzi 9,939 wa Mpango wa Elimu Changamani kwa Vijana Walio Nje ya Shule yaani Integrated Programme for Out of School Adolescents (IPOSA) kwa ajili ya kuanza mafunzo na wanafunzi 3,440 wamesajiliwa ili kuwawezesha kufanya mitihani ya hatua ya I na II katika vituo vya mradi wa IPOSA;
- (iii) imeandaa Mkakati wa Kitaifa wa Kisomo na Elimu kwa Umma yaani National Adult Literacy and Mass Education

Rolling Strategy (NALMERS) ambao ulizinduliwa Septemba, 2020; na umetafsiriwa kwa Lugha ya Kiswahili; na

(iv) imekusanya takwimu za hali ya kisomo kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara ikiwa ni hatua ya mwanzo ya utafiti wa hali ya kisomo na elimu kwa umma nchini.

78. Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza elimu ya watu wazima nchini, Serikali kupitia Taasisi imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imetoa elimu ya sekondari nje ya mfumo rasmi ambapo jumla ya vijana na watu wazima 13,050 (Wanawake: 7,050 na Wanaume: 6,000) wamepatiwa elimu hiyo;

(ii) imetoa mafunzo ya ualimu na usimamizi wa elimu ya watu wazima kwa vijana na watu wazima 6,607 kupitia utoaji wa programu za elimu masafa mikoani na kuendesha programu 13 katika kampasi za Dar es Salaam, Morogoro na Mwanza;

(iii) imewezesha programu sita (6) za elimu masafa katika vituo mbalimbali ambapo uwezeshaji wa ana kwa ana ulifanyika katika vituo 50 vya utoaji wa elimu kwa njia huria na masafa nchini; na

(iv) imetekeleza programu na miradi mbalimbali ya elimu ya watu wazima, ikiwemo mradi wa kuwawezesha wasichana kwa njia ya elimu, mradi wa sekondari kwa wasichana na Mpango wa Elimu Changamani kwa Vijana Walio Nje ya Shule (IPOSA) kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo.

79. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima imeanza kutumia mitaala mipya kwa mwaka wa masomo 2020/2021 iliyopitisha na kuidhinishwa na NACTE ambapo mitaala hiyo ni: Elimu ya Watu Wazima na Maendeleo ya Jamii (Adult Education and Community Development NTA level 4 - 8); na Elimu ya Watu Wazima na Mafunzo Endelevu (Adult and Continuing Education NTA level 4 - 8). Aidha, maboresho ya mitaala mingine ya Usimamizi wa Elimu Masafa (Management of Distance Education NTA

level 7 - 8 ODL) na Stashahada ya Elimu Masafa (Ordinary Diploma in Distance Education NTA level 4, 5 and 6 ODL) yapo katika hatua ya kuidhinishwa.

80. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi inayotolewa inakidhi vigezo vyta kuwezesha wahitimu kuendana na mahitaji ya soko la ajira, Serikali kupitia Taasisi ya Watu Wazima imetekeleza kazi zifuatazo:

- (i) imefanya ufuatiliaji wa mradi wa utoaji elimu ya sekondari kwa wasichana walio nje ya mfumo rasmi wa elimu yaani Secondary Education for Out of School Adolescent Girls (SEOSAG) unaoendeshwa kwa kushirikiana na shirika la BRAC Maendeleo katika mkoa wa Tanga katika vituo 35 vyta wilaya mbili (Tanga Mjini vituo 23 na Korogwe vituo 12);
- (ii) imetathmini maendeleo ya wanafunzi 98 waliohitimu Mafunzo ya Kuongeza Thamani ya Mazao ya Samaki, na wanaendelea na mafunzo kwa vitendo kupitia Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (Skills Development Fund – SDF) kwa lengo la kubaini manufaa yanayotokana na mradi huo;
- (iii) imehakiki vituo 151 vinavyomilikiwa na TEWW na vituo vipyta 82 vinavyotarajiwa kutekeleza Mradi wa Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP) kwa Njia Mbadala (Alternative Education Pathway - AEP);
- (iv) imefanya tathmini ya utolewaji wa elimu ya sekondari nje ya mfumo rasmi katika mikoa mitano (5) ambayo ni: Dar es Salaam, Pwani, Mbeya, Mwanza na Iringa; na
- (v) imefanya ufuatiliaji wa wanafunzi wanaosoma elimu ya sekondari nje ya mfumo rasmi kwa kuandaa na kusimamia mtihani wa Utimilifi kwa wanafunzi 5,383.

81. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, Serikali kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima imeboresha huduma za maktaba kwa

kuongeza nakala za vitabu 1,140 pamoja na kuboresha mfumo wa utoaji huduma ya maktaba kwa njia ya Kidigitali.

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST)

82. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya imetekeleza kazi zifuatazo:

- (i) imedahili wanafunzi 142 katika programu za masomo ya Ualimu wa Ufundsi (Shahada ya Ualimu wa Ufundsi 134, Stashahada ya Ualimu wa Ufundsi 7 na Stashahada ya Uzamili ya Ualimu wa Ufundsi 1);
- (ii) imesajili wanafunzi 6,817 ambapo ngazi ya Astashahada 87, Stashahada 3,228, Shahada 3,468, Stashahada ya Uzamili 1, Shahada ya Umahiri 26, na wanafunzi 7 katika Shahada za Uzamivu;
- (iii) inaendelea na ubunifu na utafiti wa kutengeneza kitanda cha kuinulia wagonjwa hospitalini;
- (iv) imeshiriki maonesho na mashindano ya MAKISATU ambapo tafiti nne (4) zilifanya vizuri na kuwezesha chuo kupata ufadhili wa **Shilingi 69,000,000** zitakazotumika kuendeleza tafiti hizo;
- (v) imeshirikiana na MATI Uyole, Hanze University of Applied Science (Netherlands) na kufanikiwa kupata mradi wenyewe thamani ya **Euro 398,052.65** unaolenga kufanya tafiti katika Kilimo cha kisasa cha viazi ambacho kitaleta tija katika uzalishaji na kutengeneza ajira; na
- (vi) imekamilisha ujenzi wa maktaba kwa awamu ya kwanza. Aidha, inaendelea na ujenzi wa hosteli yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 ambapo kukamilika kwa hosteli hiyo kutatatua changamoto ya uhaba wa malazi chuoni.

83. Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha ujenzi wa maktaba kwa awamu ya kwanza na kuendelea na awamu

ya pili ya ujenzi ambapo itakapokamilika itakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja. Aidha, inaendelea na ujenzi wa hosteli yenyewe uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 ambapo ujenzi umekamilika kwa asilimia 40. Kukamilika kwa hosteli hiyo kutatatuwa changamoto ya uhaba wa malazi chuoni. Vilevile, imeendelea na ukarabati wa karakana na mabweni katika Kampasi ya chuo Rukwa.

Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT)

84. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam imetekeleza kazi zifuatazo:

- (i) imedahili jumla ya wanafunzi 6,219 wakiwemo Stashahada 3,533 (Wanawake: 1,005 Wanaume: 2,528), Shahada ya Awali 2,622 (Wanawake: 457 Wanaume: 2,165) na Shahada ya Umahiri 64 (Wanawake: 9 Wanaume: 55);
- (ii) imekamilisha utafiti wa mfumo wa kielektroniki wa malipo na usimamizi wa hospitali "Electronic Hospital Management System" na kuusimika katika Hospitali ya Amana; na
- (iii) imepitia mitaala 15 katika ngazi za Stashahada, Shahada ya Awali na Shahada ya Umahiri. Katika fani mbalimbali ambazo ni pamoja na TEHAMA, uhandisi mitambo, uhandisi ujenzi, uhandisi umeme, uhandisi vifaatiba, uhandisi teknolojia ya nishati jadidifu, teknolojia ya sayansi ya usindikaji wa chakula, sayansi na Teknolojia ya maabara.

85. Mheshimiwa Spika katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, Serikali kupitia Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam inaendelea na taratibu za kumpata Mshauri Elekezi kwa ajili ya kusanifu mabweni mawili (2) yenyewe uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 500 na jengo la kituo cha umahiri wa TEHAMA katika kampasi ya Dar es Salaam. Aidha, inaendelea na taratibu za kumpata Mshauri Elekezi kwa ajili ya kusanifu mabweni mawili (2) yenyewe uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 600 na jengo la kituo cha umahiri wa

teknolojia ya utengezaji wa bidhaa za ngozi katika Kampasi ya Mwanza.

86. Mheshimiwa Spika, katika kuendeleza teknolojia na ubunifu nchini, Serikali kuititia Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam imeendelea kukamilisha utafiti wa teknolojia kama ifuatavyo:

- (i) imesanifu modal ya mfumo wa mawasiliano yasiyotumia nyaya katika magari yasiyo na dereva na kwa sasa taasisi ipo katika hatua ya utengenezaji wa "Prototype";
- (ii) imeanza kusanifu modal mbalimbali kwa ajili ya kufanya majaribio ya mifumo itakayosaidia katika uchakataji wa kahawa;
- (iii) imeunda injini ya kutumia mafuta ya petroli na kwa sasa maboresho yanafanyika kwa ajili ya kuongeza mfumo wa kutumia gesi asilia;
- (iv) imeanzisha kituo cha atamizi ya teknolojia ili kuwajenyea uwezo wahandisi na wanasayansi wa kutatua matatizo mbalimbali ya vifaa tiba. Kwa sasa kituo kinahudumia washiriki zaidi ya 300 kutoka ndani na nje ya nchi;
- (v) imefanya utafiti wa utengenezaji wa teknolojia za bei nafuu za kupimia hali ya hewa;
- (vi) imeboresha mfumo wa kusambaza taarifa za hali ya hewa kwa wakulima kwa njia ya ujumbe mfupi wa simu (FARMSMS). Mfumo huu una lengo la kurahisisha upatikanaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na utabiri wa siku 10, utabiri wa msimu na taarifa za hali ya majanga; na
- (vii) imeendelea kutekeleza mradi wa tiba mtando (telemedicine) wenye lengo la kufikisha huduma za afya kwa urahisi kwa wananchi. Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro zimeunganishwa katika mfumo huo.

87. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam kwa kushirikiana na Tume ya Sayansi na Teknolojia imetoa mafunzo ya mfumo wa kuhifadhi, kusambaza, kuchakata na kurahisisha upatikanaji wa taarifa za bioanwai hapa nchini kwa wafanyakazi wa baadhi ya taasisi zinazohusika na masuala ya bioanwai zikiwemo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvu Tanzania (TAFIRI) na Makumbusho ya Taifa. Aidha, imeanza ukusanyaji wa taarifa za awali za bioanwai kwa taasisi za Elimu ya Juu na taasisi za utafiti zinazohusika na maswala ya bioanwai zinaendelea kukusanywa.

Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika ya Nelson Mandela (NM-AIST)

88. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika ya Nelson Mandela imetekeleza yafuatayo:

- (i) imedahili wanafunzi wapya 120 (Uzamili 92, Uzamivu 28) na hivyo kufikisha jumla ya wanafunzi 591 ambapo Umahiri ni 212 (Wanawake: 59 Wanaume: 153) na uzamivu ni 379 (Wanawake 132: Wanaume 247);
- (ii) imezalisha bunifu mbili (2) za Mfumo wa Kurahisisha Uratibu wa Usafiri na Ugunduzi wa Jiko la Gesi Asilia;
- (iii) inaendelea na tafiti 21 ambapo hadi kufikia kipindi cha nusu mwaka kiasi cha **Shilingi 3,280,800,293.11** kilikuwa kimepokelewa kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo ikiwa ni sawa na **126%** ya lengo la **shilingi 3,025,000,000**. Fedha hizo ni kwa ajili ya kulipia ufadhilli wa wanafunzi na gharama za utafiti kwa wanafunzi na wanataluma; na
- (iv) imeongeza wadau wa kimataifa kutoka 36 hadi 38, Afrika Mashariki kutoka 37 hadi 39 na wadau wa ndani wameongezeka kutoka 21 hadi 23.

89. Mheshimiwa Spika, ili kukuza ushirikiano katika ufanyaji wa tafiti zinazolenga kutatua changamoto mbalimbali, Serikali kuititia Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika ya Nelson Mandela imeongeza wadau wa kimataifa kutoka 36 hadi 38, Afrika Mashariki kutoka 37 hadi 39 na wadau wa ndani wameongezeka kutoka 21 hadi 23.

Tathmini ya Utoaji wa Elimu na Mafunzo

90. Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha elimu yetu inaendana na mahitaji ya mipango ya nchi pamoja na soko la ajira la ndani, kikanda na kimataifa, Serikali imeendelea kuziwezesha taasisi zetu zenye majukumu ya kutathmini ubora na utoaji wa elimu kama ifuatavyo:

Baraza la Mitihani la Tanzania - NECTA

91. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kuititia Baraza la Mitihani la Tanzania imetekeleza kazi zifuatazo:

- (i) imeendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) 2020 kwa watahiniwa 1,008,307;
- (ii) imeendesha Upimaji wa Darasa la Nne (SFNA) 2020 kwa watahiniwa 1,704,404;
- (iii) imeendesha Upimaji wa Kidato cha Pili (FTNA) 2020 kwa watahiniwa 601,948;
- (iv) imeendesha Mitihani ya Kidato cha Nne (CSEE) na Maarifa (QT), 2020 kwa watahiniwa 475,981 wa Kidato cha Nne (CSEE) 2020 na watahiniwa 8,056 wa Maarifa (QT) 2020;
- (v) imesajili watahiniwa wa Kidato cha Sita 90,280 wanaotarajiwa kufanya Mitihani kuanzia tarehe 3 hadi 22 Mei, 2021;
- (vi) imesajili watahiniwa 6,742 wa Mitihani ya Ualimu wanaotarajiwa kufanya mitihani kuanzia tarehe 3 hadi 22 Mei, 2021; na

(vii) imeendelea kufanya maandalizi ya zana za upimaji wa Kusoma, Kuandika na kuhesabu – KKK unaotarajiwa kufanyika 2021.

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU)

92. Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa elimu itolewayo inawawezesha wahitimu kukidhi vigezo vya mahitaji ya soko la ajira Kitaifa, Kikanda na Kimataifa, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021, Serikali kuititia Tume ya Vyuo Vikuu imeendelea kutekeleza yafuatayo:

(i) imekagua Vyuo Vikuu 19 kwa lengo la kuhakiki ubora wake ikiwa ni sawa na asilimia 76 ya lengo la kukagua vyuo 25 kwa mwaka; na

(ii) imepokea na kuhakiki maombi manne (4) ya uanzishwaji wa vyuo vikuu vipyta na maombi mengine manne (4) ya utoaji na uhuishaji wa ithibati kwa vyuo vilivypo (Accreditation and Re-accreditation). Matokeo ya uhakiki wa maombi ya uanzishwaji wa vyuo vipyta yamebainisha kuwa kati ya vyuo vinne (4) vilivyoomba kuanzishwa, chuo kimoja kimekidhi vigezo na hivyo kupewa ithibati. Vyuo ambavyo havikukidhi vigezo vilipewa ushauri na maelekezo ya kuzingatia ili kutimiza masharti na vigezo vya uanzishaji wa chuo kikuu hapa nchini. Aidha, vyuo vilivyoomba kupewa ithibati au kuhuisha ithibati vyote vilikidhi vigezo na hivyo kupewa ithibati na/au kuhuisha ithibati zao.

93. Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa mitaala inayotolewa na Vyuo Vikuu nchini inakidhi vigezo na kuendana na mahitaji ya soko la ajira, Serikali kuititia Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania imefanya tathmini na kutoa ithibati ya Mitaala 153 iliyowasilishwa na Vyuo Vikuu nchini ikiwa ni sawa na asilimia 76.5 ya lengo la kutathmini mitaala 200 kwa mwaka.

94. Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wanaodahiliwa wanakidhi vigezo vya udahili na wanadahiliwa katika vyuo na programu zinazotambulika,

katika mwaka wa masomo 2020/21 Serikali kupitia Tume imeendelea kuratibu udahili wa wanafunzi wanojiunga na Elimu ya Juu nchini kwa ngazi ya Shahada ya Awali kwa kufanya yafuatayo:

(i) imeratibu maombi 101,354 ya wanafunzi walioomba kujunga na Elimu ya Juu kwa ngazi ya Shahada ya Awali katika vyuo 74 nchini kwa mwaka wa masomo 2020/21. Kati ya maombi hayo, jumla ya waombaji 87,371 wamedahiliwa katika vyuo mbalimbali nchini kati ya wadahiliwa hao wanawake ni 37,748 (43.2%) na wanaume ni 49,623 (56.8%);

(ii) imeandaa Mwongozo wa Udhili kwa mwaka wa masomo 2020/21 kwa ngazi ya Shahada ya Awali na kusambaza nakala laini katika tovuti ya Tume na mitando ya kijamii. Vilevile, nakala ngumu 800 zilisambazwa kwa wadau mbalimbali ili kuhakikisha wanafunzi na wananchi wanapata taarifa ya vyuo vinavyotambulika na vigezo vya udahili ili kuwawezesha kutuma maombi yao kwa usahihi; na

(iii) imeratibu programu mbalimbali za kuwajengea uelewa wanaotaka kujunga na Elimu ya Juu nchini kupitia vyombo vya habari ikiwemo Tovuti ya Tume na machapisho. Vilevile, Tume ilishiriki katika juma la Elimu ya Juu Zanzibar ambapo iliweza kutoa elimu kuhusu Elimu ya Juu kwa wanafunzi na wananchi. Aidha, kupitia kambi 17 za Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), elimu kuhusu udahili ilitolewa kwa vijana 20,500 ambao ni wahitimu wa Kidato cha Sita.

95. Mheshimiwa Spika, katika kutambua sifa za kitaaluma za wahitimu wa Elimu ya Juu iliyotolewa na vyuo vya nje ya nchi, Serikali kupitia Tume imetathmini na kutambua tuzo 4,311 kati ya 5,179 zilizowasilishwa kwa utambuzi na wahitimu waliotunukiwa na Vyuo Vikuu vya nje ya nchi.

96. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania imeendelea kuboresha mifumo ya TEHAMA katika utoaji wa huduma kwa Vyuo vya Elimu ya Juu nchini pamoja na wadau wengine na kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wakati kwa ajili ya maamuzi ya kisera, mipango na kiutendaji.

Aidha, imeendelea kufanya maboresho ya mifumo mitatu (3) ya kielektroniki ambayo ni: Programme Management System (PMS); University Information Management System (UIMS); na Foreign Award Assessment System (FAAS). Mifumo hiyo inatumika katika ithibati za mitaala, ukusanyaji wa taarifa na uratibu wa udahili pamoja na uchakataji wa tuzo za nje kwa lengo la kurahisisha utendaji kazi.

97. Mheshimiwa Spika, ili kujenga uelewa kwa jamii kuhusu kazi zinazotekelizwa na Taasisi za Elimu ya Juu, Serikali kuitia Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania imetekeleza yafuatayo:

- (i) imeratibu utoaji wa mafunzo na semina za kubadilishana uzoefu kwa Maafisa Uthibiti Ubora, Maafisa Udhili, Maafisa TEHAMA, Wasimamizi wa kanzidata, Wahadhiri na Viongozi wa Vyuo vya Elimu ya Juu kwa lengo la kuboresha utendaji kazi. Jumla ya washiriki 218 wa Vyuo vya Elimu ya Juu walinufaika na mafunzo hayo;
- (ii) imeendelea kuratibu semina na makongamano ya kubadilishana ujuzi na uzoefu kwa Wanataluma na Viongozi wa Vyuo Vikuu kuhusu masuala ya ubora wa Elimu ya Juu, uandaaji wa mitaala inayokidhi na kuzingatia mahitaji ya soko la ajira, uongozi na uendeshaji wa vyuo vikuu. Jumla ya Viongozi 312 wa Vyuo Vikuu wamenufaika na mafunzo hayo;
- (iii) imeandaa maonesho ya 15 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia ambapo taasisi 67 za ndani ya nchi zilishiriki na zaidi ya wananchi 60,000 wakiwemo wanafunzi walihudhuria maonesho hayo na kupata uelewa wa huduma zinazotolewa na taasisi za Elimu ya Juu;
- (iv) imeshiriki makongamano na mikutano inayohusu uimarishaji na Uthibiti wa Ubora wa Elimu ya Juu katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kimataifa kwa lengo la kuongeza ujuzi na weledi katika kuthibiti ubora wa Elimu ya Juu nchini; na
- (v) imeandaa mkuutano na kufanya majadiliano na wamiliki wa Vyuo Vikuu vinavyomilikiwa na taasisi binafsi kwa lengo

la kupata uelewa wa pamoja kuhusiana na taratibu, miongozo na kanuni za uendeshaji wa Vyuo Vikuu pamoja na changamoto mbalimbali zilizopo na namna ya kukabiliana nazo. Jumla ya washikiri 32 kutoka vyuo binafsi 18 walihuduria.

98. Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa kuna wataalamu wa kutosha wa kuhakiki Mitaala na kufanya ukaguzi wa ubora wa Vyuo Vikuu hapa nchini, Serikali kuditia Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania imeandaa kanzidata ya Wataalamu wa Kuhakiki Mitaala (Curricula Peer Reviewers) kutoka katika programu mbalimbali za masomo na Wakaguzi wa Vyuo Vikuu (Institutional Audit Experts) kutoka katika vyuo mbalimbali hapa nchini kwa lengo la kurahisisha na kuongeza kasi ya utoaji wa ithibati ya Mitaala na Vyuo. Aidha, imetoa mafunzo kwa Wataalamu wa Kuhakiki Mitaala na Wakaguzi wa Vyuo illi kuwajengea uwezo na umahiri wa kutekeleza majukumu yao. Jumla ya Wanataaluma 134 kutoka Vyuo Vikuu vyua umma na binafsi wamenufaika na mafunzo haya.

99. Mheshimiwa Spika, ili kulinda haki na maslahi ya wananchi na taifa kwa ujumla, Watanzania wanaokwenda kusoma nje ya nchi kuditia kwa Mawakala, Serikali kuditia Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania imeendelea kukagua Asasi/Kampuni zinazojishughulisha na uratibu wa wanafunzi wanaokwenda kusoma nje ya nchi kwa lengo la kuzitambua na kuzisajili. Kwa mwaka 2020/21, Serikali imepokea na kutathmini maombi ya taasisi tano (5) za mawakala wanaotaka kupata leseni ya kuwatafutia wanafunzi Vyuo Vikuu nje ya nchi. Lengo ni kuhakikisha watanzania wanaokwenda nje ya nchi wanasona katika vyuo vinavyotambulika kitaifa na kimataifa. Taasisi hizo ni: Tebeth Mentors and Information Centre; Sangeni International; Edukwanza Consultancy Ltd; Sultan Academics; na Cognita Consultancy Ltd.

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundı (NACTE)

100. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha usimamizi wa Elimu ya Ufundı katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kuditia Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundı imetekeliza yafuatayo:

- (i) imehakiki udahili wa wanafunzi 157,420, (Wanawake 75,194; Wanaume: 82,226) katika ngazi ya Astashahada ya Awali, Astashahada na Stashahada;
- (ii) imesajili vyuo 22 katika bodi za masomo zifuatazo: Afya na Sayansi Shirikishi 11; Biashara, Utalii na Mipango 6; na Sayansi na Teknolojia Shirikishi 5. Usajili huo umewezesha udhibiti wa uanzishwaji na uendeshaji wa mafunzo kiholela;
- (iii) imetoa ithibati kwa vyuo 26 katika bodi za masomo zifuatazo: Afya na Sayansi Shirikishi 10; Biashara, Utalii na Mipango 8; na Sayansi na Teknolojia Shirikishi 8. Utoaji wa ithibati umesaidia vyuo kukua na kukidhi viwango vya utoaji wa elimu bora;
- (iv) imeidhinisha uanzishwaji na utambuzi wa programu 20 katika vyuo kwa mchanganuo ufuataao: Afya na Sayansi Shirikishi 8; Biashara, Utalii na Mipango 6; na programu za Sayansi na Teknolojia Shirikishi 6;
- (v) imetoa mafunzo ya namna ya upimaji na ufundishaji wa mitaala inayozingatia umahiri (CBET) kwa wakufunzi 806 wa Vyuo vya Elimu ya Ufundu. Mafunzo hayo yatasaidia wahitimu kuwa mahiri katika ujuzi uliokusudiwa; na
- (vi) imefanya ufuatiliaji na tathmini ya ubora wa elimu katika vyuo 138 vya elimu ya ufundu sawa na asilimia 69 ya lengo. Katika ukaguzi huo vyuo ambavyo havikukidhi vigezo vilichukuliwa hatua stahiki ambapo vyuo vitano (5) vilifutiwa usajili na vyuo 13 vilisimamishwa kudahili wanafunzi ili kuvipa nafasi ya kurekebisha upungufu uliobainika. Vyuo vyote vilipatiwa ushauri wa kuboresha utoaji wa elimu ya ufundu na mafunzo.

101. Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha ubora wa elimu inayotolewa na kuhakikisha inawawezesha wahitimu kujajiri na kuajiriwa, Serikali kuititia Baraza imetekeleza kazi zifuatazo:

- (i) imetoa namba ya uhakiki wa tuzo (AVN) 17,234 ambazo zimewezesha kuepuka udanganyifu wa wahitimu wanaoendelea na Elimu ya Juu;
- (ii) imefanya ulinganifu wa Tuzo 1,028 ili kuthibiti viwango vya Elimu ya Ufundu nchini; na
- (iii) imehakiki Mitaala 118 ilioandaliwa na Vyuo vya Ufundu ili kuhakikisha mafunzo yanayotolewa yanakidhi mahitaji ya soko la ajira.

102. Mheshimiwa Spika, ili kusogeza huduma kwa wananchi, Serikali kupitia Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu imenunua kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa ofisi katika kanda ya Magharibi (Tabora) na hivyo Baraza kuwa na jumla ya viwanja sita (6) katika Mikoa ya Dodoma, Arusha, Tabora, Mtwara, Mwanza na Mbeya.

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET)

103. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania imeendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kutekeleza yafuatayo:

- (i) imeandaa vitabu vya kiada kwa masomo nane (8) vya Darasa la VII pamoja na viongozi vya mwalimu ili kuwezesha uwepo wa vitabu vinavyoendana na mtaala ulioboreshwa;
- (ii) imeandaa vitabu vya masomo 14 vya maandishi yaliyokuzwa kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu wa Darasa la VI na VII kwa lengo la kuhakikisha kuwa wanafunzi hao wanapata elimu sawa na wanafunzi wengine;
- (iii) imeandaa vitabu vya masomo 14 vya maandishi ya Breli kwa ajili ya wanafunzi wasioona wa Darasa la VI na VII kwa lengo la kuhakikisha kuwa wanafunzi hao wanapata elimu sawa na wanafunzi wengine;
- (iv) imetafsiri vitabu vya kiada vya masomo matano (5) vya Darasa la VII pamoja na Viongozi vya Mwalimu kwa ajili ya matumizi ya shule zinazotumia Lugha ya Kiingereza;

(v) imeandaa maudhui ya aina 31 ya Vitabu vya Kiada Ngazi ya Sekondari Kidato cha I hadi cha IV ili kukidhi mahitaji ya mtaala na kuwezesha uwepo wa vitabu hivyo;

(vi) imeandaa mitaala minne (4) na mihtasari 36 ya Elimu ya Ualimu ngazi ya Stashahada ili kukidhi mahitaji ya sasa; na

(vii) imeandaa moduli ya Kielektroniki (Cartoon Based Lessons) kwa Ngazi ya Elimu ya Awali ili kumuwezesha mtoto kujenga umahiri muhimu utakaomsaidia kujifunza na kujitawala.

104. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuhakikisha vitabu vinapatikana shulenii ambapo katika mwaka wa fedha 2020/21 imechapa na kusambaza vitabu na miongozo mbalimbali ikiwemo:

(i) nakala 4,443,586 za vitabu vya kiada kwa wanafunzi na nakala 253,408 za Kiongozi cha Mwalimu Darasa la VII katika Halmashauri zote nchini;

(ii) nakala 322,000 za vitabu vya Kiada Darasa la VI, nakala 154,000 na nakala 560 za vitabu na Kiongozi cha Mwalimu Darasa la VII kwa shule zinazotumia Lugha ya Kiingereza kufundishia katika Halmashauri zote nchini;

(iii) nakala 43,671 na 305,697 za mtaala wa Darasa la I - VII na mihtasari ya Darasa la III - VII kwa shule zinazotumia Lugha ya Kiswahili na Kiingereza kufundishia na kujifunzia katika Halmashauri zote nchini;

(iv) nakala 2,000 za Mwongozo wa Utekelezaji wa Mtaala wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV kwa Wanafunzi Viziwi na wenye Bakaa ya Usikivu Tanzania Bara na Visiwani; na

(v) nakala 4,100 za vitabu vya kiada vya Breli vya sekondari vya Wanafunzi Wasiona Tanzania Bara na Visiwani.

105. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania imeandaa mwongozo wa utekelezaji wa mtaala wa elimu ya Sekondari kwa Wanafunzi Viziwi Kidato cha I - IV

ili kusaidia ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi viziwi na kuinua kiwango cha ufaulu. Aidha, imeandaa Kamusi ya Kidigitali ya Lugha ya Alama Tanzania (LAT) kwa ajili ya kuboresha ufundishaji wa wanafunzi viziwi nchini.

106. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuwajengengea uwezo watumishi kazini ambapo katika mwaka wa fedha 2020/21 imetekeliza yafuatayo:

(i) imetoa mafunzo kwa walimu 72 wa shule 26 zenyewe wanafunzi viziwi nchini ili kuwawezesha kutumia Kamusi ya Lugha ya Alama ya Tanzania na mwongozo wa utekelezaji wa mtaala wa elimu ya sekondari Kidato cha I - IV; na

(ii) imetoa mafunzo kazini kwa washiriki 5,598 (Wakufunzi 1,206 kutoka Vyuo vya Ualimu vya Serikali na visivyo vya Serikali; Walimu 3,957 kutoka Shule za Msingi na Sekondari za Serikali na zisizo za Serikali; Maafisa Elimu Kata 226; Wathibiti Ubora 48; Walimu wa Elimu ya Awali 105; Maafisa Elimu Sekondari na Msingi 56). Mafunzo hayo yalilenga kuwawezesha watekelezaji wa mtaala kutekeleza mtaala kwa usahihi.

107. Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia agizo la Hayati John Pombe Joseph Magufu, Rais wa Awamu ta Tano, kuhusu kufundishwa kwa somo la Historia ya Tanzania kwa wanafunzi wote, Serikali kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania imetekeliza yafuatayo:

(i) imekamilisha uandaaji wa mihtasari ya Somo la Historia ya Tanzania kuanzia Ngazi ya Elimu ya Awali hadi Sekondari (Kidato cha I - VI; na

(ii) inaendelea na uandaaji wa Vitabu vya Kiada 14 vya Somo la Historia ya Tanzania kuanzia Ngazi ya Elimu ya Awali hadi Sekondari Kidato cha VI. Aidha, inaendelea na maandalizi ya mafunzo kwa walimu kwa lengo la kuwezesha kufundisha somo hilo.

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)

108. Mheshimiwa Spika, ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, Serikali kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania katika mwaka wa fedha 2020/21, imetekeleza kazi zifuatazo:

- (i) imewezesha ujenzi wa madarasa 180 (madarasa 3 kwa kila shule) katika shule 45 za msingi na 15 za sekondari ambapo ujenzi unaendelea kwa kutumia utaratibu wa Force Account;
- (ii) imewezesha ujenzi wa nyumba 100 za walimu katika shule 15 za sekondari na 10 za msingi zilizopo katika maeneo yenye mazingira magumu kwa lengo la kuimarisha makazi ya walimu na kuongeza ufanisi;
- (iii) imewezesha ujenzi wa matundu ya vyoo 360 katika shule tisa (9) za msingi na sita (6) sekondari zenye upungufu ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia;
- (iv) imeboresha miundombinu kwa Wanafunzi wenyе Mahitaji Maalumu katika shule za msingi nane (8);
- (v) imeboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika Chuo cha Karume cha Sayansi na Teknolojia kilichopo Zanzibar; na
- (vi) inaendelea kuwezesha ujenzi wa mabweni 15 katika shule 15 za sekondari zenye mazingira magumu.

Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM)

109. Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha utendaji kazi kwa watumishi kazini, Serikali kupitia Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu katika mwaka wa fedha 2020/21 imetekeleza kazi zifuatazo:

- (i) imetoa mafunzo ya Astashahada, Stashahada katika Uongozi na Usimamizi wa Elimu (DEMA) pamoja na Stashahada ya Uthibiti Ubora wa Shule kwa walimu 1,985 kwa

lengo la kuimarisha usimamizi wa elimu ngazi ya Shule, Kata, Halmashauri na Mkoa;

(ii) imetoa mafunzo ya Uthibiti Ubora wa Shule wa Ndani kwa Maafisa Elimu Taaluma Msingi 184, Wathibiti Ubora wa Shule wa Wilaya 183 na Wakuu wa Shule za Msingi 8,800 kutoka Halmashauri zote za Tanzania Bara;

(iii) imetoa mafunzo ya muda mfupi ya Uandaaji wa Mpango Mkakati, Masuala ya Manunuzi na Fedha, Uongozi na Usimamizi wa Elimu kwa Timu za Menejimenti ya Vyuo vya Ualimu ambapo wajumbe 315 walishiriki;

(iv) inagharamia watumishi watano (5) katika Shahada ya Uzamivu; na

(v) imefanya ufuatiliaji kwa Wakuu wa Shule za Sekondari na wadau mbalimbali waliopewa mafunzo na ADEM hususan wahitimu wa Programu ya DEMA kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita ilikubaini hali ya utendaji kazi wao. Tathmini ya ufuatiliaji inaendelea.

110. Mheshimiwa Spika, ili kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia, Serikali kupitia Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu imekarabati nyumba tatu (3) za watumishi katika Kampasi ya Bagamoyo zenyе uwezo wa kuchukua familia sita (6). Aidha, imewezaisha upatikanaji wa hati ya kiwanja na kukamilisha michoro ya Mpango Kabambe wa Matumizi ya Ardhi (Master Plan) ya eneo itakapojengwa Kampasi ya Mbeya.

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu

111. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imetoa mikopo kwa wanafunzi 149,398 (Wanafunzi wa mwaka wa kwanza 55,337 na wanaoendelea na masomo 94,061);

(ii) imekusanya kiasi cha **Shilingi 139,244,569,882.91** hadi kufikia Machi, 2021 ikiwa ni asilimia 72 ya lengo la kukusanya **Shilingi 194,100,000,000** ya mikopo iliyolva;

(iii) imebainisha wanufaika wapya 14,807 na kupewa ankara zao ili kurejesha mkopo. Aidha, ukaguzi umefanyika kwa waajiri 3,979 na taarifa za mkopo zimehuishwa kwa wanufaika 321,629 kupitia kwa waajiri wao;

(iv) imefanya mapitio ya makato na tozo za mikopo ya elimu ya juu ambazo zimekuwa zikitumika kwa takribani miaka 10 ili maoni ya wadau mbalimbali yenye tija ikiwemo kutunza thamani ya fedha za mikopo, kujenga uhimilivu wa mfuko wa mikopo ya wanafunzi na kuzingatia mwenendo wa viwango vya mfumuko wa bei vya sasa; na

(v) imefanya maboresho ya mfumo wa kusimamia mikopo (Intergrated Loan Management System - iLMS) kwa kufanya yafuatayo:

a) kuanzisha mfumo rahisi wa kidigitali wa urejeshaji mikopo (Loanee Individual Permanent Account – LIPA) ambao unamuwezesha mnufaika au mwajiri kupata taarifa za deni na utaratibu wa kulipa kutoka popote alipo kupitia tovuti (www.heslb.go.tz);

b) kuimarisha uhakiki wa maombi ya mikopo kutoka kwa wanafunzi waliodhaminwa katika masomo ya sekondari au stashahada ili kuepuka udanganyifu; na

c) kuimarisha mfumo wa kidigitali wa haraka wa malipo ya fedha kwa wanafunzi (Digital Disbursement System - DiDis) kwa kufikisha huduma hiyo kwa asilimia 91 ya wanufaika wote 148,012. Kupitia mfumo huu, mwanafunzi aliyesajiliwa anaweza kupokea fedha ndani ya dakika tano (5) baada ya kusaini kwa njia ya biometriki.

112. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, imeendelea kuendesha programu za elimu kwa waajiri, wanufaika na wanafunzi

kuhusu uombaji sahihi wa mikopo na umuhimu wa urejeshaji wa mikopo kwa wakati kama ifuatavyo:

- (i) imeendesha programu 15 kuhusu wajibu wa wanafunzi wanufaika kwa jumla ya wanafunzi 5,250 na viongozi wao waliopo katika taasisi za UDSM, UDOM, SAUT - Mwanza, DUCE, SUA, MU, MUST, CUCoM, TIA -MBEYA, CBE - MBEYA, TEKU, ISW, KCMC, MWUCE, na DMI;
- (ii) imeendesha programu za elimu ya uombaji sahihi wa mikopo kwa wahitimu wa kidato cha sita katika mikoa 14 ya Tanzania Bara na Zanzibar ambapo wanafunzi 9,898 walifikiwa;
- (iii) imeendesha programu za elimu ya uombaji sahihi wa mikopo kwa wanafunzi 22,681 waliokuwa wakipewa mafunzo katika kambi 18 za Jeshi la Kujenga Taifa (JKT);
- (iv) imetoa mafunzo ya kuwajengea uwezo katika ujazaji fomu za maombi ya mikopo watoa huduma za intaneti 33 katika vituo mkakati vyta ya huduma za intaneti katika mikoa ya Dodoma, Arusha na Mwanza;
- (v) imeendesha programu za elimu zilizolenga waajiri na wanufaika kuititia redio na televisheni ambapo jumla ya programu 24 ziliendeshwa na matangazo 336 yalitolewa; na
- (vi) imeendelea na kampeni ya #WeweNdioFuture kuititia vyombo vyta ya habari na mitandao ya kijamii. Kampeni hii inalenga kuhamasisha wateja wa Bodi ya Mikopo kuomba mkopo kwa usahihi ili kutimiza ndoto zao na pia kurejesha mikopo kwa wakati ili kuepuka adhabu.

Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (BOHUMATA)

113. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kuititia Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania imetekeleza kazi zifuatazo:

- (i) imeongeza vitabu 432,449 (432,144 kutoka Book Aid International, 305 kutoka Legal Deposite Law), magazeti 3,246

na majarida 13 katika vituo 43 vya Mikoa 22 kwa ajili ya watu wazima na watoto;

(ii) imetoa ushauri wa kitaalamu kuhusu uanzishaji, upangaji na uendeshaji wa maktaba za Shule za Msingi na Sekondari 33 zilizopo katika Wilaya tano (5) za Ilala, Ubungo, Kinondoni, Temeke na Kigamboni; na

(iii) imetoa mafunzo ya ukutubi na uhifadhi nyaraka kwa washiriki 648 (NTA Level 4: 318; NTA Level 5: 150 na NTA Level 6: 180) kwa lengo la kuongeza ujuzi.

Uendelezaji wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu

Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH)

114. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imekamilisha Mfumo wa Usimamizi wa Utafiti na Ubunifu (Research and Innovation Management System - RIMS) kwa lengo la kuhamasisha na kuongeza matumizi ya bunifu katika mifumo rasmi ya uchumi;

(ii) imetoa fursa kwa watafiti 13 wakiwemo wanafunzi wa Shahada ya Uzamili na Uzamivu kutoka katika Taasisi za Utafiti na Maendeleo wanne (4) na kutoka katika Vyuo Vikuu tisa (9) kushiriki kufanya utafiti katika kazi za kongano 15 zinazotekeleza mradi wa kongano bunifu. Aidha, Kongano tano (5) kati ya 15 zilizopo zimepata fursa ya kushiriki kufanya majaribio ya utekelezaji wa miongozo mitano (5) ya usimamizi wa kongano bunifu;

(iii) imewezesha taasisi nne (4) za kisekta (TALIRI, TARI, TAFIRI na TAFORI) kuandaa taratibu za uendeshaji (Standard Operating Procedures – SOPs) kwa ajili ya uanzishwaji na uendeshaji wa kamati za maadili ya utafiti (Research Ethical Committee - REC). Uanzishwaji wa kamati za kusimamia maadili ya utafiti utasaidia nchi kukuza ubora wa tafiti

ambazo zinazingatia viwango na maadili ya utafiti nchini; na

(iv) inaendelea na utekelezaji wa miradi 173 (ubunifu 106, utafiti 56 na miundombinu 11) inayotekelizwa kuititia taasisi mbalimbali za utafiti na maendeleo, Elimu ya Juu, Vyuo vya Kati na Ufundsi Stadi ambapo miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

115. Mheshimiwa Spika, Serikali kuititia Tume imewezesha upatikanaji wa maandiko 42 kutoka katika taasisi 19 vikiwemo Vyuo Vikuu. Maandiko hayo yalikuwa katika maeneo manne (4) na yalilenga kuendeleza na kuboresha:

Ng'ombe na nyama kwa ajili ya usindikaji; Teknolojia za kuchakata mazao ya killmo; Teknolojia ya kuchakata ngozi; na Teknolojia za kuchakata nishati na madini hususan kwa wachimbaji wadogo. Kati ya maandiko hayo, maandiko 13 yaliibua miradi minne (4) iliyopata ufadhili wa fedha kutoka International Development Research Cooperation (IDRC). Miradi mingine iliyofadhiliwa ni mradi wa kimkakati kutoka Zanzibar kuhusu masuala ya miti shamba (tiba asilia) na miradi miwili (2) ya utafiti kwa lengo la kukuza matokeo ya awali ya utafiti katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo na Taasisi ya NYUMBU.

116. Mheshimiwa Spika, Serikali kuititia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia imeendelea kutoa elimu kuhusu ufumbuzi wa matatizo mbalimbali ya kijamii kwa umma kwa kusambaza machapisho 83 yanayohusu sayansi, teknolojia na ubunifu katika magazeti na majarida mbalimbali, kurusha jumla ya vipindi 103 katika redio, runinga na mitando ya kijamii.

117. Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa tafiti na bunifu zinazofanyika nchini zinakidhi vigezo vya ushindani, zinaendelezwa na wabunifu/watafiti wanajengewa uwezo wa kusimamia kazi zao, Serikali kuititia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia imetekeliza kazi zifuatazo:

- (i) imetathmini bunifu 73 za wabunifu 70 walioshiriki katika mashindano ya MAKISATU kutoka mikoa 22 ya Tanzania Bara kwa lengo la kubaini mahitaji ya kila mbunifu ambapo wabunifu hao walipatiwa mafunzo ya utaratibu wa kusimamia na kuendesha miradi yao kabla ya kupatiwa ruzuku;
- (ii) imetathmini miradi 120 ya utafiti kwa lengo la kusimamia na kubaini hali ya utekelezaji ambapo tathmini ilibaini kuwa takribani miradi yote illikuwa katika hali nzuri ya utekelezaji; na
- (iii) imepitia maombi 101 ya wabunifu waliotembelewa na Tume ambapo maombi 61 yalikidhi vigezo vyta kuendelezwa kwa kupatiwa fedha, mafunzo, kutambulishwa na kuunganishwa katika taasisi mbalimbali kulingana na ubunifu wao.

118. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia imewezesha wabunifu 10 wa Tanzania wenyewe Kampuni changa (Startups) wanaotumia teknolojia katika kutatua changamoto za kijamii kushiriki mafunzo ya awali. Mafunzo hayo yalilenga kujenga uwezo wa uanzishajili wa biashara au kampuni zinazojitegemea na kuboresha ujasiriamali kwa kutetea na kunadi ubunifu kwa wawekezaji (Pitching for investors). Baada ya mafunzo hayo, bunifu 18 kutoka Tanzania, Afrika Kusini, Zambia, Namibia na Botswana zilichaguliwa kushiriki mashindano ya kiulimwengu ambapo kati ya hizo bunifu tatu (3) (Huduma smart, Medikea na Novfeed) zilikuwa za Tanzania. Bunifu moja (1) ya Tanzania (Huduma smart) ilishinda tuzo tatu (3) za Think Africa Prize ya USD 5000; Amazon Web Server; na Node by SLUSH (International Investment Matchmaking Platform) katika mashindano hayo.

Tume ya Nguvu za Atomiki (TAEC)

119. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki (TAEC) imetekeliza kazi zifuatazo:

- (i) imepima viwango vya mionzi kwa wafanyakazi 1,920 wanaofanya kazi katika vyanzo vya mionzi ambapo ilibainika kuwa viwango vya mionzi vilivyopo vinakubalika kisheria. Idadi hiyo ni sawa na ongezeko la asilimia 41.3 ikilinganishwa na wafanyakazi 1,359 waliopimwa katika mwaka wa fedha 2019/20;
- (ii) imepima viwango vya mionzi katika sampuli 11,378 ambapo kati ya hizo vyakula kutoka nje 3,266, vyakula vilivyosafirishwa nje ya nchi 7,055, mbolea 164 na tumbaku na bidhaa nyingine 893 kwa lengo la kudhibiti na kusimamia matumizi salama ya mionzi. Kiwango hicho ni sawa na ongezeko la asilimia 44.5 ikilinganishwa na sampuli 7,873 zilizopimwa katika mwaka wa fedha 2019/20;
- (iii) imekusanya mabaki ya vyanzo vya mionzi 16 na kuhifadhiwa katika kituo maalumu cha kuhifadhi mabaki ya vyanzo vya mionzi ili kulinda wananchi na mazingira yasichafuliwe; na
- (iv) imekagua vituo 364 ambavyo vinamiliki na kutumia vyanzo vya mionzi ili kudhibiti hali ya usalama kwa wagonjwa, wafanyakazi na umma ambapo vituo vilivyokaguliwa vimeongezeka kwa asilimia 74.2 ikilinganishwa vituo 209 vilivyokaguliwa katika mwaka wa fedha 2019/20.

120. Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha huduma za teknolojia ya nyuklia zinazotolewa na TAEC, Serikali imeendelea kutekeleza yafuatayo:

- (i) kusimamia kituo cha kupima uchafuzi wa hewa katika anga unaotokana na majaribio ya silaha za nyuklia chini ya mkataba wa kimataifa wa Comprehensive Nuclear Test-Ban Treaty (CTBT) for Non-Proliferation Test (NPT) of Nuclear Weapons;
- (ii) kufanya tafiti 18 za matumizi ya teknolojia ya nyuklia na tayari machapisho matano (5) yameshatoka katika majarida mbalimbali ya kisayansi; na

(iii) kutengeneza na kuhakiki vifaa/mitambo 92 inayotumia teknolojia ya nyukilia katika kuimarisha ubora wa vifaa, usalama wa wafanyakazi na jamii inayowazunguka. Idadi hiyo ni sawa na ongezeko la asilimia 76.9 ikilinganishwa na vifaa 52 vilivyofanyiwa matengenezo na uhakiki katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20.

121. Mheshimiwa Spika, ili kuboresha na kusogeza huduma za teknolojia ya nyuklia karibu na jamii, Serikali kupitia TAEC imetekeleza kazi zifuatazo:

(i) imepokea na kutathmini maombi 630 ya vibali vya umiliki, utumiaji na usafirishaji wa vyanzo vya miozi ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 26 la lengo la maombi 500;

(ii) imetoa leseni 336 za kumiliki na kutumia vyanzo vya mionzi ambapo kati ya hizo leseni za kumiliki na utumiaji wa vyanzo vya mionzi 285, uingizaji wa vyanzo vya mionzi nchini 28, kusafirisha vyanzo vya mionzi nje ya nchi 7, na usafirishaji wa vyanzo vya mionzi ndani ya nchi 16. Idadi hiyo ni sawa na ongezeko la asilimia 24.9 ikilinganishwa na leseni 269 zilizotolewa katika mwaka wa fedha 2019/20;

(iii) imesajili wataalam wa mionzi 278 ambapo kati yao wataalam wa kutoa huduma za mionzi kwa wagonjwa ni 262 na 16 wa usimikaji, uendeshaji, utengenezaji wa vifaa/ mitambo inayotoa mionzi; na

(iv) imeendelea na ujenzi wa maabara changamano awamu ya pili itakayogharimu Shilingi bilioni 10.4 ambapo ujenzi umefikia asilimia 73. Kukamilika kwa ujenzi kutaongeza uwezo wa kulinda wananchi dhidi ya madhara ya mionzi ambayo yanaweza kujitokeza pamoja na kuiwezesha TAEC kuwa Kituo cha Umahiri cha Kikanda katika Nyanja ya Sayansi na Teknolojia ya Nyuklia.

TUME YA TAIFA YA UNESCO (FUNGU 18)

122. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/21, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO ya Jamhuri ya

Muongano wa Tanzania imeratibu na kusimamia utekelezaji wa Mikataba na kazi za UNESCO nchini kama ifuatavyo:

- (i) imesimamia utekelezaji wa programu na miradi mbalimbali iliyopitishwa katika mpango wa UNESCO wa Mwaka 2020 - 2022;
- (ii) imeshirikisha wadau katika fursa mbalimbali zinazotokana na uanachama wa Serikali katika shirika la UNESCO;
- (iii) imefanya tathmini juu ya usimamizi na uelewa wa wadau na ushiriki wao katika uhifadhi wa maeneo ya Urithi wa Dunia, Binadamu na Hifadhi Hai, na Urithi wa Kijiolojia;
- (iv) imeratibu vikao vya Kamati ya Kitaifa ya Kudhibiti Matumizi ya Dawa na Mbinu za Kuongeza Nguvu Michezoni kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo;
- (v) imeratibu na kutathmini utekelezaji wa maamuzi ya Kamati ya Urithi wa Dunia ndani ya maeneo yaliyo katika Orodha ya Urithi wa Dunia ambayo ni Hifadhi ya Taifa ya Serengeti, Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro, Eneo la Hifadhi la Ngorongoro, Mamlaka ya Mji Mkongwe wa Zanzibar, Michoro ya Miambani ya Kondo na Magofu ya Kilwa Kisiwani na Magofu ya Songo Mnara;
- (vi) imefanya tathmini ya utekelezaji wa programme za kimataifa za maji (International Hydrological Programme) na pia kusimamia utekelezaji wa programme ya kamisheni ya kimataifa ya mazingira ya bahari kwenye kuelekea uchumi wa blue na tahadhari kwenye majanga yanayotokana na bahari (International Oceanography Committee); na
- (vii) imeratibu utekelezaji wa Programme za UNESCO nchini zinazohusuana na Elimu kwa wote (EFA) na Elimu ya Mafunzo ya Elimu ya Ufundı (TVET).

C. MPANGO NA BAJETI YA FUNGU 46 KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22

123. Mheshimiwa Spika, Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2021/22 yamezingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa (2025), Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 -2025/26), Ilani ya Chama Chama cha Mapinduzi (CCM) (2020 - 2025) na Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan aliyoitoa tarehe 22 Aprili 2021 mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, maandalizi yamezingatia michango ya Waheshimiwa Wabunge katika Hotuba ya Waziri Mkuu, Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI. Hivyo, Wizara itatoa kipaumbele katika kuimarisha elimu na kufanya kazi maoni na ushauri ambao umekuwa ukitolewa na wadau wa elimu. Vilevile, Wizara itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi kama yalivyoanishwa katika Hati Idhini ya waka 2016.

Maeneo ya Kipaumbele

124. Mheshimiwa Spika, Serikali itafanya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 kwa lengo la kuhakikisha kuwa inakidhi mahitaji ya sasa. Aidha, Serikali itafanya mapitio ya Sheria ya Elimu ya mwaka 1978 ili kuhakikisha inaendana na mazingira ya sasa ya utoaji wa elimu nchini.

125. Mheshimiwa Spika, Serikali itaweka msisitizo zaidi katika ufundishaji wa Masomo ya Ufundi kwa kuimarisha Mafunzo kwa Vitendo katika shule za Sekondari za Ufundi zilizopo ambazo ni: Iyunga, Ifunda, Tanga, Bwiru Wavulana, Musoma, Mwadui, Moshi na Mtwara. Vilevile, Serikali itaimarisha ufundishaji wa masomo yanayowajengea wanafunzi ujuzi katika shule za msingi na sekondari. Masomo hayo ni pamoja na Kilimo, Ufundi, Stadi za Kazi, Michezo, na Biashara.

126. Mheshimiwa Spika, Serikali itafanya ufuatiliaji na tathmini ya kina ya mitaala inayotumika kwa sasa ili kuhakikisha kuwa ufundishaji na ujifunzaji unafanyika kwa kuzingatia viwango na vigezo viliwyowekwa. Vigezo hivyo ni pamoja na uwepo

wa walimu kulingana na idadi ya wanafunzi, vitabu na mazingira ya kujifunzia. Pia Serikali itaanza kufanya mapitio ya mitaala katika ngazi zote za elimu ili kuhakikisha kuwa elimu na mafunzo yanayotolewa yanajikita katika kujenga ujuzi na kuzingatia mahitaji ya sasa.

127. Mheshimiwa Spika, Katika utekelezaji wa Maelekezo ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoystoa katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani yaliyofanyika Kitaifa Mkoani Mwanza tarehe 01 Mei, 2021, Serikali itaondoa tozo ya asilimia 6 ya kulinda thamani ya fedha katika urejeshaji wa mkopo kuanzia tarehe 1 Julai, 2021 iliyokuwa inatozwa kwa wanufaika wa Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Aidha, Serikali inaiagiza Bodi ya Wakurugenzi wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kuondoa pia tozo ya adhabu ya asilimia 10 ya mkopo ambayo inatozwa kwa wanufaika wanaochelewa kulipa mikopo hiyo.

128. Mheshimiwa Spika, Serikali itafanya kazi maoni na ushauri wa Wadau wa Elimu kuhusu utekelezaji wa Sheria ya mwaka 2018 iliyounda Bodi ya Kitaalamu ya Walimu. Aidha, Serikali itazingatia pia maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo walioutoa katika majadiliano kuhusu Kanuni za Bodi ya Kitaalamu ya Walimu yaliyofanyika tarehe **28 Aprili 2021** kati ya Wizara ya Elimu na Kamati hiyo. Vilevile, Wizara itazingatia kikamilifu maelekezo ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuhusu Bodi ya Kitaalamu ya Walimu aliyoystoa katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani yaliyofanyika Kitaifa Mkoani Mwanza tarehe 01 Mei, 2021.

Majukumu ya Msingi ya Wizara

129. Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ya Mpango na Bajeti katika mwaka wa fedha 2021/22, yatakelezwa kuititia Idara, Vitengo na Taasisi kama ilivyofafanuliwa katika majukumu ya Wizara. Malengo yatakayotekelze wa ni kama ifuatavyo:

Uendelezaji wa Elimumsingi na Sekondari

130. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha Elimumsingi na Sekondari, Serikali itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itafanya ufuatiliaji na tathmini ya uendeshaji na usimamizi wa shule Shikizi katika mikoa 15 ili kupima matokeo ya ufundishaji na ujifunzaji na kuweka afua stahiki;
- (ii) itaratibu mashindano ya insha ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya nchi zilizo Kusini mwa Afrika (SADC) kwa lengo la kuwajengea wanafunzi uwezo wa kufikiri, kuandika na kujieleza;
- (iii) itatoa mafunzo ya malezi, unasihi na ulinzi wa mtoto shuleni kwa walimu 200 wa shule za sekondari kutoka katika Kanda mbili (2) za Uthibiti Ubora wa Shule za Mashariki na Kusini ili kuwajengea uwezo na kuimarisha stadi za utoaji wa huduma za malezi shuleni; na
- (iv) itaandaa mwongozo wa kuwabaini na kuwaendeleza wanafunzi wenyе vipawa na vipaji katika shule za msingi, sekondari na vyuo vya Ualimu. Mwongozo huo utawezesha kuwatambua wanafunzi hao na kuweka mikakati ya kuwaendeleza.

Ithibati na Usajili wa Shule na Vyuo vya Ualimu

131. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu la kusimamia Sera na kuongeza fursa za Elimu na Mafunzo, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/22, itatekeleza yafuatayo:

- (i) itasajili shule 450 kwa lengo la kuongeza fursa ya upatikanaji wa elimu nchini;
- (ii) itaendesha mafunzo kwa maafisa wa Wizara na Wathibiti Ubora wa Shule katika halmashauri kuhusu Mwongozo wa Usajili na Uendeshaji wa Shule uliohuishwa pamoja na mfumo mpya wa usajili wa shule wa kieletroniki; na

(iii) itafanya ufuatiliaji katika shule 100 kati ya 450 zilizopata usajili wa masharti ya kukamilisha miundombinu iliyopungua ili kuhakiki kama wamezingatia masharti.

Usimamizi wa Elimu ya Ualimu

132. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha mafunzo ya Elimu ya Ualimu, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/22 itatekeleza yafuatayo:

- (i) itaratibu mashindano ya michezo na sanaa (UMISAVUTA) katika Vyuo vya Ualimu;
- (ii) itadahili wanachuo 8,000 wa mwaka wa kwanza katika Vyuo vya Ualimu; na
- (iii) itaratibu mafunzo ya ualimu katika Vyuo vya Ualimu vya Serikali na Visivyo vya Serikali.

Usimamizi na Uendelezaji wa Elimu Maalum

133. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa Elimu maalum, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/22 imepanga kutekeleza yafuatayo:

- (i) itanunua na kusambaza vifaa maalum vya kielimu na saidizi katika shule za Msingi, Sekondari, Vyuo vya Ualimu, Vyuo vya Ufundi na vyuo vikuu ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu, vifaa hivyo ni pamoja na viti mwendo, vifaa vya michezo, mafuta na kofia kwa ajili ya wenye ualbino na vifaa vya utengamao na uchechemuzi (bembea);
- (ii) itaendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo wakufunzi 400 wa vyuo vya ualimu, VETA na Wathibiti Ubora wa Shule kuhusu Elimu Maalumu na Elimu Jumuishi ili kuweza kuwashudumia wanafunzi wenye mahitaji maalumu;
- (iii) itawawezesha wanafunzi wenye ulemavu wanaotoka katika familia zenye kipato duni kupata mahitaji muhimu

ikiwemo ada na vifaa vya kujifunzia kwa lengo la kupunguza changamoto zinazokabili upatikanaji wa elimu katika ngazi mbalimbali;

(iv) itafanya utafiti kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi wenyewe ulemavu wa akili, usonji na viziwi ili kubaini changamoto na kuweka mikakati ya kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi hao; na

(v) itaendesha mafunzo kwa walimu 400 kuhusu ubainishaji na utoaji wa huduma stahiki kwa wanafunzi wenyewe ulemavu wa akili na wenyewe usonji ili kuongeza ufanisi katika kuwashudumia wanafunzi hao.

Kusimamia Ubora wa Elimu katika Shule na Vyuo vya Ualimu

134. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kuititia Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule na Vyuo vya Ualimu itatekeleza yafuatayo:

(i) itafanya tathmini ya jumla katika asasi 7,263 zikiwemo shule za Msingi 5,598, Sekondari 1,607 na Vyuo vya Ualimu 58;

(ii) itafanya tathmini ya ufuutiliaji katika asasi 1,453 zikiwemo shule za Msingi 1,120, Sekondari 321 na Vyuo vya Ualimu 12; na

(iii) itasimamia ujenzi wa ofisi tano (5) za Uthibiti Ubora wa Shule katika wilaya za Ubungo, Njombe Mji, Bunda DC, Pangani na Tarime.

Baraza la Mitihani la Tanzania - NECTA

135. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kuititia Baraza la Mitihani la Tanzania itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itaendesha Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) 2021 kwa wanafunzi 1,705,650;

- (ii) itaendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) 2021 kwa watahiniwa 1,140,571;
- (iii) itaendesha Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili (FTNA) 2021 kwa watahiniwa 822,509;
- (iv) itaendesha Mtihani wa Kidato cha Nne (CSEE) 2021 kwa watahiniwa 583,898 na Mtihani wa Maarifa (QT) 2021 kwa watahiniwa 9,904;
- (v) itaendesha Mtihani wa Kidato cha Sita (ACSEE) 2022 kwa watahiniwa 100,492;
- (vi) itaendesha Mitihani ya Ualimu katika ngazi ya Astashahada na Stashahada kwa watahiniwa 7,324 mwaka 2022; na
- (vii) itaendesha Upimaji wa Kitaifa wa Umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu - KKK kwa sampuli ya watahiniwa wa Darasa la Pili 2022.

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET)

136. Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha ubora wa elimu nchini katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itapitia na kuboresha mtaala wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I - VI ili kukidhi mahitaji ya sasa na kuweka mkazo zaidi katika elimu inayojenga ujuzi;
- (ii) itachapa na kusambaza vitabu vya kiada ngazi za sekondari, moduli za Elimu ya Ualimu na vitabu vya hadithi kwa darasa la I na II;
- (iii) itatoa mafunzo kazini kwa Walimu, Wakufunzi, Wathibiti Ubora wa Shule na Maafisa Elimu kuhusu mtaala ulioboreshwa;
- (iv) itafanya tathmini ya vitabu vya ziada na rejea kutoka kwa waandishi binafsi ili viweze kupatiwa ithibati; na

(v) itaboresha mtaala na mihtasari ya wanafunzi viziwi na wasioona katika ngazi ya Elimu ya Msingi.

137. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itaandika vitabu vya kiada na Kiongozi cha Mwalimu kwa masomo ya Sekondari Kidato cha I - VI ili kutatua changamoto ya upatikanaji wa vitabu katika ngazi hiyo;

(ii) itaandaa vitabu vya kiada katika mfumo wa maandishi makubwa kwa ajili ya wanafunzi wenyewe uoni hafifu na maandishi ya Breli kwa ajili wanafunzi wasioona kwa masomo ya Sekondari; na

(iii) itaandaa maudhui ya kielekroniki kwa ngazi ya Elimu ya Msingi Darasa la I na II ili kukuza stadi za kusoma na kuandika.

Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM)

138. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kupitia Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu, itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itadahili walimu 2,515 watakaosoma kozi za Stashahada ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu na Uthibiti Ubora wa Shule ili kuwapa ujuzi na maarifa katika Usimamizi, Ufutiliaji na Tathmini katika Elimu;

(ii) itaandaa Mtaala wa Shahada ya Menejimenti na Uthibiti Ubora wa Elimu (Bachelor of Education Management and Quality Assurance) ili kuimarisha usimamizi na utoaji wa elimu bora katika ngazi zote za elimu;

(iii) itatoa mafunzo ya muda mfupi kuhusu Uthibiti Ubora wa Shule wa Ndani, Uongozi na Usimamizi wa Elimu kwa Wakuu wa shule za msingi na sekondari 14,627 ili kuwajengea uwezo wa kusimamia ufundishaji na ujifunzaji wenyewe kuleta tija katika elimu;

(iv) itafanya tafiti nne (4) kuhusu Uongozi na Usimamizi wa Elimu ili kubaini upungufu na kuandaa mafunzo wezeshi kwa wahusika;

(v) itajenga jengo la ghorofa moja (1) katika Kampasi ya Mbeya na ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 katika Kampasi ya Bagamoyo ili kuimarisha ufanisi katika shughuli za utoaji wa Mafunzo ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu; na

(vi) itawezesha watumishi 66 kushiriki mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utendaji kazi.

Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)

139. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kuititia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kisomo na Elimu kwa Umma yaani National Adult Literacy and Mass Education Rolling Strategy (NALMERS) unaolenga kupunguza kiwango cha watu wasiojua kusoma na kuandika; kwa kuwajengea uwezo maafisa na wataalamu wa kisomo na kutekeleza miradi ya kisomo inayotumia mtaala wa IPOS;

(ii) itaongeza fursa za utoaji wa Elimu ya Sekondari Nje ya Mfumo Rasmi kwa kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 14,930 hadi 15,130;

(iii) itafanya utafiti wa kitaifa kuhusu hali ya kisomo na elimu kwa umma utakaoboresha utekelezaji wa mkakati wa kisomo na elimu kwa umma;

(iv) itawezesha wasichana takribani 4,000 walioacha shule kupata elimu ya sekondari kwa njia mbadala kuititia utekelezaji wa Miradi ya Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi, ikiwemo Mradi wa Elimu ya Sekondari kwa Wasichana Walio Nje ya Mfumo Rasmi (SEOSAG), Mpango wa Elimu Changamani Baada ya Elimu ya Msingi (IPPE) na Mradi wa Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP);

(v) itaongeza udahili wa wanafunzi wa Astashahada, Stashahada na Shahada kutoka 4,766 hadi 5,200;

(vi) itajenga na kukarabati miundombinu ya ufundishaji na ujifunzaji katika vituo vya taasisi vya mikoa minne (4) ambayo ni; Dar es Salaam, Dodoma, Morogoro na Mwanza; na

(vii) itafanya utafiti wa hali ya kisomo (kujuu kusoma na kutojua kusoma) katika mikoa 10 ya Tanzania Bara kwa lengo la kupata takwimu sahihi zitakazosaidia kuweka mikakati na mipango nje ya mfumo rasmi.

Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania (BOHUMATA)

140. Mheshimiwa Spika, katika kutoa nafasi kwa umma wa watanzania kutumia maktaba zote za umma kwa ajili ya kupata taarifa sahihi na maarifa ili kujikwamua katika ujinga, umaskini na maradhi; Serikali kuititia Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania katika mwaka wa fedha 2021/22, itatekeleza yafuatayo:

(i) itaimarisha na kuinua ubora wa huduma za Maktaba katika Mikoa 22 ili kuongeza fursa za kupata taarifa na maarifa yatakayo wasaidia kujikwamua katika changamoto za kimaendeleo;

(ii) itaendelea kuhifadhi nyaraka muhimu za serikali kwa kizazi cha sasa na kijacho;

(iii) itatoa mafunzo ya ukutubi na uhifadhi nyaraka kwa wanafunzi takribani 1,000;

(iv) itatoa ushauri wa kitaalamu katika vituo 350 juu ya uanzishaji, upangaji na uendeshaji wa Maktaba za shule, Vyuo, Taasisi na Halmashauri za Jiji, Manispaa, Miji na Wilaya;

(v) itaendelea kutoa elimu kwa watumishi jinsi ya kujikinga na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi na kutoa huduma kwa watumishi wanaoishi na virusi vya Ukimwi; na

(vi) itaendelea wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu kwa kujenga Maktaba katika Chuo cha Ukutubi (SLADS); na kufanya ukarabati katika Maktaba za Tanga, Arusha, Mara na Mwanza.

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)

141. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kupitia Mamlaka ya Elimu itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itawezesha ujenzi wa madarasa 210 katika shule 70 za msingi na sekondari;
- (ii) itawezesha ujenzi wa ofisi za walimu mbili (2) katika shule mbili (2) za sekondari na ujenzi wa maabara za masomo ya sayansi katika 03 shule za sekondari;
- (iii) itawezesha ujenzi wa matundu ya vyoo 1,920 katika shule 80 za msingi na sekondari;
- (iv) itawezesha ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya wanafunzi wenyewe mahitaji maalumu katika shule 10 za msingi na sekondari;
- (v) itaanza ujenzi wa jengo la ofisi za Mamlaka ya Elimu Tanzania Dodoma katika awamu ya kwanza; na
- (vi) itatoa mkopo nafuu kwa taasisi ya Umma ya Elimu ya Juu moja (1) kwa ajili ya uendelezaji wa miundombinu ya elimu.

Kituo cha Maendeleo Dakawa

142. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kupitia Kituo cha Maendeleo Dakawa, itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itaendelea kusimamia uhifadhi wa kumbukumbu za majengo, makaburi na nyaraka za makumbusho ya wapigania uhuru wa ANC ili kutunza historia;

(ii) itaendelea kukarabati nyumba za makazi ya watumishi ili kuboresha mazingira ya kazi na kuwafanya watumishi wavutiwe kuishi katika eneo hilo; na

(iii) itaendelea kupanda miti kwa lengo la kutunza na kuhifadhi mazingira.

Uimarishaji wa Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi

143. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kupitia Idara ya Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itawezesha utoaji wa mafunzo ya muda mrefu ya Ufundu Stadi na Elimu ya Wananchi (Folk Education) kwa washiriki 15,000 katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54 ili kuwawezesha washiriki kupata ujuzi na maarifa yatakayowawezesha kujajiri au kuajiriwa na pia kuweza kuongeza thamani katika shughuli za uzalishaji wanazozifanya;

(ii) itatoa mafunzo ya muda mfupi na mafunzo nje ya Chuo kwa washiriki 24,000 kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ili kupata ujuzi utakaowawezesha kujajiri au kuajiriwa;

(iii) itaratibu mafunzo kwa Wakufunzi 150 kwenye Taasisi za Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi kwa lengo la kuwaongezea uwezo wa ufundishaji wa mitaala inayoendana na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya soko la ajira;

(iv) itawezesha usimamizi na ukaguzi wa shughuli za mafunzo katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54 ili kuhakikisha mafunzo yanayotolewa yanakidhi viwango vinavyohitajika;

(v) itawezesha upatikanaji wa vifaa vya kiufundi vya kufundishia na kujifunzia katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 54 ili kuhakikisha mafunzo yanaendana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia;

(vi) itawezesha mukutano wa kimkakati wa wadau wanne (4) katika Mafunzo ya Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi ili kuwajengea uwezo wa kusimamia na kuratibu mafunzo na uandaaji wa Mitaala ya Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi;

(vii) itafanya ufuutiliaji na tathimini ya utoaji wa Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi ili kuhakikisha ubora unazingatiwa katika Taasisi za Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi kulingana na soko la ajira na mabadiliko ya sayansi na teknolojia;

(viii) itaendelea kuratibu utekelezaji wa mradi wa East Africa Skills for Transformation and Regional Integration Project (EASTRIP) katika vituo vya umahiri vinne (4) kwenye nyanja za TEHAMA - Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, Usafiri wa anga - Chuo cha Usafirishaji cha Taifa, Nishati jadidifu - Chuo cha Ufundu Arusha na Mazao ya ngozi - Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam Kampasi ya Mwanza;

(ix) itaratibu mafunzo ya muda mfupi kwenye taaluma ya ufundishaji kwa masafa kwa wakufunzi 240 wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na VETA; na

(x) itaendelea kuratibu ujenzi wa vyuo vipyta vya ufundu stadi kwenye Wilaya ambazo hakuna vyuo ikiwemo Chuo cha Ufundu cha Dodoma (DTC) kinachojengwa kwenye eneo la Nala.

Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu Stadi (VETA)

144. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Mamlaka itaendelea kuimarisha ubora wa Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itaendelea kutoa fursa sawa katika elimu ya Mafunzo ya Ufundu Stadi nchini kwa kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 357,850 hadi takribani 500,000 ambapo wanafunzi wenyewe ulemavu 1,000 na wanaotoka katika mazingira magumu 2,400 watadahiliwa;

- (ii) itarasimisha ujuzi wa wanagenzi takribani 10,000 ambao wataongeza nguvukazi yenyé ujuzi wa kiwango cha kati;
- (iii) itaandaa na kuhuisha mitaala 10 kulingana na mahitaji ya soko la ajira na kuimisha mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za soko la ajira;
- (iv) itaanza ujenzi wa vyuo vipyta vya VETA vya mikoa mitatu (3) ya Dar es Salaam (Kampasi mpya ya Kigamboni), Simiyu na Songwe;
- (v) itaendelea na ujenzi wa vyuo vya VETA vya mikoa minne (4) ya Geita, Njombe, Rukwa na Kagera;
- (vi) itaendelea na ujenzi na ukarabati wa karakana tano (5), madarasa nane (8), mabweni sita (6), nyumba za watumishi 13, bwalo la chakula na jiko katika Vyuo vya VETA 30 vya Wilaya pamoja na kujenga jengo la Ofisi za Makao Makuu ya VETA jijini Dodoma;
- (vii) itakarabati vyuo vikongwe vya mikoa mitano (5) ya Mwanza, Dar es salaam, Dodoma, Mtwara na Tanga pamoja na kununua na kusimika mitambo na zana za mafunzo;
- (viii) itakarabati Jengo la Chuo cha Mafunzo ya TEHAMA Kipawa na majengo manne (4) ya ghorofa yaliyoko Tabata – Dar es Salaam ambayo ni makazi ya watumishi;
- (ix) itaimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma na mafunzo kwa kuunganisha vyuo 11 katika mtandao wa LAN na WAN pamoja na kuandaa mfumo wa ukusanyaji taarifa za mafunzo;
- (x) itawajengea uwezo wa kitaaluma na umahiri watumishi 110 wa Mamlaka kwa lengo la kuongeza ujuzi na ufanisi katika utendaji wa kazi; na
- (xi) itanunua magari 30 kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya VETA nchini.

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE)

145. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kuitia Baraza itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itasajili vyuo 50 ili viweze kuendesha elimu ya ufundi na mafunzo nchini kwa lengo la kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu ya ufundi nchini;
- (ii) itatoa ithibati kwa vyuo 60 vinavyotoa elimu ya ufundi na mafunzo nchini kwa lengo la kuhakikisha vyuo vinakidhi viwango vya utoaji wa Elimu ya Ufundi;
- (iii) itafanya ufuatiliaji na tathmini ya ubora wa elimu katika vyuo 200 vya Elimu ya Ufundi kwa lengo la kuangalia uzingatiaji wa sheria, kanuni na miongozo ya utoaji wa elimu ya ufundi nchini na kutoa ushauri wa namna ya kuboresha utoaji wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo;
- (iv) itaratibu na kuhakiki udahili wa Wanafunzi 159,500 katika fani mbalimbali za ngazi ya Astashahada na Stashahada;
- (v) itatoa namba ya uhakiki wa tuzo (AVN) 20,000 ambayo itasaidia kuondoa udanganyifu wa wahitimu wanaoendelea na masomo ngazi ya Elimu ya Juu. Aidha, namba hii itavirahisishia vyuo kufanya uhakiki wa wanafunzi wa Stashahada wanaoomba kujunga na Elimu ya Juu;
- (vi) itafanya ulinganifu wa tuzo 1,050 ili kudhibiti viwango vya Elimu ya Ufundi nchini;
- (vii) itahakiki mitaala 150 itakayokuzwa na Vyuo vya Ufundi kwa lengo la kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa yanakidhi soko la ajira nchini na kimataifa;
- (viii) itaendelea kutoa mafunzo ya namna ya upimaji na ufundishaji wa mitaala inayozingatia umahiri (CBET) kwa wakufunzi zaidi ya 1,000 wa Vyuo vya Elimu ya Ufundi. Mafunzo hayo yatasaidia wahitimu kuwa mahiri katika ujuzi uliokusudiwa; na

(ix) itaendelea na ujenzi wa ofisi za kanda katika mikoa ya Arusha, Mtwara, Dodoma, Mwanza, Tabora na Mbeya.

Chuo cha Ufundu Arusha (ATC)

146. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kuititia Chuo cha Ufundu Arusha itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itaongeza fursa za upatikanaji wa elimu kwa kujenga bweni la wanafunzi wa kike lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 252;

(ii) itadahili jumla ya wanafunzi 3,172 ambapo ngazi ya Stashahada (NTA Level 4) 1,327, Shahada (NTA Level 7) 400 na Mafunzo ya Ufundu Stadi (VET) 1,445;

(iii) itarahisisha ufundishaji na ujifunzaji kwa njia ya TEHAMA kwa kusimika mtandao wa ndani (LAN) katika majengo ya Chuo;

(iv) itaendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kukamilisha ujenzi wa jengo la ghorofa tatu (3) lenye madarasa, maabara na ofisi za walimu ambapo ujenzi upo katika hatua ya upauaji. Kukamilika kwa mradi huu kutaongeza udahili wa wanafunzi;

(v) itaboresha utoaji wa mafunzo, uzalishaji na ushauri wa kitaalamu kwa kununua mashine mbili (2) za kisasa katika maabara mbili (2) kwa ajili ya kupima ubora wa maji na vifaa vya ujenzi;

(vi) itaongeza udahili na kuboresha utoaji wa elimu kwa kutekeleza mradi wa EASTRIP katika Kituo cha Mafunzo cha Kikuletwa. Mradi huo unahusisha ujenzi wa mtambo wa kufua umeme kwa kutumia nguvu za maji (turbine) kwa ajili ya kutolea mafunzo, madarasa, ukumbi wa mihadhara, hosteli mbili (2), karakana tatu (3), maabara moja (1), jengo la nyumba za watumishi 10, jengo la utawala, maktaba, chumba cha usanifu, ukumbi wa mikutano, canteen na sehemu za mapumziko;

(vii) itajenga kliniki (Medical Clinic) itakayohudumia wanafunzi, wafanyakazi na wananchi wa maeneo ya jirani kwa lengo la kuboresha huduma za afya zao; na

(viii) itaendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kwa walengwa mbalimbali kwa lengo la kutoa uelewa kuhusu uimara wa udongo, kokoto na lami zinazotumika katika ujenzi wa miundombinu mbalimbali, kupima ubora wa maji, usanifu wa miradi ya maji na ujenzi wa aina mbalimbali.

Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere

147. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kupitia Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere itatekeleza yafuatayo:

(i) itaongeza udahili wa wanafunzi kutoka 11,790 katika mwaka wa masomo 2020/21 hadi wanafunzi 14,564 mwaka 2021/22. Ongezeko hilo litatokana na kuimarishwa kwa mazingira ya ufundishaji pamoja na uanzishwaji wa Tawi la Pemba na uanzishwaji wa Programu za Uzamili katika idara mbalimbali;

(ii) itapitia na kuboresha mitaala ya Chuo ili iweze kukidhi mahitaji ya soko la ajira na kujajiri;

(iii) itakarabati miundombinu chakavu ya maji, umeme, barabara na majengo ya Chuo (madarasa na nyumba 8 za watumishi), mifumo ya TEHAMA na mitambo;

(iv) itawezesha tafiti 14 na ushauri wa kitalaam katika maeneo ya Uongozi na Maadili, Sayansi za Jamii, Jinsia na Ujasiriamali. Tafiti hizo na ushauri wa kitaalam zitalenga kutafuta ufumbuzi wa changamoto mbalimbali katika jamii;

(v) itagharamia jumla ya watumishi 24 katika mafunzo ya muda mrefu na watumishi 55 katika mafunzo ya muda mfupi ili kupunguza uhaba wa wataalam na kuongeza ufanisi wa utendaji wa kazi kwa watumishi wa Chuo; na

(vi) itaongeza miundombinu kwa kutekeleza miradi sita (6) ya ujenzi ambayo ni:

- a) kuendelea na awamu ya kwanza ya ujenzi wa mabweni mawili ya wanafunzi katika Kampasi ya Karume yenyewe uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 1,536 (Wanawake: 768 Wanaume: 768);
- b) kuanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa Maktaba yenyewe uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 2,500 katika Kampasi ya Kivukoni;
- c) kujenga ukumbi wa mihadhara (Lecture Theater) wenyewe uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 1,000 katika Kampasi ya Kivukoni;
- d) kujenga jengo la utawala na ofisi za watumishi katika Kampasi ya Kivukoni;
- e) kujenga nyumba tatu (3) za ghorofa za wafanyakazi zenyewe uwezo wa kukaliwa na watumishi 30 katika Kampasi ya Karume; na
- f) kujenga madarasa na bweni la wanafunzi katika Tawi la Pemba.

Usimamizi na Uendelezaji wa Elimu ya Juu

148. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kuitia Idara ya Elimu ya Juu itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itaendelea kuratibu upatikanaji wa fursa za ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu kutoka nchi rafiki na mashirika mbalimbali nje ya nchi;
- (ii) itaendelea na ufadhili wa wanafunzi 10 raia wa China waliokubalika kimkataba kusoma Lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;
- (iii) itaendelea kufadhili wanataluma 68 katika Shahada ya Umahiri na Uzamivu kutoka Vyuo Vikuu vya Umma kusoma katika fani za Sayansi, Teknolojia, Uhndisi na Hisabati;

- (iv) itaendelea kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalum waliopo katika Taasisi za Elimu ya Juu ili kuwawezesha kusoma kwa ufanisi;
- (v) itaandaa na kuhuisha daftari la kumbukumbu la wanafunzi wanaopata ufadhilli wa masomo ndani na nje ya nchi;
- (vi) itafuatilia wahitimu waliotoka kwenye taasisi za hapa nchini kama wanaajirika kulingana na ujuzi walioupata na kushauri vyombo vya uthibiti ubora na vya kitaalam ipasavyo; na
- (vii) itaratibu na kufuatilia utekelezaji wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa ajili ya kuleta Mageuzi ya Kiuchumi Higher Education for Economic Transformation (HEET).

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU)

149. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kuitia Tume ya Vyuo Vikuu itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itakagua na kufanya tathmini ya Vyuo Vikuu 25 kwa lengo la kuhakiki ubora;
- (ii) itafanya tathmini ya programu 200 za masomo mbalimbali katika Vyuo Vikuu nchini na kuzipa ithibati kwa zitakazokidhi vigezo;
- (iii) itafanya tathmini ya tuzo 5,000 zilizotolewa katika Vyuo Vikuu vya nje ya nchi na kuzitambua zitakazokidhi vigezo;
- (iv) itaratibu udahili na kuhakiki maombi ya wanafunzi 120,000 wa mwaka wa kwanza wanaotarajiwa kuomba udahili katika vyuo vya Elimu ya Juu ili kujunga na programu mbalimbali za masomo kwa ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada ya Awali na Shahada ya Umahiri;
- (v) itavijengea uwezo Vyuo Vikuu katika masuala mbalimbali ya ithibati na uthibiti ubora ili kuimarishe ubora wa Elimu ya Juu;

- (vi) itafanya utafiti kuhusu masuala mbalimbali yenyе lengo la kufanya maboresho katika mfumo wa utoaji Elimu ya Juu nchini ili kuweza kuchukua hatua stahiki;
- (vii) itaboresha mfumo wa utoaji na ukusanyaji taarifa za Elimu ya Juu kwa kutumia TEHAMA ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wakati na matumizi yake katika kupanga mipango na kufanya maamuzi;
- (viii) itakagua Asasi/Kampuni nne (4) zinazojishughulisha na uratibu wa wanafunzi wanaokwenda kusoma nje ya nchi kwa lengo la kuzitambua na kuzisajili zile zitakazokidhi vigezo;
- (ix) itashiriki katika makongamano na mikutano inayohusu uimarishaji na Uthibiti wa Ubora wa Elimu ya Juu katika ukanda wa Afrika Mashariki na kimataifa kwa lengo la kuongeza ujuzi na weledi katika kuthibiti ubora wa Elimu ya Juu nchini; na
- (x) itaratibu maonesho ya 16 ya Elimu ya Juu nchini ili kutoa elimu kwa umma kuhusu vyuo na programu mbalimbali zitolewazo.

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB)

150. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kuititia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itaimarisha mifumo ya TEHAMA ili kuwa na mifumo rafiki itakayowezesha ukusanyaji wa **Shilingi bilioni 200**;
- (ii) itaanzisha Kituo Mahsus cha Wateja (Dedicated Customer Relations Centre) jijini Dar es Salaam ili kuboresha huduma za Bodi ya Mikopo kwa wateja hususan katika urejeshaji wa mikopo;
- (iii) itasimamia uombaji, uchambuzi na utoaji wa mikopo yenyе thamani ya **Shilingi bilioni 500** kwa wanafunzi wahitaji wapataao 148,581. Kati yao, wanafunzi 50,250 watakua wa mwaka wa kwanza na wanaoendelea na masomo 98,331;

- (iv) itakamilisha mifumo ya TEHAMA kuititia Mradi wa Maboresho ya TEHAMA wa Bodi ya Mikopo (HESLB-GASi++) itakayowezesha uunganishwaji wa mifumo ya Bodi na ya wadau ili kurahisisha ubadilishanaji wa taarifa na hivyo kuongeza ufanisi katika kuwashudumia wanafunzi, waajiri na wanufaika wa mikopo;
- (v) itakamilisha tathmini ya namna bora ya kugharimia wahitimu wenyewe ufaulu wa juu na wale wanaopata skolashipu za kusoma katika vyuo maalum nje ya nchi (Presitigious Overseas' Universities) kusomea fani mahsus (High - Impact - Degree) zinazoweza kuchochea ufanisi na kuchangia ukuaji uchumi;
- (vi) itafanya mapitio ya viashiria na ving'amuzi vya uhitaji (Means - Testing) vinavyotumika kupima uhitaji wa mikopo (neediness) kwa kuzingatia hali za kimalsha (socio - economic status) kwa lengo la kuboresha utoaji wa mikopo kwa wanufaika;
- (vii) itaandaa Mpango Mkakati wa Bodi wa Awamu ya Tano (2022/23 – 2026/27) utakaolenga kujenga uwezo wa Bodi ya Mikopo kuwa himiliyu na kuijendesha kama mfuko wa mikopo (Student Revolving Loans Fund); na
- (viii) itaendeleza na kuimarishe ushirikiano na wadau wa kimkakati ili kuwafikia waajiri na wanufaika katika mikoa na wilaya mbalimbali kwa kuendesha programu mahususi za elimu ya uombaji na urejeshaji wa mikopo.

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM)

151. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kuititia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itaongeza udahili wa wanafunzi kutoka 42,745 hadi 43,600 ambapo wanafunzi wa kike wataongezeka kutoka 19,633 hadi 20,026;

- (ii) itatoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wenyе ufaulu wa juu 60 kwenye masomo ya Sayansi hususani wanafunzi wa kike waliohitimu mitihani ya Kitaifa ya Kidato IV na Shahada za Awali;
- (iii) itaendelea kutoa ufadhili kwa wanafunzi wa kigeni wa Shahada ya Umahiri katika Lugha ya Kiswahili;
- (iv) itaongeza idadi ya miradi ya utafiti kutoka 239 hadi 289 kwa kuwafadhili watafiti 50 ili wafanye tafiti katika maeneo yanayolenga uchumi wa viwanda kwa kuzingatia Ajenda ya Utafiti ya Taifa;
- (v) itaongeza idadi ya machapisho ya Chuo katika majarida ya kitaifa na kimataifa kutoka 1,172 hadi 1,238;
- (vi) itaongeza idadi ya majarida ya Chuo ya kimataifa kutoka 11 hadi 13 na kuyafanya yafikike kwa njia ya mtandao;
- (vii) itawezesha kukamilika kwa miradi miwili ya ubunifu na yenye kuchangia katika maendeleo ya taifa;
- (viii) itagharamia wanataluma 112 kusoma masomo ya uzamili katika fani mbalimbali;
- (ix) itaendelea na upanuzi wa Bweni la Dkt. John Pombe Joseph Magufulsi kwa ghorofa mbili zaidi zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,280 hivyo kufanya bweni hilo kuchukua jumla ya wanafunzi 5,120;
- (x) itaanza ujenzi wa kumbi za mihadhara zenye uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 1,000;
- (xi) itaanza ujenzi wa maabara kuu ya kemikali ambayo itatumika kwa ajili ya utafiti na kutoa huduma za kupima sampuli za viwandani hivyo kuongeza mapato ya Chuo;
- (xii) itaanza ujenzi wa miundombinu ya Kituo cha Utafiti wa Viumbe Maji Baridi yaani Multi-Disciplinary Freshwater Research Centre Chato, Mkoani Geita;

(xiii) itaendelea na ukamilishaji wa Kituo cha Wanafunzi cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambacho kipo katika hatua za umaliziaji. Vilevile, itaweka samani katika Kituo hicho; na

(xiv) itaendelea na awamu ya kwanza ya ujenzi wa Jengo la Shule Kuu ya Uchumi.

Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE)

152. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kupitia Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itadahili wanafunzi 2,100 wa mwaka wa kwanza ambapo kati yao 600 ni wa fani ya Sayansi kwa lengo la kuongeza wataalam wa Sayansi nchini;

(ii) itagharamia mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 3,800 kwa lengo la kukazia maarifa yatolewayo kwa njia ya nadharia;

(iii) itagharamia mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi 50 na muda mrefu kwa wafanyakazi 65 (wanataluma 55 na waendeshaji 10) ili kuongeza tija na ufanisi katika kazi;

(iv) itagharamia ununuvi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum 57 pamoja na vifaa vya utafiti kwa wanataluma kwa lengo la kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji;

(v) itaandaa mitaala minne (4) mipy ya Stashahada za Uzamilli, Shahada za Awali, Umahiri na Uzamivu ili kuongeza fursa za watanzania kunufaika na Elimu ya Juu;

(vi) itafanya tafiti 20 zinazotatua matatizo ya jamii na kutoa huduma tano (5) za ushauri wa kitaalamu katika maeneo ya Elimu, Sayansi na Sayansi za Jamii;

(vii) itaendelea na awamu ya tatu ya ujenzi wa Jengo la Utawala ili kuongeza ofisi 50 za wafanyakazi na vyumba vya utafiti;

(viii) itakarabati mabweni na kumbi za mihadhara na kuimarisha miundombinu ya TEHAMA ili kuboresha miundombinu ya ufundishaji na ujifunzaji;

(ix) itanunua samani kwa ajili ya hosteli za wanafunzi 500 (NSSF Mtoni Kijichi) ili kupunguza tatizo la uhaba wa malazi kwa wanafunzi; na

(x) itaendelea na ujenzi wa madarasa kwa ajili ya wanafunzi 450 katika shule ya Msingi Mazoezi Chang'ombe na madarasa kwa ajili ya wanafunzi 920 na maabara nne (4) za sayansi katika shule ya Sekondari ya Mazoezi Chang'ombe kwa lengo la kuimarisha mafunzo kwa vitendo kwa walimu. Aidha, ujenzi huo utatoa fursa kwa wanafunzi wanaosoma katika shule hizo kufundishwa na kujifunza katika mazingira rafiki.

Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE)

153. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kupitia Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa itatekeleza yafuatayo:

(i) itaongeza udahili wa wanafunzi kutoka 6,399 hadi kufikia 6,670 kwa Shahada za Awali na Shahada za Uzamili;

(ii) itatekeleza miradi 25 ya utafiti, miradi mitatu (3) ya ushauri, kuongeza machapisho kufikia 60 na kuratibu kongamano moja (1) la kitaaluma;

(iii) itaanzisha Shahada mpya za Awali tatu (3), Umahiri tatu (3) na kununua vifaa vya TEHAMA, majarida, vifaa vya maabara, vitabu kwa lengo la kuongeza fursa za mafunzo na kuboresha ufundishaji na ujifunzaji;

(iv) itaendeleza watumishi 75 katika mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya Shahada ya Awali, Umahiri na Uzamivu;

(v) itawezesha wanataaluma 100 kusimamia mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza na wa pili ili kuimarisha ufundishaji kwa vitendo; na

(vi) itaendelea na ujenzi wa maabara ya Baiolojia na kuanza ujenzi wa maabara ya Fizikia.

Chuo Kikuu Mzumbe

154. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kuititia Chuo Kikuu Mzumbe itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itadahili wanafunzi wapya 5,355 (Astashahada 475, Stashahada 393, Shahada ya kwanza 3,973, Shahada ya Umahiri 499 na Shahada ya Uzamivu 15) kwa lengo la kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu;

(ii) itaandaa programu 15 mpya za masomo kwa lengo la kuongeza fursa za masomo;

(iii) itachapisha machapisho 35 katika majarida ya Kitaifa na Kimataifa na kuchapisha jarida la "Uongozi" la Chuo Kikuu Mzumbe kwa lengo la kuwezesha jamii kupata maarifa;

(iv) itaandaa mapendekezo 15 ya kazi za utafiti na mapendekezo 30 ya kazi za ushauri wa kitaalamu kwa lengo la kutatua changamoto zilizopo katika jamii;

(v) itafadhili masomo kwa watumishi 70 wakiwemo Shahada ya Uzamivu 60 na Shahada ya Umahiri 10;

(vi) itawezesha watumishi 48 kuhudhuria warsha, semina na makongamano ndani na nje ya nchi ili kuongeza ujuzi na ufanisi katika kazi; na

(vii) itaweka jenereta na taa za barabarani zinazotumia mwanga wa jua (solar lights) Kampasi Kuu.

155. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji, Serikali itaendelea kuboresha miundombini katika Kampasi Kuu na Ndaki ya Mbeya. Aidha, itaendelea kutekeleza shughuli mbalimbali za ujenzi na ukarabati kwa kufanya yafuatayo:

(i) itaweka samani katika hosteli za wanafunzi katika Kampasi Kuu ikiwa ni pamoja na kujenga jengo la utawala, itaendelea na ujenzi wa jengo la kumbi za mihadhara na madarasa, bwalo la chakula, kujenga mfumo wa majitaka na kuweka vifaa nya kisasa nya kudhibiti moto; na

(ii) itakarabati bwalo la chakula katika Ndaki ya Mbeya.

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA)

156. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kuititia Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo itatekeleza yafuatayo:

(i) itaongeza udahili wa wanafunzi wa mwaka wa kwanza wakiwemo wanafunzi wa Shahada za awali (Shahada, Stashahada na Astashahada) kutoka 5,499 hadi 6,000 na Shahada za Uzamili kutoka 248 hadi kufikia 275; na

(ii) itaanzisha Shahada mpya za Awali tano (5) na Shahada za Uzamili tatu (3) ili kuendana na mahitaji ya soko la ajira.

157. Mheshimiwa Spika, katika kuongeza fursa za udahili ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, Serikali itaongeza miundombinu mipyta ya kufundishia kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) itajenga na kuweka samani kwenye ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,500 katika Hosteli ya kihonda;

(ii) itajenga daharia, vibanda nya biashara, chanzo kipyta cha maji na kuboresha miundombinu ya maji, vyoo vinne (4) nya nje, benchi za zege katika kampasi ya Solomon Mahlangu pamoja na wodi katika Hospitali ya SUA;

(iii) itajenga maegesho ya magari, eneo la kuoshea magari, daharia katika kituo cha National Carbon Monitoring Centre, kuboresha miundombinu ya maji pamoja na kuanzisha shamba la mbegu na katika Kampasi ya Edward Moringe; na

(iv) itaboresha miundombinu katika Kampasi ya Mizengo Pinda kwa kujenga jengo la maabara, viwanja vya michezo, chanzo kipyä cha maji, maeneo ya kuhifadhiya mifugo kwa ajili ya mafunzo, lango kuu la kuingia chuoni, maegesho ya magari na daharia.

158. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na ukarabati mkubwa wa miundombinu ya hosteli nane (8) za wanafunzi katika Kampasi ya Edward Moringe na Kampasi ya Solomon Mahlangu. Vilevile, itakarabati nyumba za wafanyakazi, kiwanda cha chakula cha mifugo pamoja na kupanda miti katika kituo cha mafunzo Madaba na kituo cha mafunzo na Maendeleo ya Msitu wa Kitulanghalo.

159. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika kampasi zote ikiwemo kampasi ya Mizengo Pinda- Katavi kwa kuweka mfumo wa kuhutubia umma/mhadhara (PA system), projekta, kemikali na vifaa vya maabara na jukwaa la kufundishia (podium).

160. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha mafunzo kwa vitendo na kutoa huduma katika jamii, Serikali itatekeleza yafuatayo:

- (i) itaboresha Kitengo cha Uchapishaji cha SUA katika kampasi ya Edward Moringe kwa kununua na kufunga vifaa vya uchapaji;
- (ii) itaanzisha Shamba Darasa la Mfano ikiwa ni pamoja na kuboresha shamba la Nyuki katika kampasi ya Mizengo Pinda;
- (iii) itaanzisha mfumo wa chelezo (back-up system) nje ya mtandao na chumba cha kufufua data Olmotonyi;
- (iv) itaongeza uzalishaji wa malisho na kufufua kitengo cha ufugaji katika shamba la mifugo la Solomon Mahlangu. Vilevile, itafunga mita za umeme na maji katika kampasi ya Edward Moringe na Solomon Mahlangu;

(v) itaboresha bustani ya mimea katika kampasi ya Edward Moringe; na

(vi) itaongeza na kuboresha miundombinu ya TEHAMA na kutoa elimu kwa wafanyakazi katika nyanja hiyo.

Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS)

161. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kuititia Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili itatekeleza yafuatayo:

(i) itaongeza udahili wa wanafunzi wa Shahada ya Uzamivu, Shahada ya Uzamili, Shahada ya Awali na Stashahada kutoka 1,485 hadi 1,634 (ikiwa ni ongezeko la asilimia 10) ili kuongeza idadi ya wataalam katika kada ya Afya;

(ii) itaongeza udahili wa wanafunzi wa kike kutoka 486 hadi 535 (ikiwa ni ongezeko la asilimia 10) ili kuongeza uwiano wa kijinsia katika fursa za elimu;

(iii) itaboresha na kuongeza utoaji huduma katika vitengo mbalimbali vya chuo ikiwemo Shule Kuu ya Meno na kuanza matayarisho ya ujenzi wa Kliniki ya Uporoto (Uporoto Polyclinic) kwa lengo la kuimarisha mazingira ya kufundishia, kutafiti na kutoa huduma za tiba; na

(iv) itaongeza matumizi ya TEHAMA katika kufundishia na kujifunzia kutoka asilimia 50 hadi 70.

162. Mheshimiwa Spika, ili kujenga uwezo wa ndani wa kuandaa na kufanya tafiti zenyetija katika jamii pamoja na kutoa huduma za ushauri, Serikali itatekeleza yafuatayo:

(i) itaimarisha makundi ya kitafiti (Research Clusters) na kutoa mafunzo kwa viongozi wa makundi hayo ili kujenga uwezo wa ndani wa kuandaa na kufanya tafiti zenyetija katika kutatua changamoto za afya;

(ii) itaanzisha miradi mipyä miwili (2) ya tafiti na kutoa huduma tano (5) mipyä za ushauri wa kitaalamu pamoja na kuanzisha

mahuiano na wenyewe viwanda watatu (3) ili kuongeza uwezo wa kuzalisha rasilimali watu katika kada ya afya watakaoleta tija katika kuendeleza viwanda; na

(iii) itafanya kongamano la tisa (9) la kisayansi (9th MUHAS Scientific Conference) na kuendelea kufanya Kongamano za kitafiti nne (4) za ndani ya Chuo ili kusambaza matokeo ya tafiti kwa wadau ikiwemo watunga sera za afya.

163. Mheshimiwa Spika, ili kuzalisha rasilimali watu wenyewe utaalamu wa kutafiti, kutibu na kukinga magonjwa ya moyo na mishipa ya damu, Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu ya tafiti na kufundishia kwa kukamilisha kituo cha umahiri wa magonjwa ya moyo na mishipa ya damu (Center of Excellence in Cardiovascular Sciences) katika kampasi ya Mloganzila. Aidha, itaendeleza majengo ya maabara, mgahawa, hosteli, ofisi za wahadhiri na maktaba katika kampasi ya Mloganzila na kufanya ukarabati katika kituo cha kufundishia na tafiti cha Bagamoyo (Bagamoyo Training Unit).

Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM)

164. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Dodoma itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itaongeza udahili wa wanafunzi wa Shahada ya Uzamili kutoka 680 hadi 1,000 na wanafunzi wa shahada ya kwanza kutoka 28,629 hadi 35,067;

(ii) itaananza programu mpya 10 za Uzamili na 4 za Shahada ya Awali;

(iii) itaandaa machapisho 480 kwenye majarida mbalimbali na itachapisha maandiko ya kitaaluma 240 katika majarida yanayotambulika;

(iv) itawawezesha wafanyakazi 220 wa Chuo (wanataluma na waendeshaji) na wanafunzi kushiriki katika Maonesho ya Kitaifa na Kimataifa;

(v) itafanya maonesho ya wazi ya kutangaza programu za mafunzo, taratibu, ubunifu, bidhaa na huduma; na

(vi) itanunua magari matatu (3) kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Chuo.

165. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Dodoma itafanya mapitio ya ajenda ya utafiti, sera, miongozo na kanuni zake kulingana na vipaumbele vya tafiti za kitaifa na maendeleo, mapitio ya Mpango Mkakati wa Chuo, Sera ya Uwekezaji na mapitio ya programu 10 za Uzamili.

166. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha matumizi ya miundombinu ya TEHAMA, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Dodoma itatekeleza yafuatayo:

(i) itanunua **server** nne (4) za kuongeza ufanisi wa matumizi ya mifumo na kununua vifaa vya maabara;

(ii) itaweka mifumo ya kieletroniki ya kumbukumbu za wanafunzi na maktaba;

(iii) itanunua kompyuta 62 kwa ajili ya Ndaki ya Mafunzo ya Biashara na Uchumi (CoBE) na Shule Kuu ya Sheria (SoL); na

(iv) itaboresha mtandao wa kompyuta katika miundombinu ya Chuo na kuongeza upatikanaji wa intaneti katika maeneo 12 karibu na Ndaki, Shule Kuu, Taasisi na Hospitali ya Chuo.

167. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha masuala ya ufuatiliaji na tathmini, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Dodoma itafanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo na tafiti za soko la ajira.

168. Mheshimiwa Spika, katika kuongeza ufanisi wa kazi, Serikali kupitia Chuo itawajengea uwezo watumishi wa kada mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji ya Chuo ili kuboresha utendaji kazi kwa kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu

ambapo jumla ya watumishi 280 watashiriki katika mafunzo hayo.

Aidha, Serikali itatekeleza yafuatayo:

- (i) itagharamia mafunzo kwa wanataluma 100 katika Shahada za Uzamivu 85 na Umahiri 15;
- (ii) itaendesha warsha za kuwajengea uwezo viongozi wa Chuo;
- (iii) itawajengea uwezo wafanyakazi ili waweze kutoa mafunzo kwa mtandao; na
- (iv) itawawezesha watafiti 175 kushiriki katika makongamano ya kisayansi.

169. Mheshimiwa Spika, ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Dodoma itaendelea kujenga na kukarabati majengo mbalimbali kama ifuatavyo: kujenga nyumba 33 za watumishi; kujenga maabara katika Ndaki ya Sayansi Asilia na Hisabati; na kujenga geti katika lango la kuingia chuongi kutokea lyumbu. Aidha, itaendelea na ukarabati wa ukumbi wa Chimwaga pamoja na miundombinu ya majengo 34 yanayotumika katika shughuli za taaluma na utawala.

Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU)

170. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itadahili wanafunzi wapya 5,100 kati yao, wanafunzi wa Astashahada ni 1,800, Stashahada 800, Shahada za Awali 2,380 na Shahada za Uzamili 120;
- (ii) itatekeleza mradi wa kimkakati wa utafiti katika nyanja ya ushirika kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika nchini ili kuendelea kubaini na kutatua changamoto katika sekta ya ushirika;

- (iii) itachapisha machapisho 69 ya kitaaluma kwa lengo la kueneza matokeo ya tafiti kwa jamii;
- (iv) itaandaa miradi ya utafiti 20 kwa kushirikiana na taasisi na vyuo vingine ndani na nje ya nchi kwa lengo la kusambaza elimu inayokidhi mahitaji ya sasa ya jamii ili kupunguza umaskini;
- (v) itatoa na kueneza elimu ya ushirika kupitia ofisi za Chuo zilizopo katika mikoa 13 ya Tanzania ili kuchochea ari ya maendeleo ya sekta ya ushirika na jamii kwa kushirikiana na wadau wengine, hususan Wizara ya Kilimo; Tume ya Maendeleo ya Ushirika; Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika; Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania na Vyama vya Ushirika nchini na katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki;
- (vi) itafanya mapitio ya programu nne (4) za mafunzo ili ziendane na uhitaji wa soko la ajira;
- (vii) itaandaa programu mpya tatu (3) za mafunzo kwa lengo la kupanua wigo wa mafunzo hivyo kuongeza fursa ya elimu kwa Watanzania; na
- (viii) itaendelea kudhamini wafanyakazi 69 katika mafunzo ya Shahada za Uzamivu, Umahiri na Awali.

171. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, Serikali itatekeleza yafuatayo:

- (i) itanunua samani na vifaa vya kufundishia na kujifunzia ili kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji;
- (ii) itaendelea na ujenzi wa maktaba yenye uwezo wa kuchukua wasomaji 2,500 kwa wakati mmoja pamoja na ujenzi wa kumbi za mihadhara ili kuimarisha mazingira ya kufundishia na kujifunzia;

(iii) itakarabati ofisi za wafanyakazi zilizopo Kampasi Kuu ya Moshi na ofisi za Chuo za mikoani na kununua gari kwa ajili ya shughuli za uendeshaji wa Chuo; na

(iv) itaendelea na ukarabati wa nyumba za makazi zilizopo Kampasi Kuu ya Moshi, Kituo cha Kufundishia Kizumbi na ofisi za Chuo zilizopo mikoani.

Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT)

172. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kuititia Chuo Kikuu Huria cha Tanzania itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itadahili jumla ya wanafunzi 15,700 wa fani mbalimbali katika yao, wanafunzi wa Astashahada 3,000, Stashahada 3,000, Shahada ya Awali 7,000, Shahada ya Umahiri 2,500 na Shahada ya Uzamivu 200;

(ii) itafanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika maeneo mbalimbali yakiwemo mazingira, TEHAMA, nishati, kilimo na chakula, uongozi na biashara, maendeleo ya utalii, sheria, uthibiti wa ubora, utawala na maendeleo, watu wenye mahitaji maalumu, maliasili, umaskini, utamaduni, haki za binadamu, maendeleo ya watu na mawasiliano. Pia kutakuwa na tafiti mbalimbali katika lugha na fasihi;

(iii) itajenga jengo katika Kituo cha Uratibu Zanzibar litakalotumiwa kwa matumizi ya ofisi na Ukumbi wa Mitihani na ujenzi wa Kituo cha Uratibu cha Pemba; na

(iv) itakarabati majengo ya ofisi za vituo vya Mikoa ya Kagera, Mbeya, Morogoro, Shinyanga, Singida, Pwani na kituo kipyaa cha uratibu Mafia.

Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K. Nyerere cha Sayansi ya Kilimo na Teknolojia

173. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kuititia Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K. Nyerere cha Kilimo na Teknolojia itatekeleza yafuatayo:

- (i) itaandaa Mpango Kabambe (Masterplan) ya Maeneo ya Chuo ambayo Hati Miliki zimeshapatikana. Maeneo hayo ni Kinesi - Rarya (Ekari 95), Kisangura- Serengeti (Ekari 136) na Oswald Mang'ombe Butiama (Ekari 86);
- (ii) itakarabati majengo yaliyopo katika Kampasi ya Oswald Mang'ombe na kujenga bweni moja lenye kuchukua wanafuzi 400;
- (iii) itaendelea kufanya mapitio ya Mitaala 35 iliyandaliliwa mwaka 2016 kwa lengo la kuiboresha kabla ya kuiwasilisha kwa ajili ya kuidhinishwa;
- (iv) itaendesha mafunzo na kutoa huduma za ugani kwa jamii za wakulima, wafugaji, wajasiriamali, wachimbaji madini wadogo wadogo 300 walio jirani na chuo ikiwemo mkoa wa Mara;
- (v) itaandaa maandiko ya utafiti sita (6) kwa ajili ya kutafuta fedha kutoka kwa Wadau wa Maendeleo mbalimbali;
- (vi) itaanzisha na kuendeleza kozi za muda mfupi katika kilimo; biashara na ujasiriamali kwa wakulima, wafugaji, wavuvi, na wachimbaji madini wadogo wadogo na vikundi vya vijana na kinamama; pamoja na afya na usalama kwa wafanyakazi wa migodini; na
- (vii) itaendelea kupanua Mashamba Darasa kwa ajili ya mafunzo kwa wakulima.

Chuo Kikuu Ardhi (ARU)

174. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kupitia Chuo Kikuu Ardhi itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itadahili wanafunzi 5,746 wakiwamo wa Shahada ya Awali wanafunzi 5,355, Shahada ya Umahiri 288, na Shahada ya Uzamivu 103;

- (ii) itaandaa mitaala mpya mitatu (3) ya shahada ya Awali na mingine mitano (5) ya Shahada ya Umahiri ili kuongeza wigo wa mafunzo na kukidhi mahitaji ya soko la ajira;
- (iii) itafanya miradi ya tafiti 25 zinazolenga kutatua changamoto za jamii hususan katika maeneo ya matumizi bora ya ardhi, utunzaji wa mazingira, kujikinga na maafa, usimamizi bora wa ardhi, makazi na ujenzi. Aidha, itaandaa machapisho 100 katika maeneo ya usimamizi wa ardhi na mazingira, makazi na majengo;
- (iv) itatoa huduma za ushauri wa kitaalam kuhusu matumizi bora ya ardhi, upimaji na tathmini, usanifu majengo na usimamizi wa ujenzi. Vilevile, Serikali itatoa mafunzo matano (5) ya kitaalam kwa jamii (community outreach) kuhusiana na matumizi bora ya ardhi, kujikinga na majanga, kutengeneza bidhaa kwa kutumia mabaki ya mazao ya kilimo, kutunza kumbukumbu za biashara ndogondogo na utunzaji wa mazingira; na
- (v) itatoa mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi 36, ambapo tisa (9) ni wa Shahada ya Uzamivu, 20 wa Shahada ya Umahiri, wawili (2) Shahada ya kwanza, na watano (5) Stashahada.

175. Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, Serikali kupitia Chuo Kikuu Ardhi itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itaendelea na ujenzi wa bweni lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 592 pamoja na ujenzi wa Jengo la Ardhi (Lands Building) 'Wing A' na kuweka samani;
- (ii) itaendelea na ukarabati wa karakana, madarasa, maabara, mabweni ya wanafunzi na miundombinu ya barabara na TEHAMA;
- (iii) itasanifu na kuandaa michoro kwa ajili ya ujenzi wa ukumbi wa midahalo (Multipurpose Pavillion) na kuweka samani na vifaa vya TEHAMA; na

(iv) itatekeleza Mradi wa Ukarabati na Ujenzi katika Chuo Kikuu cha Ardhi kwa kuwezesha ujenzi wa maabara changamano (Multi-purpose Laboratory) pamoja na ujenzi wa hosteli ya Wanafunzi awamu ya pili.

Sayansi, Teknolojia na Ubunifu

176. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kupitia idara ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu itaendelea kuibua, kutambua, na kuendeleza ubunifu, ugunduzi na teknolojia zilizozalishwa nchini. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza yafuatayo:

- (i) itaboresha uratibu wa shughuli za Sayansi, Teknolojia na Ubunifu katika ngazi mbalimbali kwa kushirikiana na Mamlaka za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kuwafikia wabunifu na wagunduzi wachanga hususan vijiji;
- (ii) itawaibua, kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu na wagunduzi wachanga kupitia Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) ili ubunifu na ugunduzi wao uchangie kikamilifu katika ujenzi wa uchumi imara na endelevu;
- (iii) itatambua bunifu na teknolojia zinazozalishwa nchini ili zижilikane na kutumika katika kutatua changamoto mbalimbali katika jamii;
- (iv) itakamilisha uandaaji wa Mwongozo wa kuanzisha Kampuni Tanzu zinazotokana na tafiti na bunifu katika taasisi za Elimu ya Juu;
- (v) itaelimisha umma juu ya matumizi na manufaa ya Sayansi Teknolojia na Ubunifu katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii; na
- (vi) itaendelea kusimamia matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia katika sekta mbalimbali za kijamii na kiuchumi.

177. Mheshimiwa Spika, Serikali itaainisha matokeo ya utafiti unaofanywa na wataalamu katika Taasisi za Utafiti na Elimu ya Juu ili kubaini matokeo yenye manufaa ya moja kwa moja katika jamii na hivyo kuchangia kikamilifu katika ujenzi wa uchumi imara na endelevu. Aidha, itajenga uwezo wa Taasisi za Elimu na utafiti nchini ili zitumike kuhamasisha na kuendeleza ubunifu nchini kwa manufaa ya kijamii na kiuchumi.

Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH)

178. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itaendeleza mradi angalau mmoja (1) kati ya miradi ya ubunifu inayoendelea itakayofanyiwa tathmini ili kuflikia hatua ya ubiasharishaji kwa lengo la kuongeza ajira na bidhaa sokoni;
- (ii) itaandaa maandiko matatu (3) ya matokeo ya utafiti kwa lugha nyepesi na rahisi kueleweka (policy briefs) na kuzisambaza kwa wadau wakiwemo watunga sera ili kuweza kufanya maamuzi kwa kutumia matokeo ya tafiti hizo;
- (iii) itaaniszha dawati la usajili na uhawilishaji wa teknolojia kwa lengo la kubaini teknolojia zilizopo na kuimarisha matumizi ya teknolojia kutoka ndani na nje ya nchi;
- (iv) itafanya majaribio ya kituo kimoja (1) cha teknolojia cha mfano (piloting of one technological station) kwa ajili kuwekeza na kuendeleza teknolojia za ndani na kulijengea taifa uwezo wa kiteknolojia (national technological capability); na
- (v) itaaniszha Kigoda cha Utafiti (Research Chair) kimoja (1) katika taasisi itakayoshinda kukiratibu na itaendelea kuratibu vigoda viwili (2) vya Oliver Tambo vilivyoko SUA na NM - AIST. Lengo la vigoda vya utafiti ni kuweza kutengeneza mtandao wa watafiti wabobezi katika sekta za kipaumbele za afya,

kilimo, mifugo na madini. Vilevile, kuimarisha uwezo wa taasisi za utafiti; kujengea watatifiti uwezo na kuwa bobezi katika tafiti mahususi; na kuwa na utafiti ambao unachangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini na Afrika kwa ujumla.

179. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu pamoja na kuboresha mifumo ya ubunifu kwa kutekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itaendelea kugharamia miradi 17 ya utafiti na ubunifu ambapo minne (4) ni kutoka Taasisi za Maendeleo ya Utafiti na Vyuo vikuu na Miradi 13 ni kutoka katika sekta za kipaumbele;
- (ii) itaendeleza wabunifu 15 waliofikia hatua ya awali ya ubiashariashaji ili kuwawezesha kuanzisha kampuni changa za ubunifu (Innovation Startups) ambazo zitaongeza ajira na kukuza uchumi wa nchi kwa maendeleo na ushindani wa kibiashara;
- (iii) itaendeleza kumbi bunifu 10 ili kuimarisha mahusiano baina ya vyanzo vya teknolojia na wadau wengine muhimu wanaowezesha mazao ya utafiti na ubunifu kuwafikia watumiaji wa teknolojia kwa manufaa ya matumizi ya zao la ubunifu na huduma za ubunifu;
- (iv) itaboresha mfumo wa TEHAMA wa taarifa za utafiti na ubunifu ili kuleta ufanisi na kurahisisha upatikanaji wa taarifa za watafiti na wabunifu katika kushughulikia maombi ya vibali vya utafiti na ufadhilli wa miradi;
- (v) itaimarisha miundombinu ya TEHAMA kwa kuboresha mfumo wa taaifa za utafiti na ubunifu ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za watafiti na wabunifu, kupunguza muda na urasimu katika kushughulikia maombi ya vibali vya utafiti na maombi ya ufadhilli wa miradi ya ubunifu na utafiti;
- (vi) itaendelea na utekelezaji wa kazi za ubunifu kupitia mradi wa South African Innovation Support (SAIS) unaotekelizwa

katika nchi tano kusini mwa Bara la Afrika ili kuhamasisha ushirikiano, ujuzi na ubora wa ubunifu wa wabunifu nchini na katika nchi tano (5) za Bara la Afrika; na

(vii) itawezesha uanzishwaji wa kituo kimoja (1) cha umahiri (center of excellency) katika sekta ya afya hususan utafiti wa dawa asilia. Lengo ni kuwa na watafiti wabobezi katika dawa za asili kwa ajili ya kuthibitisha ubora na ufanisi wa dawa hizo kwa ajili ya matumizi ya binadamu.

180. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia COSTECH itaendelea kuandaa na kukamilisha mwongozo wa uhawilishaji wa teknolojia kupitia uwekezaji wa nje (Foreign Direct Investment - FDI) pamoja na uhakiki wa teknolojia zinazoibukia kwa lengo la kuthibitisha ubora wake, kurasimisha, kuratibu, na kulinda haki na hati miliki za wabunifu nchini.

Tume ya Nguvu za Atomiki (TAEC)

181. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kupitia Tume ya Nguvu za Atomiki (TAEC) itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itaendelea na ujenzi wa maabara changamano awamu ya pili ambayo itaboresha utoaji huduma na ufanisi katika kuendeleza teknolojia ya nyuklia;

(ii) itaendelea na ujenzi wa maabara ya Zanzibar na kanda katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Dodoma, na Mbeya;

(iii) itafanya upembuzi yakinifu kwa mradi wa kinu cha tafiti za kinyuklia (Research Reactor);

(iv) itasajili vituo vipyta vinavyotumia vyanzo vya mionzi nchini;

(v) itakusanya, kusafirisha na kuhifadhi mabaki ya vyanzo vya mionzi yasiyotumika kutoka vituo vinne (4) na kuyahifadhi katika kituo maalumu cha kuhifadhi mabaki ya mionzi (Central Radioactive Waste Management Facility- CRWMF);

(vi) itaimarisha na kupima mionzi kwenye mazingira katika vituo 40 ambavyo vimekuwa vikiendeshwa kwa ushirikiano na taasisi nyingine;

(vii) itaendelea kituo cha kupima uchafuzi wa hewa katika anga unaotokana na majaribio ya silaha za nyuklia chini ya mkataba wa kimataifa wa Comprehensive Nuclear Test-Ban Treaty (CTBT) for Non - Proliferation Test (NPT) of Nuclear Weapons; na

(viii) itafungua ofisi tatu (3) za TAEC katika Kanda na mipaka mbalimbali nchini ili kuongeza uwezo wa udhibiti mionzi na kuwashudumia wananchi.

182. Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha afya za wafanyakazi wanaotumia teknolojia ya nyuklia zinakuwa salama, Serikali kuititia TAEC itatekeleza yafuatayo:

(i) itakagua migodi saba (7) ya madini ili kubaini hali ya usalama wa mionzi kwa wafanyakazi katika migodi hiyo;

(ii) itakagua vituo 600 vyenye vyanzo vyta mionzi ili kubaini hali ya usalama wa mionzi kwa wagonjwa, wafanyakazi na umma kwa ujumla; na

(iii) itapima na kudhibiti viwango vyta mionzi kwa Wafanyakazi 1,920 wanaofanya kazi kwenye mazingira ya vyanzo vyta mionzi.

183. Mheshimiwa Spika, ili kulinda umma wa Tanzania na mazingira yake yasichafuliwe na mabaki ya vyanzo vyta mionzi, Serikali kuititia Tume ya Nguvu za Atomiki itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itapokea na kutathmini maombi 600 ya vibali vyta umiliki, utumiaji na usafirishaji wa vyanzo vyta mionzi ili kuhakikisha usalama wa wananchi; na

(ii) itakagua vituo 120 vinavyotoa mionzi isiyoayonisha (Non - Ionizing Radiation) kama vile minara ya simu, redio, runinga

na vifaa vingine vyatia mionzi ili kubaini usalama wa wakazi wa maeneo husika.

184. Mheshimiwa Spika, katika kuongeza thamani ya mazao na kuchochea uchumi wa viwanda, Serikali kupitia TAEC itaendelea na utekelezaji wa mradi wa kuhifadhi mazao ya kilimo ikiwemo vyakula viharibikavyo kirahisi, vifaa tiba na vyatia viwandani kwa kutumia teknolojia ya mionzi.

Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT)

185. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kupitia Taasisi ya Teknolojia Kampasi Kuu ya Dar es Salaam itatekeleza yafuatayo:

- (i) itadahili wanafunzi wapya 2,865 na hivyo kuwa na jumla ya wanafunzi 6,612;
- (ii) itawajengea uwezo watumishi 300 wa taasisi na kuongeza viwango vyatia ubora katika ufundishaji na utawala (ISO Certification) kupitia mradi wa EASTRIP;
- (iii) itaandaa mitaala mipyta mitatu (3) na itaboresha mitaala nane (8) kwa lengo la kuzalisha wataalam wenye ujuzi unaohitajika katika soko la ajira kupitia mradi wa EASTRIP;
- (iv) itajenga mabweni mawili (2) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 na jengo la kituo cha kikanda cha umahiri wa TEHAMA kwa ufadhili wa mradi wa EASTRIP;
- (v) itakarabati miundombinu ya kufundishia, mitambo na mabweni;
- (vi) itaendeleza dhana ya elimu ya ufundishaji viwandani (teaching factory) itakayowawezesha wahitimu katika kila ngazi kutoka na ujuzi na maarifa yatakayowawezesha kuajiriwa na kujajiri;
- (vii) itasimika miundombinu ya TEHAMA katika jengo la Teaching Tower Complex; na

(viii) itaendelea kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 643 wanaodhaminiwa na Serikali.

186. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kupitia Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam Kampasi ya Mwanza itatekeleza yafuatayo;

(i) itadahili wanafunzi wapya 240 na hivyo kuwa na jumla ya wanafunzi 326;

(ii) itajenga mabweni mawili (2) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 600 na jengo la kituo cha umahiri wa uchakataji ngozi kupitia fedha za mradi wa EASTRIP;

(iii) itaanzisha mitaala miwili (2) na kuboresha mtaala mmoja (1) katika programu ya ngozi chini ya mradi wa EASTRIP;

(iv) itaendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi katika teknolojia ya ngozi kwa wanafunzi 250; na

(v) itaendelea kuwezesha mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi 80 wanaodhaminiwa na Serikali.

187. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kupitia Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam Kampasi ya Myunga itatekeleza kazi zifuatazo;

(i) itadahili wanafunzi wapya 68 na hivyo kuwa na jumla ya wanafunzi 83;

(ii) itajenga miundombinu ya kufundishia ikiwemo madarasa matano (5) na mabweni mawili (2) yenye uwezo wa kubeba wanafunzi 160;

(iii) itaanzisha na kuendeleza programu mbili (2) za mafunzo ya ufundi stadi;

(iv) itaanzisha programu ya stashahada ya uhandisi ujenzi; na

(v) itaendelea kutoa mafunzo ya ufundi ya muda mfupi kwa wanafunzi 33 kwa kushirikiana na VETA.

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST)

188. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itaongeza udahili wa wanafunzi kutoka wanafunzi 6,817 kwa mwaka wa masomo 2020/21 hadi wanafunzi 8,000 ili kuongeza upatikanaji wa rasilimaliwatu inayokidhi mahitaji ya soko la ajira;
- (ii) itanunua vifaa vyta kisasa vya maabara na karakana ili kuboresha utoaji wa mafunzo katika fani mbalimbali za sayansi na teknolojia na hivyo kuendana na mabadiliko ya teknolojia duniani;
- (iii) itafanya tafiti zinazolenga kuongeza ubunifu na kuendelea kutoa ushauri elekezi katika nyanja za Sayansi na Teknolojia ili kuchochaea ukuaji wa uchumi wa viwanda na hivyo kuongeza kasi ya maendeleo katika jamii;
- (iv) itaendeleza ushirikiano na Hanze University of Applied Sciences (Netherlands) na MATI Uyole ili kuboresha mnyororo wa thamani wa zao la viazi na hivyo kuboresha kilimo cha zao hilo;
- (v) itakamilisha ujenzi wa Hosteli mbili (2) za wanafunzi zitakazokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja;
- (vi) itaendelea na ujenzi wa jengo la madarasa la Ndaki ya Usanifu na Teknolojia ya Majengo;
- (vii) itakamilisha ujenzi wa jengo la maktaba awamu ya pili lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja ili kukidhi mahitaji ya huduma bora za maktaba kwa wanafunzi na wahadhiri;

(viii) itaendelea kuongeza matumizi ya nishati juu ili kupunguza ghamama za umeme katika kuendesha shughuli za Chuo;

(ix) itaimarisha Kituo cha Teknolojia Vijiji ni katika Kampasi ya Rukwa ili kuchochaea matumizi ya teknolojia stahiki (appropriate technology) katika maeneo ya vijiji; na

(x) itaendelea kufanya ukarabati wa miundombinu ya majengo ya madarasa, hosteli na nyumba za watumishi.

Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika ya Nelson Mandela (NM-AIST)

189. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kuititia Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika ya Nelson Mandela itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itadahili wanafunzi wapya 140 (Shahada ya Uzamili 110 na Shahada ya Uzamivu 30); na

(ii) itaimarisha mahusiano na wadau wa kimataifa kwa kuongeza idadi ya washirika kutoka 39 hadi 43, kwa washirika wa kanda ya Afrika Mashariki kutoka 42 hadi 44 na kwa washirika wa ndani ya nchi kutoka 23 hadi 26. Lengo ni kukuza ushirikiano katika tafiti mbalimbali zinazolenga kutatua changamoto katika jamii.

190. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza miradi ya maendeleo, Serikali kuititia Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika ya Nelson Mandela itaendelea na ujenzi wa bweni la wanafunzi litakalokuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 500. Aidha, itaongeza uwezo wa ofisi katika uendeshaji kwa kutumia TEHAMA zaidi kwa kuongeza vitendea kazi mbalimbali.

191. Mheshimiwa Spika, katika kazi za utafiti na ubunifu kwa mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kuititia Taasisi ya Afrika ya Nelson Mandela ya Sayansi na Teknolojia itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itaendelea na miradi 24 ya utafiti na ubunifu kwa kufadhili wanafunzi na kulipa għarama za utafiti kwa wanafunzi na wanataaluma ili kuendelea na kuzalisha bunifu mbalimbali;
- (ii) itaratibu shughuli za ubiasharishaji wa bunifu nne (4) kwenda hatua ya atamizi;
- (iii) itaanzisha viwanda vidogo vidogo viwili (2) "Container-Based Factory" ambavyo vitatumiwa na wabunifu kuzalisha bidhaa zinazotokana na bunifu zao. Viwanda hivyo vyā mfano pia vitasaidia kuvutia wawkezajji watakaojenga viwanda vikubwa; na
- (iv) itaendelea na utekelejji wa shughuli za kigoda cha utafti cha Oliva Tambo

Usimamizi wa Rasilimali za Wizara

192. Mheshimiwa Spika, katika kusimamia Rasilimali za Wizara katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali itatekeleza yafuatayó:

- (i) itafanya ukaguzi wa taratibu za ununuzi na usimamizi wa Mikataba inayotekelezwa na Wizara ikiwemo mikataba ya Ujenzi na ukarabati;
- (ii) itafanya ukaguzi wa matumizi ya fedha za Wizara Makao Makuu ya Wizara;
- (iii) itakagua matumizi ya fedha katika Taasisi za Wizara; na
- (iv) itaendelea na ukaguzi wa ukusanyajji wa maduhuli na matumizi katika Taasisi za Wizara.

193. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kuitipia idara ya Usimamizi na Uendelezajji wa Rasilimaliwateru itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itaendelea na ujenzi wa jengo kuu la ofisi za Wizara Mtumba -Dodoma kulingana na miqongozo na maelekezo ya Serikali; na

(ii) itakamilisha usimikaji wa Mfumo wa mawasiliano wa Kielektroniki (Eoffice) wa kupokea, kutunza na kusambaza nyaraka za ofisi kwa lengo la kuleta ufanisi, kupunguza gharama na kuongeza kasi ya mawasiliano katika ofisi.

194. Mheshimiwa Spika, katika kuleta ufanisi na weledi kwa watumishi, Serikali itaendelea kufanya mapitio na utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo wa Wizara pamoja na kuratibu mafunzo ya muda mrefu na mfupi yakiwemo: Mafunzo Elekezi; kujenga uelewa juu ya uzingatiaji viwango vya ubora katika utekelezaji wa Mkataba wa Huduma kwa Mteja Wizarani Makao Makuu; katika Vyuo vya Ualimu; Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi; na Ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule; UKIMWI na magonjwa sugu yasiyoambukizwa; na Utumiaji wa Mfumo wa Wazi wa Mapitio ya Tathmini ya Utendaji Kazi (Open Performance Review and Apraissal System – OPRAS). Aidha, itaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wanaokaribia kustaafu ili kuijandaa na maisha baada ya kustaafu.

Uendelezaji na Uboreshaji wa Sera, Sheria na Miongozo ya Elimu

195. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali itaendelea kuendeleza na kuboresha Sera, Sheria na Miongozo ya Elimu kama ifuatavyo:

(i) itatoa ushauri wa kisheria kuhusu sera, nyaraka, miongozo na mikakati ya sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia;

(ii) itaandaa na kuwasilisha katika ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali masuala ya madai, usuluhishi au jinai yanayohusu Wizara;

(iii) itaandaa na kuwasilisha katika ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali maandalizi ya miswada ya sheria, mapendekezo ya marekebisho ya sheria na kanuni zinazoihusu sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia hususani marekebisho ya Sheria ya Elimu, Sura ya 353;

(iv) itaendelea kuimarisha ushirikiano na wadau wa maendeleo wa Sekta ya Elimu ikiwa ni pamoja na Sekta Binafsi kwa lengo la kuboresha utoaji wa elimu nchini; na

(v) itatangaza kwenye Gazeti la Serikali sheria, kanuni na taratibu zilizohuishwa za taasisi zote za Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na kushauri kufanyiwa marekebishio au kuandaliwa upya pale inapohitajika ili kukidhi mahitaji ya taasisi husika.

USIMAMIZI NA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYO CHINI YA WIZARA

196. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kupitia Wizara itatekeleza miradi ifuatavyo:

Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu (Education Programme for Results – EP4R)

197. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu (EP4R) kwa mwaka 2021/22 itatekeleza shughuli zifuatazo:

(i) itakamilisha ujenzi wa Hosteli mpya katika Chuo Kikuu cha Mzumbe na kununua samani;

(ii) itaendelea kuwezesha ujenzi wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili - Kampasi ya Mloganzila;

(iii) itaimarisha Mfumo wa Wizara wa Education Management Information System (EMIS) kwa kuhuisa zana za kukusanya takwimu na viashiria vya mfumo pamoja na kuunganisha mifumo ya sub – sector;

(iv) itafanya ufuutiliaji na tathmini ya kazi za ujenzi na ukarabati katika ngazi ya Mikoa na Halmashauri kwa lengo la kuhakiki ubora na thamani ya fedha;

(v) itaendelea kuwezesha mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 68 wa Vyuo Vikuu;

(vi) itaendelea na ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Mfano Dodoma;

(vii) itawezesha ujenzi wa chumba cha mihadhara chenye uwezo wa kuchukuwa wanafunzi 500 kwa wakati mmoja katika Wakala wa Maendeleo ya Menejimenti ya Elimu - ADEM;

(viii) itanunua magari 25 kwa ajili ya Ofisi 25 za Uthibiti Ubora wa Shule katika halmashauri ili kuimarisha utendaji wa shughuli za uthibiti ubora wa shule na vyuo vya ualimu;

(ix) itaendelea na ujenzi wa Vyuo vya Ualimu ambavyo ni Sumbawanga, Mhonda na Dakawa vinavyojengwa upya; na

(x) itawezesha ujenzi wa Ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule tano (5) katika Halmashauri za Njombe TC, Tarime DC, Bunda DC, Temeke MC na Ubungo MC.

Mradi wa Elimu na Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi (Education and Skills for Productive Jobs - ESPJ)

198. Mheshimiwa Spika, Mradi wa Elimu na Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi (ESPJ) unatakelezwa kwa utaratibu wa Lipa Kulingana na Matokeo - Payment for Results (P4R). Katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kupitia Mradi huu itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itawezesha kujenga uwezo wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 53 na Vyuo vya Ufundji Stadi 39 kupitia mafunzo ya ujuzi yanayolenga kuongeza ufanisi katika kuendeleza Sekta sita za kipaumbele ambazo ni: Kilimo Biashara, Utalii na Ukarimu, Nishati, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano;

(ii) itaendelea kutoa ufadhili wa mafunzo ya ujuzi kwa vijana, wanawake na wajane wanaoishi katika mazingira magumu kupitia Mpango wa Bursary Scheme;

- (iii) itawezesha mafunzo ya wanagenzi- wahandisi walio katika mfumo rasmi wapatao 2,000 na wanagenzi walio katika mfumo usio rasmi wapatao 4,000;
- (iv) itawezesha ununuvi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia vinavyoendana na mahitaji ya Mkakati wa Kitaifa wa Kuendeleza Ujuzi katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 53 na Vyuo vya Ufundi Stadi 39; na
- (v) itaanza ujenzi wa Chuo cha Ufundi cha Dodoma.

Mradi wa Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) – Mradi wa Kuimarisha Ufundishaji na ujifunzaji kwa Elimu ya Awali na Msingi (GPE – LANES II)

199. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mradi wa Kuimarisha Ufundishaji na Ujifunzaji kwa Shule za Msingi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 itatekeleza kazi zifuatazo :

- (i) itawezesha uchapaji na usambazaji wa vitabu 6,755,428 vya Kiada na Kiongozi cha Mwalimu kwa masomo yote kwa darasa la VI na VII pamoja na vitabu vya kiada vya nyongeza 6,386,535 kwa masomo yote ya darasa la I na II;
- (ii) itawezesha uchapaji na usambazaji wa vitabu vya ziada 10,644,224 kwa wanafunzi wa darasa la I na II;
- (iii) itawezesha Upimaji Kitaifa wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa wanafunzi wa Darasa la pili na kuandaa, kuchapa na kusambaza vitabu vya uchambuzi wa matokeo ya upimaji na mitihani kwa mwaka 2021 (Pupils' Item Response Analysis - PIRA: Standard Two National Assessment – STNA; Standari Four National Assessment - SFNA; na Primary School Leaving Examination - PSLE;
- (iv) itawezesha Wathibiti Ubora wa Shule kufanya Tathmini ya Jumla ya Shule kwa shule za msingi 2,550;
- (v) itawezesha Wathibiti Ubora wa Shule kufanya vikao vya tathmini ili kuimarisha Mfumo wa Uthibiti Ubora wa Shule;

(vi) itawezesha uandaaji wa maudhui ya kielektroniki ya ufundishaji na ujifunzaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK);

(vii) itawezesha mafunzo ya Usimamizi na Uendeshaji wa Vituo vya Walimu (Teachers resources Centers - TRC) kwa Waratibu wa Vituo, Maafisa Elimu Kata 966, Wathibiti Ubora wa Shule, Maafisa Elimu Mikoa 26 na Halmashauri 184;

(viii) itawezesha mafunzo kazini kupitia Vituo vya Walimu (TRC) kwa Walimu wa Elimu ya Awali, Msingi, Wawezeshaji wa MEMKWA na Walimu wa Elimu Maalum;

(ix) itawezesha uchapishaji na usambazaji wa nakala 2,000 za Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu 2021/22-2025/26 pamoja na kutoa mafunzo kwa Maafisa Elimu 26 wa Mikoa na 184 wa Halmashauri kuhusu uandaaji wa mipango ya Elimu kwa kuzingatia Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Elimu (ESDP) na Kufanya Ufutiliaji na Tathmini; na

(x) itawezesha mafunzo kwa Walimu Wakuu 8,288, Maafisa Elimu Kata 3,945 na Wathibiti Ubora wa Shule 1,626 kuhusu usimamizi wa Shule kwa kuzingatia Kiunzi kipyaa cha Uthibiti Ubora wa Shule.

Mradi wa Kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu (TESP)

200. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2021/22 Wizara kupitia Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Ualimu (Teacher Education Support Programme - TESP) itatekeleza yafuatayo:

(i) itawezesha ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia vikiwemo vifaa vya maabara na vivunge vya sayansi kwa ajili ya Vyuo vya Ualimu 31 vya Serikali ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji;

(ii) itawezesha ununuzi wa vitabu vya kiada vya shule za Msingi na Sekondari kwa ajili ya Vyuo vya Ualimu 35 vya Serikali;

- (iii) itawezesha ukarabati na ununuzi wa samani katika Maabara za Sayansi, Maabara za ICT na Maktaba katika Vyuo vya Ualimu 7;
- (iv) itawezesha mafunzo kuhusu majukumu na usimamizi wa vyuo kwa Wajumbe wa Bodi za Vyuo vya Ualimu 35 vya Serikali ili kuimarisha utendaji;
- (v) itawezesha mafunzo kazini kwa Walimu wa shule za Msingi na Sekondari wa somo la Hisabati katika Halmashauri 20 zenyе ufaulu wa chini katika somo hilo;
- (vi) itawezesha uanzishwaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Usahihishaji (E-MaS) wa Mtihani wa Elimu ya Ualimu;
- (vii) itaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa Chuo cha Ualimu Kabanga kwa kuimarisha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji;
- (viii) itawezesha Mafunzo kuhusu mbinu za ufundishaji na ujifunzaji kwa Wakufunzi 400 wa masomo ya Sayansi na Hisabati; wakufunzi 170 wa masomo ya Biashara, Kilimo, Development Studies, Physical Education na Fine Art; wakufunzi 482 wa masomo ya lugha pamoja na Elimu ya Awali, Malezi na Makuzi ya Mtoto; na wakufunzi 338 wa masomo ya Historia na Jiografia; na
- (ix) itawezesha uunganishaji wa Vyuo vya Ualimu katika Mtandao wa Optical Fibre.

Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu (UTC)

201. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2021/22 Wizara kuititia Mradi wa Ukarabati wa Shule na Vyuo itatekeleza yafuatayo:

- (i) itakamilisha ujenzi na ukarabati wa Vyuo vya Ualimu vinne (4) (Kitangali, Mpuguso, Ndala na Shinyanga); na

(ii) itawezesha ununuzi wa vifaa vya maabara kwa ajili ya Vyuo vya Ualimu vya Kitangali, Mpuguso, Ndala na Shinyanga ili kuimarishe ufundishaji na ujifunzaji.

Mradi wa Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni

202. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kuititia mradi wa Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni itatekeleza yafuatayo:

(i) itawezesha ujenzi wa vyoo na miundombinu ya maji katika Shule za Msingi 675 ili kuboresha mazingira ya shule;

(ii) itafanya tathmini ya utekelezaji wa mradi kulingana kiashiria namba 4 (Disbursement Linked Indicator - DLI 4) kinachohusu Usafi wa Mazingira Shuleni katika Shule za Msingi 675 zitakazojengewa vyoo na miundombinu ya maji ili kubaini hali ya utekelezaji; na

(iii) itawezesha ununuzi wa magari matatu (3) ili kuimarishe ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mradi.

Mradi wa Kuimarishe Ubora Elimu ya Sekondari - SEQUIP

203. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2021/22 Wizara kuititia Mradi wa Kuimarishe Ubora wa Elimu ya Sekondari (Secondary Education Quality Improvement Programme - SEQUIP)

(i) itawezesha Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kuchapisha na kusambaza miongozo na moduli 5,000 kwa ajili ya kutoa Elimu kwa njia mbadala – Alternative Education Pathway – AEP;

(ii) itawezesha ujenzi wa vituo vipyta 12 vya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima na upanuzi na ukarabati wa vituo 10 vitakavyotumika kutoa Elimu kwa Njia Mbadala;

- (iii) itawezesha Taasisi ya Elimu Tanzania kuchapa na kusambaza vitabu na Kiongozi cha Mwalimu kwa masomo ya Sayansi na Hisabati kwa kidato cha 1 - 4;
- (iv) itaandaa mwongozo kwa ajili ya kufanya tathmini ya upimaji wa kwa Elimu ya Sekondari;
- (v) itatoa mafunzo kwa wakuu wa shule na walimu 3,600 kutoka katika shule za Sekondari za umma kuhusu ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia jinsia na mazingira rafiki kupitia Programu ya Shule Salama;
- (vi) itawezesha mafunzo kazini kwa walimu 5,000 wa masomo ya Sayansi na Hisabati, 3,600 wa somo la English na walimu 1,000 kuhusu matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji;
- (vii) itawezesha kuanza ujenzi wa shule za sekondari za wasichana 10 kati ya shule 26 zinazotarajiwa kujengwa ndani ya muda wa utekelezaji wa mradi ambapo kila mkoa utajengewa shule moja (1) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi wasichana 1,500 kwa lengo la kuongeza fursa za upatikajinaji wa elimu ya sekondari kwa wasichana;
- (viii) itaandaa mkakati wa upatikanaji wa walimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati; na
- (ix) itanunua magari saba (7) ili kuimarisha usimamimizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mradi.

Mradi wa Kujenga Ujuzi Afrika Mashariki - East Africa Skills for Transformation and Regional Integration Project (EASTRIP)

204. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kupitia Mradi wa Kujenga Ujuzi Afrika Mashariki - EASTRIP itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itaendelea kuwezesha ujenzi wa vituo vyta umahiri katika Chuo cha Ufundi Arusha, Taasisi ya Teknolojia kampasi ya Dar

es Salaam na Mwanza, na Taasisi ya Taifa ya Usafirishaji katika Nyanja za nishati, usindikaji wa ngozi, uchukuzi na TEHAMA;

(ii) itawezesha uandaaji wa miongozo ya mitaala ya Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi;

(iii) itaunda Mfumo wa Kuvileta pamoja Vyuo vya Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi, Taasisi za Usimamizi wa Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi, na Viwanda (Tripple Helix System) kwa lengo la kuhakikisha kuwa teknolojia mpya na sehemu za kujifunza kwa vitendo wanafunzi vinapatikana;

(iv) itawezesha uidhinishaji wa mitaala 100 ya EASTRIP, National Qualification Framework - NTQF, na mpango wa kitaifa wa ujuzi wa kidigitali;

(v) itapitia na kuidhinisha viwango vya kazi vya Mradi wa EASTRIP kwa sekta za kipaumbele (nishati, usindikaji wa ngozi, uchukuzi na TEHAMA); na

(vi) itawezesha maonesho na mashindano ya ufundu na ujuzi kwa mwaka 2021/22.

Mradi 4296: Mradi wa TANZIS (Tanzania Innovation Systems)

205. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kupitia Mradi wa TANZIS itatekeleza kazi zifuatazo:

(i) itawezesha kuibua, kutambua na kuwaendeleza wabunifu wachanga 70 kutoka katika Vyuo Vikuu, Vyuo vya Ufundu, Vyuo vya Kati vya Mafunzo ya Ufundu Stadi, Shule za Msingi na Sekondari, vituo vya kuendeleza teknolojia pamoja na Taasisi za Utafiti;

(ii) itawezesha vituo vya kuendeleza teknolojia na ubunifu pamoja na Taasisi za Utafiti kuendeleza teknolojia na bunifu zilizoibuliwa; na

(iii) itawezesha utoaji wa vifaa kwa wabunifu, ujuzi na maarifa pamoja na kusaidia ubiasharishaji wa bunifu na teknolojia katika masoko ili kuimarisha mazingira ya uvumbuzi.

Mradi 4315: Kuendeleza Elimu ya Juu kwa ajili ya Mageuzi ya Kiuchumi (Higher Education for Economic Transformation Project - HEET)

206. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Serikali kupitia Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Juu kwa ajili ya Maendeleo ya Uchumi itatekeleza kazi zifuatazo:

- (i) itawezesha ujenzi na ukarabati wa Miundombinu katika Taasisi 17 za Elimu ya Juu;
- (ii) itawezesha ununuzi wa Magari matano (5) kwa ajili ya kuimarisha ufuutiliaji wa utekelezaji wa mradi; na
- (iii) itawajengea uwezo watumishi 170 wa Taasisi za Elimu ya Juu, watumishi 100 wa Wizara Makao Makuu, watumishi 110 wa Wizara ya Fedha na Mipango Makao Makuu pamoja na wanataluma wa Taasisi Tano (5) zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuwaendeleza kitaaluma na kitaalamu.

TUME YA TAIFA YA UNESCO (FUNGU 18)

207. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/22, Tume ya Taifa ya UNESCO ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itatekeleza kazi zifuatazo;

- (i) itahamasisha upatikanaji wa elimu bora kwa wote kwa kujenga utamaduni endelevu wa kujifunza;
- (ii) itasimamia utekelezaji wa Programu na miradi mbalimbali iliyopitishwa katika mpango wa kimataifa wa UNESCO;
- (iii) itashirikisha wadau katika fursa mbalimbali zinazotokana na uanachama wa Nchi yetu katika shirika la UNESCO;

- (iv) itatoa mafunzo ya uelewa kwa masuala ya UKIMWI na Rushwa katika mazingira ya kazi;
- (v) itaimarisha mazingira ya utendaji kazi kwa kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi na upatikanaji vitendea kazi;
- (vi) itashiriki kwa niaba ya Serikali katika kupanga, kutekeleza na kutathmini shughuli za UNESCO zinazotekelizwa kwa ufadhili wa mashirika mengine ya Umoja wa Mataifa; na
- (vii) itapokea taarifa za utekelezaji wa shughuli na miradi yote ya UNESCO iliyotekelizwa hapa nchini, itazipitia na kuandaa na kuwasilisha taarifa ya nchi katika UNESCO.

D. SHUKRANI

208. Mheshimiwa Spika, napenda kutambua mchango mkubwa wa viongozi wenzangu katika kutekeleza na kufanikisha majukumu ya Wizara yangu. Kipekee kabisa namshukuru Mheshimiwa Omari Juma Kipanga (Mb), Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ushirikiano mkubwa anaonipa katika kusimamia Wizara hii. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu, Dkt. Leonard Douglas Akwilapo, Naibu Katibu Mkuu Profesa James Epiphan Mdoe, Naibu Katibu Mkuu Profesa Carolyne Nombo, Kamishna wa Elimu, Wakurugenzi, Wakuu wa Idara na Vitengo, na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara kwa ushirikiano wao wa karibu katika kusimamia na kutekeleza majukumu ya kila siku ya Wizara.

209. Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru viongozi wa vyama vyaya wafanyakazi, Watumishi wa Wizara na Taasisi zake, Walimu, Wanafunzi na Wadau wote Elimu kwa ushirikiano wao. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wamiliki wa Shule, Vyuo na Taasisi Binafsi ambao wamekuwa wakishirikiana na Serikali katika utoaji wa elimu hapa nchini.

210. Mheshimiwa Spika, Nawashukuru sana wananchi wa Kasulu Mjini kwa kuniamini na kunichagua kwa kura nyingi sana ili niwe mwakilishi wao. Nawaahidi utumishi uliotukuka.

211. Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Washirika wa Maendeleo na Wadau wa Elimu wote ambao wamechangia kufanikisha utekelezaji wa Mipango na Miradi ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Naomba kuwatambua baadhi yao kama ifuatavyo: Serikali za: Algeria, Austria, Brazil, Canada, China, Cuba, Finland, Hungary, India, Indonesia, Italia, Israel, Japan, Korea ya Kusini, Malta, Marekani, Malaysia, Misri, Morocco, Netherland, New Zealand, Norway, Palestine, Romania, Saudi Arabia, Sweden, Thailand, Ufaransa, Urusi, Uswisi, Uingereza, Uholanzi, Ujerumani na Venezuela. Aidha, natambua pia mchango wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika.

212. Mheshimiwa Spika, napenda pia kuyashukuru mashirika ya kitaifa na kimataifa yaliyochangia kufanikisha miradi na programu za Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo ni pamoja na; Benki ya Dunia, Foreign, Commonwealth and Development Office (FCDO), Swedish International Development Agency (SIDA), Umoja wa Nchi za Ulaya, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Jumuiya ya Madola, Global Partnership in Education (GPE), United Nations International Children's Emergency Fund (UNICEF), United Nations Development Programme (UNDP), United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization (UNESCO), USAID, Inter University Council for East Africa (IUCEA), Human Development Innovation Fund (HDIF), Deutscher Akademischer Austauschdienst (DAAD), British Council, Campaign for Female Education (CAMFED), Commonwealth Secretariat, Aga Khan Education Services, Japan International Cooperation Agency (JICA), Karibu Tanzania Organization (KTO), Korea International Cooperation Agency (KOICA), WaterAid, Plan International, Tanzania Education Network/Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET), Christian Social Services Commission (CSSC) na Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA).

E. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2021/22

213. Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha utekelezaji wa malengo kwa mwaka wa fedha 2021/22, Wizara ya Elimu, Sayansi na

Teknolojia (Fungu 46) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,384,414,801,000.00** kwa mchanganuo ufuatao:

(i) **Shilingi 480,474,878,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya kawaida ya Wizara ambapo **Shilingi 447,214,694,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 33,260,184,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo; na

(ii) **Shilingi 903,939,923,000.00** zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi 706,639,923,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 197,300,000,000.00** fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

214. Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya UNESCO (Fungu 18) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,679,073,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Mishahara ni **Shilingi 1,146,780,000** na Matumizi Mengineyo ni **Shilingi 1,532,293,000.00**).

215. Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa naomba sasa Bunge lako tukufu likubali kupokea, kujadili na kuitisha Makadirio ya Bajeti ya Mafungu yote mawili (Fungu 46 na Fungu 18) yenye jumla ya **Shilingi 1,387,093,874,000.00**.

216. Mheshimiwa Spika, napenda kuhitimisha kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

217. Mheshimiwa Spika, Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni <http://www.moe.go.tz>.

218. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:
Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa lamuliwe)

SPIKA: Hoja imetolewa na kwa kweli imeungwa mkono, tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu,

Sayansi na Teknolojia kwa matumizi mazuri ya muda na kwa kuwasilisha hoja ambayo imeeleweka vizuri sana kwa Waheshimiwa Wabunge wote. Hotuba nzima Waheshimiwa ipo kwenye vishkwambi vyetu, natumaini mmeionna na hotuba inayofuata ya Kamati pia imo katika *tablets* zetu.

Nitoe matangazo mawili, tunao wageni pia ni Dkt. Daniel Baheta ambaye *Chief Education* kule UNICEF, ni Mwenyekiti wa DPS. Pia yupo Madam Emmaculata Tibaihana ambaye yupo kwenye Sekretarieti ya mambo ya Waziri huko; tunatambua uwepo wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Anna Lupembe anawaomba wale waumini ambao huwa wanafanya ibada basi wakutane kwenye ukumbi wao wa kawaida wa ibada saa saba mchana mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge waweze kuungana na wanamaombi wengi kabisa walliokuja leo kwa ajili ya ibada.

Waheshimiwa Wabunge, moja kwa moja namuita Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii. Anakuja Mwenyekiti mwenyewe Mheshimiwa Haroon karibu sana.

MHE. STANSLAUS H. NYONGO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII: Mheshimiwa Spika, ifuatayo ni taarifa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kuhusu makadirio na mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kukushukuru kwa kunipa fursa hii, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio

ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, Naomba taarifa yote ya Kamati iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 17(1) ya Kanuni ya Kudumu ya Bunge, Toleo la Juni, 2020 Kamati ilipaswa kufanya au kuchambua bajeti na kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha wa 2020/2021. Hata hivyo, kufuatia kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Kamati ilikatisha ziara katika Mkoa wa Arusha na hivyo haikuweza kukagua miradi licha ya kwamba tayari ilikuwa imekwisha kupokea taarifa zake mapema.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2020/2021. Vilevile ilifanya uchambuzi wa utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kati ya maoni, ushauri na mapendekezo saba yaliyotolewa na Kamati yapo baadhi ya mambo hayajatekelezwa kikamilifu. Kamati itaendelea kuyasisitiza tena masuala hayo kwenye taarifa hii ambayo naisoma leo.

Mheshimiwa Spika, tulifanya uchambuzi kuhusu ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Katika mwaka huo wa fedha Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Fungu Na.46 ilijiwekea malengo ya kukusanya maduhuli yenye thamani ya shilingi bilioni 555.6 na kufikia Februari, 2021 wizara ilikuwa imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 307.2 ambayo ni sawa na asilimia 55.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati iliangalia upatikanaji wa fedha kutoka Hazina mwaka 2020/2021. Wizara kupitia Fungu Na. 46 katika mwaka wa fedha huo ilidhinishiwa na Bunge lako Tukufu bajeti ya shilingi triliioni 1.34. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 491 sawa na asilimia 36.4

zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 857.5 sawa na asilimia 63.6 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kufikia Februari, 2021, Wizara iliweza kupokea jumla ya shilingi bilioni 690.2 sawa na asilimia 51 ya bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo, shilingi 351.4 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambayo ni sawa na asilimia 71.2 ya Matumizi ya Kawaida yaliyoidhinishwa na shilingi bilioni 336.7 ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo sawa na asilimia 39.5 ya bajeti yote ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tume ya UNESCO yenyе Fungu Na.18, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, iliyodhinishwa na Bunge lako Tukufu jumla ya shilingi bilioni 2.2. Kufikia Februari 2021, kiasi cha bilioni 1.2 sawa na asilimia 54.4 ya bajeti iliyodhinishwa kilikuwa kimepokelewa kama inavyoonekana katika vielelezo tulivyoitao.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati ilifanya uchambuzi wa mpango wa makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka wa fedha 2021/2022. Uchambuzi wa Makadirio wa makusanyo ya maduhuli kwa mwaka huo Wizara kuitia Fungu 46 katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 imekadiria kukusanya maduhuli ya shilingi bilioni 530.9. Kamati imefanya uchambuzi wake na kubaini kuwa makadirio ya makusanyo kwa mwaka 2021/2022 yameshuka kwa asilimia 2.6 ukilinganisha na mwaka 2020/2021 kama inavyoonekana kwenye taarifa yetu. Kamati ilihoji sababu zilizopelekea makadirio na makusanyo kushuka ilielezwa kuwa ni kutokana na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (*FDCs*) kuruhusiwa kubakia na kiasi cha fedha za makusanyo yaani retention na hivyo zimetolewa zisionekane kwenye maduhuli au orodha ya maduhuri.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa makadirio na matumizi ya kawaida ya miradi ya maendeleo kwa mwaka 2021/2022. Katika eneo hili Kamati imefanya uchambuzi wa aina mbili; uchambuzi wa kwanza ni wa bajeti ya Wizara yenye kwa maana ya Fungu Na. 46 na Na. 18. Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara inaomba kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu jumla ya shilingi trilioni 1.38. Kati ya fedha

hizo, Matumizi ya Kawaida yanaombewa ni shilingi bilioni 480 ambayo ni sawa na asilimia 34.7 na fedha ya miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 903.9 sawa na asilimia 65.4 kama inavyoonekana katika vielelezo tulivyovitoo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa bajeti kwa Fungu Na. 46 imeongezeka kwa asilimia 2.7 na ongezeko zaidi ni kwenye fedha za maendeleo na hasa katika Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Kamati inapongeza Serikali kwa kuendelea kuongeza bajeti na kutenga fedha zake za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo na hususan katika Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Nchini ili kuwezesha wanafunzi wengi kupata mikopo hiyo. Pamoja na ongezeko hili, Kamati imebaini pia upungufu wa fedha za Matumizi Mengineyo yaani *OC* kwa takribani asilimia 54.1.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilihoji sababu za kupungua kwa bajeti hiyo na nini athari zake na ilielezwa kuwa, upungufu huu unatokana na kuhamishwa kwa tengeo la bajeti ya uendeshaji wa mitihani kutoka fungu la Matumizi Mengineyo kiasi cha shilingi bilioni 40 kwenda katika fungu la maendeleo. Kielelezo Na.6 kinaonesha ulinganisho wa bajeti ya Fungu Na. 46 kwa mwaka 2020/2021 na 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tume ya UNESCO, Fungu namba 18, katika mwaka wa fedha 2021/2022, imekadiria kutumia shilingi bilioni 2.2. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa bajeti ya mwaka huu ya Tume imeongezeka kwa asilimia 0.70 kutokana na ongezeko la mishahara kwa ajira mpya kama inavyoonekana kwenye kielelezo ambapo Kamati imeongoosea Serikali kwa kuendelea kuona umuhimu wa kuongeza watumishi katika Tume hii.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi mwingine tuliofanya ni uchambuzi wa bajeti wa Fungu Namba 46 kwa kulinganisha na Mpango wa Maendeleo wa Taifa. Kamati ilifanya uchambuzi kulinganisha bajeti ya Fungu Namba 46 dhidi ya bajeti ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2021 kwa lengo la kubaini masuala mbalimbali ikiwemo asilimia

ya bajeti ya Wizara katika Mpango huo yaani Bajeti ya Taifa kati ya mwaka 2020/2021 na 2021/2022 na pia kuona ni kwa kiasi gani ongezeko au upungufu wa bajeti hiyo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaathiri vipi mwendeno wa bejeti ya Fungu Namba 46.

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi huo, Kamati imebaini masuala mbalimbali ikionekana kwenye kielelezo ambacho tumekitoa. Cha kwanza, bajeti Fungu Na. 46 kwa mwaka 2021/2022 ni asilimia 3.82 ya bejeti yote ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa. Bajeti hii imeshuka kutoka asilimia 3.87 ya mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, cha pili, ni bajeti ya mishahara ya Fungu Na. 46 dhidi ya bajeti ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa, imeongezeka kutoka asilimia 5.39 kwa mwaka 2020/2021 hadi asilimia 5.49 ya 2021/2022. Tatu, ni bajeti ya Maendeleo ya Fungu 46 dhidi ya bajeti ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa imeongezeka kutoka asilimia 6.6 kwa mwaka 2020/2021 hadi asilimia 6.82 mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, cha tano, ilikuwa wakati wa bajeti, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/2022 ikiwa imeongezeka kwa asilimia 3.95 kutoka shilingi trillioni 34.8 mwaka 2021 hadi shilingi trillioni 36.235 mwaka 2021/2022. Bajeti ya Fungu Na. 46 imeongezeka kwa asilimia 5.6 kutoka shilingi trillioni 1.34 mwaka 2020/2021 hadi trillioni 1.38 mwaka 2021/2022, wakati bajeti ya mishahara ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa ikiwa imeongezeka kwa 5% mwaka 2021/2022 ikilinganishwa na 2021, bajeti ya mishahara kwa Fungu 46 imeongezeka kwa asilimia 6.8 na wakati bajeti ya Maendeleo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa imeongezeka kwa asilimia 2.76; na bajeti ya Maendeleo ya Fungu hili la 46 imeongezeka kwa asilimia 5.4.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla ulinganisho huu unatupa tafsiri kuwa bajeti ya Fungu hili Na. 46 imekuwa ni sehemu ya kipaumbele ukilinganisha na ongezeko katika bajeti ya Taifa ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kama ilivyoonekana kwenye kielelezo ambacho tumekitoa.

Mheshimiwa Spika, Kamati katika sehemu ya tatu ya Taarifa hii, tumetoa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati. Kutokana na uchambuzi huo na yale yaliyobainika, Kamati imetoa maoni, ushauri na mapendekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, moja, jambo la kwanza ni uhaba wa walimu na watumishi. Changamoto ya uhaba wa watumishi katika Sekta ya Elimu bado ni kubwa. Kamati inafahamu Vyuo Vikuu na vyuo vingine vina changamoto ya Wahadhiri. Siyo hivyo tu, pia shule nyingi zina upungufu wa walimu, hasa walimu wa sekondari wa masomo ya sayansi, jambo ambalo linachangia kuathiri ubora wa elimu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mahatma Gandhi amewahi kusema; *I have always felt that the true textbook for the pupil is his teacher.*" Yaani kitabu kizuri kwa wanafunzi ni mwalimu mwenyewe. Kutokana na umuhimu huo wa walimu, Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Serikali na hususan Utumishi itoe vibali kwa ajili ya kuajiri watumishi wa sekta hii waweze kuajiriwa ili kuondoa upungufu uliopo katika shule za msingi, sekondari, vyuo vyote nchini na kipaumbele kitolewe kwa walimu wale wanaojitolea;

(b) Kwa Vyuo Vikuu, utaratibu uliokuwa unatumika zamani wa kuwabakiza wanafunzi wanaofanya vizuri ili wawe wakufunzi wasaidizi (*tutorial assistants*) uanzé kutumika ili kupunguza au kuondoa pengo hili la walimu au wakufunzi au wahadhiri wa vyuo hivyo.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni mfumo wa elimu. Dira, dhima na malengo ya Sera yetu ya Elimu ya Mafunzo ya mwaka 2014 inasema kuwa, msingi wa elimu na mafunzo utajikita katika kumjengea Mtanzania misingi bora ya malezi, maadili, ujuzi, umahiri na kumwezesha kujitegemea. Elimu ya kujitegemea itaendelea kuongoza utoaji wa elimu na mafunzo kwa kuzingatia mabadiliko yanayotokea katika jamii kisiasa, kiuchumi, kisayansi na kiteknolojia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mwongozo mzuri wa sera hii, Kamati inaona mfumo wetu wa elimu bado hauendani na sera yetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashukuru sana na inamshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Sauluhu Hassan kwa kuona changamoto hii pia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, Kamati inaona bado kuna kazi ya kufanya katika mfumo wetu wa elimu. Mwanazuoni MC, Arora M, katika jarida lake la *Journey of Life Continued*, amewahi kusema; “*education can bring the desired change in the future. If you want to shape the future, shape the education system accordingly.*” Kama tunataka kubadilisha au kuwa na *future* nzuri ya kielimu, lazima tubadilishe mfumo wetu wa elimu. Hivyo basi, Kamati inashauri yafuatayo:-

(a) Serikali iandae mpango wa kukuza ujuzi nchini (*skills development plan*) ili kuwezesha wanafunzi kupata stadi mbalimbali za kazi ambazo zitawasaidia kujajiri na hivyo kusaidia kukua kwa uchumi wa nchi yetu;

(b) Kwa kuwa nchi yetu ipo kwenye uchumi wa kati ambao ni uchumi wa viwanda, hivyo basi kuna kila sababu ya kuhakikisha elimu yetu inaendana na sera hii kwa kuzalisha mafundi sanifu na sadifu ambao ndiyo watendaji wa kazi na kuboresha *course zao*, yaani tutoe zile *full technician certificate*;

(c) Serikali ianzé kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaochaguliwa kujunga kwenye vyuo vingine vilivyo chini ya *NACTE*. Wanafunzi hao ambao wengi wao wanatoka katika familia duni, mara baada ya kuhitimu masomo yao ndio watakuwa watendaji kazi hususan katika muktadha wa Tanzania ya Viwanda. Hii itasaidia kuzalisha wataalam wengi zaidi ambao ndiyo nguvukazi katika uchumi wa viwanda; (*Makofi*)

(d) Mpango wa kujenga vyuo vya VETA katika kila wilaya usimamiwe vizuri ili kila wilaya iwe na Chuo cha VETA; na

(e) Serikali iandae mjadala mpana wa Kitaifa ambao utashirikisha wadau wote wa elimu, lengo likiwa ni kupata suluhu ya kujuu ni elimu ipi na wakati gani inayofaa kutolewa kwa watoto wetu wa Kitanzania na Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, suala lingine tumeliona ni mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu. Kamati inaipongeza Serikali kutokana na manufaa yanayopatikana tangu kuanza kutolewa kwa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu nchini, kwani bajeti ya idadi ya wanufaika imekuwa ikiongezekwa mwaka hadi mwaka jambo ambalo ni jema sana.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kamati imebaini kuwa malalamiko yamekuwa ni mengi kutokana na baadhi ya wanafunzi kutoka katika familia masikini kushindwa kupata mikopo hiyo na pia kutokana na tozo nyngi ambazo zimekuwa zikitozwa kwa wanufaika hao wa mikopo.

Kamati inampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa uamuzi wake wa kuondoa tozo ya kutunza thamani ya fedha (*retention*), tozo hiyo ambayo ni asilimia sita. Hakika Rais anastahili pongezi ya hali ya juu. Pamoja na hayo, kamati vile vile inaendelea kutoa ushauri ufuata:-

(a) Wizara iandae tena vigezo vinavyotumika katika utoaji wa mikopo na kuhakikisha wanafunzi wote wanaostahili kupata mikopo hiyo hasa wale wanaotoka katika familia masikini waweze kunufaika na kupata mikopo hiyo.

(b) Serikali iendelee kuangalia tozo na makato mengine ya adhabu ya asilimia 10 ambayo inatozwa kwa mwanafunzi anayechelewa kurejesha mkopo baada ya miaka miwili ya kuhitimu masomo hayo.

Mheshimiwa Spika, hatukuona ni kwa nini wameweka miaka miwili kwa sababu suala la kukosa ajira ni tatizo kubwa, hivyo basi, hiyo tozo ya asilimia 10 waiangalie upya.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni tozo ya udhamini. Kamati inaendelea kusisitiza, ushauri ambaao umekuwa ukitolewa na Kamati iliyopita ya kuanzisha tuzo ya udhamini kwa wanafunzi wanaomaliza kidato cha sita na kuwa na ufaulu wa juu, Wizara imeeleza kuwa imeanza mchakato wa kutoa tuzo hizo kwa wanafunzi hapa nchini wanaoenda Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza jitihada hizo lakini inaona bado kuna hoja ya kupeleka vijana wetu nje ya nchi hasa wale wanaofaulu vizuri masomo ya sayansi ili kujifunza zaidi kwa kutumia utaratibu wa tuzo iliyopendekezwa na Kamati. Vijana hawa watakuwa na msaada mkubwa kwa Taifa na ikizingatiwa tuko katika uchumi wa kati ambaao unachochewa zaidi na ukuaji wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine tumeliona ni kuhusiana na Chuo cha Ufundı cha Arusha. Pamoja na kazi kubwa ambayo Chuo cha Ufundı Arusha imekuwa ikifanya, bado inakumbana na changamoto ya miundombinu chakavu na isiyotosheleza mahitaji. Bunge lako Tukufu limekuwa likiidhinisha fedha kwa ajili ya chuo hiki, lakini fedha hizo zimekuwa haziendi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Chuo kilitengewa jumla ya shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa bweni ambalo litasaidia katika kuongeza udahili wa wanafunzi wa kike ambaao wengi wamekuwa wakishindwa kujunga na chuo hicho kutokana na ukosefu wa malazi. Hata hivyo, fedha hizo bado hazijatoka mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri, Serikali iangalie chuo hiki kwa jicho la pekee na kuhakikisha inatoa fedha hizo ili wanafunzi wa kike waweze kujunga na chuo hiki kwa wingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, vile vile tumeangalia kuhusiana na bajeti ya Tume ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*). Tume ya Sayansi na Teknolojia ndiyo chombo pekee kwa kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu masuala yote yanayohusu utafiti wa sayansi na teknolojia. *COSTECH* imekuwa ikigharamia tafiti za kisayansi na kuboresha mazingira ya utafiti ikiwemo miundombinu na vitendea kazi. Nchi yetu ikiwa kwenye uchumi wa kati, uchumi wa viwanda na masuala ya utafiti na ubunifu yanapaswa kupewa kipaumbele cha kipekee kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa *UNESCO Institute of Statistics*, ili kufikia ukuaji wa uchumi endelevu na utekelezaji wa lengo la 9.5 na malengo ya Maendeleo Endelevu (*SDG's*) kuimarisha utafiti wa kisayansi, kuboresha uwezo wa kiteknolojia wa Sekta ya Viwanda katika nchi zetu hasa nchi zinazoendelea ni jambo la msingi sana. Wakati Umoja wa Ulaya wameweka lengo la nchi wanachama ziwe zinatenga asilimia tatu ya pato lake la Taifa kwa ajili ya utafiti ifikapo 2020, Umoja wa Afrika umeweka lengo la 1% tu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, taarifa ya *UNESCO Institute of Statistics* inaonesha kuwa nchi nne tu za Kusini mwa jangwa la Sahara ndiyo ziko karibu na lengo hili ambazo ni Afrika ya Kusini, Kenya, Burkina Faso na Rwanda. Wao wametenga kati ya asilimia 0.8 hadi 0.7.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa utafiti katika maendeo ya nchi yetu, Kamati inashauri, bajeti ya *COSTECH* iongezwe na itolewe yote kwani katika mwaka wa fedha 2021/2022 ni shilingi bilioni 3.8 tu ndiyo zimetengwa kwa ajili ya Mfuko wa Utafiti wa Maendeleo (*Research and Development Fund*). Kiasi hicho ambacho ni kidogo, tunaomba kitolewe chote kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu miundombinu ya elimu ya juu. Mojawapo ya changamoto katika Taasisi ya Eelimu ya Juu nchini ni uhitaji mkubwa wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu pamoja na vifaa vyatia kisasa vyatia kufundishia au kujifunzia. Kamati inashauri Serikali

itenge bajeti ya kutosha kuwezesha ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya taasisi hizo na ununuzi wa vifaa vyta kisasa vyta kufundisha na kujifunzia. Aidha, fedha hizo zinazotengwa ziende zote kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la Idara ya Udhibiti Ubora. Idara ya Udhibiti Ubora wa Shule ni idara muhimu katika sekta ya elimu hasa ukizingatia kuwa ndiyo wenyewe jukumu la kuhakikisha shule zetu zinatoa elimu yenyewe ubora unaotakiwa, wenyewe kuzingatia utekelezaji na mitaala ipasavyo. Ili kutekeleza majukumu haya kikamilifu na kwa ufanisi, bajeti ya kutosha ni jambo la msingi. Hata hivyo, idara hii imekuwa haitengewi fedha za kutosha kufanya kazi zake. Kamati inashauri bajeti ya kutosha itengwe kwa ajili ya idara hii, watendaji waweze kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni muundo wa Wizara hii. Kamati imebaini kuwa muundo wa sasa wa Wizara haumpi majukumu ya kitaalam moja kwa moja Kamishna wa Elimu nchini. Kamati inashauri Serikali ipitie upya muundo wa Wizara hii ya Elimu hususan majukumu ya Kamishna wa Elimu ili kumwezesha Kamishna kuwa msimamizi wa idara zote za kitaalam au za kitaaluma na hivyo kupunguza mzigo wa usimamizi huu ngazi nyingine na vile vile kuzingatia ubora wa majukumu haya.

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kusema, nakushukuru tena kwa nafasi uliyonipa na kuweza kuwasilisha taarifa hii ya kwanza ya Kamati yetu mbele ya Bunge lako Tukufu. Kipekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa imani walijonipa na kunichagua kuwa Mwenyekiti wa Kamati. Aidha, namshukuru sana Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakinipa na zaidi katika kushiriki vyema katika Vikao vyta Kamati ikiwemo uchambuzi wa bajeti wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, pia naomba majina yao yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge. Napenda kukushukuru wewe

na Naibu Spika kwa kuendelea kuongoza vyema Bunge letu. Hakika ninyi ni viongozi wa mfano kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Profesa Joyce Lazaro Ndalichako, Mbunge; Naibu Waziri Omari Juma Kipanga, Mbunge; Makatibu Wakuu wa Wizara wakiongozwa na Dkt. Leonard Akwilapo; Katibu Mkuu Profesa James Mdoe; Naibu Katibu Mkuu, Profesa Caroline Nombo; Naibu Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakinipa au wakiipa Kamati wakati wote pamoja na kushirikiana vyema katika vikao vya uchambuzi wa bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Katibu, Ndugu Stephen Kagaigai kwa ushirikiano ambao amekuwa akiipa Kamati yetu katika kutekeleza majukumu yetu. Napenda pia kumshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Kamati yetu Ndugu Gerald Magili, Msaidizi wa Kamati, Ndugu Jane Ndulesi na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake bila vikwazo.

Mheshimiwa Spika, kipekee niwashukuru sana Makatibu wa Kamati yetu, Ndugu Pamela Pallangyo na Ndugu Nyamwanja Chilemeji kwa kuendelea kuishauri vyema Kamati kuhakikisha majukumu yake yanatekelezwa bila vikwazo ikiwemo kuhakikisha taarifa hii inakamilika wakati wote.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, baada ya maelezo haya, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Fungu Namba 46 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya shilingi trilioni 1.38 na Fungu Na. 18 jumla ya shilingi billioni 2.2.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. (*Makofii*)

**TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI YA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA KWA MWAKA
WA FEDHA 2020/2021 PAMOJA NA MAONI, USHAURI NA
MAPENDEKEZO YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO
NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA
2021/2022 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kukushukuru kwa kunipa fursa ili kwa mujibu wa Kanuni ya 108 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu na Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, Mojawapo ya Majukumu ya Kamati hii kama zilivyo Kamati nyingine za Kisekta ni pamoja na kushughulikia Bajeti ya Wizara inazozisimamia [Nyongeza ya Nane (7) (1) (a) iliyochini ya Kanuni ya 137 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020]. Kamati ya Huduma na Manedeleo ya Jamii katika vikao vyake vilivyofanyika Mwezi Machi, 2021 hapa Dodoma, ilichambua na kujadili bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kama ilivyoainishwa kwenye Kanuni za Kudumu za Bunge. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020 Kamati ilipaswa kabla ya kuchambua Bajeti, kukagua Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha wa 2020/2021 kwa lengo la kuona hatua ya utekelezaji wa miradi hiyo ili kuwa katika nafasi nzuri ya kuweza kuishauri Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipanga kukagua Miradi mitatu iliyochini ya Wizara hii ambayo ipo katika Mkoa wa Arusha.

Miradi hiyo ni pamoja na Mradi wa ujenzi wa jengo la Tume ya Nguvu za Atomiki; Mradi wa Ujenzi wa Bweni katika Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknoloja ya Nelson Mandela (NM-AIST); na Mradi wa Ujenzi wa Bweni katika Chuo cha Ufundis Arusha. Hata hivyo, kufuatia kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Kamati ilikatisha ziara katika Mkoa wa Arusha na hivyo haikuweza kukagua miradi hiyo licha ya kwamba tayari ilikuwa imepokea Taarifa zake mapema.

1.1 MUUNDO WA TAARIFA

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii ya Kamati imegawanyika katika maeneo makuu yafuatayo:-

- a) Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti na Maoni ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021;
- b) Uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022; na
- c) Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

Mheshimiwa Spika, Katika vikao vya Kamati vilivyofanyika Mwezi Machi, 2020 hapa Dodoma, Kamati ilichambua na kujadili Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na kutoa Moani, Ushauri na Mapendekezo mbalimbali kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara. Taarifa ya Utekelezaji huo kama ilivyochambuliwa na Kamati ni kama ifuatavyo;-

2.1 UTEKELEZAJI WA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA 2020/2021

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni mnamo tarehe 29 Aprili 2020 kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, ilijumuisha pamoja na mambo mengine Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati yapatayo saba (7). Kamati ilipokea Taarifa ya utekelezaji wa maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati lakini bado iliona kuwa kuna baadhi ya maoni hayajatekelezwa kikamilifu. Baadhi ya maoni, ushauri na mapendekezo ambayo Kamati bado iliona hayajatekelezwa kikamilifu ni pamoja na Mfumo wa Elimu nchini, Uhaba wa Watumishi, Tuzo ya udhamini pamoja na Uhaba na uchakavu wa miundombinu. Kamati itaendelea kuyasisitiza tena masuala haya kwenye Taarifa hili.

2.2 UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021


Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia **kupitia Fungu 46** ilijiwekea malengo ya kukusanya Maduhuli yenye thamani ya **Shilingi 555,651,650,346.52**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 15,459,750,000.00** zilikadiriwa kukusanywa kutoka vyanzo vya Idara na Vitengo na **Shilingi 540,191,900,346.52** kutoka katika Taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijulishwa kuwa, kufikia tarehe 28 Februari 2021, Wizara ilikuwa imefanikiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 307,254,682,022.00** sawa na **asilimia 55** ya makadirio. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kati ya kiasi hiko kilichokusanya, **Shilingi 5,493,239,388.80** zilikusanywa na Idara na Vitengo sawa na **asilimia 35.5** ya makadirio na **Shilingi 301,761,442,634.00** zilikusanywa na Taasisi zilizo chini ya Wizara sawa na **asilimia 55.9** ya lengo kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 1.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa kina na kubaini kuwa, baadhi ya vyanzo hasa vilivyopo chini ya Wizara ukusanyaji wake ni chini ya **asilimia 50**. Kwa mfano baadhi ya Vyuo Vikuu makusanyo yao ni chini ya **asilimia 50** kama vile Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (**37%**), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (**36%**) na Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (**32%**). Kamati ilihoji sababu za makusanyo haya madogo na ilielezwa kuwa, chanzo kikubwa cha mapato ya vyuo hivi ni ada za wanafunzi ambazo kwa kiasi kikubwa zinallipwa na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Na kwa utaratibu huo, fedha hizi huwa zinatoka Muhula wa Pili ambaao unaanza mwezi Aprili. Hivyo basi, Kamati ilihakikishiwa kuwa makadirio hayo ya makusanyo yatafikiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini pia kuwa, Taasisi ya Elimu Tanzania makadirio ya makusanyo yalikuwa **Shilingi Milioni 950**, lakini kufikia Februari 2021 makusanyo yallkuwa yamefikia **Shilingi Bilioni 3.66** sawa na **asilimia 386**. Kamati ilipongeza makusanyo haya makubwa lakini pia ilihoji sababu za makusanyo kuzidi makadirio, ambapo ilielezwa kuwa, ni kutokana na juhudhi ambazo Taasisi imezifanya za kuwaelimisha wamiliki wa shule binafsi kuhusu umuhimu wa kutumia vitabu vya kiada vinavyoandikwa na Taasisi ya Elimu Tanzania hatua ambayo imeongeza sana mauzo ya vitabu. **Kamati inapongeza sana Taasisi ya Elimu Tanzania kwa kuendelea kuwa wabunifu. Aidha, Kamati inaendelea kusisitiza Wizara kuweka makadirio ya maduhuli ya uhakika na uhalisia.**

Kielelezo Na.1



Chanzo: Randama Fungu 46 (Machi 2021) na Usanifu wa Kamati

2.3 UPATIKANAJI WA FEDHA KUTOKA HAZINA MWAKA 2020/2021

Mheshimiwa Spika, Wizara kuititia **Fungu 46**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu bajeti ya **Shilingi 1,348,563,375,000.00** kwa ajili ya kuwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake na miradi mbalimbali ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 491,049,151,000.00** sawa na **asilimia 36.4** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 857,514,224,000.00** sawa na **asilimia 63.6** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa kufikia tarehe 28 Februari 2021, Wizara ilikuwa imepokea Jumla ya **Shilingi 690,223,909,576.81** sawa na **asilimia 51** ya bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 351,473,408,966.04** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambayo ni sawa na **asilimia 71.2** ya Matumizi ya Kawaida yaliyoidhinishwa na **Shilingi 338,750,500,610.77** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo sawa na **asilimia 39.5** ya bajeti yote ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wake na kubaini kuwa, kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida

zilizopokelewa, **Shilingi 276,940,905,503.55** ni kwa ajili ya mishahara sawa na **asilimia 66.1** ya bajeti ya Mishahara (PE) na **Shilingi 74,532,503,462.49** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) sawa na **asilimia 103** ya bajeti ya Matumizi Mengineyo. Kwa upande wa Fedha za Miradi ya Maendeleo, kiasi cha **Shilingi 338,750,500,610.77** kimepokelewa kwa mfumo wa *exchequersawa* na **asilimia 40** ya bajeti yote ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 293,934,186,848.53** ni fedha za ndani sawa na **asilimia 48** na **Shilingi 44,816,313,762.24** ni fedha za nje sawa na **asilimia 17** kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.2.


Mheshimiwa Spika, Kamati ilihoji sababu za fedha za matumizi mengineyo kupokelewa kwa **asilimia 103** kwani kwa wastani inakadirisha upatikanaji wa fedha kufikia Februari uwe ni **asilimia 66.6** na ilielezwa kuwa, ni kutokana na Serikali kuanza kulipa madeni ya Wahadhiri, Wazabuni na Watumishi wa Wizara. **Kamati inapongeza Wizara na Serikali kwa ujumla kwa hatua hii kwani kilikuwa kilio cha muda mrefu cha Kamati.** Aidha, Kamati inashauri Wizara ijtahidi kusiwepo na malimbikizo ya madeni ambayo yamekuwa yakishusha morali ya watumishi hawa katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, Kamati haikuishia hapo, ilifanya uchambuzi wa fedha za Miradi ya Maendeleo na hususan fedha za nje na kubaini kuwa, kiasi kilichopokelewa ni **asilimia 17 tu**. Kamati ilihoji sababu ya upatikanaji huu mdogo wa fedha na namna ulivyoathiri utekelezaji wa miradi na ilielezwa kuwa, Wizara imepokea fedha za nje kwa **asilimia 94** ambayo ni zaidi ya asilimia inayooneshwa kwenye Taarifa (**asilimia 17**). Ilielezwa kuwa, tofauti hiyo inatokana na kutumia utaratibu wa Dfund ambapo uhuishaji wake wa kihasibu bado unaendelea na taarifa sahihi za miradi hii hujumuishwa kwenye taarifa ya Wizara baada ya taratibu za kihasibu kukamilika. Hivyo, jumla ya **Shilingi Bilioni 191** zimeshatolewa kuititia mfumo huo kwa miradi miwili ambayo ni Mradi ya Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo - *Education Programme for Results – EP4R* (**Shilingi Bilioni 162**) na Mradi wa Kukuza Stadi za Kazi Kwa Ajili ya Shughuli za Kuzalisha na

Kukuza Uchumi -Education and Skills for Productive Job –ESPJ (Shilingi Bilioni 28).

Kielelezo Na.2

UPATIKANAJI WA FEDHA FUNGU 46 MWAKA 2020/2021				
MATUMIZI		KILICHOIDHINISHWA	KILICHOPKELEWA	ASILIMA
KAWAIDA	MSAHARA	418,711,372,325.00	276,940,905,503.55	66.1
	OC	72,337,778,675.00	74,532,503,462.49	103.03
	JUMLA	491,049,151,000.00	351,473,408,966.04	71.6
MAENDELEO	NDANI	606,715,000,000.00	293,934,186,848.53	48.45
	NJE	250,799,224,000.00	44,816,313,762.24	17.87
	JUMLA	857,514,224,000.00	338,750,500,610.77	39.50
JUMLA BAJETI		1,348,563,375,000.00	690,223,909,576.81	51.2



Chanzo: Randama Fungu 46 (Machi 2021) na Usanifu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tume ya UNESCO yenye **Fungu 18**, katika Mwaka wa Fedha 2020/2021, ilidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 2,239,181,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 706,888,000** sawa na **asilimia 31.6** ya bajeti ni kwa ajili ya Mishahara ya watumishi wa Tume na **Shilingi 1,532,293,000** sawa na **asilimia 68.4** ni kwa ajili ya Matumizi ya Mengineyo ya Tume. Hadi kufikia Februari 2021, kiasi cha **Shilingi 1,218,876,333.28** sawa na **asilimia 54.4** ya bajeti

Iliyoidhinishwa kilikuwa kimepokelewa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 350,681,000** sawa na **asilimia 49.6** ya bajeti ya Mishahara ilikuwa imepokelewa na **Shilingi 868,195,333.28** sawa na **asilimia 56.7** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo nayo ilikuwa imepokelewa kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.3.

Kielelezo Na.3 UPATIKANAJI WA FEDHA (FUNGU 18) 2020/2021



Chanzo: Randama Fungu 18 (Machi 2021) na Usanifu wa Kamati

SEHEMU YA TATU

3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 imojiwekea malengo mbalimbali kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Taifa (2025), Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2020/21 -2025/26); lakini pia llani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 na Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Elimu 2015/16 2020/21). Baadhi ya ¹malengo ambayo Wizara imojiwekea ni pamoa na kuongeza fursa na

¹ Randama ya Bajeti ya Mapato, Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2021/22

ubora wa elimu na mafunzo katika ngazi zote; kuratibu na kuimarisha maendeleo ya tafiti na bunifu kwa ajili ya kukuza uchumi wa jamii na maendeleo ya viwanda na kuimarisha mazingira ya kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika utoaji wa huduma. Ili kuweza kutekeleza malengo haya pamoja na majukumu yake mbalimbali, Wizara iliyasilisha mbele ya Kamati, Randama yake yenye kuonyesha Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli na Matumizi kwa lengo la kuchambuliwa na kujadiliwa na Kamati. Kamati ilifanya kazi hiyo na uchambuzi wake ni kama ifuatavyo:-

3.1 CHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA 2021/2022


Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia **Fungu 46** katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 imekadiria kufanya makusanyo ya maduhuli ya **Shilingi 540,943,008,495.63**. Kati ya makadirio hayo, **Shilingi 8,680,995,000.00** sawa na **asilimia 1.6** zinatarajiwu kukusanya kutoka vyanzo vya Idara na Vitengo vya Wizara na kiasi cha **Shilingi 532,262,013,495.63** sawa na **asilimia 98.4** kinakadiria kukusanya kutoka vyanzo vilivyopo chini ya Taasisi za Wizara.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wake kwa kulinganisha makadirio ya makusanyo kwa mwaka 2020/2021 dhidi ya yale ya mwaka 2021/2022 na kubaini kuwa, makadirio ya makusanyo kwa mwaka 2021/2022 yameshuka kwa **asilimia 2.6** kutoka **Shilingi 555,651,650,347** mwaka huo hadi **Shilingi 540,943,008,496.00** mwaka 2021/2022. Upungufu zaidi unaonekana katika vyanzo vya Wizara kutoka **Shilingi 15,459,750,000.00** hadi **Shilingi 8,680,995,000.00** sawa na upungufu wa **asilimia 43.85**. Kwa upande wa Taasisi, makusanyo yameshuka kwa **asilimia 1.47** kutoka **Shilingi 540,191,900,346.52** mwaka 2020/2021 hadi **Shilingi 532,262,013,495.63** mwaka 2021/2022 kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.4.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilihoji sababu zilizopelekea makadirio ya makusanyo kushuka kwa kiasi hicho na ilielezwa kuwa, ni kutokana na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs) kuruhusiwa kubakia na kiasi cha fedha za makusanyo (*Retention*) na hivyo zimetolewa zisionekane kwenye maduhuli.

Kielelezo Na.4

ULINGANISHO WA MADUHULI 2020/2021 NA 2021/2022



Chanzo: Randama Fungu 46 (Machi 2021) na Usanifu wa Kamati

3.2 CHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2021/2022

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili Kamati imefanya uchambuzi wa aina mbili kama ifuatavyo:-

a) Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara (Fungu 46 na 18)

Mheshimiwa Spika, uchambuzi huu unalenga kufanya ulinganisho wa bajeti ya mwaka 200/2021 na 2021/2022 [Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020] kwa lengo la kuona mwenendo wa bajeti ya Wizara hii. Katika Randama iliowasilishwa mbele ya Kamati na Wizara kuhusu makadirio yake ya matumizi kupitia **Fungu**


46 kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu Jumla ya **Shilingi 1,384,414,801,999**. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida yanaombewa **Shilingi 480,474,878,999.00** sawa na **asilimia 34.7** na **Shilingi 903,939,923,000.00** sawa na **asilimia 65.3** zinaombwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa fedha hizo ambao pia unaonekana katika kielelezo Na. 5 ni kama ifuatavyo:-

- i) Mishahara ya Watumishi (PE) **Shilingi 447,214,694,999.00** sawa na **asilimia 32**;
- ii) Matumizi Mengineyo (OC) **Shilingi 33,260,184,000.00** sawa na **asilimia 3**;
- iii) Fedha za Ndani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo **Shilingi 706,639,923,000.00** sawa na **asilimia 51; na**
- iv) Fedha za Nje kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo **Shilingi 197,300,000,000.00** sawa na **asilimia 14**

Kielelezo Na. 5

BAJETI FUNGU 46 2021/2022



Chanzo: Randama Fungu 46 (Machi 2021) na Usanifu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wake kwa kulinganisha Bajeti ya **Fungu 46** kati ya Mwaka 2020/2021 na 2021/2022 na kubaini kuwa, kuna ongezeko la bajeti kiasi cha **Shilingi 35,760,446,999.00** sawa na ongezeko la **asilimia 2.7** kutoka **Shilingi 1,348,654,355,000.00** mwaka 2020/2021 hadi **Shilingi 1,384,414,801,999.00** mwaka 2021/2022. Ongezeko zaidi linaonekana kwenye fedha za maendeleo za ndani kwa **asilimia 39.8** kutoka **Shilingi 606,715,000,000.00** mwaka 2020/2021 hadi **Shilingi 706,639,923,000.00** mwaka 2021/2022. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, ongezeko hili la bajeti linahusisha pia ongezeko la **Shilingi Bilioni 36** katika Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. **Kamati inapongeza Serikali kwa kuendelea kuongeza bajeti na kutenga fedha zake za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo na hususan katika Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu nchini ili kuwezesha wanafunzi wengi zaidi kupata mikopo.**

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini pia kuwa, kuna ongezeko la mishahara kwa **asilimia 6.8**. Kamati ilihoji sababu ya ongezeko hilo na ilielezwa kuwa, ni kutoptera na ongezeko la idadi ya watumishi kutoptera na ajira mpya, mabadiliko ya ngazi za mishahara kwa baadhi ya watumishi kutoptera na kupanda vyeo au madaraja. **Kamati inapongeza Wizara kwa kuona umuhimu wa kutenga bajeti ya nyongeza ya mishahara kwa watumishi waliopanda vyeo lakini pia kuendelea kuajiri watumishi wapya.**


Mheshimiwa Spika, pamoja na ongezeko hili, Kamati imebaini pia kuna upungufu wa fedha za Matumizi Mengineyo (OC) kwa takribani **asilimia 54.1**. Kamati ilihoji sababu za kupungua kwa bajeti hiyo na nini athari zake na ilielezwa kuwa, upungufu huu unatokana na kuhamishwa kwa teneo la bajeti ya uendeshaji wa mitihani kutoka fungu la Matumizi Mengineyo kiasi cha **Shilingi Bilioni 40** kwenda katika fungu la maendeleo.

Kielelezo Na. 6 kinaonesha ulinganisho wa bajeti ya Fungu 46 kwa mwaka 2020/2021 na 2021/2022.

Kielelezo Na. 6

ULINGANISHO WA BAJETI YA FUNGU 46 KWA MWAKA 2020/2021 NA 2021/2022

ULINGANISHO WA BAJETI YA FUNGU 46 KWA MWAKA 2020/2021 NA 2021/2022					
MATUMIZI		2020/2021	2021/2022	ONGEZKO/ UPUNGUFU	%
KAWAIDA	MISHAHARA	418,711	447,214	28,503	6.8
	OC	72,428	33,260	-39,168	-54.1
	JUMLA	491,140	480,474	-10,665	-1.8
MAENDELEO	NDAN	606,715	706,639	99,924	39.8
	NJE	250,799	197,300	-53,499	-21.3
	JUMLA	857,514	903,939	46,425	5.4
JUMLA BAJETI	JUMAKUU	1,348,654	1,384,414	35,760	27




Chanzo: Randama Fungu 46 (Machi 2021) na Usanifu wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Kwa upande wa Tume ya UNESCO (Fungu 18), katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 imekadiri kutumia Shilingi 2,254,777,000. Kati ya fedha hizo, Shilingi 722,484,000.00 sawa na **asilimia 32** ni kwa ajili ya mishahara na Shilingi 1,532,293,000.00 sawa na **asilimia 68**. ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Tume.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wake na kubaini kuwa, bajeti ya mwaka huu ya Tume imeongezeka kwa **asilimia 0.70** kutoka **Shilingi 2,239,181,000** mwaka 2020/2021 hadi **Shilingi 2,254,777,000** mwaka 2021/2022. Ongezeko zaidi linaonekana kwenye mishahara kutoka **Shilingi 706,888,000.00** mwaka 2020/2021 hadi **Shilingi 722,484,000** mwaka 2021/2022 sawa na ongezeko la **asilimia 2.21** kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na. 7. Kamati ilihoji sababu ya ongezeko la mishahara na iliezwa kuwa, ni kutokana na ajira mpya. **Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuona umuhimu wa kuongeza watumishi katika Tume hii.**

Kielelezo Na. 7

ULINGANISHO WA BAJETI 2020/2021 NA 2021/2022 (FUNGU 18)



Chanzo: Randama Fungu 18 (Machi 2021) na usanifu wa Kamati

b) Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara (Fungu 46) kwa kulinganisha na Mpango wa Maendeleo wa Taifa

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa kulinganisha bajeti ya Fungu 46 dhidi ya bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/2022 kwa lengo la kubaini masuala mbalimbali ikiwemo asilimia ya bajeti ya

Wizara katika Mpango huo (Bajeti ya Taifa) kati ya mwaka 2020/2021 na 2021/2022, lakini pia kuona ni kwa kiasi gani ongezeko/upungufu wa bajeti hiyo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaathiri vipi mwenendo wa bajeti ya Fungu 46.

Mheshimiwa Spika, Katika uchambuzi huo, Kamati imebaini masuala mbalimbali kama ifuatavyo:-

- i) Bajeti ya **Fungu 46** kwa ujumla wake kiasi cha **shilingi 1,384,414,801,999** kwa mwaka 2021/2022 ni **asilimia 3.82** ya Bajeti yote ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa ya **Shilingi 36,258,806,000,000**. Bajeti hii imeshuka kutoka **asilimia 3.87** mwaka 2020/2021;
- ii) Bajeti ya Mishahara ya **Fungu 46** dhidi ya bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa imeongezeka na kutoka **asilimia 5.39** kwa mwaka 2020/2021 hadi **asilimia 5.49** mwaka 2021/2022; na
- iii) Bajeti ya Maendeleo ya **Fungu 46** dhidi ya bajeti ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa imeongezeka kutoka **asilimia 6.65 mwaka 2020/2021** hadi **asilimia 6.82** mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, Kielelezo Na. 8 kinaonyesha ulinganisho huo.

Kielelezo Na. 8

ULINGANISHO WA BAJETI YA FUNGU 46 DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2020/2021 NA 2021/2022

ULINGANISHO WA BAJETI YA FUNGU 46 DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2020/2021			
MATUMIZI	BAJETIKUU YA TAIFA	BAJETIFUNGU 46	% FUNGU 46
O C	3,741,137,000,000	72,428,758,675	1.94
MISAHARA	7,762,389,000,000	418,711,372,325	5.39
MAENDELEO	12,899,433,000,000	857,514,224,000	6.65
MALIPO MADENI	10,476,834,000,000		
MAHITAJI YA TANAPA, TAWA NA NCNA	-		
JUMLA	34,879,793,000,000	1,348,654,355,000	3.87

ULINGANISHO WA BAJETI YA FUNGU 46 DHIDI YA BAJETI YA TAIFA 2021/2022			
MATUMIZI	BAJETIKUU YA TAIFA	BAJETIFUNGU 46	% FUNGU 46
O C	3,944,164,000,000	33,260,184,000	0.84
MISAHARA	8,150,509,000,000	447,214,694,999	5.49
MAENDELEO	13,255,855,000,000	903,939,923,000	6.82
MALIPO MADENI	10,663,278,000,000		
MAHITAJI YA TANAPA, TAWA NA NCNA	245,000,000,000		
JUMLA	36,258,806,000,000	1,384,414,801,999	3.82

Chanzo: Mpango wa Maendeleo wa Taifa, Randama Fungu 46 (Machi 2021) na usanifu wa Kamati

iv) Wakati bajeti Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2021/2022 ikiwa imeongezeka kwa **asilimia 3.95** kutoka **Shilingi Triliioni 34.8** mwaka 2020/2021 hadi **Shilingi Triliioni 36.25** mwaka 2021/2022, Bajeti ya Fungu 46 imeongezeka kwa **asilimia 5.6** kutoka **Shilingi Triliioni 1.34** mwaka 2020/2021 hadi **Shilingi Triliioni 1.38** mwaka 2021/2022;


v) Wakati bajeti ya Mishahara ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa ikiwa imeongezeka kwa **asilimia 5** mwaka 2021/2022 ikilinganishwa na mwaka 2020/2021, bajeti ya mishahara ya Fungu 46 imeongezeka kwa **asilimia 6.8**; na

vi) Wakati bajeti ya Maendeleo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa ikiwa imeongezeka kwa **asilimia 2.76**, bajeti ya Maendeleo ya Fungu 46 imeongezeka kwa **asilimia 5.4**.


Kwa ujumla ulinganisho huu unatupa tafsiri kuwa, Bajeti ya Fungu 46 imekuwa ni sehemu ya kipaumbele kwa kuwa na ongezeko zaidi ikilinganishwa na ongezeko katika Bajeti ya Taifa (Mpango wa Maendeleo wa Taifa) kama inavyoonekana kwenye Kielelezo Na.9.

Kielelezo Na. 9

ULINGANISHO WA BAJETI YA TAIFA 2020/2021 NA 2021/2022 (KWA MILIONI)				
MATUMIZI	BAJETI KUU YA TAIFA 2020/2021	BAJETI KUU YA TAIFA 2021/2022	PUNGUFU/ONGEZKO	
OC	3,741,137	3,944,164	203,027	5.43
MISHAHARA	7,762,389	8,150,509	388,120	5.00
MAENDELEO	12,899,433	13,255,855	356,422	2.76
MAIPO MADEN	10,476,834	10,663,278	186,444	1.78
MAHITAJI YA TANAPA, TAWA NA NCAAA	0	245,000	245,000	
JUMLA	34,879,793	36,258,806	1,379,013	3.95



Chanzo: Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Usanifu wa Kamati



Chanzo: Randama ya Wizara (Fungu 46) na Usanifu wa Kamati

SEHEMU YA NNE

4.0 MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi huo na yale yaliyobainika, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo yafuatayo:-

4.1 UHABA WA WALIMU NA WATUMISHI

Mheshimiwa Spika, Changamoto ya uhaba wa Watumishi katika Sekta ya Elimu bado ni kubwa. Kamati inafahamu Vyuo Vikuu na Vyuo vingine vina changamoto ya wahadhiri. Si hivyo tu, lakini pia shule nyingi zina upungufu wa walimu hasa wa walimu wa sekondari wa masomo ya Sayansi jambo ambalo linachangia kuathiri ubora wa Elimu yetu. Mahtma Gandhi amewahi kusema *"I have always felt that the true text-book for the pupil is his teacher"*. Kutokana umuhimu huo wa walimu Kamati inashauri:-

- Serikali na hususan UTUMISHI itoe vibali vya ajira ili watumishi wa Sekta hii waweze kuajiriwa ili kuondoa upungufu uliopo katika shule za msingi, Sekondari na Vyuo vyote nchini na kipaumbele kitolewe kwa wale wanaojitolea; na

b) Kwa Vyuo Vikuu, utaratibu uliyokuwa unatumika zamani wa kuwabakiza wanafunzi wanaofanya vizuri ili wawe wakufunzi wasaidizi (*Tutorial Assistance*) uanze kutumika ili kupunguza au kuondoa pengo hili la walimu/ wakufunzi/ wahadhiri.

4.2 MFUMO WA ELIMU

Mheshimiwa Spika,² Dira, dhima na malengo ya Sera yetu ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 inasema kuwa "**Msingi wa elimu na mafunzo utajikita katika kumjengea Mtanzania misingi bora ya malezi, maadili, ujuzi, umahiri na kumwezesha kujitegemea. Elimu ya kujitegemea itaendelea kuongoza utoaji wa elimu na mafunzo kwa kuzingatia mabadiliko yanayotokea katika jamii kisiasa, kiuchumi, kisayansi na kiteknolojia**"

Mheshimiwa Spika, pamoja na mwongozo mzuri wa Sera hii, Kamati inaona mfumo wetu wa Elimu bado hauendani na Sera yetu. Kamati inamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuionna changamoto hii pia. Pamoja na hayo Kamati inaona bado kuna kazi ya kufanya katika mfumo wetu wa elimu. Mwanazuoni Ms Arora M katika Jarida lake la ³Journey of life continues amewahi kusema "**Education can bring the desired change in the future, if you want to shape the future shape the education system accordingly**". Hivyo basi, Kamati inashauri yafuatayo:-

a) Serikali iandae Mpango wa Kukuza Ujuzi nchini (*Skills Development Plan*) ili kuwezesha wanafunzi kupata stadi mbalimbali za kazi ambazo zitawasaidia kujiajiri na hivyo kusaidia kukua kwa uchumi wa nchi;

b) Kwa kuwa nchi yetu ipo kwenye Uchumi wa kati ambao ni Uchumi wa Viwanda hivyo basi kuna kila sababu ya kuhakikisha elimu yetu inaendana na sera hii kwa kuzalisha mafundi sanifu na sadifu ambao ndiyo watenda kazi kwa kuboresha kozi zao (*Full Technician Certificate - FTC*);

- c) Serikali ianze kutoa Mikopo kwa wanafunzi wanaochaguliwa kuijunga kwenye vyuo vingine vilivyo chini ya NACTE. Wanafunzi hawa na ambao wengi wao wanatoka katika familia duni mara baada ya kuhitimu masomo yao ndio watakuwa watenda kazi hususan katika muktadha wa **Tanzania ya viwanda**. Hii itasaidia kuzalisha wataalamu wengi zaidi ambao ndio nguvu kazi katika Uchumi wa viwanda;
- d) Wizara iweke mfumo utakaowezesha aina ya elimu inayotolewa sasa iweze kubadilika kulingana na wakati na mazingira;
- e) Mpango wa kujenga Vyuo vya VETA katika kila Wilaya usimamiwe vizuri ili kila Wilaya iwe na chuo cha VETA; na
- f) Serikali iandae mjadala mpana wa kitaifa ambao utashirikisha wadau wote wa elimu lengo likiwa kupata suluhu ya kujuu ni elimu ipi na kwa wakati gani inayowafaa watoto wa kitanzania na Taifa kwa ujumla.

4.3 MIKOPO YA WANAFUNZI WA ELIMU YA JUU

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza Serikali kutokana na manufaa yaliyopatikana tangu kuanza kutolewa kwa mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini kwani bajeti na idadi ya wanufaika imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka jambo ambalo ni jema sana. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa, malalamiko yamekuwa ni mengi kutokana na baadhi ya wanafunzi kutoka katika familia maskini kushindwa kupata mikopo hiyo, lakini pia kutokana na tozo nydingi ambazo zimekuwa zikitozwa kwa wanufaika hao wa mikopo. Kamati inapongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa uamuzi wake wa kuondoa tozo ya kutunza thamani ya fedha za mikopo (**asilimia 6**). Hakika Rais anastahili pongezi. Pamoja na hayo, Kamati inashauri yafuatayo:-

- a) Wizara iangalie tena vigezo vinavyotumika katika utoaji wa mikopo na kuhakikisha wanafunzi wote wanaostahili kupata mikopo hiyo hasa wale wanaotoka katika familia maskini wanafanikiwa kupata mikopo;

b) Serikali iendelee kuangalia tozo na makato mengine yaliyopo kama adhabu ya **asilimia 10** inayotozwa kwa wanafunzi wanaochelewa kurejesha mikopo baada ya miaka miwili ya kuhitimu masomo yao; na

c) Mfumo wa kielektroniki wa kuhakiki taarifa za wanufaika wa Bodi ya Mikopo uboreshwe ili kurahisisha utaratibu wa ulipaji wa madeni.

4.4 TUZO YA UDHAMINI

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kusisitiza ushauri ambao umekuwa unatolewa na Kamati iliyopita ya kuanzisha Tuzo ya Udhamini kwa wanafunzi wanaomaliza kidato cha sita na kuwa na ufaulu wa juu. Wizara imeeleza kuwa imeanza mchakato wa kutoa tuzo hizi kwa wanafunzi hapa nchini wanaoenda Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. **Kamati inapongeza jitihada hizo, lakini inaona bado kuna haja ya kupeleka vijana wetu nje ya nchi hasa wale wanaofaulu vizuri masomo ya Sayansi ili kujifunza zaidi kwa kutumia utaratibu wa tuzo iliyopendekezwa na Kamati. Vijana hawa watakuwa msaada kwa Taifa na ikizingatiwa kuwa tuko uchumi wa katiba ambao unachochewa zaidi na ukuja wa viwanda.**

4.5 CHUO CHA UFUNDI ARUSHA

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Ufundi kinatoa elimu kwa ngazi za Astashahada, Stashahada na Shahada katika fani mbalimbali katika michepuo ya Sayansi, Teknolojia na Ufundi. Pamoja na kazi kubwa ambayo Chuo hiki kinafanya, bado kinakumbana na changamoto za miundombinu chakavu na isiyotosheleza mahitaji;

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu limekuwa likiidhinisha fedha kwa ajili ya chuo hiki, lakini fedha hizo zimekuwa haziendi. Katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Chuo kilitengewa jumla ya **shilingi 1,500,000,000** kwa ajili ya ujenzi wa bweni ambalo litasaidia katika kuongeza udahili wa wanafunzi wa kike ambao wengi wamekuwa wakashindwa kuijunga na chuo hicho kutohana na ukosefu wa malazi. Hata hivyo,

fedha hizi bado hazijatoka mpaka sasa. **Kamati inashauri Serikali ikiangalie chuo hiki kwa jicho la pekee na kuhakikisha inatoa fedha hizo ili wanafunzi wa kike waweze kujinga na chuo hiki kwa wingi zaidi.**

4.6 BAJETI YA TUME YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA (COSTECH)

Mheshimiwa Spika, Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) ndio chombo pekee cha kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu masuala yote yanayohusu Utafiti wa Sayansi na Teknolojia. COSTECH imekuwa ikigharamia Tafiti za kisayansi na kuboresha mazingira ya utafiti ikiwemo miundombinu na vitendea kazi. Nchi yetu ikiwa kwenye Uchumi wa Kati Uchumi wa Viwanda masuala ya utafiti na ubunifu yanapaswa kupewa kipaumbele cha pekee.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa ⁴UNESCO Institute of Statistics (UIS) ili kufikia ukuaji wa uchumi endelevu na utekelezaji wa Lengo Na. 9.5 la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG's), kuimarisha utafiti wa kisayansi, kuboresha uwezo wa kiteknolojia wa sekta za viwanda katika nchi zote, haswa nchi zinazoendelea ni jambo la msingi sana. Wakati Umoja wa Ulaya umeweka lengo la nchi wanachama ziwe zinatenga asilimia 3 ya Pato lake la Taifa kwa ajili ya utafiti ifikapo 2020, Umoja wa Afrika umeweka lengo la asilimia 1. Hata hivyo, taarifa za UIS zinaonyesha kuwa ni nchi nne tu za Kusini mwa Jangwa la Sahara ndio ziko karibu na lengo hili ambazo ni Afrika ya Kusini, Kenya, Burkina Faso na Rwanda (kati ya asilimia 0.8 - 0.7).

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa Utafiti katika maendeleo ya nchi yetu, Kamati inashauri Bajeti ya COSTECH iongezwe na iwe inatolewa yote kwani katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 ni Shilingi Bilioni 3.8 tu ndio zimetengwa kwa ajili ya Mfuko wa Utafiti na Maendeleo (Research and Development Fund – COSTECH) kiasi ambacho ni kidogo sana.

4.7 MIUNDOMBINU YA ELIMU YA JUU

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya changamoto katika Taasisi za elimu ya juu nchini ni uhitaji mkubwa wa ujenzi na ukarabati

wa miundombinu pamoja na vifaa vyta kisasa vyta kufundishia na kujifunzia. **Kamati inashauri Serikali itenye bajeti ya kutosha kuwezesha ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Taasisi hizo na ununuzi wa vifaa vyta kisasa vyta kufundishia na kujifunzia.** Aidha, fedha hizo zinazotengwa ziende zote na kwa wakati.

4.8 IDARA YA UDHIBITI UBORA

Mheshimiwa Spika, Idara ya uthibiti ubora wa shule ni moja ya idara muhimu katika Sekta ya Elimu hasa ikizingatiwa kuwa ndiyo yenye jukumu la kuhakikisha shule zetu zinatoa elimu yenye ubora unaotakiwa wenyewe kuzingatia utekelezaji wa mitaala ipasavyo. Ili kutekeleza majukumu hayo kikamilifu na kwa ufanisi bajeti ya kutosha ni jambo la msingi. Hata hivyo, Idara hii imekuwa haitengewi fedha za kutosha kufanya kazi zake. **Kamati inashauri bajeti ya kutosha itengwe kwa Idara hii ili watendaji waweze kutekelza majukumu yao kikamilifu.**

4.9 MUUNDO WA WIZARA

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa Muundo wa sasa wa Wizara haumpi majukumu ya kitaalamu moja kwa moja Kamishna wa Elimu ncini. **Kamati inashauri Serikali ipitie upya muundo wa Wizara ya Elimu na hususan majukumu ya Kamishna wa Elimu ili kumwezesha Kamishna kuwa msimamizi wa Idara zote za kitaaluma na hivyo kupunguza mzigo wa usimamizi kwa ngazi za juu.**

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru tena kwa nafasi uliyonipa ya kuweza kuwasilisha Taarifa hii ya kwanza ya Kamati yetu mbele ya Bunge lako Tukufu. Kipekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa imani waliyonipa na kunichagua kuwa Mwenyekiti wa Kamati. Aidha, namshukuru sana Makamu Mwenyekiti Mhe. Aloyce John Kamamba, Mb pamoja na wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakinipa na zaidi katika kushiriki vyema katika vikao vyta Kamati kikiwemo cha uchambuzi wa Bajeti ya

Wizara hii. Naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa majina kama ifuatavyo:-

- | | |
|---|--------------|
| 1. Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo, Mb - | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Aloyce John Kamamba, Mb - | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb - | Mjumbe |
| 4. Mhe. Eng. Samwel Hhayuma, Xaday Mb - | Mjumbe |
| 5. Mhe. Husna Juma Sekiboko, Mb - | Mjumbe |
| 6. Mhe. Tecla Mohamedi Ungele, Mb- | Mjumbe |
| 7. Mhe. Rose Cyprian Tweve, Mb - | Mjumbe |
| 8. Mhe. Kassim Hassan Haji, Mb - | Mjumbe |
| 9. Mhe. Francis Leonard Mtega, Mb - | Mjumbe |
| 10. Mhe. Jumanne Abdallah Sagini, Mb - | Mjumbe |
| 11. Mhe. Latifa Khamis Juakali, Mb - | Mjumbe |
| 12. Mhe. Kabula Enock Shitobela, Mb - | Mjumbe |
| 13. Mhe. Cecilia Daniel Paresso, Mb - | Mjumbe |
| 14. Mhe. Bernadeta Kasabago Mushashu, Mb- Mjumbe | |
| 15. Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb - | Mjumbe |
| 16. Mhe. Neema Kichiki Lugangira, Mb - | Mjumbe |
| 17. Mhe. Mussa Ramadhani Sima, Mb - | Mjumbe |
| 18. Mhe. George Ranwell Mwenisongole, Mb - Mjumbe | |
| 19. Mhe. Dkt. Paulina Daniel Nahato, Mb - | Mjumbe |
| 20. Mhe. Salome Wycliffe Makamba, Mb - | Mjumbe |
| 21. Mhe. Abdallah Dadi Chikota, Mb - | Mjumbe |
| 22. Mhe. Khamis Kassim Ali, Mb - | Mjumbe |
| 23. Mhe. Khalifa Mohamed Issa, Mb - | Mjumbe |
| 24. Mhe. Hassan Ziddu Kungu, Mb - | Mjumbe |
| 25. Mhe. Nashon William Bidyanguze, Mb - | Mjumbe |
| 26. Mhe. Hamisi Shabani Taletale, Mb - | Mjumbe |

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe na Naibu Spika, kwa kuendelea kuongoza vyema Bunge letu. Hakika ninyi ni viongozi wa mfano.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Joyce Lazaro Ndalichako (Mb), Naibu Waziri Mhe. Omary Shaban Kipanga (Mb), Makatibu Wakuu za Wizara hii wakiongozwa na Dkt. Leonard Akwilapo - Katibu Mkuu, Prof. James Mdoe - Naibu Katibu Mkuu na Prof. Caroline Nombo- Naibu Katibu Mkuu pamoja na

Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati wakati wote pamoja na kushiriki vyema katika vikao vya uchambuzi wa bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa ushirikiano ambao amekuwa akiipa Kamati yetu katika kutekeleza majukumu yetu. Pamoja nae, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein na Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Kamati yetu Ndugu Gerald Magili, Msaidizi wa Kamati Ndg. Jane Ndulesi na Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake bila vikwazo. Kipekee tunawashukuru sana Makatibu wa Kamati yetu Ndg. Pamela Pallangyo na Ndg. Nyamwanja Chilemeji kwa kuendelea kuishauri vyema Kamati na kuhakikisha majukumu ya Kamati yanatekelezwa bila mkwamo ikiwemo kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia **Fungu 46** kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, jumla ya **Shilingi 1,384,414,801,999** na **Fungu 18** jumla ya **Shilingi 2,239,181,000.00**

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha, naunga mkono Hoja.

Stanslaus H. Nyongo (Mb),
MWENYEKITI
KAMATI YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII

04 MEI, 2021

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa MwenyeKITI wa Kamati kwa kuunga mkono hoja na kwa hotuba nzuri ambayo mmeiandaa kama Kamati. Kwa kweli ina mambo mengi yanayoonesha kwamba palikuwa na uchambuzi wa ndani kabisa wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu.

Waheshimiwa Wabunge, kama mnavyoju, Wizara ya Elimu ina mambo mengi na ni moyo wa nchi yetu kwa kweli kwa watoto wetu na hatima ya vijana wetu. Kwa hiyo, tunategemea uchangiaji ambao utakuwa *vibrant*, ambao utatusaidia kuona twende namna gani, yaani uchangiaji wenye tija. Tuna leo na kesho.

Basi nadhani nimpe Mheshimiwa Mpina kuwa mchangiaji wetu wa kwanza, atafuatiwa na Mwalimu Grace Tendega. Karibu Mheshimiwa Mpina, dakika kumi, kumi.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa ili niweze kutoa mchango wangu katika hii sekta muhimu sana kama ambavyo umeshaeleza hapa kwamba huu ndiyo moyo wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nimesikiliza vizuri sana hotuba ya Mheshimiwa Waziri na nimesikiliza vizuri sana taarifa ya Mwenyekiti wetu wa Kamati ambayo maeneo mengi mbalimbali wameyagusa, lakini nataka tu kujikita katika mambo haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo mengi ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi kwa haraka ili kuwezesha utoaji wa elimu katika sekta shule zetu za sekondari na msingi ili kwenda vizuri zaidi. Kwa mfano, tunalo tatizo kubwa sana sasa hivi la vyoo vya kisasa katika shule zetu za msingi na sekondari ambavyo maeneo mengi kutokana na ukosefu wa hivi vyoo vya kisasa, vinajaa kila siku. Kwa sababu vinajaa na vyoo vile siyo vya kisasa, inabidi kila kinapojaa mbomoe miundombinu ile mjenge mingine.

Mheshimiwa Spika, kuna shule moja eneo lilidochimbwa vyoo sasa hivi limefikia ekari tatu. Kwa hiyo, itafika mahali eneo la shule lote litachimbwa vyoo kila sehemu. Kwa hiyo, ni lazima Wizara ya Elimu pamoja na TAMISEMI kuja na mkakati wa haraka sana wa kujenga vyoo vya kisasa, lakini pamoja na kuandaa madampo ya kisasa kwa ajili ya kumwaga zile taka. Hilo ndio litakalotuwezesha

kuwa salama zaidi, ili vijana wetu katika shule za msingi na sekondari wasome vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii kampeni lazima tuende nayo kwa *speed* kubwa sana ya ukamilishaji wa magofu ambayo wananchi wameyaanzisha. Tuna upungufu mkubwa wa madarasa, magofu yapo wananchi walishajenga wamefikia ile hatua, lakini bado hayajamaliziwa. Tuna maabara, bado hazijakamilika, nyingine zimejengwa zimekamilika, lakini vifaa hamna, tuna mahitaji makubwa sana ya *hostels*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi kubwa sana iliyofanywa katika Serikali ya Awamu ya Tano, lakini bado kuna mahitaji makubwa ambayo tunatakiwa kuhakikisha kwamba, tumeyakamilisha kikamilifu ili vijana wetu waweze kufanya kazi vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ni muhimu sana, limezungumzwa na kila tukizungumza suala la ajira, tunazungumza suala la ujuzi. Mambo haya ni makubwa sana na wewe umekuwa *uki-comment* hapa Bungeni, lakini nataka niseme hivi tunataka kupata vijana wenye ujuzi, vijana ambao wameandaliwa. Tunawapataje...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge nawaomba sana, kama kawaida yetu tumpe nafasi anayezungumza, tumsikilize vizuri.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, tunawapataje vijana wenye ujuzi wakati masomo ambayo yangeweza kuwawezesha vijana hawa kupata ujuzi hayapo, yameondolewa. Kwa mfano, leo hii vijana wanaoenda *internship* ni wale tu wanaosoma masomo ya udaktari wa binadamu, lakini wale wanaosoma masomo ya udaktari wa mifugo hawaendi *intern*. Wale wanaoenda kusoma mafunzo mengine ya uvuvi, mafunzo mengine ya kilimo, ili tuweze kuandaliwa wataalam ambao wamepitishwa kwenye tanuru na wakaiva, lakini hawaendi *intern*. Sasa mwisho wa siku unategemea unawapata wapi vijana wenye ujuzi wanaoweza kutumika sawasawa?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo unakuta kwa upande wa Madaktari kwa sasa hivi wanafanya vizuri sana kwa sababu, wanapata mwaka mmoja kwa ajili ya *intern* na wanaliipiwa na Serikali. Sasa shida iko wapi kwa vijana wengine hawa? Tunahitaji Maafisa wa Mifugo na Madaktari wa Mifugo walioandaliwa vizuri, wanafundishwaje? Tunahitaji wataalam wa uvuvi walioandaliwa vizuri, wamefundishwaje? Tunahitaji wataalam wa kilimo walioandaliwa vizuri, wanafundishwaje na mtaala wetu unasemaje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tulifika mahali hapa masomo kwa mfano ya kilimo yaliondolewa shulen; shule ya msingi yakaondolewa, sekondari yakaondolewa, lakini unafundisha vijana shule ya msingi, unafundisha vijana sekondari ambao unatarajia baada ya kumaliza masomo yao asilimia 70 waende kulima, halafu somo lenyewe la kilimo halifundishwi na lilondolewa shulen. Sasa tunategemea mabadiliko gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, somo la ujasiriamali nalo kwa nini halijawekwa kuwa la lazima? Kwa sababu, hata ukisoma udaktari si lazima ujifunze kutunza hizo fedha na huo mshahara ili uweze kukutosheleza? Si lazima ujifunze ku-debit na ku-credit ili ujue matumizi yako unasimamiae mwisho wa mwezi? Kuna shida gani somo la ujasiriamali kufundishwa kwa kada zote kuanzia shule za msingi, vijana wakafundishwa vizuri ujasiriamali, wanafika sekondari wanafundishwa vizuri? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa unafundisha watu waende kulima, wakienda kule hawajui hata kufungua *tractor*, hawajui hata kuwasha *tractor*, hawajui hata kuswaga *plough*, hawajui hata kushika jembe, halafu Taifa lenyewe ni la wakulima hili. Sasa Taifa la wakulima, somo la kilimo limehujumiwa, halifundishwi, sasa sababu za kuhujumiwa somo la kilimo ni nini? Sababu za kuhujumiwa somo la ujasiriamali ni nini? Naona ni kufanya Tanzania hii itengeneze watu ambao hawana uwezo wa kwenda kutumika sawasawa katika kulitumikia Taifa lao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni suala la utafiti. Limeelezwa ukisoma vizuri sana wanaongea hapa, lakini niseme suala la utafiti katika nchi yetu halijapewa kipaumbele kinachotakiwa. Hili suala tusipolipa kipaumbele kama inavyotakiwa tutaendelea tu kuanguka kila mwaka kwa sababu, leo hii tunazungumzia udahili wa wanafunzi na tunasema udahili umeongezeka, chuo kikuu umeongezeka, vyuo vya ufundi umeongezeka, lakini nani anayefanya *trace study* ya kuwajua hawa watoto baada ya kumaliza masomo yao wanaenda wapi? Wanaenda kufanya nini? Wako wapi? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wakati nikiwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi tulifanya utafiti wa kufuatilia vijana wanaomaliza, waliosoma masomo ya mifugo baada ya kumaliza masomo hayo wanaenda wapi. Katika vijana 8,000 vijana mia saba na kitu tu ndio walioonekana kupata ajira na vijana asilimia 90.5 hawajulikani wako wapi na wanafanya nini. Sasa kama tafiti hizi haziwezi kufanywa mtakuwa mnasema tu tunadahili wanafunzi, udahili umeongezeka. Sasa udahili umeongezeka, umeongezeka kwenye jambo gani?

Mheshimiwa Spika, bado tuna vijana leo anataka sasa achague kozi yake anataka kwenda kusoma mchepuo gani. Anataka kwenda kusoma kilimo, anataka kwenda kusoma uvuvi, anataka kwenda kusoma uhasibu, anataka kwenda kusoma biashara, lakini utafiti uliofanyika wale waliosoma masomo hayo leo wako wapi? Atachaguaje sasa? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pengine unaenda kuchagua unataka kwenda kusoma biashara, vijana toka mwaka 2005 waliosoma biashara *graduates* hawajapata kazi. Sasa wewe leo unachagua kwenda kusoma biashara ili uajiriwe na nani? Soko la ajira linasema nini? Linahitaji nini? Linahitaji kijana gani aliyeandaliliwa wapi? Takwimu hizi na utafiti huu kwa nini haufanywi?

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Eilmu kwa nini utafiti huu haufanyiki, ili vijana wakapata *base* ya kuchagua kwamba, sasa hivi nataka mimi kwenda kusoma mifugo. Sasa nataka

nijue vijana waliosoma mifugo ajira katika sekta binafsi ajira zipo? Hamna, ingeoneshwa *percent* kwamba, leo hii ajira katika sekta ya mifugo ni asilimia mbili. Leo hii ajira katika uvuvi ni asilimia kadhaa, leo hii katika kilimo ni kadhaa, vijana wetu wangeweza kuchagua kulingana na mahitaji ya ajira kwa wakati huo. Hivyo, hata udahili wa wanafunzi sasa hata vyuo vyetu vinavyoweza kupanua udahili vianue udahili kulingana na madai na mahitaji ya soko yaliyopo kwa sasa, sio tu mtu anachagua tu kwa hiyari mimi naenda kusoma *accounts*, mimi naenda kusoma *business administration*; unaenda ku-*administer* wapi? Mahitaji yako wapi?

Mheshimiwa Spika, lakini hata *training* pia ya Maprofesa wetu na Madokta wetu tunaowapeleka chuoni kwa sasa bado kuna shida kubwa kwa sababu kijana anayebakishwa shulenii kwa ajili ya kuwa *lecturer* ni yule aliyepata "A" nyingi, lakini si yule aliyepata *practice* katika ille eneo. Kwa hiyo, unafundishwa biashara na mwalimu ambaye amepata "A" nyingi, lakini hajawahi kufanya biashara yoyote na wala hajawahi ku-*practice* eneo lolote. Kwa hiyo, mwisho wa siku utatengeneza vijana gani wa namna hiyo? Kwa nini mfumo huu usibadilishwe?

Mheshimiwa Spika, leo hii tunafanya vizuri sana na nataka nipongeze kabisa, kwa sababu, mara nyingi wanaowafundisha madaktari wetu ni wale ambao wanatibu binadamu, kwa hiyo, wanakuwa na *experience* ya kutosha katika eneo hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunayo safari kubwa ya kufanya mageuzi kwenye nchi yetu na mageuzi ya kweli yatafanyika kwa kufanya mageuzi makubwa katika sekta ya elimu. Tukishajipanga vizuri kwenye sekta ya elimu, leo hii tunazo taasisi ambazo zinafanya shughuli ya utafiti, kwa mfano kwenye uvuvi tuna *TAFIRI*, kwenye mifugo tuna *TARIRI*, kwenye kilimo tuna *TARI*, kwenye misitu tuna *TAFORI*, tuna *COSTECH*, tuna *NBS*. Hizi taasisi zinakutana wapi? Nani anaandaa zile *agenda* za utafiti? Ile *database* ya tafiti zinazofanyika nchini tutaiona wapi? Hizo tafiti zinazoandaliiwa

zinawafikiaje watu? Kanuni zilizopo kwa ajili ya tafiti hizo, kuzilinda zile tafiti zipo wapi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu saa nyingine hata taasisi zetu za utafiti zinafanya hata mambo ya nje ambayo wakati mwingine hayana manufaa kwenye Taifa letu. Tufanye mageuzi ya kweli katika sekta hii. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Luhaga Mpina. Najua ulihitaji kama nusu saa hivi ili uteremke sawasawa, lakini sasa muda wetu ndio huo. *Topic* ya elimu huwa ni *topic* ambayo inagusa.

Sasa twende kwa Mwalimu Grace Tendega. Atafuatiwa na Mwalimu Mussa Ramadhan Sima.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Nianze kwa msemo usemao; *if education is expensive try ignorance.*" Kwa tafrisi ya kawaida tu inasema kwamba, kama elimu ni gharama jaribu ujinga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nazungumza hivi kwa sababu, tunaangalia jinsi ambavyo elimu ya nchi hii inavyokwenda. Nashukuru sana Kamati ilivyotoa maoni yake kwa ajili ya kujenga na kuboresha Wizara hii ya elimu. Naafiki kabisa maoni na mawazo ya kamati ambayo yametolewa, yatasaidia sana kuboresha katika Wizara hii ya Elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, najikita katika sehemu kubwa kuhusu udhibiti ubora, kwa maana ya kwamba, zamani tulikuwa tunasema ni ukaguzi. Tunazungumza, watu wengi wanazungumza kwamba, ooh, tubadilishe mitaala, tufanye hiki, tufanye vile, ili tuendane na hali halisi ya maisha yanavyokwenda. Ni kweli ni vizuri tukafanya hivyo, lakini kitendo cha kubadilisha, yaani *total over hauling* ya *curriculum* inachukua miaka mingi sana. Kwa hiyo, huwa tunakwenda tunabadilisha, labda tunaboresha wakati tun-

plan kubadilisha hiyo mitaala kulingana na haja kamili tunayoitaka ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nchi mbalimbali zinakuwa na *targets* kwamba, sisi tunataka nchi yetu iwe ya namna gani? Tunataka wananchi wa Tanzania wajikite kwenye mambo gani? Kilimo, muziki ama ni watu wa viwanda sana au kitu kama hicho? Kwa hiyo, lazima kuwe na tafiti ya muda mrefu na wananchi wakubaliane na wadau kujua kwamba, tunataka nchi yetu iendeje na uchumi wetu uweje?

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sababu bado hatujaanza huo mchakato, nashauri katika usimamizi ubora wa elimu, udhibiti ubora.

Sasa nikianza na hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu alioitoa hapa, ukurasa wa tisa na ukurasa wa 15 nimeona kuna *contradiction* kidogo ya taarifa zake katika namba. Waziri amezungumzia kwamba, katika mwaka huu uliopita walikuwa wameweza, *plan* yao ilikuwa ni kukagua shule 4,700 za msingi, lakini walikagua shule 2,755, kati ya shule 2,726 ambayo ni asilimia 101.

Mheshimiwa Spika, ujue tuna shule 18,152. Sasa tukiwa tunajipima hivyo kwamba, hapa tumekagua asilimia 100, lakini hali halisi tunaiona, shule zetu hazikaguliwi na usipokagua watu hawafanyi kazi kwa ufanisi, walio wengi. Sasa kwa sababu, hawafanyi kazi kwa ufanisi mtaona kama ile mitaala haifanikiwi, lakini kumbe ufanisi, ukimkagua mtu anaongeza juhudhi, anaongeza *speed* ya kufanya kazi. Sasa kutokuweka idadi kubwa na *targets* zao za kukagua sana shule zetu wataona changamoto zilizopo kati ya shule za Serikali na shule za *private*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, shule za *private* zinakaguliwa na zinakaguliwa kwa sababu shule zile zinatoa pesa wakaguzi wanakwenda kukagua zile shule. Kwa hiyo, utakuta kwamba, mara nydingi wale wanafanya kazi kwa juhudhi kwa sababu, kuna ukaguzi uko pale, lakini shule zetu zinakwenda tofauti na hivyo.

Mheshimiwa Spika, sasa nitajikita katika udhibiti ubora katika shule zenyе mahitaji maalum. Katika Ripoti ya *CAG* amezungumza kwamba, kuna changamoto ya usimamizi wa ubora wa elimu katika hizi shule, unakuta kuna miaka inapita hazikaguliwi kabisa. Na kama hazikaguliwi, lakini tuna uhaba wa Walimu wa kwenda kukagua hizo shule, ni wachache. Katika, anasema ni asilimia nane tu ndio waliopo ambapo tuna mahitaji ya Walimu 1,306, sisi tuna asilimia nane tu.

Mheshimiwa Spika, hawa ni wenzetu, watu wenye ulemavu ni wenzetu. Shule zipo, lakini tuna chuo kimoja tu kinachotoa Walimu wa watu wenye ulemavu ambacho kiko Patandi. Walimu wakisomea pale wanapelekwa katika shule ambazo hazina watu wenye mahitaji maalum. Kwa hiyo, unakuta kwamba, Wizara inaweza ikawa inapeleka watu kusomea hicho kitu, lakini hawapangiwii kule, matokeo yake inakuwa ni changamoto ileile inaendelea. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi, imeonesha kwamba, hakuna vifaa vya kufundishia asilimia 68 katika shule 17 kati ya 18 walizotembelea, lakini hakuna utaratibu endelevu wa kugharamia ukaguzi katika hizo shule. Mwaka jana walitenga shilingi milioni 272 katika Wizara ya Elimu kwenda kukagua hizo shule.

Mheshimiwa Spika, kwa kitendo ambacho kinaumiza kabisa badala ya kwenda kukagua, Wizara ilipeleka hizo fedha kwa ajili ya mitihani ya darasa la nne na pia ilipeleka kwenye mashindano ya lugha ya Kiingereza Afrika Mashariki. Sasa utaona jinsi ambavyo zile pesa zilitengwa, lakini hazikwenda kwenye ukaguzi wa hizo shule. Matokeo yake ni nini? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, utaona kwamba, tunapata changamoto kubwa ya kuziendesha hizi shule kwa sababu, hakuna wakaguzi, hatuna Walimu, hakuna uendelevu wowote wa utengaji wa fedha katika hili. Nimwombe Mheshimiwa Waziri aweze ku-*considerna* hii sekta kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, niende sasa katika mafunzo kwa Walimu kazini. Tulikuwa na kawaida miaka iliyopita Walimu kazini walikuwa wanapata mafunzo wanapelekwa kwenye vyuo; Chuo cha Songea, Butimba, Morogoro na vyuo vingine kwa miezi mitatu, mitatu angalau kunolewa kuona ni nini ambacho watakwendwa kufundisha. Mkiboresha mitaala kuwa ya *competence-based curriculum* hiyo, unachukua Walimu wale wakapate ile *knowledge* ya kufundisha hivyo, kwa sababu, kila mara kuna mabadiliko yanatokea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hiki kitendo kimekuwa ni cha, kama wanatoa ni kidogo sana, lakini Walimu wanahitaji kupata haya mafunzo ili waweze kunolewa kwenda na wakati. Kama tunavyosema kwamba, tunataka mitaala iende na wakati, lakini tunataka na Walimu waende na wakati, ili waweze kufundisha vizuri wanafunzi wetu tusilalamike kwenye matokeo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia Taarifa ya CAG inaonesha kwamba, hakukuwa na mpango wowote wa kutoa mafunzo kwa Walimu wa sekondari. Walimu wa sekondari hawakupata kabisa mafunzo hayo kazini ambapo ndipo wanaponoa wanafunzi wetu waweze kufanya vizuri katika masomo yao.

Mheshimiwa Spika, pia nakubaliana na Kamati wanavyosema kwamba, tuweze kuwawezesha kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaochaguliwa kwenda kwenye vyuo ambavyo vinasimamiwa na NACTE kwa sababu pale ndio tutapata wanafunzi ambao wakitoka ndio watakuja kuwa watenda kazi katika viwanda ambavyo tunavitarajia kuvijenga. Kwamba, tutakuwa na viwanda, watenda kazi watakuwa ni wale wanafunzi watakuwa kule, lakini kama hawatakuwa wanapewa mikopo ni changamoto bado inabaki kuwa kubwa kupata hii kada ya chini ambayo ndio ya watenda kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kweli, kwa kutoa ile asilimia ambayo ilikuwa kwenye Bodi ya Mikopo, asilimia sita na pia Mheshimiwa Waziri amezungumza

hana pia, wametoa hata ile asilimia nytingine 10. Nipongeze kwa hilo kwa sababu, hiki kilikuwa ni kitu ambacho kinawaumiza sana vijana wengi na wengi amba wanasona elimu ya juu kuona kwamba, wanawenza kulipa namna gani, mishahara ilikuwa inakatwa, walikuwa wanashindwa kufikia malengo. Napongeza kitendo hicho kinasaidia sana, kitasaidia watu kufanya kazi kwa juhudi na kujua kwamba, Serikali yao inawajali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niende sasa kwenye jambo ambalo sio la mwisho kwa umuhimu, tuna wanafunzi wa kike wanaopata ujauzito kwa bahati mbaya. Sihalalishi kwamba, wale wanaofanya hivyo kwamba, ni halali, hapana, lakini kuna wanafunzi kwa mazingira yaliyopo kule vijiji na maeneo mengine wana mazingira magumu ambayo inafikia wanakutwa na hali hiyo. Nakumbuka mwaka 2015 kulikuwa na swali lilitolewa hapa na Mheshimiwa Magreth Sita na Naibu Waziri akaahidi kwamba watatengeneza mwongozo wa namna ya kuwahakikisha hawa vijana wanarudi shule. Kwa hiyo naomba mheshimiwa Waziri unapohitimisha basi tujue wanafunzi wetu watafikia wapi.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nakumbuka mwaka 2015 kulikuwa na swali lilitolewa hapa na Mheshimiwa Margaret Sitta na Naibu Waziri akaahidi kwamba watatengeneza mwongozo wa namna ya kuwahakikisha hawa vijana wanapata kitu.

SPIKA: Ahsante.

MHE. GRACE V. TENDEGA: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba mheshimiwa Waziri unapohitimisha basi tujue wanafunzi wetu watafikia wapi ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Grace Tendega tunakushukuru sana kwa mchango wako nilishakutaja Mheshimiwa Mwalimu Mussa Ramadhani Sima na atafuatiwa na Mheshimiwa Prof. Mwalimu Jumanne Kibera Kishimba, Mheshimiwa Sima. (*Makofii*)

MHE. MUSSA R. SIMA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini pia nianze pia kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa kwanza mwanamke kwa asilimia 100 ndani ya Chama Cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitakuwa narejea mbalimbali za viongozi kuhusiana na mjadala unaoendelea wa Wizara ya Elimu, nianze na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika hotuba yake ya kwanza akiwa Chamwino anaapisha viongozi alizungumzia juu ya mabadiliko ya elimu hasa elimu ya ujuzi, lakini pia tukiwa Chimwanga kwenye maombi maalum ya Hayati Mpendwa wetu Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mipango yake ama vipaumbele vyake 18 kipaumbele cha tano kilikuwa ni cha elimu na ni elimu ya ujuzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini akiwa anahutubia Bunge pia, alizungumzia mabadiliko ya mtaala na mtaala huu huzungumzia hasa kwenye ujuzi, narejea pia katika rasimu ya Mpango wa Maendeleo ya Miaka Mitano wakati tunafanya majadala hapa ukurasa wa 25 ilitolewa taarifa ya Tume ya Mpango, Tume ambayo ilionesha kabisa soko la ajira. Soko la ajira haliendani na elimu ya ujuzi inayotolewa sasa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini nimshukuru Waziri wa Fedha alitusikiliza na kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano amekuja ameeleza vizuri katika mambo manne ambayo Wizara ya Elimu inapaswa kuyatekeleza, moja

ilikuwa Sayansi, Teknolojia na ubunifu kwa maana ya SATU.
(Makof)

Mheshimiwa Spika, na nimemsikiliza Waziri vizuri kwenye hotuba yake nimpongeze sana hapa Waziri ameeleza pia na wao kwenye eneo la Sayansi, Teknolojia na Ubunifu amelieleza vizuri. Lakini kuna eneo ambalo tunahitaji tulieleze vizuri. Katika maelezo yake amesema wale walioshinda ubunifu ndio watawaendeleza, lakini pia ameeleza wataendelea na mashindano kwa watu watakaokuwa wanashinda wataendeleza mashindano na wale watakaoshinda ubunifu ndio wataendeleza.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu hapa ubunifu tunaouzungumza, teknolojia tunayoizungumza sayansi hii tunayoizungumza tunapaswa kwenda mbali zaidi twende tukauhishe vyuo vyetu vya ufundi badala ya kuhangalika na walioshinda. Leo tunayo Tanga *Technical*, Arusha *Technical*, *tuna* Moshi *Technical*, vyote hivi ukienda kuangalia mazingira yao haifanani kama ilivyo *FTC* zamani, wakati tunazalisha tunatafuta wazalishaji leo tumeenda ku-*transform* tumeweka watu wa kusimamia, wasimamizi *administrates*. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, sasa nataka nimuomba Mheshimiwa Waziri wakati anapokuja kueleza vizuri kwenye eneo hili la kuhakikisha tunatekeleza Mpango huu wa Serikali tusibaki na watu walioshinda kuwa wabunifu, twende kuboresha vyuo vyetu tutenge bajeti ili vyuo vyetu hivi viweze kufanya vizuri. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, kipo Chuo cha Nelson Mandela ameeleza vizuri hapa Mheshimiwa Waziri na kimetengewa fedha na hizi fedha sio za kwetu za wafadhili zaidi ya bilioni 3.2 nataka niseme jambo hapa hakuna *donor* ambaye anakuletea fedha ya kufanya utafiti hajakuwekea masharti maana yake atataka ufanya utafiti kwa kile ambacho anataka yeye. Lakini Je, sisi Watanzania tunataka nini, nilitaka Serikali ijielekeze kwa kile tunachokitaka sisi, Chuo cha Nelson Mandela nakumbuka mwaka 2001 Mkutano Mkuu wa Wakuu

wa Nchi za Afrika ulipokaa ulijadiliana namna gani tunakabiliana na teknolojia tuliyonayo sasa hivi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Nelson Mandela na Mkutano huu ninakumbuka uliudhuriwa na Rais wa *World Bank* wa wakati huo Dkt. James David Worson ambaye ushauri ultoka vianzishwe vyuo vinne Afrika moja ya chuo kilichojengwa ni *Burkina Faso* kingine kilijengwa *Nigeria* na hichi cha tatu kimejengwa Tanzania Arusha-Nelson Mandela *Institute* cha nne nadhani kitajengwa Zimbabwe. Sasa Serikali yetu na hapa nimshukuru Rais wa Awamu nne Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alitoa fedha Dola milioni 60 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya chuo cha Nelson Mandela. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, alifanya kazi nzuri sana leo tunazungumza Chuo cha Nelson Mandela kinapata fedha za wafadhili, wafadhili ambaao wao wametoa masharti yao ya tafti wanazozitaka wao yawezekana kwetu sisi zikawa sizo tunazozitaka kwa hali tuliyonayo sasa hivi, nataka nimuombe Mheshimiwa Waziri sisi lazima pia tuweke mkono wetu tutoe fedha kwa ajili ya kufanya tafti zitakazotusaidia tuendane na haya maelekezo ambayo Mheshimiwa Rais ameyatoa lakini na Mpango wetu wa Maendeleo. Kwenye eneo hili litakuwa limetusaidia kupata wataalam wengi wenye utaalam lakini tutakuwa tumepata ubunifu mwingu ambaao tutaweze kuusimamia na kuhakikisha watoto wetu wanaweza kujajiri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunapotaka kuwa na wazalishaji, sisi tumekwenda mbali zaidi tumegeuza maana yake sasa hivi unawazungumzia hawa wa *full technician* na wengine hawa wa *graduate engineers* huwezi kumfananisha *full technician* wa wakati ule na *graduate engineer* wa leo wala hatujachelewa, hatujachelewa kama China wameweza kuondoa vyuo vyao 600 vyuo vikuu kwenda kuwa vyuo vya Elimu ya Katu sisi hatuwezi kuchelewa tunapaswa na sisi tutafakari kwamba umefika wakati tuimarishe vyuo vyetu vya katu ili kupata wazalishaji wengi zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini kuna eneo moja hapa muhimu sana *competence basic education*, nakumbuka tunapozungumzia *competence basic education* elimu ya maarifa, elimu ya maarifa leo tunazungumzia *academic tunazungumzia teaching and learning*. Amesema vizuri Mheshimiwa Mpina pale huku nyuma tulikuwa na watu, mtoto anaweza anajifunza kilimo, anajifunza biashara anajifunza vitu vingi sana lakini leo hakuna kwasababu tupo kwenye msingi wa *education* tu peke yake kwa maana watoto wana ujifunzaji lakini watoto hawana ujuzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka nishauri hapa badala ya kuwa na masomo mengi ni lazima tuweke somo la lazima kama somo la Kilimo lianzie darasa la kwanza mpaka chuo kikuu, asome michepuo yake yote lakini awe anasoma badala ya kubaki tu unafundisha mtoto *development study what does it mean development study* maana yake lazima ajue kabisa anasoma package ya *agriculture ambayo imecompose* vitu vingine vyote vilivyopo ndani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa nataka nishauri Serikali, ushauri wangu wa kwanza kamati imeeleza vizuri lazima tuwe na mjadala mpana wa elimu ambao utawahuishwa watu wote na kada mbalimbali ili tujue elimu tunayoitaka sisi ipi. Lakini jambo langu moja la msingi tunapaswa kuwa na Baraza la Taifa la Elimu, Baraza la Taifa la Elimu ndilo litakalokwa linamshauri Waziri, litakalokwa linamshauri Rais lakini ndilo litakalosimamia elimu kwa ujumla, hii ndio itakuwa *ambarella* kubwa. Lakini tuna *NACTE* na *TCU* hapa tumevigawa vyuo *NACTE* wanavyuo vikuu *TCU* wana vyuo vikuu hizi *regulator* zote mbili zinatuchanganya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwanini tusiwe na *regulator* moja inayosimamia elimu ya juu yaani tunazungumzia kama *TCU* wasimamie *Universities* wabaki kusimamia *Universities* kwa ajili ya *degree* lakini kama *NACTE* wanasmamia vyuo vya katil wabaki kusimamia vyuo vya katil. Lakini suluhu ya haya yote maana yake msingi wake lazima tuwe na Baraza la Taifa la Elimu litakalotufikisha mahali sisi tunapokutaka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunajengewa shule za kata kwa kata ambazo hazina shule kama shule 300 kwa malengo kuanzia mwaka huu, lakini tutafakari kwa wote shule 300. Nina kata moja tu Mandewe ina shule za msingi saba watoto wanaomaliza pale hawapungui 600 wa kwenda kidato cha kwanza sasa unajiuliza shule moja ya kata niliyonayo ukajenga nyine kwenye kata ambayo haina maana yake hawa watoto 700 unakwenda kuwaweka, maana shule nzima ni *form one* peke yake hakuna uwezekano mwingine.

Mheshimiwa Spika, nilitaka niishauri Serikali katika Mpango huu, huu Mpango uishirikishe jamii, jamii ishiriki na yenye we badala ya shule moja tunaweza kujenga shule mbili mpaka tatu na kuendelea ili kukabiliana na tatizo ambalo tulilonalo na Watoto wengi wanakwenda shule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia nikushukuru sana wewe kwa namna ambavyo umeniweka kwenye Kamati hii ya huduma za jamii umenisaidia sana nimalizie pia kuwatakia kila la kheri wale wote ambao wamegombea nafasi hizi kwenye Bunge letu hili nikiwemo na mimi Mussa Sima, ninawashukuru sana na Mungu awabariki. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana, naona watu wapo *canteen*, wapi, sijui wapi kampeni zinaendelea hakuna uchaguzi, kuna uchaguzi gani? Eee! watu wanahangaika tu hakuna uchaguzi, uchaguzi uko wapi? Spika hajatangaza uchaguzi ahsante sana, tunaendelea michango yetu kwenye elimu mambo ni mengi kwa kweli tunaendelea vizuri *so far*. (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Profesa nina moja dogo hivi siku hizi watoto Waheshimiwa Wabunge kama mmeshawaona wa darasa la pili darasa la tatu la nne wana mabegi mazito! Wanabeba mpaka wanapinda migongo mabegi mazito! Mimi ninajiuliza hivi hii ni nini? Wana mzigo...basi nimeona nichekeshe kidogo lakini *in fact*, yaani vitoto vinabeba mabegi. Mheshimiwa Profesa Jumanne Kishimba na atafuatiwa na Mheshimiwa Benardeta Mushashu, Mwalimu Benardeta Mushashu. (*Kicheko*)

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Elimu ya juu, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Waziri wa TAMISEMI kwa zoezi waliloanza sasa hivi la kupeleka wanafunzi kwenye vyuo vya VETA kwa muda wa miezi sita ninampongeza sana. Ninaona suala langu kidogo umelianza lakini lipo eneo lile lile, juzi hapa kulikuwa na mjadala kati ya Mheshimiwa Nyongo na Mheshimiwa Waziri, kuhusu suala la watu *stress* sijui presha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Waziri miongoni mwa asilimia 50 ya presha ambayo wazee na watu wanayo sasa hivi ni suala la elimu, na suala hili la elimu sio kwenye elimu yenye kama ulivyosema. Leo bahati nzuri ulivyosema nimkuja na *sample* hapa nina *sample* ya daftari ambazo zinasomea shule za *private*, shule ya *private* inasomea daftari la shilingi 200 ambapo kwa mwanafunzi kwa madaftari 11 itakuwa shilingi 2,200 lakini shule ya Serikali inasomea *counter book*. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *counter book* 11 ni sawa sawa na shilingi 55,000 kwa kijjini ambaao ni sawa sawa na gunia zima la mpunga au mahindi. Sasa inawezekanaje matajiri wakasomea daftari la shilingi 200 maskini wakasomea daftari la shilingi 5,500? Na mnasema kwamba watu wana *stress* ni kweli watu hawana raha na shule, hawana raha wananchi na shule nina-*sample* ya *uniform* hapa. (*Kicheko/Makofi*)

*(Hapa Mhe. Jumanne K. Kishimba alionesha
mfano wa uniform)*

MHE. JUMANNE K. KISHIMBA: Mheshimiwa Spika, *uniform* za *private* ni rangi hizi (*blue* bahari) *uniform* za shule za Serikali ni rangi nyeupe ni vipi mzazi atawea kufua kila siku, haiwezekani Mheshimiwa Waziri wa Elimu na TAMISEMI wote ni Wabunge wa kuchaguliwa ni kweli ni sahihi? Kwanini *private* wasomee za rangi wanafunzi wa shule za Serikali wasomee nyeupe. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo kutwa nzima wazazi wanaendelea kushinda wanunu sabuni na kufua, tunaongeza umaskini badala ya kuongeza elimu. Ni kweli Mheshimiwa Waziri ni lazima kabisa alifikirie upya wananchi wamechoka hawataki kabisa shule, kwasababu sasa hivi kijijiini ukifika unakuta mahali unauliza ng'ombe za hapa mlizipeleka wapi? wanasema ng'ombe amemaliza ndugu yako shulenii, hakuzimaliza kwa ajili ya kulipia shule alimaliza kwa ajili ya kulipia vifaa vya shule ambavyo havihuiani na elimu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, matokeo yake mtu anaona bora kuzaa watoto wajinga huwezi kafilisika kuzaa kuliko kuzaa watoto wenye akili. (*Kicheko/Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunamuomba sana Mheshimiwa Waziri na Waziri wa TAMISEMI walifikirie sana. Nakuona kila siku unalalamika kwamba timu zetu za Taifa watu hawana nguvu lakini watoto wanatoka asubuhi wamebeba huo mzigo uliousema sasa hivi wa hizi *counter book* 11 wana miaka minane mpaka saa tisa jioni wamekataliwa kubeba chakula kwamba kinaitwa kiporo. Kilibatizwa kitaitwa kiporo wanakwenda bila kula, lakini je wakirudi kutoka shulenii kuna mzazi atapika chakua *fresh* kwa yule mtoto, si atampa kiporo, sasa ulimkataliaje kubeba kiporo asubuhi kwenda nacho shule. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, matokeo yake sasa hivi unaweza ukaongea lugha nyingine ambayo sio nzuri, lakini watoto hawana afya, hawali chakula. Sisi Waislamu tumefunga lakini tunakula daku saa kumi lakini saa saba ukikutana na Muislamu mkali kama pilipili na ni saa saba mchana. Vipi huyu mtoto wa shule ambaye alitoka saa 12 hajala kitu chochote kule kwetu vijijiini hakuna chai wewe mwenyewe unatoka huko. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hakuna chai anakwenda mpaka kule anarudi saa tisa, saa tisa kama walikuja wageni walipewa kile chakula wakakila anaambiwa subiri usiku atakuwa na afya huyo mtoto? Na hizo mimba mnazosema

za shuleni zitakosekana kama mtu ameshinda bila kula ataacha kutongozwa kweli? Ni kweli twendeni kwenye mambo ambayo yapo *straight* kabisa. Wenzetu Wizara ya Elimu lazima wafikirie haiwezekani leo hii kwenye shule za University wame-introduce tena wanataka simu ya WhatsApp wanataka na *laptop*.

Mheshimiwa Spika, ukiongea *laptop* kwa mtu wa kijjini au mama ntilie na simu ya WhatsApp ni shilingi Milioni 1,000,000 tayari kuna miji haijawahi kuishika laki 500,000 kwa miaka 30 anaweza akafanyaje huyo mtu? Lakini je kweli toka mme -introduce hizi *laptop* na hizi elimu imepanda? Na je, watu wamekuwa *efficient*? Kwa kuwa leo mmeweeka *laptop* mbona ndio mdololo umeongezeka zaidi. Haiwezekani lazima wenzetu wafikirie upya, wanawabebesha mizigo mizito mno wazazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, leo tunalazimishwa vitatu unaambiwa kiatu cheusi kweli inawapa wazazi wakati mgumu mno kila unapofika kijjini ukiwaita watu kwenye mikutano kuwaambia habari ya shule baada ya dakika 10 unabaki una watu sita tu. Maana yake wanaona umewaletea lile zimwi ambalo linakula haliishi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naungana sana na Mheshimiwa Mpima maneno aliongea mengi kule kuhusu suala zima la elimu ni kweli kabisa kunahitaji mabadiliko makubwa. Lakini kabla ya mabadiliko Mheshimiwa Waziri atupe waraka unaoonesha kwamba wanafunzi wanatakiwa wasomee nini.

Mheshimiwa Spika, wa tajiri aje la *laptop* wa maskini atengenezewe hata *internet cafe* pale shuleni ili walipe shilingi 500 waangalie hizo *laptop* mnazotaka wa *download* watoke lakini sio kuwabebesha *laptop*.

Mheshimiwa Spika, leo hii wote humu ndani ni wazazi kila asubuhi unagongewa hodi na mtoto na ndio wanamwambia mgongee wewe hawezikukasirika, ukiamka asubuhi unawakuta wanne wanataka hela ya kwendea shule

wakanunue chakula kweli itawezekana na kila siku utalala na chenji? Je hatuoni kama watoto tunawafundisha wizi maana yake kila wakirudi ukiwauliza chenji wanasema tulinunua hiki, tulinunua hiki wana ku- *blackmail* je, huyu mtu baada ya miaka 10 hatakuwa mwizi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, si atakuwa mwizi sasa mnakataaje watoto wasipike chakula wao wenyewe asubuhi waondoke nacho waendenacho shule, na vile vile kama tunawakatalia wakale maandazi na mikate! Je, maandazi na mikate yenewe sio kiporo, si mkate una-expire baada ya siku 14 sasa haujawa kiporo na una amira. Kwa hiyo, tunamuomba Waziri wa Elimu wafikirie kama tunawatumikia wananchi wa Tanzania ambao ni maskini, hapa hatuna mpango wa kumjadili tajiri, tajiri atapeleka *private* atapeleka kila mahali *private* lakini sisi tunayemjadili ni mtu maskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni suala hili ya *University* ni kweli ukiongea wakati mwingine unaweza kuwa kama unaongea kichwa kama hakipo. Lakini makampuni yote duniani sasa hivi yanafanya biashara yanakwenda yanatafuta wateja yanatafuta hiki, lakini sijaona *University* wakiwatemblea watu waajiri haijatokea kwa wale watu wa *University* ni kwasababu wao wanasukumiwa wateja kwa hofu ya dunia kwamba usiposoma shauri yako. Kwa nini na wao wasiwe wanaenda wanatatuwa kazi kwenye makampuni ndiyo wanatangaza kwamba bwana sasa hivi tumepata kazi *NBC* mshahara shilingi 800,000, tumepata *NSSF* na Bakhresa, kwa hiyo, tayari tunazo nafasi za kazi 4,000, kama unataka kusajili lete shilingi 10,000,000 baada ya kupata *degree* na kazi hii hapa.

Mheshimiwa Spika, nalisema kwa mara ya kwanza duniani linaonekana kama ni neno la kipuuzi, lakini inaweza ikasaidia sana kwa sababu inawezekana hata ile elimu wanayotoa wao, wale watu wa ajira hawaihitaji. Kama watakuwa wameongea na mwajiri atakuja sasa kuuliza nataka niwaone vijana wangu kama wameelewa. Inawezekana muda wa kusoma badala ya miaka mitatu ya *degree* ya biashara ikatosha miezi minane huyu benki

akasema mimi wanantosha nipe nikaanje nao. Kuliko sasa hivi mimi nikishasema ni Profesa nina *degree* kazi yangu inakuwa ni kuchukua milioni 10 za watu na kuwa-*dump*, haiwezekani ni lazima na vyuo navyo viwe *committed* pia, vikatafute na vyenyewe ajira ndiyo visajili. Vyuo vikaongee na waajiri ili hata hiyo mitaala vitabadilisha sasa kulingana na soko lenyewe watakalokutana nalo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala hili la elimu kwa kuwa Mheshimiwa Rais ameliongea vizuri tuanze kulijadili kwa mapana. Mheshimiwa Mpina na Mheshimiwa Sima wameliongea lakini kwa nini elimu tunaiongea Kizungu peke yake, kuna ubaya gani watu wakafundishwa kuchunga ng'ombe za kienyeji shulenii ni kosa? Mwalimu mle ndani akawemo Mmasai, Msukuma au Mtaturu akawa anawaambia ili ufuge ng'ombe wa kienyeji unatakiwa uwatoe asubuhi kwa mwelekeo huu, uwapeleke maji kwa mwelekeo huu, je, itakuwa ni kosa? Ni lazima mtu afundishwe Kizungu? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, maana karibu wanafunzi wote wanarudi kijiji sasa hatuna mwalimu, kama alivyosema Mheshimiwa Mpina elimu ya biashara inafundishwa na Profesa wa biashara lakini hajawahi kufanya biashara. Kwa nini hatuna kitabu cha Bakhresa au *Mohamed Enterprise* ili tukitumia kwenye masomo tukafanye biashara? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kama tumesema elimu iwe wazi tusiifichefiche kama uchawi tuendee nayo tu moja kwa moja. Madaktari wanosomea hospitali ndiyo maana hatuna mgogoro na daktari lakini huku kwingine unasomea manunuzi, mnaita *procurement* kweli manunuzi ni miaka mitatu, unajifunza kununua nini miaka mitatu. Haiwezekani manunuzi miaka mitatu kweli inawezekana? (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, wale wazazi kule mtoto hawamuoni, unamrudisha kule ni miaka 25 ukimuliza umesomea nini, anasema nimesomea manunuzi. Sasa haya maduka yote nani atakuajiri maana watu wote wanunua bidhaa zao wao wenyewe. Haiwezekani! Tuongee moja kwa

moja ili wananchi waanze kuona kweli tunaongea kitu ambacho wanakielewa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo kwa kumalizia tu, nimuombea Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI watupe *regulation* ya mahitaji ya shule ili na sisi iwe rahisi kuwajibu kule majimboni kwetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kishimba, nakushukuru sana sana. Unatufundisha sana namna ya Wabunge kufikiri na kuyaona mambo kutoka kwenye ukweli halisi na tunapokuja kwenye Mipango ya Kitaifa hapa kujaribu kuainisha kutoka kwenye shida halisi hasa wale tunaotoka vijijini. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

Nilikuwa nawaza juzi tulikuwa na Sherehe ya Mei Mosi, Waziri wa Kazi yupo hapa na tumekuwa nazo Sherehe za Mei Mosi ni sikukuu ya wafanyakazi; *key word* pale ni kazi, maana ni wafanya kazi, kwa hiyo, walikuwepo hao watu wa kazi. Wale wanaokuwepo kwenye sherehe hizi ni waajiri na waajiriwa na hoja yao kubwa marupurupu, mshahara zaidi na kadhalika lakini Ulaya hiyo picha ni sawa kwa sababu Ulaya kila mtu anaajiriwa, asiyekuwa na ajira anapata ile *social/nini* sijui ya kila wiki lakini *almost everybody* anaajiriwa.

Ulaya – Marekani Sikukuu ya Mei Mosi ni ya Taifa zima lakini sisi hapa ina wenyewe, wanaoitwa wafanyakazi. Tunakuja kwa Mheshimiwa Kishimba, kwa hiyo, wanaolima, wanaofuga, wavuvi, mama lishe, bodaboda hawafanyi kazi? Zile shughuli zetu sisi Watanzania maana sisi ni *society* tofauti na ile ya Ulaya, sisi kazi kwetu ni hizi Mheshimiwa Kishimba na Mheshimiwa Mpina wanazoeleza. Ilitakiwa Mei Mosi iwe ni siku ya kujadili changamoto za kazi za wakulima, wafugaji, bodaboda, watu wote wanaofanya kazi ni sikukuu yao, ni sikukuu ya kitaifa kabisa lakini imetekwa nyara na historia ya

industry revolution ya posho na mtoa posho; ATE (Chama cha Waajiri) na wanaoajiriwa basi. (Makof)

Ndiyo maana hata kwenye uwanja wale walio wengi ambao hawashughuliki waje wafanye nini? Kwa hiyo, walimu na nani ndiyo wanakwenda kuandamana. Kidogo tunatakiwa tulitazame kwa jamii yetu na ndiyo inaathiri hata shuleni kama anavyosema Mheshimiwa Kishimba kwa nini asije mfugaji maarufu wa kijiji mwenye ng'ombe 3,000 akazungumza na watoto kuhusu ufugaji, ufugaji ni utajiri mkubwa, kilimo na uvuvi kutegemeana na jamii ya watoto wale. Kwa sababu hizi *activities* ndizo zitakazoajiri watu wengi sana na ndiyo hali halisi kabisa, ujasiriamali kwa ujumla kama walivyoeleza. (Makof)

Kwa hiyo, hili neno kazi lina shida katika *definition* yetu sisi katika jamii kama ya kwetu. *Definition* yetu sisi ya kazi, kazi ya kujiajiri siyo kazi, kazi ni lazima uajiriwe wakati sisi hapa jamii yetu watu wengi sana ni wanaojiajiri. (Makof)

Tunaendelea na Mheshimiwa Benardeta Mushashu.

MHE. BERNADETA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na wataalamu wote kwa hotuba nzuri lakini kwa utekelezaji mzuri wa llani ya Chama cha Mapinduzi ndani ya Wizara kwa maana ya uboreshaji wa miundombinu. Tumeona madarasa mengi yakijengwa, vyuo vya ualimu vikikarabatiwa, shule kongwe zikikarabatiwa; kwa kweli kwenye upande wa miundombinu mmeefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri ya kuboresha miundombinu bado kuna matatizo makubwa mawili ambayo nitayaongelea. Kwanza, shule zimepanuka au zimeongezeka, wanafunzi wameongezeka mara dufu lakini walimu wameendelea kuwa wachache. Nataka niwahahakishie mimi kama mwalimu kwamba kwenye *setting* yoyote ya elimu mwalimu ni *central*, hata ukiwachukua wanafunzi ukaweka chini ya mti lakini ukamuweka mwalimu ambaye ana ujuzi

uliokamilika yule mtoto ataelimika. Ukimchukua mwanafunzi ukamuwekea madarasa na vitabu ukamuondoa mwalimu hakuna kitu chochote kitakachowenza kuendelea. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona kwamba mwanafunzi anamaliza *form four* kutoka kwenye shule A ana *division one* na *division two*, *division three* anachaguliwa kwenda *high school* anapelekewa kwenye shule, labda anaenda kusomea tahasusi ya *PCB (Physics, Chemistry na Biology)* anakuta kuna mwalimu mmoja wa *Biology* anasoma somo moja kwa miaka yote miwili *form five* na *six at the end of the story* mtihani anapewa ule ule kama aliyejewa na walimu katika masomo yote matatu na mwisho anaambibiwa kwamba ameshindwa kwa sababu atakuwa ameshinda somo moja tu. Huyu mtoto hawezikwenda chuo kikuu, hawezikwenda mahali popote anakuwa ameharibiwa maisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwamba Serikali sasa ingeweka mkakati wa makusudi kuhakikisha kwamba wanaajiri walimu. Nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan juzi ametangaza kwamba sasa angalau tuanze na kuziba zile nafasi zile 6,000 kwa wale walitoka kwenye ualimu kwa maana ya kustaa fu au kuwa kuacha kazi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naomba katika mazingira hayo wanapokwenda kuajiri hao walimu 6,000 waungalie Mkoa wa Kagera; hadi sasa tuna upungufu wa walimu 7,607 katika shule za msingi na tuna upungufu wa walimu 1,340 katika shule za sekondari. Huo ni mkoja mmoja, je, Taifa zima ikoje? Kwa hiyo, napendekeza kwamba kuwe na mkakati wa makusudi, vibali vitolewe, walimu waajiriwe ili wanafunzi waweze kuipata elimu tarajiwa.

Mheshimiwa Spika, tatizo la pili, kuna malalamiko makubwa sana juu ya elimu itolewayo kwamba haikidhi matarajio ya wanaopata. Utawakuta wasomi wanalamika, waajiri wanalamika kwamba wanafunzi wanaowapata hawana zile stadi zinazohitajika katika viwanda na

makampuni yao. Pia wahitimu na wenyewe wanalamika kwamba elimu waliyoipata haiwapi ajira na wala haiwawezeshi kuweza kujajiri.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwamba labda tungejifunza kutoka kwenye nchi ya China. China kwenye miaka 1970 walikuwa wanafahamika kwamba ni nchi maskini duniani, lakini wakagundua kwamba ili waweze kutoka kwenye huo mkwamo lazima waboreshe elimu yao. Wakafumua mfumo wao wa elimu, sasa hivi China ni ya viwanda, *it's a second largest economy in the world*, vilevile ni wazalishaji wa mali mbalimbali ambazo zinasambazwa kote duniani. Hii ni kwa sababu waligundua kwamba elimu watakayokuwa nayo ni lazima iwe ni elimu ambayo inakuza ujuzi. Ili tufikie kwenye Tanzania ya viwanda lazima tubadiliike, tutoke kwenye hii kufundisha *general academic knowledge* twende kufundisha elimu ambayo inakuza ajira na ujuzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, China wao walirekebisha sheria zao za elimu, lakini kilichowafanya wafumue mfumo wao wa elimu ni walipogundua kwamba wanahitaji *skilled labor* ya kuweza kufanya kazi kwenye viwanda wakakuta kwamba huo utaalamu hawana. Tangu wabadilishe mfumo wao uchumi ukakua na kama mnavyojuwa sasa hivi uchumi wa China unakua kwa asilimia 10 kila mwaka, kwa hiyo wana uchumi mkubwa duniani. Serikali ikaweka fedha nyngi katika elimu, wakafanya *reforms* mbalimbali na wakaweza kufikia hapa walipofikia.

Mheshimiwa Spika, kitu cha kwanza walichofanya wakahakikisha kwamba elimu msingi ambayo inaenda mpaka sekondari ikawa *compulsory* (ni ya lazima). La pili, wakarekebisha mitaala. Mitaala yao sasa hivi 1/3 ya mtaala ndio inafundisha *general academic knowledge*, 1/3 ya mtaala wa China, elimu kuhusu fani mbalimbali zinazohitajika katika Maisha lakini 1/3 lazima huyu mtoto ajifunze kazi mojawapo ambayo inapatikana katika Serikali yake ya Mtaa kwa sababu wanategemea kwamba ataenda kuajiriwa kule. Vilevile wameanzisha kozi mbalimbali ili kufikia mahitaji ya

viwanda. Kuna mahusiano na mikataba inawekwa kati ya shule na viwanda kila mwisho wa *term* wanafunzi wanaenda kwenye viwanda kusudi waweze kunoa ule ujuzi wao na wanafunzi kutoka kwenye familia masikini walikuwa wanalipiwa karo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, elimu ya kukuza ujuzi wanaianza mapema kabisa wakiwa kwenye *junior secondary school* ambapo sasa si watoto wameshapata ujuzi huu, wanapomaliza *junior secondary school* ambayo iko kama kwenye *form two* hapa wao asilimia 11.6 wanaenda moja kwa moja kwenye ajira kwa sababu tayari wana ujuzi, wanaweza kuajiriwa sehemu mbalimbali. Asilimia 88.4 hawa wanaendelea na *senior secondary school* lakini kati ya wale walioenda kwenye *senior secondary school* asilimia 47 wote wanaenda kwenye *VETA* na vyo vya ufundi kusudi sasa waweze kupata ujuzi ambaou unahitajika. Mwisho wa muhula wanafunzi wanaenda kwenye viwanda lakini kabla ya *graduation* kila mwanafunzi lazima apite kwenye *internship* kama tunavyoona hapa madaktari wanafanya.

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa upande wa walimu ili uweze kufundisha kwenye *secondary* lazima uwe na angalau *degree* moja. Sisi hapa tunapeleka *division three* na *there was a time* tulikuwa tunapeleka hata *division four*. China wanapeleka wale *cream* ndiyo waweze kuwa walimu waje wawafundishe Watoto vizuri.

Mheshimiwa Spika, wakati wa likizo walimu lazima waende viwandani, wawasiliane na wenye viwanda na wenye makampuni wajue, je, wanachofundisha darasani ndiyo kinachohitajika? Aidha, walimu ambaou wako kwenye vyo vya ufundi ni lazima kila mwaka aende kukaa kiwandani kwa muda wa mwezi mmoja akiwa ananoa *skills* zake. Ili mwalimu apande cheo kama tunavyoona kwa mapolisi lazima kwanza afanye *practical training* kwenye kiwanda. Kama tunavyoona polisi lazima asomee vyeo na wao wanaenda wanafundishwa ndiyo wanaweza kupanda vyeo.

Mheshimiwa Spika, mwisho wanawa-expose hawawafungii, wanaenda kwenye nchi mbalimbali wanajifunza *best practices* halafu wakija wanaboresha mfumo wao wa elimu. Pamoja na kozo ndefu lakini wana kozi fupi za kumnoa mtu. Sisi hapa mtu akiajiriwa mpaka astaaufu hajawahi kwenda kwenye kozi nytingine. Kwa hiyo, anafundisha hata elimu ambayo imepitwa na wakati, wao wana *re-training, on job training* na kadhalika. Ndugu zangu nasisitiza elimu ya ujasiriamali kwa China ni lazima. Kwa hiyo, nafikiri tukiiga mfano huu tunaweza tukaboresha elimu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Wizara ya Eilimu na wote wanaohusika na mambo ya elimu wakubali kwamba kuna tatizo kwenye mfumo wetu wa elimu. Wafungue mjadala mpana kusudi Serikali, waajiri kwa maana ya makampuni na viwanda, wasomi pamoja na watunga sheria kwa maana ya Bunge tujadili tuangalie mfumo wetu kuna tatizo wapi? Kitu gani kinakosekana na tuongeze nini hiyo ndiyo itaweza kutupeleka kwenye dira yetu ya uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana Mwalimu Benardeta Mushashu kwa kutupa uzoefu wa China.

Tunaendelea na Mheshimiwa Judith Kapinga atafuatiwa na Mheshimiwa Nusrat Hanje.

MHE. JUDITH S. KAPINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Aliyekuwa Rais wa South Afrika Hayati Nelson Mandela, Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi, aliwahi kusema na nitamnukuu: “*From the poorest of countries to the richest of nations, education is the key to moving forward in any society*”. Kwa lugha yetu ya Taifa anasema kuanzia kwenye nchi masikini kabisa hadi mataifa tajiri kabisa elimu ndiyo ufunguo pekee wa maendeleo katika jamii yoyote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, maneno haya kwa namna moja ama nyingine yalielezwa na Rais wetu mpendwa na anayewapenda Watanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan tarehe 6 Aprili, wakati wa hafla ya kuwaapisha Makatibu Wakuu na Manaibu Makatibu Wakuu na alisema napenda nimnukuu: "Lazima kufanya tathmini ya elimu itakayomsaidia Mtanzania. Tuangalie mitaala yetu tuone mtaala utakaotupeleka mbele na kukuza Taifa letu". (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, maneno haya ya Rais wetu mpendwa kwa namna moja ama nyingine yanatuonyesha umuhimu wa mfumo wa elimu katika kuongeza kasi ya maendeleo kwa taifa letu. Mfumo wa elimu kwa namna moja ama nyingine ndiyo unaoamua nguvu kazi ya taifa letu itasukuma vipi gurudumu la uchumi katika nchi yetu. Mfumo wa elimu ndiyo unaoamua ajira za wananchi wa Tanzania zitapatikana vipi na kwa kiasi gani. Mfumo wa elimu ndiyo unaoamua umaskini katika taifa letu utaondolewa ama utapungua kwa kiasi gani na kwa wakati gani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nasema haya kwa sababu mengi yameongelewa kuhusiana na kubadilisha mfumo wa elimu lakini mimi napenda kujikita katika namna ya kulinda mfumo wa elimu. Hata kama tutafanya mabadiliko ya mfumo wa elimu tusipolinda mfumo wa elimu ni sawasawa na kutwanga maji kwenye kinu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijaenda kwenye kueleza namna gani tunapaswa kulinda mfumo wa elimu, hapa ningependa nimpongeze mama yangu Mheshimiwa Prof. Joyce Ndalichako; kwa kipindi hiki ambacho amekua Waziri tumeona mabadiliko yasiyo na tija na ya haraka katika mfumo wa elimu, kidogo yameweza kuwa *contained*. Huko nyuma mabadiliko katika mfumo wa elimu yanikuwa yanaweza yakafanyika *abruptly*, muda wowote na ku-*disturb* walaji ambao kwa kiasi kikubwa ni vijana wa Taifa hili. Kwa hiyo, Mheshimiwa Prof. Ndalichako kwa kipindi hiki ambacho amekua Waziri, amejitahidi sana kuwalinda walaji ambao ni vijana wa Tanzania. Hongera sana mama yangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda nijielekeze ni kwanini tunapaswa kulinda mfumo wa elimu, kwa sababu mabadiliko yoyote katika Mfumo wa Elimu yanaweza kuathiri vijana wa Taifa hili kwa kiasi kikubwa sana. Tunashukuru Mungu leo tuna Mheshimiwa Prof. Ndalichako, kesho hatutakuwa naye. Kwa mantiki hiyo, inatupasa kulinda mfumo wa elimu kwa kuweka taratibu ambazo zitalinda misingi ya mfumo wa elimu. (*Makofii*)

Mhehimiwa Spika, hapa napenda kutoa mifano michache ili muweze kunielewa. Mwaka 1997 aliamka mtu akafuta *UMITASHUMTA*, lakini tunashukuru Serikali ilirudisha *UMITASHUMTA* mashulen na sasa hivi inafanyika katika utaratibu mzuri tu. Hii ilikuwa hatari sana kwa sababu wote tunajua michezo namna ilivyo *multibillion industry* duniani.

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano wa pili. Kuna kipindi pia kuna mtu aliamka akaamua akataka kuunganisha *Chemistry* na *Physical*; yaani kipindi kile somo hili lilitakiwa liitwe *Physics with Chemistry*. Tunashukuru mambo haya hayakuweza kufanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nitatoa mfano wa tatu, mwaka 2014, Kidato cha Nne waliwekewa alama zao za ufaulu kwa kutumia wastani wa *point* ama kwa lugha nydingine *GPA*. Vijana waliomaliza 2014 na 2015 waliwekewa kwa mfumo huu na sababu zilizotolewa kipindi kile, ni ili tuwe na *system* inayofanana. Mwaka 2016 tukarudisha mfumo ambao tumeuzoea wa *division*. Kwa hiyo, tuna wanafunzi katika nchi hii ambao kuna kipindi waliwekewa *marks* zao kwa mfumo wa *GPA*, baadaye ikabadilishwa ikarudisha *division*. Nasema haya ili mnielewe ni kwa nini inatupasa kulinda mfumo wetu wa elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mfano mwengine, Serikali iliwahi kugharamika kupeleka walimu nje waweze kujifunza *programme* za *re-entry*, kuwasaidia watoto wa kike wanaopata ujauzito waweze kuwa *accommodated* tena katika mfumo wa elimu. Zoezi hili lilikuwa *frustrated* kwa sababu lilikuwa halilindwi. Baadaye ikaonekana halina

mantiki, likawekwa kwenye kapu, lakini tayari tuligharimika kuwasomesha walimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine, ilitokea programme ya voda fasta ya walimu kusomeshwa miezi mitatu. Walimu walismeshwa na wakapelekwa kufundisha watoto wetu na kuambiwa kwamba wana-*qualify*. Miezi hii, mitatu! Naeleza haya ili kuonesha ni kwa nini tulinde mfumo wetu wa elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo hii mtoto wa miaka mitatu yuko *boarding school*. Mtoto wa miaka mitatu mama yake au baba yake amempelea *boarding school*. Naeleza haya ili tuweze kuona hatari hizi na kuona umuhimu wa kulinda mfumo wetu wa elimu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo ningependa sasa nilieleze hapa, leo hii kuna vijana katika nchi hii walisoma miaka mitatu chuo, walivyomaliza wakaambiwa vyeti vyao havitambuliki. Inawezekana sisi tukawa tumesahau, lakini wale vijana hawajasahau, wamelibeba hili kwenye mabega yao na kwa machozi zaidi ya miaka saba sasa wanatembea nalo bila kupata msaada. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama mnakumbuka, Chuo kilikuwa kinaitwa Chuo cha Kilimo Mbeya (*Mbeya Polytechnic College*) kati ya mwaka 2013 mpaka 2016. Chuo hiki kilipewa usajili na *NACTE*, vijana walisajiliwa na kudahiliwa na walisoma pale miaka mitatu. Baada ya kusoma miaka mitatu, vijana hawa wakaambiwa vyeti vyao havitambuliki. *NACTE* wakasema Chuo chenu kilikuwa hakilipi ada za usajili. (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Mheshimiwa Jidith, muda hauko upande wako.

MHE. JUDITH S. KAPINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Katika Wabunge vijana, Mheshimiwa Judith Kapinga, tofauti ya elimu ile ya mwanzo wa uhuru na elimu hiyo unayosema ina mabadiliko ya kunavyokucha, nafanya utani; ni kwamba elimu ya zamani ilikuwa chini ya Wizara ya Elimu ya Taifa. Elimu ya sasa iko chini ya Wizara ya Elimu. Kuna tofauti, *I am joking*. Mheshimiwa Nusrat. (*Kicheko/Makofi*)

MHE. NUSRAT S. HANJE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie katika Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia na nitaomba niseme yafuatayo kwanza. Wanafunzi wanaweza kuwa 20% tu ya *population* yetu. Yaani *students may be 20% of our population, but they are 100% of our future*. Kwa sasa tunaweza tukaona wanafunzi kama sehemu tu, kwa sababu ni sehemu ndogo ya jamii yetu, lakini kwa maisha yetu yajayo, wanafunzi ndio watakuwa sisi, yaani watakuwa 100% ya *population* yetu. Maana yake kuna umuhimu mkubwa sana wa kuwekeza nguvu zetu na uwezo wetu wote kwenye mfumo wetu wa elimu Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Sera ya Elimu ya mwaka 2014 dhima yake ni kuwa na Mtanzania mwenye maarifa, ustadi, umahiri, uwezo, na mtazamo chanya katika kuchangia maendeleo ya Taifa. Sasa katika mambo haya ambayo tunasema ndiyo dhima ya elimu katika Sera ya Elimu ya mwaka 2014, hatuwezi kuyazungumza haya bila kutaja ubora na kuboresha mfumo wetu wa elimu.

Mheshimiwa Spika, nitazungumza kidogo kuhusu udhibiti ubora. Ripoti ya CAG inaonyesha kwamba kumekuwa na upungufu mkubwa sana wa udhibiti ubora kwa 8%, baadhi walishazungumza. Tumepeleka wadhibiti ubora 98 katи ya 1,306 ambayo ilikuwa ndiyo kusudio. Sasa kwa kutekeleza hili, maana yake hawa ndio wanaoenda kuangalia ubora wa elimu yetu. Sasa tumetekeliza kwa 6% tu, ni jambo ambalo linavunja moyo kiasi kubwa. Kwa hiyo, hata kama kuna mambo makubwa tunayapanga, lakini katika ufuatiliaji, tunawategemea watu ambao ni wadhibiti ubora kwa ajili ya kwenda kuangalia utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, hili siyo jambo la kihisani, ni suala ambalo liko kisheria. Katika Sheria ya Vyuo Vikuu ya Mwaka 2005 kifungu cha 27 inaeleza hayo, lakini pia katika Sheria ya Baraza la Elimu ya Ufundii ya Taifa (*NACTE*) ya Mwaka 1997 Kifungu (5) na (1) kinavitaka Vyuo Vikuu na Vyuo vya Ufundii kuwa na utaratibu na kujivekeea miongozo ya kudhibiti ubora ili kuhakikisha kwamba elimu yetu inayotolewa Tanzania kweli iaakisi 100% ya *population* yetu ya Taifa *in the future*, ambayo *future* hatuzungumzi miaka 3,000 ijayo.

Mheshimiwa Spika, hawa hawa wanafunzi baadaye watakuja kuwa Mawaziri na watakuja kuwa watendaji. Sasa ubora wa elimu yetu tunategemea hawa watu wakadhibiti, lakini tumeweza kwa 8% tu jinsi ambavyo hatuweki nguvu katika udhibiti ubora. Ni jambo ambalo linasikitisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumze kidogo kuhusiana na mtaala. Kwanza ni-*declare interest*, mimi ni mwalimu *professionally*. Nimeona vivu kidogo, kuna wenzangu wameanza kuchangia wameitwa Walimu; kwa hiyo, kwenye *record* yako naomba iingie kwamba nami pia ni Mwalimu. (*Makofii*)

SPIKA: Mwalimu Nusrat Hanje. Nashukuru tumefahamu sasa. (*Kicheko/Makofii*)

MHE. NUSRAT S. HANJE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza elimu yetu ina tatizo kubwa sana. Kimsingi ninakusudia kuleta maelezo binafsi kwenye Bunge hili kushauri kama mionganoni mwa watunga sheria kwenye Bunge hili Tukufu namna ambavyo elimu yetu inaweza kusaidia vijana wetu na hasa ambao tunategemea watakua 100% of our future. Elimu yetu inakosa mambo matatu ya msingi. Inakosa kitu kinaitwa *Person Development*. Juzi ljumlaha niliuliza swali kwenye Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kuhusiana na kufanya *topic* ya *life skills* kuwa somo kuanzia Darasa la Tano mpaka *Form Four* na tutaangalia *Form Five* na *Six* tuone namna bora ya kujenga uwezo wa kibinadamu, uwezo na utashi wa kimtu, kwa sababu ndiyo dhima ya Sera ya Elimu ya Mwaka 2014, ambayo inataka kujenga Mtanzania

mwenye maarifa, ustadi, umahiri na uwezo na mtazamo chanya katika kuchangia maendeleo ya Taifa. Sasa tunakosa kitu kinaitwa *personal development*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ushawahi kutoa tafakuri tunduizi hapo hapo kwenye kiti chako kwamba unashangaa kwamba Watanzania hatuna uaminifu? Kwa nini mtu anaaminiwa afanye kitu na anashindwa ku-*perform* kama ambavyo aliyemwamini amempa wajibu huo? Hilo siyo katika biashara tu, kuna vitu vingi ambavyo Watanzania; vijana wanaotoka vyuoni wanashindwa ku-*perform*.

Mheshimiwa Spika, leo watu kama Marehemu Ruge, kwa kweli tunatambua mchango wake mkubwa kwenye Taifa hili, anaonekana ni *genius*. *Everybody is genius, but if you judge a fish by its ability to climb a tree it will live its whole life believing it is stupid.* Yaani kila mtu ana akili, lakini kama tutamhukumu samaki kwe uwezo wake wa kupanda mti, hataweza kushindana na nyani. Nyani ana uwezo wa kupanda mti kuliko Samaki. Samaki anaweza kuogelea. Kwa hiyo, samaki ana uwezo wa kuogelea, kwa hiyo, anatakiwa apelekwe baharini na nyani apelekwe kwenye miti kwa sababu ndiyo ana uwezo huko. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa mfumo wetu wa elimu unawafanya watu baadhi wenye mawazo mbadala kwa sababu ya kujipa maarifa kwingine waonekane wana uwezo mkubwa. Tumeshasema, ili ulime kilimo cha biashara, ni lazima uanzie sokoni, ukajue soko linahitaji nini ndiyo ukalime. Huwezi kulima ndiyo ukatafute soko. Sasa mtu akizungumza hivi, anaonekana ni *genius*, lakini ni suala ambalo tunatakiwa *train vijana* wetu kwenye Taifa, kwenye *personal development*; uwezo wa kuthubutu. Tuna tatizo la kubwa la uthubutu. Watu hawawezi kuthubutu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nitaleta maelezo binafsi kuelezea kwa nini tunasema vitu vitatu vinakosekana katika elimu yetu? Jambo la pili ambalo linakosekana ni kitu kinaitwa *financial literacy*. Sisi walimu tunafundisha shulenii *financial knowledge*, ndiyo tunafundisha *accounts*, yaani mtu

anafundishwa kufugua makabati; anatakiwa akajibu mitihani ili aonekane ana akili, afaulu aende darasa la mbele. Leo ninyi hapa Bungeni tulivoapishwa tu, tuliletewa wataalamu wa fedha waje kutushauri *how much do we spend? How much do we invest? How much do we save? How should we donate?* Spirit ya donation watoto wanatakiwa wafundishwe kwenye nchi hii. Tunatakiwa tuanze ku-*train* vijana wetu wakiwa mashulen i *financial literacy*, siyo *financial knowledge*. *Financial Knowledge* inamfanya akajibu mitihani afaulu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala la tatu, ambayo elimu yetu haitupatii, ni kitu kinaitwa *Career Development*, amezungumza Mheshimiwa Mpina, ambayo inamfanya kijana aliyepo shulen ajue, akutane na watu ambao wanafanya kitu ambacho anatamani kukifanya. Siyo mimi nina kipaji cha kucheza mpira, lakini kwa sababu sijawa *trained* vizuri, mimi *role model* wangu anakuwa mwanasiaya, *come on!* Yaani tunatakiwa tuwa-*connect* vijana wetu na watu ambao wana- *inspire* kwenye maisha, tangu wakiwa shulen. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, vitu tatu vya msingi, kama kuna mwalimu humu katika walimu uliowataja au wataalamu ma-*professor* ataniambia hivi vitu vinapatikana kwenye mfumo wetu wa elimu, basi nitakuwa nimekosea, lakini kwa sababu ninajua hivi vitu tunavisoma tukitoka; kuna watu wanaitwa *motivational speakers* mnawajua, ndiyo vitu wanavyovizungumza, ni hivi hivi kwa sababu wanajua mfumo wetu wa elimu hauwapi hivi vitu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mfumo wetu wa elimu upo *Paper Oriented*. Duniani *model* ya elimu bora kabisa duniani, *the best education system in the world* ni ya Finland. Kuna watu wanazungumza kuhusu China; kwenye uchumi, sawa ni China kwa sababu tunaona *performance outcome* yake, lakini *the best education system in the world* ni ya Finland. Wameweza kufanikiwa kwa sababu watoto hawafanyi mitihani. *Standardized testing*; kuna watu wamefeli *Form Four*, lakini leo ndiyo *billionaires*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuna waliofaulu sana tunawajua sana ma-*professor*wapo hapa, tunakutana nao huko na nini, tunashukuru, tunawapongeza kwamba mmesoma na nini, lakini tunawajengea watoto wetu uelewa mbaya kuhusiana na nikifeli, maana yake sina uwezo. Yaani mfumo wa elimu unanilazimisha mimi hata kwa *cram*, hata kwa kuibia, ndiyo maana tuna watoto wanamaliza Darasa la Saba hajui kusoma na kuandika na utashangaa amefanya mtihani kafafulu. Vipi? Kumbe kuna watu wana vipaji vyatupiga chabo. Mnajwa chabo!

Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu tulikuwa tunasema kudesa. Kuna watu wana uwezo wa kudesa, anafaulu, lakini hana uwezo. Yaani *the output, material* ambayo inatoka chuoni haiwezi kuwa *challenged* kwa sababu iko *very low*. Yaani ile *output* ya kutoka vyuoni bado kuna shida kwa sababu tupo *Paper Oriented*.

Mheshimiwa Spika, bado kuna tatizo kubwa sana la...

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mwenye taarifa endelea, Mheshimiwa Saashisha.

TAARIFA

MHE. SAASHISHA E. MAFUWE: Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge anavyochangia madini ya kutosha hapo, lakini nillitaka nimpe taarifa tu kwenye eneo aliosema la *career development* kwamba kwenye hoja yake sasa ni vizuri *career development* ikaingizwa kwenye kozi za ile tunasema ni *seven, four, two, three plus*. Ile mwaka wa mwisho, *career development* ifundishwe hapo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu msemaji anayeendelea kuzungumza, kama hayatafundishwa, wanafunzi wanafika chuoni ndiyo wanaanza kujadiliana,

anayemaliza *Form Six*, wewe unataka kwenda kusoma nini? Mwanasheria; au mwingine baba yake kwa sababu alifanya vizuri kwenye Hesabu, anamwambia kasome Hesabu, lakin kuna kitu kinaitwa *core curriculum*. Kama haya mambo yote yakiunganishwa na hii *career development*, hata watoto wanapomaliza kwenye ile *seven* ya mwisho, wafundishwe kwamba wewe kwa namna ulivyo, tunavyokuona, tunadhani uende hivi na utashi ulionao kwa kuzingatia mawazo ya watoto.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitaka nimwongeze tu kwamba *career development* ni sehemu muhimu sana ya kubadilisha na ku-transform *mindset* za wasomi wa nchi hii. Ahsante. (*Makof!*)

SPIKA: Mheshimiwa Nusrat, unapokea ushauri huo?

MHE. NUSRAT S. HANJE: Mheshimiwa Spika, napokea. Kimsingi nampongeza pia aliyezungumza. Pia, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa sababu wakati nauliza swali alisimama mwenyewe akasema kwamba atafungua mjadala kwa ajili ya wadau kutoa maoni yao. Nafikiri hayo pia ni sehemu ya maoni ambayo tutayatoa. Kwa hiyo, naipokea. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie katika eneo moja. Wakati tunarekebisha mitaala yetu tukumbuke kwamba kuna wale vijana ambao wanamaliza shule ya msingi wanashindwa kuendelea na Sekondari na kuna wale wanaomaliza *form four* wanashindwa kuendelea na elimu ya juu zaidi; wale kwenye mtaala wetu tuwawekee utaratibu ambao katika stadi za kazi wanazosoma shule wakafundishwe vitu kutokana na uchumi wa maeneo yao husika.

Mheshimiwa Spika, mathalani, maeneo ambayo kuna migodi... (*Makof!*)

(Hapa Mhe.Nusrat S. Hanje sauti yake ilikauka sauti)

SPIKA: Pole sana Mwalimu. Hakuna maji karibu hapo!
(*Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Amefunga.

SPIKA: Amefunga loh! Pole sana. (*Kicheko*)

MHE. NUSRAT S. HANJE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nimalizie taratibu taratibu. Maeneo ambayo labda kuna migodi, maziwa na mito ambapo tunategemea watu wa pale wengi ni wavuvi...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Naambiwa ya pili tayari. Basi sentensi moja tu.

MHE. NUSRAT S. HANJE: Mheshimiwa Spika, basi tunategemea pia wale wananchi na wanafunzi wanaopewa elimu katika maeneo husika, basi wakafundishwe kwa sababu wengi wakimaliza wanashindwa kuendelea na vyuo, wanarudi mtaani, halafu wanaanza kujifunza upya kuhusu kilimo, kuhusu uvuvi, kuhusu uchumi unaopatikana kwenye hilo eneo. Kwa hiyo, stadi za kazi zikafundishwe kutokana na uchumi wa eneo husika ili wale vijana wanaoshindwa kuendelea na vyuo waende kufanya shughuli za uzalishaji mali katika maeneo husika. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Nusrat. Wabunge vijana hao. Halafu watu wanasema, Bunge la Ndugai limezubaa. Hao watu wako wapi? Hili Bunge kweli kweli! / am proud of you Wabunge wangu. Ahsanteni sana, mnatubeba. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Neema Lugangira, atafuatiwa na Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Aloyce Kamamba.

MHE. NEEMA K. LUGANGIRA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwanza kabisa, napenda kuipongeza Serikali kwa

kuja na Sera ya Elimu bure na uwekezaji mkubwa katika miundombinu. Napenda niseme kwamba, kama tutaendelea kutotilia maanani suala la lishe shulen, jitihada hizi zote zipo hatarini.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu mtoto anapokuwa darasani lazima aweze kufikiri, kuelewa, kuchakata na kukariri kile anachofundishwa na mwalimu; lakini kama ubongo wake haufanyi kazi vizuri, kama ubongo wake haujapata virutubisho sahihi, basi mtoto huyu hawezi kujifunza ipasavyo na hiyo ni sawa sawa na kutegemea gari lisilo na mafuta liweze kutembea.

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wanatoka nyumbani alfajiri, wengi wanakuwa hawajala, wanakwenda shule wanashinda njaa, akiwa darasani tumbo linanguruma, tumbo linanguruma kwa sababu linakosa kitu cha kusaga na kupeleka kwenye ubongo. Kwa hiyo mwanafunzi anakosa umakini kiasi kwamba Mwalimu anaweza kutoka kufundisha, ukamuuliza mwanafunzi mwalimu kasema nini akasema sijui. Mtoto yule ukahangaika kumpiga na kusema kwamba ni mtukutu, hana adabu, hasikilizi darasani lakini kumbe ubongo wake uli-cease kufanya kazi kwa sababu ya njaa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ningependa kuikumbusha Serikali kwamba pia hali ya udumavu nchini inachangia kwa kiasi kikubwa kwa watoto kutoweza kufaulu na kufundishika shulen. Wenzetu wataalam wa lishe TAMISEMI wanatuambia kwamba katika kila darasa la watoto 45, watoto 15 hawafundishiki. Sasa tupate picha tuna jumla ya wanafunzi milioni 11, kama katika kila 45 15 awafundishiki ina maana pamoja na jitihada zote hizi tunaendelea kufifisha hizi jitihada kutokana na uwelewa na ufaulu ndio maana unakuwa huko chini.

Kwa hiyo naiomba Serikali iweke mikakati madhubuti ya kuhakikisha kwamba kila shule hususani za kutwa pia wanazalisha mazao yenye lishe kwa mfano viazi lishe, maharage lishe, mahindi lishe na mengineyo ili kuhakikisha kwamba watoto hawa hawashindi shulen wakiwa na njaa.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kusema kwamba pamoja na jitihada zote za elimu bure pamoja na jitihada zote za miundombinu bora, ikiwa bado tutaliweka pembeni suala la lishe shulenii jitihada hizi zote zitafifisha malengo ya Serikali ya kuhakikisha kwamba elimu yetu inanufaisha watoto wa kitanzania. Kwa hiyo naiomba sana Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ije na mkakati madhubuti tunakwenda kufanya nini ili kuhakikisha watoto wanapata lishe shulenii.

Mheshimiwa Spika, eneo langu la pilii ni upande wa hedhi salama. Naipongeza sana Serikali kwa mikakati mbalimbali iliyowekwa kuhakikisha mtoto wa kike anabaki shulenii, kuhakikisha kwamba mtoto wa kike analindwa ili apate elimu. Hata hivyo, mtoto huyuhuyu wa kike kila mwezi anapofika umri wa kubalehe anakosa siku tano mpaka siku saba kwa sababu ya kuwa kwenye hedhi. Kwa hiyo suala hilli pia naiomba Serikali illilie mkazo. Nafahamu kuna bajeti ndogo kwenye elimu bure ya kupata msaada wa taulo za kike kwa dharura lakini Serikali iweke wazi kwa sababu dharura zinakuwa nyingi, lakini pia Serikali ije na mkakati madhubuti katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano mdogo tu, kwenye shule za msingi kuna wanafunzi wa kike 5,481,982; kwenye shule za sekondari kuna wanafunzi wa kike milioni 1,284,410; kati ya hawa wote tukichukulia tu asilimia 20 wako kwenye umri wa kubalehe ina maana tuna jumla ya watoto milioni 2,380,806 ambaao kila mwezi wako hatarini kukosa shule siku tano mpaka siku saba. Hili ni jambo zito sana ambalo Wizara inabidi iliangalie kwa jicho la kipekee. Wale ambaao wanakwenda shule, wanatumia vitu ambavyo ni hatari sana kwa afya zao, wanatumia mabanzi, wanatumia magazeti, wanatumia vitu ambavyo vinapelekea na naamini kwamba vinachangia kwa ongezeko kubwa la kansa ya shingo ya kizazi. Kwa hiyo naiomba sana Serikali ione namna gani itaweza kusaidia na kuhakikisha kwamba mtoto wa kike hakosi shule kwa sababu ya kuwa kwenye hedhi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia naamini kwa sababu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ni mama yetu

Profesa Ndalichako na haya masuala yote mawili lazima yanamgusa moja kwa moja kama mama, naamini kabisa atakuja na mpango madhubuti wa kuhakikisha moja watoto wanapata lishe shulenii, lakini pili, mtoto wa kike hakosi shule kwa sababu ya kuwa kwenye hedhi. Nashukuru sana. (*Makofii*)

TAARIFA

MBUNGE FULANI: Taarifa Mheshimiwa Spika.

SPIKA: Nadhani siiruhusu kwa sababu ameshamaliza kuongea, hiyo taarifa imechelewa. Ahsante unaweza kuitoa kwa mwongeaji mwingine.

Kuhusu lishe kwa mfano shule nyingi kama Mkoa wa Dodoma na mikoa mingine mingi, shule zina maeneo makubwa tu ya ardhi yanayofaa kulima, lakini unakuta shule haina hata magunia mawili ya mahindi au mtama kwa sababu hii ya sera ya sasa hivi ya kwamba watoto wasichangamke kidogo na vijembejembe kwenye maeneo yao ya shule, wangeweza kabisa kila shule ikapata hata magunia 70, 50 kwa kuanzia tu kabla ya kuwaambia wazazi wachangie.

Sasa mtoto umemchukua umempeleka shulenii, kwa hiyo mzazi umempunguzia nguvu kazi ya kufanya nayo kazi nyumbani, amehangaika peke yake, kiangazi kikifika unamwambia aende kuchukua chakula apeleke shulenii. Hivi ni vitu vyta kuvitazama kwa sababu baadhi ya vitu ni kujipanga tu, kwa sababu ardhi tunayo.

Mheshimiwa Aloyce Kamamba na muda ukiruhusu basi Mheshimiwa Festo Sanga.

MHE. ALOYCE J. KAMAMBA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye bajeti hii ya Elimu. Kwanza niipongeze Wizara ya Elimu kwa kazi kubwa nzuri sana ya kuratibu na kusimamia elimu nchini, hongereni sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pili, nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuitia hotuba yake ya juzi katika Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi aliweza kuondoa kwenye asilimia ile inatozwa kwa wafaidika wa mkopo, asilimia sita, tunapongeza sana kwamba hiyo alizingatia na kuondoa. Vile vile nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuratibu mafunzo kwa vijana wetu waliomaliza darasa la saba na kidato cha nne ambayo utekelezaji wake unaendelea sasa.

Mheshimiwa Spika, elimu bora ni ile inayotoa maarifa stadi na ujuzi kwa yule anayejifunza ili yamsaidie kukabili Maisha. Sasa kwa upande wa mtaala wa elimu katika nchi yetu mtaala uko vizuri, upungufu wake ni kumwongea maarifa stadi yule anayemaliza ili aweze kukabili maisha. Wapo vijana wamemaliza darasa la saba, wapo vijana wamemaliza kidato cha nne, wapo waliomaliza kidato cha sita, wapo waliomaliza *degree* na tunao mfano Walimu wako mitaani, wapo Madaktari wapo mitaani, muda huu wana maarifa ya ziada ya kuweza kuyakabili maisha wanaposubiri kuajiriwa. Kinachotokea hapo ni kwamba hapana, ndicho hicho ambacho sasa tunashauri kwamba Wizara iangalie katika mtaala wake waongeze maarifa hayo yatakayokuja kuwasaidia vijana wetu katika maisha.

Mheshimiwa Spika, nilifanikiwa kuwepo Uganda na Kenya kule kwa upande wa shule ya msingi wana somo linaitwa uchumi. Hilo wanasoma kuanzia Shule ya Msingi lakini kwa wale wanaosoma kwa hatua ya cheti au *degree* na kadhalika, huyo ambaye anategemea kusoma hawezi akapewa *degree* yake bila kusoma somo la ujasiriamali au *entrepreneurship*. Kwa hiyo, kwa maana ile asipopata yale maarifa hawezi akapewa *degree* yake. Ninachoomba kiongezwe hicho katika mitaala yetu, anapokuwa chuoni anasoma Ualimu au anasoma Udaktari aongezewe maarifa hayo ili yamsaidie, anapokosa kwenye ile kozi iweze kumsaidia kwenye maisha yake.

Mheshimiwa Spika, kwenye upande wa wale wanaomaliza kwenye kidato cha nne au kidato cha sita,

wengi wamezungumza masuala ya *VETA*. Niombe sana *VETA* ziongezwe kila wilaya kwa makusudi ya kwamba yejote ambaye hakufanikiwa kwenda kidato cha sita, amemaliza kidato cha nne au amemaliza darasa la saba hakufanikiwa kwenda kidato cha kwanza mpaka cha nne, basi aweze kupata maarifa chuoni. Inaweza ikawa kwenye ufundi ujenzi, ufundi mbao au kilimo, hayo yatamsaidia.

Mheshimiwa Spika, katika hilo kuna mkopo unaotolewa kwenye vyuo vikuu, naona haja ya kushauri Serikali iweke mikopo kwa wanafunzi ambao wana soma kwenye vyuo hivi vyta kat. Kuna nchi kama Uchina...

SPIKA: Mheshimiwa Kamamba sikukatizi, lakini kwa nini tunajenga hii *concept* ya kwamba *VETA* ni kwa wale wasiofanikiwa yaani hiyo inajenga kama kitu fulani *inferior* hivi. Endelea tu na mchango wako Makamu Mwenyekiti.

MHE. ALOYCE J. KAMAMBA: Mheshimiwa Spika, nazungumza hivi kwa sababu hilo kundi ambalo linakuwa limeachwa, lakini vilevile kwetu kwa sababu mimi ni Mwalimu kutokana na uelekeo wa mwanafunzi, huwa tunawashauri kwamba, kwa uelekeo huu anaweza akaenda akasoma kozi hizo, lakini yule ambaye anafanikiwa kwenda moja kwa moja sawa, lakini kwa yule ambaye anakuwa ameshindwa kupata nafasi ndio nawaangalia zaidi katika hoja yangu ambayo naijenga sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe waweke mkopo nao; kwanza wanatoka katika jamii yetu ni wanafunzi wa kawaiidakawaida, lakini anapomaliza masomo yake, tuna hakika anaajiriwa moja kwa moja, anajajiri, lakini pia huyu anakopesha kwa sababu akimaliza mafunzo yake, atakwenda kujajiri na kwake anapata nafuu ya kuweza kurejesha mkopo huo kwa wakati, tofauti na huyu ambaye tunampeleka kwenye chuo kikuu, anasoma kwa miaka mitatu ama minne, anarudi mitaani, hana ajira, kwa hiyo si rahisi hata kurudisha ule mkopo anaokuwa amekopeshwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa hawa ambao wanakwenda kwenye vyuo wanasomea kazi tena kwa muda mfupi na ni wengi na anamaliza moja kwa moja anakwenda kupata kazi yake, ni rahisi kurudisha huo mkopo. Kwa hiyo, niombe katika mikopo ambayo inatolewa kwenye vyuo vikuu vilevile mkopo uweze kupolekwa kwenye vyuo nya kati.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye upande wa ukaguzi au udhibiti ubora wa shule. Wadhibiti Ubora wa shule ndio jicho la Serikali katika kuhakikisha kwamba elimu inatolewa kwa usahihi. Bahati mbaya hawawezeshwi nya kutosha kuweza kusimamia na kuratibu elimu nchini. Niombe wapewe fedha za kutosha waweze kusimamia elimu ya nchi yetu waweze kufanya ufuatilaji waweze kushauri kwa wakati ili zile changamoto zilizopo katika shule zetu ziweze kurekebishwa, ziweze kusimamiwa na hatimaye elimu iweze kutolewa vizuri kupitia Wadhibiti Ubora. Kwa hiyo, naomba sana Wadhibiti Ubora ambao wapo katika halmashauri zetu zote wawezeshwe ili kuweza kusimamia.

Mheshimiwa Spika, hii inakwenda sambasamba na kuwapa stahili zao. Wadhibiti Ubora wa Wilaya wapo ambao wanasmamia idara. Kuna waraka ulishatolewa wa wao kupewa stahili za Ukuu wa Idara, lakini hawajaweza kupewa stahili hizo. Niombe wapewe hili ziwasaidie katika kusimamia elimu hiyo kupitia ukaguzi ambao wanaufanya.

Mheshimiwa Spika, wapo vijana ambao ni wabunifu, tunawaona kila siku na juzi nimemwona kijana mmoja amebuni mashine ya kukamua muwa kupata juisi. Wapo wengi, niombe Wizara iwachukue hao kwa sababu tayari wameshakuwa wabunifu, lakini wanachoeleza hawana fedha za kuweza kuwasaidia kuendeleza ule ubunifu.

Naomba watafutwe, wafuatiliwe wapewe fedha, waendelezwe na hatimaye naamini kwamba wakiendelezwa kwenye ule ubunifu ambao wameshaanzisha, utawasaidia sana kujongezea kipato lakini itasaidia kuweza kuongeza wabunifu wengi katika nchi hii na kuweza kuboresha miundombinu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kuna mmoja alitengeza mashine ya kutengeneza juisi, lakini yupo mwingine alitengeneza mashine kubwa ya kuchambua nyuzi za katani, niliona Tanga. Kwa kuanzia hawa wafuatiliwe, washauriwe na wavezeshwe ili waweze kuingizwa katika mfumo rasmi na hatimaye waweze kupata fedha za kuweza kusaidia katika kuendeleza ujuzi wao.

Mheshimiwa Spika, kwa leo naomba kuchangia hayo tu. Ahsante sana. (*Makofî*)

SPIKA: Nakushukuru sana Mwalimu Aloyce Kamamba, Mbunge wa Buyungu. Mheshimiwa Festo Sanga.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kabisa nimpongeze Waziri wa Elimu, Profesa Ndalichako kwa hotuba yake, lakini pia na Kamati nzima kwa hotuba ambayo wameitoa.

Mheshimiwa Spika, najikita kwenye mambo matatu ya haraka. Jambo langu la kwanza, ukifutilia kwenye hotuba ya Rais wetu ukurasa namba 28 anazungumzia suala la elimu akiwa anazungumzia kwenye kujikita kuimarisha miundombini mashulen, mimi nitazungumzia suala la madawati. Suala la madawati ni bado changamoto kwenye nchi yetu licha ya kwamba TAMISEMI wanakuja na mpango wa mkakati wa dawati za milioni saba kwa mwaka unaofuata, lakini nina mapendekezo kwenye Serikali na hasa Wizara ya Elimu kwamba tunahitaji kuongeza kiwango cha madawati kwa kuwa na mkakati wa pamoja.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali sisi Makete, Njombe na Iringa ndio wazalishaji wakubwa wa malighafi za mbao. Ubao wa mbao unaouzwa Mwanza shilingi elfu saba elfu nane, Makete unaouzwa shilingi elfu mbili ubao ambaou unaouzwa Dodoma shilingi elfu saba Makete unaouzwa shilingi elfu moja. Je, hatuoni kama kuna haja sasa kwa Serikali kujenga kiwanda cha kimakakati na sekta binafsi, ikaingia mkakati binafsi na *private sector* ikajenga kiwanda katika Mkoa wa Njombe pale Makete au ikageuza VETA ya Makete

kuwa sehemu ya uzalishaji wa madawati tu, mwaka mzima, miaka mitatu, miaka mitano wanazalisha madawati tu kwa ajili ya Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, tuna JKT, tuna Magereza lakini tuna vijana wa VETA wengi tu ambao wanamaliza ufundi seremala, tungeweza kuwapa hizo ajira wakatengeneza madawati na tukaanza kusambaza kwenye Taifa hili kwa sababu magari ya jeshi yako mengi ya kuweza kusambaza mashulen i kwetu na changamoto ya madawati ingekuwa imemalizika kwenye Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, sisi Makete tuna eneo, tuna mbao, tuna malighafi za katosha, tunaomba Wizara ya Elimu waone kama hii ni haja ya Serikali kuliko kumwachia Waziri Mkuu, ikifika siku ya *enrolment* mwezi Januari aanze kusema watumishi wa Serikali msiondoke maofisini hadi madawati yapatikane. Sasa twende na mpango mkakati wa kuwa na kiwanda maalum cha kuzalisha madawati na fanicha za nchi hii.

Mheshimiwa Spika, jambo langu la pili...

TAARIFA

SPIKA: Haya mwenye taarifa nampa ruhusa, Mheshimiwa Tabasamu

MHE. TABASAM H. MWAGAO: Mheshimiwa Spika, kusafirisha dawati kutoka Makete mpaka Sengerema au mpaka Bukoka ni gharama kubwa kuliko kusafirisha mbao.

Mheshimiwa Spika, naomba kama mbao zipo aishauri Serikali sisi tuweze kuletewa mbao tutengeneze dawati kutokea kwake sio kubeba dawati kulipeleka Sengerema na sisi tuna vijana wa kufanya kazi.

SPIKA: Unapokea hiyo taarifa, Mheshimiwa Festo Sanga.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimwa spika sijaipokea kwa sababu, sisi tuna uwezo wa kulisafirisha dawati kama dawati tunafanya *assembling* Sengerema ili tuwe na madawati mengi yanayosafirishwa kwa wakati mmoja kwenye magari ammbayo tunaona yanafaa kama magari ya jeshi. Sasa niseme jambo moja magari ya jeshi yapo na kazi maalum ipo, nchi hii haina vita na wanaomba bajeti za mafuta kila mwaka, tungetumia magari ya jeshi kwa ajili ya kwenda kusafirisha mizigo kama hiyo kuliko kufanya hiki ambacho Mheshimiwa Mbunge anakishauri.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo nataka kushauri ni kwenye sekta ya michezo, Mheshimiwa Ndalichako, mawakala na Wabunge wengi asilimia 90 waliopo humu ndani wanaahadi nyingi mashulenii kwenye suala la kugawa vifaa vy a michezo. Tunaomba Wizara ya Elimu, Wizara ya Habari na Wizara ya TAMISEMI waone haja ya kutengeneza agency, wakala wa vifaa vy a michezo mashulenii wa Serikali ili waweze kutoa ruzuku au kupunguza kodi, vifaa vy a michezo mashulenii viweze kupatikana kwa wingi, kuliko kuendelea kusubiria kila Mbunge hapa aagize vifaa China, aweze kusambaza mashulenii, wakati tuna uwezo wa kutengeneza wakala wa vifaa vy a michezo na tukasambaza nchi nzima na vijana wetu wakapata.

Mheshimiwa Spika, ile hoja ya Wizara ya Michezo na Wizara ya Elimu kuona UMITASHUMTA na UMISETA vinakuwa kwenye hii nchi ingekuwa kama tungekuwa na hili jambo. Naomba Wizara iifikirie na hili kwa kweli nimwambie Mheshimiwa Waziri kabisa nitashika shilingi kama watakuwa hawana majibu ya kujibu.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho, lilikuwa kwenye taulo za kike. *Kwanza / call for the ladies of this country even the girls' student* wa nchi hii. Hili taifa kwa sasa ndio kwa wakati mmoja limeanza kupata viongozi sita wanawake watupu. Naanza wa kwanza mtu wa kwanza ni Raisi wetu mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ni mwanamama; mtu wa pili ni Mheshimiwa Ndalichako Professor Waziri wa Elimu ni mwanamama; mtu wa tatu ni

Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dorothy Ngwajima ni mwanamama; mtu wa nne ni Mheshimiwa Jenista Mhagama ni mwanamama; mtu wa tano ni Naibu Spika, Mheshimiwa Tulia ni mwanamama na akina mama wengine wote na Mheshimiwa Ummy Mwalimu Waziri wa TAMISEMI ni mwanamama.

Mheshimiwa Spika, watoto wa na nchi hii watawalilia kama suala la taulo za kike hawataweza kuli-*solve*, wanategemea halmashauri zitenge bajeti kwa ajili ya taulo za kike, ni jambo ambalo sikubaliani nalo. Nawaomba na nawashauri kwamba Tanzania tuingie ubia na viwanda, tuweze kutengeneza taulo za kike zenye ubora ambao watoto wanaweza wakazitumia, kwa sababu watoto wengi wa kike wanakosa masomo...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge wanawake kweli mmeja humu mnategemea Festo Sanga ndio awaongelee hili jambo. Mheshimiwa Festo nakuunga mkono malizia hoja yako.

MBUNGE FULANI: Taarifa.

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Spika, kwa ripoti ya UNESCO inaonyesha kati ya watoto kumi wa kike kwa siku watoto wawili au watatu wanakosa kuingia darasani kwa sababu ya hedhi isiyo salama. Nataka ninukuu wanasema *menstruation is not a problem but hygiene is a problem*.

MBUGE FULANI: Taarifa.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge wanaume mpigieni makofi Mheshimiwa Festo Sanga (*Kicheko*)

MHE. FESTO R. SANGA: Mheshimiwa Spika, naomba wasimalize dakika zangu naomba nizungumze

MBUGE FULANI: Taarifa.

SPIKA: Ahsante sana, wananyanyuka wenyewe Bunge nitalishindwa dakika za mwisho, wenyewe wanataka kuja moto, hapa Waheshimiwa mnasaidiwa kazi hapa. (*Kicheko*)

Kwa hiyo Wabunge wanaume kumbe tuna faida na sisi. Ahsante sana umetubeba Mheshimiwa Festo Sanga.

Waheshimiwa Wabunge, mjadala wa elimu ni mjadala mkubwa katika Bunge letu kwa sababu kama mlivyosema wenyewe ndio hatma ya Taifa letu tunakokwenda kwa vijana wetu. Kwa hiyo mnaochangia muendelee kujiardaa na tujitahidi kupata nafasi kadri ya inavyowezekana na kesho tutaendelea na mjadala huu pia, tumsaidie Mheshimiwa Profesa Ndalichako na wasaidizi wake wote kuweze *ku-chart out* njia ya kweli kwa sababu ndio mshauri mkuu wa Serikali, kwa hiyo tufanya kazi yetu ya ushauri ipasavyo.

Waheshimiwa Wabunge, mmewasemea sana Wadhibiti Ubora nami naungana na ninyi kabisa, ni watu wanaohitaji kutazamwa, ila wana jambo lao moja ambalo mimi huwa linanipa tabu. Kuna Kijiji hakina shule kabisa, wananchi wanaamua kabisa wajenge shule, wanajitahidi wanapata darasa la chekechea na la kwanza wana vyumba viwili, wameweke msingi wa chumba cha tatu, Wadhibiti Ubora hawataki kuandikisha hiyo shule, wanasema mpaka wajenge sijui vyumba sita na nyumba ya Mwalimu na sijui vingine vingapi.

Sasa leo sisi tuna darasa la kwanza, tujenge vyumba sita hivi vitano vinakaa vinapiga hewa, mpaka mwaka gani ndio hao watoto waje wafike huko waweze kujaa. Hivi Wadhibiti Ubora hawaoni tu *logic* ya kawaida, kuandikisha shule ni kuangalia kigezo na umuhimu wa shule kuwepo pale. Sasa ikishaandikishwa ndio shule hiyo inaweza hata ikapata misada ya kiserikali. Kama hajaandikishwa, haipo popote nani atakuja kujua? Mpaka waje wajenge, wahangaike wenyewe wafikishe vyumba sita, wajenge nyumba ya Mwalimu, wachimbe vyoo, wenyewe peke yao, haiko

kwenye mfumo wowote wa kiserikali na tunajua kama kijiji hiki hakina shule na sera ya Chama Cha Mapinduzi imesema kwamba watoto wote waende shule, wewe kuandikisha hutaki, unasema nadhibiti ubora, ubora upi sasa unaodhibiti?

Andikisheni shule, panapostahili kuandikishwa shule paandikishwe shule, halafu ninyi wa ubora, wazazi, halmashauri, Serikali Kuu, ni jukumu letu wote sasa kuhakikisha shule inaboreka, inajengeka, lakini wenzetu hawataki kuandikishwa shule. Yaani wao kama wametoka mwezini; hamjafanya nini na nini haiandikishwi hii. Mnachangisha wanakijiji mnawaita tena, hii bado madirisha, milango, sijui hajifanyaje, bwana we, shule yetu wote, ya Serikali, sasa haya maneno yote ya nini? Hebu kwenye eneo hilo tuelewane, sijui Waheshimiwa Wabunge kama hampati shida hiyo. (*Makof*)

Hiyo ni shida kubwa sana, hawaandikishi shule kama ni kwenye *private schools* kwa sababu ni *private* wekeni hayo masharti, mimi sijali sana ingawaje na kwenyewe *is irrelevant* mtu awe na vyumba kumi wakati ana watoto wanaoanza, lakini siongelei habari ya *private school* sasa hivi naongela *public schools*, shule ni ya umma inahitajika, watoto hivi, unakuta watoto mia mbili darasa la kwanza halafu haiandikishwi, kisa Wadhibiti Ubora wanasema sisi bwana tuna maelekezo yako hivi, hapana. Twendeni pamoja kama Taifa wote kwa pamoja mpaka halmashauri ifanye, mpaka fulani afanye, halmashauri, Serikali kuu, wazazi, Wadhibiti Ubora Elimu wote, hii ni kazi yetu wote. Shule iandikishwe, kama ina umuhimu, vigezo vile kwamba hapa panastahili shule andikisheni, halafu mwendelee kuwabana sasa hawa wote waliobaki ili shule iwe shule. Ni ushauri tu.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea saa kumi, kwa hiyo nasitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi kamili jioni ya leo.

(Saa 7.08 Mchana Bunge lilitfungwa mpaka Saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirejea)

SPIKA: Waheshimiwa tukae.

Katibu!

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA
ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA KWA MWAKA
WA FEDHA 2021/2022**

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea. Lakini niwakumbushe kwamba baada ya kumaliza shughuli hizi tuna futari leo jioni na kwa kweli imeandaliwa vizuri sana. *(Makofi)*

Tunaendelea na majadiliano, kwamba sasa mkubali na mpokee kuitisha makadirio, lakini myajadili kwanza, kwa hiyo, tunaendelea na mjadala wa kuhusiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Katika ambao wameshaingia nimemuona Mheshimiwa Hamida Mohamed, hebu uanze kuchangia.

MHE. HAMIDA M. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuendelea na mjadala ambao uko Mezani wa bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Profesa Ndalichako, pamoja na timu yake nzima ya Wizara yake kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita. Tumeona mafanikio makubwa katika sekta ya elimu, lakini bado katika mpango wa bajeti ya Wizara hii katika utekelezaji wa kipindi hiki cha 2021/2022 tumeona bajeti namna ambavyo inakwenda

kuendelea kuboresha sekta ya elimu katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu mbalimbali ikiwemo shule za msingi, sekondari pamoja na vyuo. Hauwezi kwenda chuo ama chuo kikuu bila kuanza shule ya msingi. Tumeona namna ambavyo shule zetu za msingi, hasa zile zilizojengwa tangia miaka ya 1960, 1970, shule ambazo mpaka sasa hivi zinatumika lakini ni shule ambazo zimekuwa chakavu mno. Mabati yameshaiza. Wakati wa mvua watoto wanashindwa kukaa madarasani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba katika mpango wa kuboresha shule kongwe ambao ulitekelezwa kwa kipindi kilichopita ambao Mheshimiwa Prof. Ndalichako alianza nao, tunaomba tuendelee kuboresha shule zetu za msingi ziweze kuwa katika hali nzuri na tuendelee kuzitumia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, waswahili wanasema usipojenga ufa utajenga ukuta, kwa hiyo, kuna kila sababu sasa ya Serikali kuona namna gani tunakwenda kuboresha shule za msingi. Na nina hakika maeneo mengi Waheshimiwa Wabunge wanayalamikia katika shule hizi za msingi kuona kwamba zina uchakavu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Lindi Manispaa tunazo shule karibia 12, shule ambazo ni chakavu mno kupitiliza. Lakini unajua kwamba Mji wa Lindi ni mji mkongwe sana ambao walianza kukaa wakoloni huko. Kwa hiyo tuna kila sababu sasa ya kutusaidia Lindi kwa sababu maeneo mengi tumerithi kutoka kwa wakoloni kwa hiyo majengo yamekuwa machakavu mno. Ninaiomba sasa Serikali kuangalia namna gani wanawenza kutusadia kuhakikisha kwamba shule hizi za msingi zinaendelea kuboreshwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niishukuru Serikali kupitia fedha za *EP4R*; zimekuwa ni msaada mkubwa na zimesaidia kwa kiasi kikubwa sana kumaliza maboma ambayo wananchi

wamejitolea. Na pale Lindi tumefaidika na fedha hizi, zaidi ya milioni 200 zimekuja na zinafanya kazi ya kuendelea kukamilisha madarasa haya ili yawe katika sura nzuri na watoto wetu waendelee kupata masomo yao.

Mheshimiwa Spika, zipo changamoto za jumla upande wa shule za msingi na sekondari. Waheshimiwa Wabunge tumekuwa tukizungumzia karibia wiki nzima, kuna upungufu mkubwa sana wa walimu katika maeneo haya, na Mheshimiwa Rais ameshatoa katika hotuba yake kuajiri watu 600. Ninaomba tuzingatia katika sekta ya elimu kupeleka walimu wa kutosha ili watoto wetu waendelee kusoma vizuri lakini tuweze kupunguza kwa kiasi kikubwa changamoto hiyo ya walimu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa kuna changamoto ya wlaimu wanaostaifu kutopewa malipo yao kwa wakati. Hizi ni hoja za jumla ambazo zimezungumziwa, pamoja na kupandisha madaraja lakini nina hakika kwamba wahusika wataendelea kusimamia kuhakikisha kwamba changamoto hizi zinaondoka.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha mwaka hadi mwaka kuhakikisha kwamba inatenga fedha kwa ajili ya kwenda kuwekeza katika vyuo vya VETA ambavyo vinawasaidia watoto wetu wanaomaliza darasa la saba wakashindwa kuendelea, pamoja na *form four* wanaoshindwa kuendelea na masomo ya juu. Kwa hiyo, vimekuwa vikisaidia sana kuwapa mafunzo mbalimbali vijana wetu ili waweze kupata ufundi stadi na waweze kutengeneza ajira. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Lindi Manispaa tumbahatika kuwa na Chuo hiki cha VETA na kimejengwa muda mrefu. Kuna changamoto; vifaa vya kufundishia vimeendelea kuwa chakavu lakini hata magari yameendelea kuwa chakavu kwasababu kuna masomo pia ya udereva katika vyuo hivi vya VETA.

Mheshimiwa Spika, vijana hawa wanaokwenda kupata mafunzo katika vyuo vya VETA ninaishauri Serikali kuwa na mahusiano kati ya chuo cha VETA, wanafunzi na halmashauri kwasababu wanavyokwenda kusoma VETA wanapata mafunzo mbalimbali, wanaporudi kwao baada ya kumaliza masomo wanashindwa kujiendeleza kwasababu wanakuwa hawana fedha za kuendelea kuzalisha na kukuza uchumi pamoja na kwenda kuwekeza kwenye viwanda vidogovidogo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kwasababu halmashauri tuna asilimia kumi ya mapato, ingeweza kutumika kwenda kuwaboresha vijana hawa ambao tayari wanapata mafunzo kutoka VETA ili sasa kuwawezesha vijana kuendeleza yale mafunzo waliyopata ili kuendelea kukuza uchumi na kuendelea kumudu kuendesha maisha yao. Nafikiri tukifanya hivyo tutakuwa tumepunguza mzigo mkubwa kwa Serikali, lakini tutakuwa tumewawezesha vijana hawa kujiendeleza kiuchumi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Lindi Manispaa tumetoa ardi kwa ajili ya ujenzi wa vyuo vikuu, kampasi ya Lindi. Chuo Kikuu kampasi ya Kilimo tumetoa zaidi ya ekari 120 lakini mpaka leo ujenzi haujaanza. Lakini pia tumetoa ekari 150 kwa ajili ya Chuo Kikuu cha masuala ya Uvuvi na Usafirishaji Baharini.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali sasa kutoa fedha ili kuendeleza ujenzi huu, kuhakikisha kwamba vyuo vikuu hivi kampasi ya Lindi vinaendelea kujengwa, lakini watakaofaidika na vyuo vikuu hivyo siyo Wanalindi peke yake, Kanda nzima ya Kusini watapata elimu pale. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaiomba sana Serikali kuhakikisha kwamba tunaendelea kuvisimamia vyuo vikuu hivi ili viweze kukamilika katika ujenzi wake hata kama si kwa asilimia 100 lakini kila mwaka tungeweza kutenga fedha na hatimaye tungeweza kumaliza kuhakikisha kwamba ujenzi huo unakamilika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tuna chombo kinachoitwa *SIDO*; *SIDO* inatoa mafunzo ya ufundi stadi lakini inasimamia masuala mbalimbali ya wajasiriamali pamoja na wanaoingia katika uanzishwaji wa viwanda vidogovidogo. Ninaomba Serikali kuendelea kutumia *SIDO* katika maeneo yetu, maeneo ambayo chombo hiki kipo ili kuwezesha fedha za kutosha na kuendelea kuwawezesha vijana wengi kuingia katika maeneo haya ya ufundi stadi na uwekezaji wa viwanda vidogovidogo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja, nakushukuru sana. Ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Hamida Mohamed, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Lindi. Sasa tumsikilize Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei.

Mheshimiwa Dkt. Kimei tafadhali, utafuatiwa na Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa fursa hii ya kuchangia kwenye mjadala huu amba ni muhimu sana kwasababu ya jukumu la Wizara hii katika kuendeleza nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Profesa Ndalichako, na Naibu wake pamoja na uongozi mzima wa Wizara kwa kazi nzuri kwenye mazingira ambayo ni magumu na kwenye changamoto nydingi.

Mheshimiwa Spika, kwasababu uchumi wowote unapobadilika haraka sana sekta ya elimu inatakiwa na yenye we iweze kujibadilisha na kuwa bunifu ili iweze kutengeneza wahitim u amba wanakidhi mahitaji ya wakati huo. Sasa tukiangalia na tukijaribu kufikiria kwamba tuko wapi na tunakwenda wapi katika dunia hii, utajikuta kwamba sekta hii inatakiwa ibadilike sana kwa namna ambavyo tunakwenda mbele.

Mheshimiwa Spika, sekta ya viwanda ilivyobadilika, *industrial revolution* ilivyoingia, tija kwenye kilimo iliongezeka sana na hivyo bei za vyakula zikashuka kwa hiyo faida kwenye kilimo ikashuka pia. Kwa hiyo, watu wakaamua kukimbilia mijini wakapata kazi kwasababu viwanda vile vilikuwa vinazalisha ajira.

Mheshimiwa Spika, lakini sasa hivi viwanda havizalishi ajira. Bahati mbaya ukienda kiwanda chochote kikubwa utakuta kwamba *robots* *wame-automate* na *artificial intelligence* utakuta kwamba pengine ma-*robot* yanafanya kazi. Hata kule kwenye mabenki yetu sasa hivi unakuta kwamba watu hawaajiri, walikuwa wanaajiri watu 400 sasa hivi hawaajiri kwasababu tunatumia *sim banking* na vitu kama hivyo ambavyo vina-*replace employment* ya watu.

Mheshimiwa Spika, sasa tunapokwenda hii karne siyo ya viwanda ambavyo ni *labor intensive*, ni kadri sasa ya TEHAMA na hii TEHAMA inatupeleka mbali sana tukijifikiria vizuri. Tukijifikiria vizuri tutafanya mambo mengine na ni kweli kwamba vyuo hivi ambavyo tumekuwa tunazungumza toka asubuhi kwamba tuviboreshe, tufanye hiki na kile, tukichunguza vyuo hivi vya ufundi vya kuwasaidia vijana wetu wapate maarifa na ujuzi waweze kutenda kazi na waweze kujiajiri.

Mheshimiwa Spika, pengine kwanza havifai kwenye karne hii, havina karakana na vifaa vya kufundishia vitu ambavyo vinahitajika kwenye uchumi wa kisasa, kwenye uchumi huu ambao sasa hivi ndiyo tunakwenda. Na mtu akisema kwamba hatujui tunakokwenda ni mtu ambaye haoni kwasababu ukweli ni kwamba tunakokwenda ni tofauti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sekta zinazozalisha ajira ni sekta za huduma; mawasiliano, kwa sekta kama za usafiri, uchukuzi, afya itazalisha utalii, itazalisha utawala, *sales and marketing*, lakini ukiangalia upande huu wa viwanda hawatazalisha kwasababu *automation* imefika mbali sana na tija imekwenda mbali sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niseme kwamba tunapoangalia hivi vyuo kuvipa uwezo lazima na walimu wale wapite kwenye mafunzo tofauti na waweze ku-*identify* ni kitu gani ambacho watafundisha ili tuweze kuwasaidia watu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niseme kitu ambacho nakiona ni kwamba vyuo vilivyo kila kata kuna vyuo. Sasa vyuo hivi usipofanya vikawa-*specialized* hutaweza kuvi-*equip* na vile vitu ambavyo vinahitajika; hutaweza.

Kwa hiyo, lazima viwe *specialized* na vitangazwe kwa wananchi wajue kwamba nikienda Bukoba ntapata chuo ambacho kinatengeneza watu wanaojifunza kutengeneza simu, au nikienda Lindi kule ntapata watu amba wanaweza wakatengeneza au kuhudumia mashine za *oil and gas, and so forth*. Kwa hiyo, ni lazima tuvifanye viwe *specialized* kidogo angalau kuwe na *specialization* kidogo ili tujue ni vipi na viko wapi.

Mheshimiwa Spika, lakini nikihesabu kule kwangu kuna Vyuo viwili; Mshiri na kingine kiko kule Mwika, hakina hata walimu, hata hao ambao tunasema kwamba ni wa kale ambao sidhani kama wanaweza waka-*cope* na *skills* zinazohitajika, bado hawapo hata hao walimu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niombe kwamba pengine, kwanza hiyo kanzidata ya walimu wa vyuo hivi vya ufundi na stadi mbalimbali ijlukane ili waweze kuwa *allocated properly*. Hayo majengo ambayo yamekaa *idle* hayaendeshi kozi zozote kwasababu ya kukosa walimu yaweze kutumika lakini cha msingi ni kwamba wapate *training*, wapelekwe hata nje.

Mheshimiwa Spika, hata tukikaribisha Wachina na Wahindi wakaja wakatuonesha wao wanafanyaje na wanakwendaje kwasababu nchi nyingi sasa zinajikita kwenye upande wa *training* ya mambo haya ya hudua na kutengeneza vitu vya kisasa, siyo kutengeneza magari ya, hata magari *manual* siku hizi hakuna kabisa.

Mheshimiwa Spika, sasa niseme hivi; kwasababu watu wa ku-*train* ni wengi sana hebu tufikirie wazo moja. Kwa mfano tunasema mambo ya *soft skills* hizi za watu kuwa na tabia ya kuweza kujituma, kuweza kuheshimu kazi na kadhalika, zinapatikana zaidi kule JKT.

Mheshimiwa Spika, ukienda JKU sasa hivi ukaweza kupiga *mark time* pale vizuri halafu jioni ukafundishwa *skills* zozote hizi ambazo tutakuwa tumesema Ruvu wafundishe hiki na hiki, ukifundishwa hivyo ukimaliza pale baada ya miezi mitatu au sita unakwenda unaajiriwa na utakuwa na heshima na utakuwa mwaminifu na utafanya kazi vizuri kwasababu umejifunza *discipline* na *skills* kwa namna ambayo itasaidia sana watu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri hiyo ndiyo njia ambayo inaweza ikafanya kwa haraka sana watu ambao wanamaliza *form six*, hata wanaomaliza *university* wanaambiwa piteni kule mtapata *skills* kwa ujumla kwa haraka zaidi na kule kuna vifaa vya kufanyia majaribio na kadhalika. Kwa hiyo, hicho ni kitu ambacho mimi nafikiri kingekuwa cha msingi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia niseme kwamba tukizingatia kwamba kuna haja ya kuwa wabunifu kwenye hii nyanja ya TEHAMA, kuna haja ya vyuo vyetu hivi vikuu sasa hivi viwe na vitengo. Kila chuo *at least* kiwe na kitengo cha *incubation* ambapo mtu akiwa na wazo lake anakwenda kwenye kitivo au kitengo kile cha chuo kikuu, wanamsaidia kuboresha na kumuonesha namna gani anaweza aka-*implement*.

Mheshimiwa Spika, wanaweza wakamuonesha pia kwamba pengine mashine za namna hii zinapatikana *TEMDO*, zinapatikana wapi, hebu tukusaidie, wanamsaidia *kina-take off* wanamuachia anaendelea na watu wataajiriwa wengi.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa namna hii ambayo tunaona naona kuna shida sana; ijasiriamali haufundishwi darasani, unafundishwa kwenye *field*. Mtu kama umemaliza

kama usipopata *on job training* hutaweza. Sasa hivi vyuo vina watu, walimu wako wengi ambao wana-*retire*, maprofesa wana-*retire*, wajasiriamali wengi nao wana-*retire*.

Mheshimiwa Spika, kwa nini tusiwapeleke tukawaombe waanzishe hivi vitengo ili watu waweze kupata *skills* zao wakajifunza. Kuna mmoja alisema kwa nini akina Dewji hawaandiki vitabu. Watu wamejifunza kutoka kwa akina Dewji waka-*implement* mambo ambayo yataleta tija katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nafikiri kwamba kule kwenye jimbo letu, na nitafurahi sana kama kweli tutaweza kupata *specialization* ya mambo ya...

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Kimei, muda hauko upande wako.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Nakushukuru sana, ahsante sana.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naunga mkono hoja kwa asilimia 100; ahsante. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Paulina Nahato.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Spika, kwanza mimi badala ya kumpa hongera wifi yangu, Mheshimiwa Prof. Ndalichako, namna pole maana najua hapa kabeba mzigo mzito sana ambao ndiyo roho ya nchi yetu; nakupa pole sana.

Mheshimiwa Spika, na wakati nikiangalia kwa nini tumefikia hapa tulipofikia kwamba wanafunzi wetu anamaliza mpaka chuo kikuu anatembea na *briefcase* ya *certificate* kutafuta kazi; tatozo liko wapi. Nikaona niangalie maeneo mawili; la kwanza nimeangalia tulipoacha ile – sijui tunaita sera au nini – Mwalimu Nyerere alituweka katika njia ya kufikiria kwamba uhuru na kazi na pili, elimu ya kujitegemea. Nakumbuka elimu ya kujitegemea miaka hiyo nikwa sekondari tulikuwa na mashamba kama ulivyokuwa unasema, tunalima tunapata chakula cha shule, lakini sasa hayo tumeyaacha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine nililoona tumekuwa *donor dependent so much that* hiyo imetulemaza. Hata Mheshimiwa wifi yangu Profesa akizungumza alitaja wafadhili au wadau wengi wanaotusaidia katika elimu yetu. Hii imetulemaza kiasi kwamba hatukutaka kujijengea njia ya kujitegemea wenyewe na kutafuta hela, badala yake tumetegemea sana wafadhili. Sehemu kubwa ya pesa ya maendeleo mfadhili asipoileta kwa wakati tunaanguka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hapo natumia *theoryya mtaalam mmoja* Mmarekani anaitwa Ajzen na *theoryyake ya planned behavior*, aliandika mwaka 1991. Alisema kwamba: “*An individual attitude is shaped by subjective norms in the leaving environment and later such attitude forms intention within an individual and consequently this becomes a behavior*”. Kwa Kiswahili ambacho labda siyo sahihi sana alisema: “Fikra ya mtu iliyojengwa na mazingira anayoishi humpelekea kuwa na nia ya kutenda kila kitu fulani na nia hiyo ikiendelezwa baada ya muda fulani hugeuka kuwa tabia”. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivyo? Sasa hivi tuliwajengea wanafunzi wetu kwamba akimaliza shule lazima aajiriwe, hiyo kuwatoka haijawa rahisi. Nataka tu-*compare* na nchi za wenzetu ambao walikuwa maskini au walikuwa wako nyuma wakati wakipata uhuru. Tanzania tukilinganisha na nchi ambayo ni ya China na Japan; nataka kuzitumia

hizo maana najua hali zao zilikuwa duni wakati wakipata uhuru. Kwa mfano, tukipata uhuru sisi mwaka 61 China walikuwa wamepata uhuru wao mwaka 49 na Japan 51, tulipishana kama miaka kumi au kumi na miwili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia umri wa kuanzia masomo ya wanafunzi wao wa *primary* ni ile ile miaka sita kama sisi. Miundo yao ya elimu hajatofautiana sana na sisi, tunakuja kupishana sehemu moja au mbili. Sehemu moja uwiano wa walimu na mwanafunzi, hapo sasa hivi ndiyo tuna shida kubwa sana. Mwalimu mmoja wa Tanzania anakuwa na wanafunzi wengi kiasi kwamba hawezi kujuua kila mwanafunzi ana karama gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Japan mwalimu mmoja anahudumia wanafunzi 16.1, China 16.43, hii ni ripoti ya *UNICEF* siyo yangu sisi ni 50.63. Pia wameonyesha katika ripoti yao, ni ya siku za nyuma kidogo inawezekana mambo yamebadilika, wameonyesha kwamba wanafunzi wanaofaulu kwenda sekondari kwa Tanzania ni asilimia 54, Japan ni asilimia 98.8 na kwa China 97. *What does that mean?* Ina maana wao kwa vile ni *compulsory* na wanatumia ile *system* yao ambayo tangu *primary school* lazima wawe na vipindi vya ufundi na ufundi ule wanapewa *equipment* (vitendea kazi) kwamba hawa-*relay* kwenye nadharia kama sisi *instead* wao wanafanya kwa vitendo na zile *product* wanazotengeneza zinakuwa na *value* zinaenda hata kuuzwa.

Mheshimiwa Spika, hawa wanafunzi wakifika *form four* wengine wanakwenda kwenye shule za ufundi na wengine wanaenda shule za sekondari. Kiasi kwamba kama hakuweza kwenda chuo kikuu ameshajenga msingi na anajua aende akafanye kazi gani maana amepata zile *skills*. Kwa hiyo, zile *skills* zinawafanya wajenge tabia ya kujitegemea tofauti na sisi tunajenga tabia ya kwenda kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, wenzangu walikuwa wanasema tuwe na Baraza la Taifa la Elimu, lakini nafikiri hapo tutakuwa tumeji-*confine* sana, labda tuwe tunasema *think tank* ya

kuangalia mfumo wetu mzima ambao utakuwa na *linkage* na viwanda, kilimo na Hazina kuona kwamba huu uchumi wetu na hasa shule zetu tunazi-*revamp* namna gani kusudi tujenge ile tabia ya kujitegemea. Kinyume cha hapo tutasema hatuja-*improve* hiki na hiki lakini wakijengewa tabia ya kujitegemea na tangu mwanzo tunaweka vifaa vya kutosha kwenye zile karakana na mwanafunzi akifika *form four* ameshajua anataka kwenda wapi. Hawa wenzetu hata *university wana-liaise* na viwanda, wanafanya *attachment*, wanakwenda kuona tunaweza kui-*improve* vifi viwanda vyetu au viwanda vinaweza kusaidiaje wale wanafunzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hapa kwetu sasa hivi tunafanya kazi kwa mtazamo mmoja, kama ni elimu tume-*drawn a line* ni elimu, kilimo ni kilimo. Sijui kama kuna mahali ambapo tuna-*converge*, tukitaka kuanzisha kiwanda lazima tuangalie *skills* gani tunawapa wanafunzi wetu, kwa *priority* ipi na kwa viwanda vifi. Bila kuweka huo muelewano kwamba hawa wa viwanda wanajua *priority* ya viwanda vyetu ni hizi, kwa hiyo tunapoweka mitaala yetu tunalenga kwamba wanafunzi wetu lazima wafundishwe au wapitie huku wajue kwamba tunalenga kwenye viwanda hivi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, pamba sasa hivi bado pamba tunapeleka nchi za nje tuna-*create employment* kwa wenzetu. Tunanunua mitumba au tunanunua nguo kwa bei mbaya. Baada ya kufanya kazi na hawa wenzetu *donors* wanapenda tuwe *donor depended so much that* tusiweze kujitegemea maana *once* tumeweza kujitegemea hawataweza kupata *raw materials* waka-*create employment* kwao. Ndiyo maana wakija wanakuja na watu wao wenye skills. Sisi tunasema ooh wale ambao hatuna mje nao kwa nini sisi hatu-*train* watu wetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiria kama alivyokuwa anasema Mheshimiwa Kimei pale walimu wetu wapelekwe nje wapate *exposure, short of that* tutakuwa hatufiki mbali. (*Makofi*)

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa napunguza muda kutoka dakika kumi kwenda dakika saba na kengele itakuwa moja tu. Tunaanza Mheshimiwa Dkt. Paulina Nahato, dakika saba na wengine wote itakuwa hivyo hivyo.

MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda sana kumpongeza Profesa Ndalichako, mwalimu wangu ambaye najivunia sana kumuona akiwa kwenye kiti hicho, anatosheleza. Ni mwalimu mahiri na yupo vizuri sana. Kwa hiyo, hapo alipo pamoja na Naibu Waziri wametosheleza kwa jinsi ninavyomfahamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza sana kwa kuwakilisha taarifa yake nzuri sana. Nami ni mwalimu kwa hiyo mambo yote ambayo kwa kweli kama mwalimu nilikuwa nategemea yasemwe, nimeyasikia. Kwa hilo nimeburudika sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia napenda kukushukuru sana wewe na kwa sababu muda ni mdogo naomba niende moja kwa moja kwenye uchangiaji. Kwa kuwa na shule ya wasichana ya Bunge, Kamati tumefika kuiona, ile shule ni nzuri sana na ni ya sayansi tunategemea kupata madaktari na engineers. Tuliwaona wamekuja hapa Bungeni, wanang'aa kwa hiyo tuna uhakika baada ya muda fulani tutakuwa na kada ya watalaamu wanawake wa kutosha. Hiyo ni sifa kubwa sana kwa wanawake, kwa hiyo, hongera sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wanawake tuliosoma miaka ya nyuma masomo ya sayansi yalikuwa si ya wanawake. Mwanamke akisoma masomo ya sayansi alikuwa anaonekana kama yupo tofauti na hii ilikuwa ni mtizimano fulani ambaa ulikuwa umejengeka hata wanawake wenyewe tulikuwa tunaona hivyo. Juzi Rais wetu alipokuwa anahutubia alisema moja kwa moja kwamba akili ya mwanamke na mwanaume zipo sawa tofauti yetu ni masuala ya biolojia tu kwamba mwanamke anabeba mimba na anazaa mtoto na mwanaume ana mbegu ya kuweka mimba kwa mwanamke, hiyo ndiyo tofauti. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, masuala mengine yote tupo sawa kabisa kuanzia kwenye akili, kwenye matendo, hamna kazi ambayo mwanaume anafanya mwanamke hawezi kufanya, hakuna. Ni utamaduni uliojengeka tu, *is a socially constructed idea*. Kwa hiyo, tunapoona wanawake wanasoma sayansi hao ndiyo tunaotegemea wawe *ma-engineer*, watengeneze *caterpillars*, viwanda watakuwa wanawake wakipanda juu na kutengeneza mashine. Nataka kusema nini hapa? Nataka shule za wasichana ziongezwe hasa katika michepuo ya sayansi ili kuwe na ile *notion* ya zamani ambayo wengine tuliikosa katika masomo ya sayansi sasa tunapoenda kwenye *fifty fifty* wanaume kwa wanawake pia kwenye masuala ya sayansi tuwepo.

Mheshimiwa Spika, nini sasa tufanye ili tuweze kufikia pale? Kwa tafiti ambazo zimefanyika zinaonyesha kwamba wasichana wanapokuwa wenyewe katika shule zao, wanaposhindana wenyewe wanafanya vizuri sana. Mtakubaliana na mimi tunapoangalia zile shule ambazo zimefanya vizuri, japokuwa zipo pia na za wanaume wenyewe kwa wenyewe lakini za wanawake zinaoongoza ni zile ambazo wanawake wako wenyewe.

Mheshimiwa Spika, sijajua sababu ni kitu gani lakini mojawapo ni kwamba wanawake wanapokuwa wenyewe wanakuwa na ile hali ya kujiamini zaidi kwa sababu yale mambo ya kuona aibu na maneno maneno ambayo yalikuwa siku za nyuma yanakuwa hakuna. Kwa hiyo,

wanaposhindana wenyewe kwa wenyewe kunakuwa na kujiamini.

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiria siku zijazo angalau tufike hata kila wilaya kuwa na shule za bweni za wasichana ambazo zitakidhi mahitaji ya wasichana. Hata masuala aliooongea Mheshimiwa mambo ya taulo za kike, ile sisi tumejisikia vibaya lakini ndiyo ukweli ila kwa vile ameongea mwanaume tukajisikia vibaya, tuondoke tu ni mwanaume kasema ni sawa.

Mheshimiwa Spika, kwa kusema hivyo Mheshimiwa Waziri nafikiri baadaye tutawaza kuona kwamba kila wilaya inakuwa na shule ya wasichana na itiliwe mkazo masomo ya sayansi. Ili chuo kikuu basi zile *faculty* zote za sayansi tuone wanaume na wanawake ili baadaye wanapoingia katika soko la viwanda wanawake wawepo wengi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nizungumzie suala moja la mfumo wa mikopo. Suala hili tunaishukuru Serikali kwamba sasa hivi angalau imeongeza pesa. Takwimu inaonyesha kwamba itakapofika 2525 wanafunzi watakaokuwa wanaingia shulenii mara mbili. Hii ina maana kwamba *form four, form six* na chuo kikuu wataongezeka mara mbili, tumejiandaaje? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mfumo wa mikopo uliopo sasa hivi una changamoto, haupo sawa. Kuna wanafunzi ambao wanakosa mikopo, hawa wanaotoa mikopo kuna masharti ambayo wanasesma ni lazima huyu kijana anayepata mkopo awe yatima, wazazi wake waonyeshe hawana uwezo na vitu kama hivyo. Sasa utawezaje kupima kwamba huyu kijana ni maskini hiyo ni kazi kubwa sana. Matokeo yake nini? Wanafunzi wanaingia chuo kikuu wanakosa mikopo na mbaya zaidi hawa wanaokosa mikopo ni wale ambao kabisa kwa ukweli ni maskini na hivyo wanashindwa kumaliza masomo yao. (*Makofii*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Paulina Nahato.

MHE. DKT. PAULINA D. NAHATO: Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Umependekeza shule za wanawake ziwe kila wilaya hatukatai lakini tulianza na sera ya hamsini kwa hamsini sasa naona *increasingly* wanawake wanaanza na sera mpya ya mia kwa sifuri. (*Makofi/Kicheko*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Issa Mtemvu atafuatiwa na Mheshimiwa Zaytun Swai.

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie Wizara hii. Mimi nitajielekeza kwenye eneo la tafiti tu, limesemwa na wajumbe wengi lakini na mimi niseme hapa kidogo.

Mheshimiwa Spika, kwanza muhimu ni vizuri tuje hata nini maana ya tafiti katika elimu ya juu. Mwananzaoni mmoja anaitwa Godwin Kalibao anasema, utafiti unahusisha kukusanya *data*, habari na ukweli kwa ajili ya kuendeleza ujuzi. Yupo mwingine anaitwa John W. Gasswell anasema, utafiti ni mchakato wa hatua za kukusanya na kuchambua habari ili kuongeza uelewa wetu wa mada na masuala mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nimesikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kwa kina sana na nilimsikiliza vizuri wakati anaendelea kuzungumzia baadhi ya vyuo vyuo vytu kuanzia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo cha Mzumbe, DUSE na vyuo vingine vya ufundi na zaidi katika eneo la tafiti. Nampongeza kwa sababu kama Serikali pia bado inaendelea kutoa fedha kidogo kwa ajili ya machapisho na tafiti mbalimbali lakini hazitoshelezi. Ukiangalia uhitaji wenyewe kwa takwimu mbalimbali ambazo unaweza ukazipata, mimi nimejaribu sana kwenda kwenye taasisi zetu za tafiti mbalimbali kuanzia NBS na nyininge nydingi, inaonyesha tunahitaji tafiti na machapisho mbalimbali kwa kiasi kikubwa kuliko ambavyo vimewasilishwa katika bajeti ya 2021 hata matarijio ya bajeti

yetu tunayokwenda nayo sasa au tunayoianza hii ya 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, pamoja na faida nyingi za tafiti, kwa muda siwezi kusema yote, zipo faida mbalimbali; moja, ikiwa ni kupata taarifa muhimu kuhusu suala linalotafitiwa; kuongeza hazina za maarifa katika eneo hilo lakini kupima joto la hali, fikra na mitazamo mbalimbali. Pamoja na faida hizi zote katika maeneo ya tafiti hatujafanikiwa kama taifa kwa sababu ya changamoto zilizopo. Changamoto kubwa kama Taifa ni mbili; ya kwanza ni gharama na ya pili ni wataalam wabobezi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hili la gharama nimefurahi sana, Mwenyekiti wa Kamati alivyokuja mbele hapo amesema kwenye eneo hili hatujafanikiwa sana na akatolewa mfano COSTECH wameweka shilingi bilioni 3.8 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 na anasema hazitoshi kabisa, sasa hili ni eneo moja tu. Pia Mwenyekiti amesema katika nchi za Ulaya wameweka makadirio ya mchango wa Pato la Taifa liwe ni asilimia tatu ambayo inaenda kwenye utafiti lakini kwenye nchi za Afrika ni asilimia moja. Unaweza ukaona bado kama Afrika tunahitaji kujivuta sana *in particular* ni Tanzania sisi tupo wapi. Hali yetu bado si nzuri sana katika eneo la gharama.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine nijaribu kusema, hili la gharama mara nyingi tumeendelea kutegemea wafadhali ndio maana katika bajeti yetu hatuwezi kuiona imeweuka kiasi kikubwa kwa ajili ya tafiti. Tunakubali, tunahitaji wafadhali watusaidie tufanye tafiti lakini ukweli hawa wafadhali ili watupe fedha zao tufanye tafiti ni lazima tafiti zitaenda kwa ajili ya majibu yao na hiyo ndio changamoto. Hizi tafiti sisi tunazotaka kuzifanya ni za aina mbili tu, tafiti za msingi ambazo wanaziita *basic research* lakini na tafiti tumizi *applied* au *pure research*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kama Taifa lazima tujue hizi tafiti za msingi ambazo ndio zinatumika kwa muda mrefu, je, tunazo kwa kiasi gani? Hitaji letu ni lipi? Zimepungua kwa kiasi gani? Zinahitaji gharama gani? Tunashindwa kufika hapo. Hizi

za muda mfupi ambazo ni tafiti tumizi, tunazo kwa kiasi gani? Mpaka sasa zimetafitiwa kwa kiasi gani katika hitaji lipi la jamii katika maeneo mbalimbali? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamezungumza hapa, tunapokosekana kwenye eneo hili la tafiti, tunashindwa kujielekeza katika mipango yetu mbalimbali. Mheshimiwa Mpina asubuhi amezungumza juu ya kushindwa kujielekeza kujua kwa sasa tunahitaji elimu ipi? Elimu yenye ujuzi kwa kiasi gani? Watu wafundishwe nini ili wakaombe, wakapate soko la ajira ambalo linafanana na elimu wanayoihitaji? Yote ni kwa sababu ya kukosa tafiti.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo ya kilimo, Mheshimiwa Naibu Waziri mara nyingi anasimama hapa, anatueleza juu ya uhitaji wa mbegu za kisasa na kadhalika. Huwezi kujua hitaji la mbegu kwenye nchi kama hatuna tafiti za msingi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika maeneo mengine ya afya na usalama wa wananchi wetu, ili tuweze kujua yote ni lazima tafiti mbalimbali za muda mfupi na mrefu ziweze kufanyika. Nilisema maeneo mawili ni changamoto. Eneo la pili, ni la wataalam wabobezi. Hao wanaweza kuwa ni wale wenye shahada za uzamivu na umahiri, *Ph.D* na *Masters*, lakini zaidi ni hawa za uzamivu *Ph.D*.

Mheshimiwa Spika, wewe utakuwa ni shahidi, Mwenyekiti pia kasema, changamoto ya kwanza katika elimu ni upungufu wa wataalam katika vyuo vyetu. Hili wote tunakubaliana kwamba ni kweli, tuna changamoto ya wahadhiri. Hata katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ameendelea kueleza udahili wa wanafunzi katika eneo hili la umahiri na uzamivu, kote amesema katika vyuo vyote; nami nimeendelea kuweka pale 28, 34, 18, 64 wanaingia. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ukimtafuta Mheshimiwa Profesa Ndalichako ambaye ni mbobezi wa zaidi ya miaka 18 mpaka 20 ni sawa na wale wanaoenda kufundishwa leo! Nataka kusema nini? Nataka kusema, leo tuna changamoto ya ubora

wa elimu katika nchi yetu (*quality*). Katika hili hatupingani. Tunakubali watoto wetu wanakwenda, *enrollment* ni kubwa katika kipindi cha miaka mitano mfululizo, lakini katika wataalam hakuna ongezeko. Yaani ukitafuta hizi mbili, *line* moja inaenda katika kuongeza watoto wengi mashulenii kwa kipindi cha miaka mitano... (*Makofi*)

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Issa Mtemvu. Muda hauko upande wako. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. ISSA J. MTEMVU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Zaytun Swai atafuatiwa na Mheshimiwa Rose Tweve na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar atafuatia.

MHE. ZAYTUN S. SWAI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Wizara hii muhimu ya Elimu. Mchango wangu utajikita hasa kwenye kuishauri Serikali katika mambo kadhaa ambayo yanaweza kuinua ubora wa elimu yetu ili kutoa wahitimoo wenye weledi na wenye ujuzi sahihi ambaao unahitajika katika soko letu la ajira. Naomba vile vile, niwapongeze Kamati ya Huduma za Jamii kwa maoni yao ambayo yanaonesha dira ya kuinua kiwango cha elimu katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuongelea suala la mikopo ya elimu ya juu. Naomba kwanza nianze kwa kumshukuru Rais wetu mpewda Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kuweza kufuta ile *retention fees* ya 6% iliyokuwepo katika mikopo ya elimu ya juu. Tunamshukuru sana mama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Elimu, nimesikiliza hotuba yake leo na ameweza kufuata maoni ya Wabunge wengi na kuifuta ile

asilimia 10 ya *penalty*, tunashukuru sana Mheshimiwa Waziri.
(Makof)

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la mikopo bado kama Serikali, inabidi tufanye kazi sana, tuendelee kuondoa vikwazo na changamoto mbalimbali ikiwemo masharti magumu kwa wahitimu wetu wenyewe kupata mikopo hii ya elimu ya juu. Asilimia 15 ya marejesho ya mikopo hii bado ni kubwa kwa wahitimu wetu. Wahitimu wetu wengi wakiajiriwa wanapata mishahara ya kima cha chini na walio wengi hawazidi shilingi laki tano. Kuwatoza asilimia 15 ya marejesho ya mikopo ya elimu ya juu, bado kuna kodi na pensheni pamoja na tozo nyingine kwa kweli hatuwatendei haki wahitimu wetu. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kupitia Bodi ya Mikopo iweze kupunguza asilimia hii hadi kufikia basi angalau asilimia 10 ili tuweze kuwawezesha wahitimu wetu waishi maisha mazuri. Vilevile, tuwape nafasi wale ambao wanaweza kuchangia zaidi ya asilimia 10, basi wapeleke marejesho yao katika Bodi ya Mikopo. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, tatizo la ajira kwa wahitimu wetu bado ni changamoto. Naishauri Serikali, ili kukabiliana na tatizo hili, basi Serikali ianzishe *scheme* maalum ya mikopo kwa wahitimu wetu ili basi, wakimaliza pale vyuo vikuu kama hawajapata ajira, waweze kujiajiri wenyewe katika sekta ambazo siyo rasmi. Vile vile, nashauri mikopo hii tuishushe kwenye vyuo vyetu vya katika ikiwemo *VETA* ili basi wahitimu wetu *wa-applyujuzi* wao na kwa kutumia mikopo hii waweze kujiajiri na kujitegemea. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la TEHAMA. Sasa hivi dunia yote inaelekea kwenye *digital economy*. Naomba Serikali kupitia Wizara ya Elimu iweze kuwekeza katika masomo ya TEHAMA hususan katika shule za sekondari ili basi, tuweze kuwawezesha vijana wetu kupambana na huu uchumi wa kidijitali. *(Makof)*

Mheshimiwa Spika, leo hii ukitaka kuongeza ukusanyaji wa mapato kidijitali, unahitaji wataalam wazuri wa *TEHAMA*; ukitaka kupata wataalam wa masoko ya mazao yetu na bidhaa nyingine, tunahitaji wataalam wazuri wa *TEHAMA*. Kwa hiyo, basi naweka msisitizo katika Wizara hii ya Elimu tuweze kuwekeza kwenye masomo ya *TEHAMA* ili tuwasaidie vijana wetu wapambane na changamoto za uchumi wa kidijitali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, ili kuinua elimu yetu ya msingi na sekondari, nashauri, tuweze kuboresha mazingira mbalimbali ya utoaji wa elimu ikiwemo kuweka miundombini ambayo ni bora zaidi, ikiwemo nyumba za walimu, madarasa na maabara hususan kwenye shule zile za sayansi. Tukiweka mazingira bora ya kufundishia na vile vile, tukiwapa motisha walimu wetu hususan wale wenyewe kufundishia vizuri na kufaulusha na wale wenyewe kufundishia kwenye mazingira magumu labda shule za pembezoni, sasi tutaweza kuinua elimu yetu kwa kiasi kikubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata kule Loliondo Ngorongoro, Karatu, Mang'ola, Lokisale, Monduli walimu wetu watapenda kwenda kufundisha wanafunzi wetu na kwa ujumla tutaweza kuinua kiwango chetu cha elimu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mbunge kijana, Mheshimiwa Zaytun Swai. Mheshimiwa Rose Tweve atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Nassor Amar.

MHE. ROSE C. TWEVE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii ya Elimu ambayo ni muhimu sana. Awali ya yote namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Elimu kwa namna ambavyo amewasilisha bajeti yake hapa ili sasa sisi Wabunge tuweze kutoa mchango wetu na maoni yetu.

Mheshimiwa Spika, nitajikita zaidi kwenye Bodi ya Mikopo. Nachukua fursa hii kuipongeza sana Serikali kwa namna ambavyo iliona ni muhimu kuhakikisha mtoto yejote wa Kitanzania ambaye atakuwa hana uwezo wa kulipia elimu ya juu, basi Serikali ikatengeneza mkakati maalum wa kutengeneza *funds* ambapo tulipata chombo cha Bodi ya Mikopo ili kuratibu hili zoezi la utoaji mikopo kwa vijana wetu wa Kitanzania. Hili lilikuwa ni jambo jema na lengo lilikuwa na nia njema, lakini namna ya utoaji wa hii mikopo ndipo kwenye changamoto. Hapa ndipo *tulipo-create crisis.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mikopo hii namna ambavyo inatolewa haikuzingatia nini kama Taifa tunahitaji hasa kwa sasa hivi? Pia haijafanya utafiti. Mheshimiwa Mpina hapa amesema asubuhi, hivi wenzetu wa Wizara ya Elimu mnafanya utafiti kuona sokoni ni nini kinahitajika? Mheshimiwa Waziri wa Elimu, asubuhi umekuja hapa umetueleza kuwa tumeongeza sasa Bodi ya Mikopo kutoka *4.6 billion* sasa hivi zitakwenda kwenye *five billion*. Ni jambo jema, lakini zinakwenda kufanya nini? Zinakwenda kusaidia vijana wa aina gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa Bodi ya Mikopo walikuja kutupa mtiririko wa namna ya hizi fedha zimetumika *so far*. Kwenye kada ya sayansi ya jamii na sanaa, maana yake *Bachelor of Art, 64.9 percent; Uhandisi 5.3 percent; Afya 4.7%; Sayansi ya kilimo, inaendelea kushuka 1.8, Uhandisi wa Mafuta na Gesi ndio kabisa, 0.10 na mengineyo.*

Mheshimiwa Spika, hapa ndipo *tulipo-create crisis.* Kama mikopo hii yote; *64 percent* ya hii mikopo inakwenda *ku-fund* vijana ambao wana *degree* ambazo ziko mitaani, sasa hivi soko liko *saturated*. Nikawa najiuliza, hivi Wizara ya Elimu hatujalionia hili? Sasa hivi na hizo *five billion* tunaenda bado *ku-create* hawa vijana wa *Bachelor of Arts* ambao bado tunaenda *ku-create degrees* ambazo hazihitajiki kwenye soko la elimu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimezidi kujiuliza, *what's wrong na vyuo vyetu vya kati?* Vyuo vya ufundu, ndio *doers*, hawa ndio wanaoingia kule *field*. Tulishauri hapa Mheshimiwa Waziri, nchi za wenzetu ambazo zinaendelea sasa hivi China inakua kwa asilimia 10, lakini bado wameona umuhimu wa kuhakikisha wanarudi kwenye vyuo vya kati. Kwa sababu mmesema kigezo kikubwa ni mtoto kutokuwa na uwezo wa kujilipia.

Je, hivi vyuo vya kati hakuna watoto wa masikini wanaohitaji hii mikopo? Hawa ndio *doers* Mheshimiwa Waziri. Ukienda Kituo cha Afya, tuna daktari mmoja, lakini wale wasaidizi karibia watu 30 wote ni wa elimu ya kati. *Who is funding these people? (Makof)*

Mheshimiwa Spika, *engineer pale anatengeneza daraja, tunahitaji ma-engineerwangapi?* Ni *engineermmoja* na watu wenye ujuzi wa kati. *Who is funding these people?* Nina uhakika tungekwenda huko, *I am not arguing what, tupunguze kiasi.* Kama tutapeleka *at least three billion, at least* hizi *two billion* zije huku ziwasaidie watoto wa uchumi wa kati kuendeleza uchumi wa kati. Moja, hawa watoto wataweza kulipa hii mikopo kwa sababu, hizo taaluma zao ndizo zinahitajika huku. Pili, wataweza hata kuongeza pato la Taifa kwa sababu, wataweza kulipia mikopo na kujikumu na shughuli zao za kilasiku na kutunza familia zao. Kwa hiyo, *focus yetu... (Makof)*

SPIKA: Waheshimiwa ambao mlikuwa mnachangia hapa, mnaona Mbunge mzoefu anavyokwenda? Yeye amechagua Bodi ya Mikopo na anavyoiona Bodi ya Mikopo na *analysis* yake. Dakika saba siyo nyingi, huwezi kuongea vitu vitano. Endelea Mheshimiwa Rose. *(Makof)*

MHE. ROSE C. TWEVE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Bado narudi kwenye umuhimu wa hivi vyuo vya kati. Tulikuwa na *CBE*, Mipango, Chuo cha Tengeru; sasa hivi kaka yangu amesema hata Chuo cha Mwanza, kile cha Uvubi, sasa hivi watu wote wanakwenda kwenye *degree*. *Why are we expect* na hivi vyeti wakati tunahitaji hivi vyuo vya kati?

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, hii Bodi ya Mikopo ije na sura na mikakati ambayo Watanzania tunaitaka. *We can not be doing the same thing over and over and expect different results.* Kama hawa watoto wa artndio wamejaa kule na mwakani tena *Bachelor of Art* zimejaa mtaani, manung'uniko lazima yataendelea na *tuna-create* bomu ambalo kuja kulizima itakuwa ni kazi sana Mheshimwa Waziri. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, ushauri wangu kwa Serikali utakuwa kama ifuatavyo: Moja, kama *tume-create special window* kwa ajili ya kilimo, *why not education?* Sasa hivi tutakapokuja hapa iwe ni Bodi ya Mikopo *not* Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. *Tuzi-involve* na sekta nyingine kama *banks* ili nao waje wawe na michango katika kuendeleza elimu yetu nchini.

Mheshimiwa Spika, la mwisho,....

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Natamani nikuongeze muda, lakini...

MHE. ROSE C. TWEVE: Mheshimiwa Spika, hili ni la mwisho.

NAIBU SPIKA: Bahati mbaya.

MHE. ROSE C. TWEVE: Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, tulikuwa na *new formula* ya *capitation* kwenye kutoa ruzuku shulenii. Mheshimiwa Dada Grace amesema pale asubuhi, hali ni mbaya, tulishajulishwa ianze kutumika, imekwama wapi Mheshimiwa Waziri? Ni kwenu Wizarani au Wizara ya Fedha? Hii ndiyo ilikuwa *more practical/inajibu* zile shule ambazo ziko mbali na shule ambazo zina uhitaji maalum ili waweze kupata pesa zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Rose Tweve. Anastahili makofi makubwa zaidi ya hayo. (*Makofi*)

MHE. ROSE C. TWEVE: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Kwa kweli umetuchokoza na umemchokoza Profesa. Yaani Profesa kweli asilimia 60 inaenda kwenye *Bachelor of Arts*? Ili iweje? Wanapata madeni 60 percent sijui riba, watapata wapi mahali pa kufanya kazi? Hatudharau *Bachelor of Arts* wala nini, lakini si tunakwenda kwa wakati? Unaangalia mahitaji ya hali halisi na mambo, soko na kadhalika. Umeongea *point* ya maana sana.

Asilimia nne kwa afya, asilimia tano kwa *engineering*, hatuwezi kwenda! Lazima upunguze. Piga ibaki *20 percent*, sijui *30*, kadri utakavyoona *zero point something, geology* na kadhalika. Yaani yale mambo ambayo ndiyo yenyewe; hata jina lile la Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, umependekeza vizuri, likaangaliwe. Kama ni sheria iletwe hapa turekebishe. Tulikuwa na nia hiyo mwanzoni, lakini tumegundua kumbe siyo lazima mikopo iende elimu ya juu peke yake, inaweza ikaenda elimu ya katni nyingine.

Tunakushukuru sana Mheshimiwa Rose.

Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, atafuatiwa na Mheshimiwa Jafari Chege. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia. Kwanza, nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha mimi pamoja na sisi sote humu ndani kuwa na afya njema. Pia, niipongeze Waziri na Naibu Waziri pamoja na Watendaji wa Wizara kwa hotuba yao nzuri sana.

Pia, niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano kwa kutoa elimu bure kwa wanafunzi wa shule za msingi pamoja na sekondari kwa nchi nzima, ikiwemo Wilaya ya Nyang'hwale

ambayo imeweza kupokea fedha hizo zaidi ya bilioni tatu. Naipongeza sana Serikali. Pia, kuna changamoto mbalimbali nyingi, lakini nitazungumza chache.

SPIKA: Mheshimiwa Amar.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Spika, naam.

SPIKA: Wenyewe wanaiita Elimu Bila Malipo kama sikosei, lakini siyo Elimu Bure. Watansahihisha baadaye. Wanasema kuna tofauti katika vitu hivyo viwili.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nirekebishe kauli, Elimu Bila Malipo.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali imeweza kutuletea fedha zaidi ya shillingi billioni tatu kwa ajili ya Elimu Bila Malipo upande wa shule za msingi pamoja na sekondari. Kuna changamoto nyingi kwenye upande wa elimu lakini nitazungumza chache, hususan kwenye upande wa Wilaya yetu ya Nyang'hwale.

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa kwamba upungufu wa vyumba vya madarasa kwa nchi nzima upo, lakini nitazungumzia kwa upande wa Wilaya yetu ya Nyang'hwale. Tuna upungufu sana katika shule za msingi, mahitaji ya madarasa ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tunahitaji madarasa 1,138, lakini yaliyopo ni 616, upungufu ni madarasa 522. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri hili alichukue, lakini nitakuwa na ushauri huko mbele. Pia, tuna upungufu wa madarasa kwenye shule zetu za sekondari zaidi ya vyumba 30, lakini pia tuna upungufu wa Walimu. Upande wa shule za msingi tuna upungufu wa Walimu 342 na upande wa sekondari tuna upungufu wa Walimu 180.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa ushauri kwa Mheshimiwa Waziri kwamba tumekuwa tukiandaa vijana wetu na wanapomaliza masomo ama kutokuendelea na

masomo wanarudi mtaani. Mfano, vijana wetu wanaoshindwa kuendelea na elimu ya juu, wanarudi mitaani wanakuwa hawana kazi. Naomba kushauri kwamba Wilaya ya Nyanghwale tuweke utaratibu mzuri hapo mwakani Wizara iingize ndani ya bajeti iweze kutujengea Chuo cha Ufundidi Stadi ili wale wanafunzi wanaoshindwa kuendelea na elimu ya juu, basi waweze kujifunza ufundidi ili waweze kujajiri wenyewe.

Mheshimiwa Spika, nataka nifikishe pia kilio cha Walimu wetu wastaaifu. Kuna Walimu wastaaifu wapatao 20, leo wana zaidi ya miaka sita wanadai mafao yao na wameshakuja hapa Dodoma nimewapeleka kwenye ofisi husika zaidi ya mara nne, wamehakikiwa.

SPIKA: Mheshimiwa rudia hiyo *point* yako, Waziri wa Nchi alikuwa hakusikilizzi.

MHE. HUSSEIN N. AMAR: Mheshimiwa Spika, kuna Walimu wastaaifu zaidi ya 20, wakidai mafao yao zaidi ya miaka sita. Wamekuja hapa Dodoma nimewafikisha sehemu husika zaidi ya mara tatu, wanaambiwa tumeshahakiki subirini malipo yenu. Mpaka leo hii wamenipigia simu wanasema Mheshimiwa hatujalipwa mafao yetu na wengine ni wagonjwa, hali zao si nzuri. Naomba nilifikishe hilo kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba kutoa ushauri kama walivyoshauri wenzangu kuhusu wanafunzi wetu wanaotoka majumbani saa 12, wanarudi jioni wakiwa hawajanywa chai, hawajala chakula, naomba uwekwe utaratibu ulio mzuri ili wanafunzi wetu waweze kupata chakula. Kipindi cha nyuma kulikuwa na utaratibu huo wa kutoa chakula kwenye shule zetu, lakini pakawa na upotevu wa chakula ambacho kilikuwa kikilimwa na wale wanafunzi. Tujaribu kuweka utaratibu mzuri, Bodi ya Shule iwashirikishe wazazi pindi watakapokuwa wanalima wanafunzi chakula chao, wazazi na wenyewe washughulike kuhakikisha kile chakula kinatumia ipasavyo; ili wale wanafunzi wapate chakula. Nitatoa mfano, kuna vijana wa sekondari wanatoka

eneo moja kwenda eneo lingine maili saba kwenda kusoma kuanzia saa 12 mpaka jioni, wanarudi wakiwa hawajala chakula. Nadhani hawatakuwa na mafanikio mazuri kuhusu elimu yao, ndio maana tunatengeneza vijana wengi ambao wanashindwa kuendelea na masomo yao.

Mheshimiwa Spika, sina mambo mengi ni hayo tu machache ya ushauri, lakini naomba suala la Walimu wangu wastaafu lichukuliwe kwa umakini, walipwe haraka fedha zao kwa sababu leo ni miaka sita wanafuatilia mafao yao.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii.
(Makof)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Nyang'wale. Sasa twende Rorya Mheshimiwa Jafari W. Chege.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi.

SPIKA: Na atafuatiwa na Mheshimiwa Mwantumu Zodo.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Spika, nianze tu kwa kusema ukisikiliza toka asubuhi mijadala ya Bunge letu hili Tukufu, Bunge la Kumi na Mbili, lakini pia ukisikiliza wadau wanavyozungumzia hasa kwenye wizara na sekta nzima ya elimu; utagundua wote tunajikita kwenye sera ya elimu yetu ilivyo kwa maana sera ya mwaka 2014. Lakini pia tunazungumzia...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa mara nyingine tena.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Spika, pia tunazungumzia mfumo wa utoaji wa elimu nchini namna ulivyokaa. Ukisikiliza hotuba ya Mheshimiwa Rais, alivyozungumza juzi kipindi anahutubia Bunge, amezungumzia namna Serikali ilivyojikita kwenda kuitia Sera

ya Elimu Nchini. Hata hivyo, sote hapa ni mashahidi huko tunapotoka kwenye majimbo, kwenye maeneo yote ya mijini, namna ambavyo wananchi na wadau mbalimbali wamekuwa wakizungumzia muundo na Sera ya Elimu ilivyokaa na namna gani ambavyo wameshauri jinsi ya kutoka hapa.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaenda kwenye kuchangia. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kwenye majumuisho yake, kwa sababu leo tunajikita kwenye bajeti, basi kama haitatupendeza, Bunge hili la Kumi na Mbili kwa mikutano inayofuata Mheshimiwa Waziri waende kama Serikali, waende wakaanze mchakato wa kukaa na wadau, kuona namna gani ya kuifumua Sera ya Elimu na mfumo mzima wa elimu namna ulivyokaa ili Bunge linalofuata kwa maana kikao kinachofuata iwe kama *section*, iwe ni sehemu maalum ya kujadili namna ya mfumo na Sera ya Elimu jinsi ilivyokaa, kwa sababu pale tutakuwa na uwanja mpana wa kujadili elimu yenye kama ilivyokaa Nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pili, tutakuwa tunazungumzia yale ambayo wao wamekaa na wadau angalau wamepata mawazo yote kwa ujumla ili Bunge lako Tukufu, hili Bunge la Kumi na Mbili, tutoke na maazimio namna gani tunakwenda kufumua mfumo mzima wa elimu ili tutakapokuwa tunazungumza kama Wabunge tuwe angalau tumeshiriki kwenye hili ambalo kimsingi ukitazama kila mtu anayezungumza, anazungumzia namna ya mfumo na sera jinsi ilivyokaa ya utoaji elimu nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Waziri atakapokuja angalau atuhidi hiyo, kwamba angalau baada ya Bunge hili watakopkenda waweze kuangalia namna gani tunaweza tukarudi mara ya pili kwenye vikao vinavyofuata ili tuweze kulijadili hili kwa upana wake na kwa ujumla ili tutoke na kitu kimoja kama Taifa ambacho kitakuwa na mustakabali mzuri wa kтуongoza kwenye sekta ya elimu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maoni hayo, nirudi tu kuzungumzia masuala baadhi ndani ya jimbo langu. Nilikuwa

natamani sana Wizara ya Elimu na Wizara ya TAMISEMI wafanye kazi kwa ukaribu sana kwa kushirikiana. Leo ulikuwa unazungumza hapa asubuhi, kuna mahali ukienda ndani ya jimbo langu mathalan, mimi nina shule mbili ambazo moja imejengwa tangu 2005, wamejenga wananchi kuanzia msingi. Wamejichangisha wenyewe wamejenga msingi, wamejenga maboma zaidi ya matano kule, lakini namna ya kupewa idhini sasa ya kufunguliwa iwe shule, kwa maana ya kufanya usajili mpaka leo ninavyoungumza hawajapewa usajili. Kila wakienda kwa hawa mabwana ambao wanajiita watu wa ukaguzi wanawaambia bado ongezeni majengo mawili. Unaweza ukatazama maboma matano na choo na ofisi za Walimu wamejenga wananchi, hapa Wabunge wengi wanatoka maeneo ya vijijini wanajua namna inavyokuwa kwa wananchi wakati mwingine kwenye kuchangishana ili kujenga haya maboma.

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine mtu *ana-sacrifice*, alikuwa ana shilingi elfu moja, anaacha kwenda kununua mboga yake, kununua mahitaji yake ya ndani anachanga ili aweze kujenga ile shule. Badala yake wanapomaliza bado hatuwezi kuwapa usajili kwenye shule hii. Nini maana yake? Unakuta shule nydingine ambayo mwanafunzi anatakiwa kwenda ipo zaidi ya kilomita tano kutoka maeneo wananchi wanapoishi na wakati mwingine katikati ya maeneo hayo kati ya shule na wananchi wanapoishi kuna majaruba ya maji. Ili mwanafunzi huyu wa miaka saba au nane aweze kufika kule wakati mwingine wakati wa mvua inamlazimu kupita kwenye yale majaruba. Wananchi kwa kutambua umuhimu huo wakaamua kujenga shule yao. Leo ukiwaambia huwezi kuwasajilia na wakati ni suala la kuzungumza kati ya Wizara ya Elimu na TAMISEMI tukaona namna gani tunawasaidia, tunakuwa hatuwatendei haki wananchi hawa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa ku-*wind up* anisaidie kwenye shule zangu hizi mbili hizi; kuna Shule ya Tacho ipo Kata ya Kirogo na Shule ya Kuruya ipo Kata ya Komuge. Hizi ni shule ambazo zimejengwa na wananchi; hivi ninavyozungumza maana yake Shule ya

Kuruya hata wanafunzi hawajakwenda mwaka huu, wameambiwa hatuwezi kuwapa wanafunzi kwa sababu hajjasajiliwa, lakini wamejenga wananchi kwa kuepuka huo umbali wa kusafiri muda mrefu. Niombe sana Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho angalau wananchi nao wapate ahueni kutokana na nguvu zao ili mwisho wa siku wasije kuona nguvu zao zimetumika bila ya kuwa na maana yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la pili, naomba sana, Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho angalau apitie yale madai mbalimbali ya Walimu. Walimu wamekuwa na manung'uniko mengi sana na naamini kabisa hili lipo ndani ya uwezo wa Waziri. Manung'uniko haya anaweza akayatatua kwa muda mfupi sana. Wananchi wengi, Walimu wengi wamekuwa wakilalamikia miundombinu yao; maeneo wanayofundishia siyo rafiki kwao, lakini wengi wamekuwa wakilalamikia madeni ya likizo na madeni mbalimbali ya malimbikizo ambayo yamelimbikizwa huku nyuma. Naamini kupitia Mheshimiwa Waziri kwa sababu tayari nimeambiwa alikuwa ni Mwalimu na alikuwa Mwalimu mzuri atawenza kuwasaidia katika hili.

Mheshimiwa Spika, pia wana madai ya likizo ambazo walikuwa nazo. Ni imani yangu Mheshimiwa Waziri atawasaidia hili. Pili, tunapofanya mabadiliko ya mtaala, tunapowapelekea Walimu niombe sana tutengeneze fedha angalau za kuwatengezea *capacity building*, tuwajenge ili waendane na ule mtaala mpya tunaowapelekea. Kwa sababu unapobadilisha mtaala Mwalimu bado alikuwa anajua *skills* za nyuma zilizopita, ukimbadilishia anapata wakati mgumu sana kuendeana na ule mtaala mpya ambao umeupeleka kipindi hicho. Tuweze kuwapa mafunzo ili waendane na mtaala mpya ambao tumewapelekea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabisa, ningependa sana kuzungumzia kuhusiana na ujenzi wa Vyuo vya VETA. Mimi Rarya nimepaka na Tarime, *population* ya haya majimbo mawili au hizi halmashauri ni zaidi ya watu 600,000.

Hata kama bado Serikali inajipanga namna gani ya kupeleka Chuo cha *VETA* kila halmashauri, tuwekeeni chuo kimoja hata ukiweka pale *VETA* katikati ya Tarime na Rarya angalau tuweze kuwasaidia wanafunzi wote wanaotoka ndani ya halmashauri zote mbili...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Chege.

MHE. JAFARI W. CHEGE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Nakushukuru sana kwa mchango wako. Nami napigia mstari hoja yako ya shule hizi ambazo hazilandikishwi. Watoto wanafika darasa la saba, shule haijaandikishwa. Watu wa udhibiti ubora wana vipengele tu, inafika darasa la sita, la nne, la tano na shule hiyo ambayo haijaandikishwa haipelekewi Walimu rasmi. Wazazi wanachanga kujenga shule, wanachanga kuweka mwalimu, wanachanga kila kitu wenyewe. Serikali mpaka inafika darasa la sita majengo yote hajjawahi kutoa shilingi moja. Inachofanya Serikali ni kuweka masharti, kuweka masharti, lazima tuliangalie hili jambo. Shule iandikishwe ili zipate mwalimu rasmi lakini wananchi tuendelee kujenga kama kawaida hata kama wananchi tunajenga wenyewe, Serikali haiweki mkono haina shida, lakini itambulike ili ipate Mwalimu, ipate *registration*, iwe katika utaratibu mzima.

Mnashindanisha mashule baada ya mtihani wa darasa saba; sijui wilaya hii ya mwisho, hii wilaya ya ngapi, ya ngapi! Wilaya nyiningine ina shule 20 sijui ngapi katika kundi hili la shule zinaitwa shikizi sijui! Unategemea watoto wa darasa la saba wa shule shikizi wamesoma mpaka darasa la tano hawana mwalimu rasmi, wamesoma mpaka darasa la sita au wamemaliza darasa la saba hawana mwalimu rasmi unategemea matokeo yatafanana na wale ambao shule zao zote zimeandikishwa. Hayawezi kufanana hii ni shida

kubwa; watu wa ubora twende pamoja na nia ile ya Serikali na ya Chama Cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Watoto wale wanastahili shule kama hao wenye miundombinu yote inayotosha. Ni muhimu sana hilo, watoto hao wananyanyasika sana, lakini zaidi wazazi tunawavunja moyo kwelikweli. Unawakuta wazazi wamejenga madarasa mpaka darasa la sita halafu unakwenda Mbunge kuwahamasisha waendelee kujenga shule yao, wanakwambia sisi tumejitahidi mpaka hapa; shule yetu haiandikishwi, hivi Mbunge jibu lako linakuwa nini? Ukienda kwa watu wa ubora wanakwamba hizo shule za kisiasa, sio za kisiasa hizo ni shule. Waheshimiwa Wabunge tushughulikie hili jambo liishe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri kesho hapa, kwa kweli uje na maelezo. Kwa nini watu wanakataa shule zetu za wananchi, hiyo Sera wameitoa wapi ya kukataa shule za wananchi? (*Makofi*)

Nilikutaja Mheshimiwa Mwantumu Zodo, atafuatiwa na Mbunge wa Mpwapwa Mheshimiwa George Malima.

MHE. MWANTUMU M. ZODO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nikushukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii muhimu ya Elimu. Naomba nianzie kwenye sensa ya watu na makazi ya mwaka 2002. Kwa mujibu wa matokeo ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2002, tulikuwa tupo watu milioni 34 Tanzania. Lakini baada ya miaka kumi sensa ya 2012 tulitoka milioni 34 mpaka milioni 45. Ni nini tafsiri yake. Tafsiri yake ni kuwa kila mwaka kutoka 2002 mpaka 2012 tulikuwa tunaongeza kwa wastani wa watu milioni moja kila mwaka. Kwa maana hiyo pia kila mwaka tuna wajibu wa kuongeza madawati, madarasa, Walimu, vifaa mashulenii kwa sababu idadi ya watu haishuki bali inaongezeka na itaendelea kuongezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukiangalia kwenye ajira za Serikali. Serikali imeajiri watu 480,000 tu mpaka sasa. Kutoka kwenye watu milioni 45 ni sawa na asilimia moja, lakini wengine

wameajiriwa kwenye sekta binafsi na wengine wamejajiri kwenye kilimo na biashara nyingine kama ujasiriamali na vitu vingine kama hivyo. Sasa tukiangalia takwimu hizo, ipo haja sasa ya kufanya maboresho makubwa kwenye mtaala, kwa sababu ni kiwango kidogo sana kinaajiriwa, asilimia 99 ya watu wanatakiwa wajajiri wenye we ndio tafsiri yake. Kwa maana hiyo sasa tunatakiwa tuboreshe mitaala na tuongeze yale masomo ambayo mwanzo tulikuwa tumeyafuta. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, zamani wakati mimi nasoma, kulikuwa na masomo ya sayansikimu, kulikuwa na masomo kama sayansi kilimo, kulikuwa kuna masomo kama maarifa ya nyumbani. Masomo yale yalikuwa yanafundisha vitu mbalimbali, mkiwa kule shulenii mnafundishwa kilimo, upishi, mnapika keki na nini, lakini sasa hivi tunawekeza fedha nyingi sana kwenye elimu bure, tukishamaliza hapo mwanafunzi anamaliza darasa la saba, anakwenda kutoa 350,000 tena kufundishwa kupika keki. Sasa sijui tunamsaidiae? Tumewekeza fedha nyingi kwenye kumsomesha, halafu bado akatafute tena ujuzi mdogo tu wa kupika keki kwa 350,000. Anakwenda kujifundisha ushonaji ambao mwanzo yalikuwepo hayo masomo, lakini sasa anakwenda kujifundisha kwa 200,000, anakwenda kujifundisha ujasiriamali kwa 500,000.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Serikali ya Tanzania inawekeza fedha nyingi sana kwenye elimu bure. Kama tunawekeza fedha nyingi kwenye elimu bure, ipo haja ya kufanya maboresho kwenye mtaala wetu umwezeshe mwanafunzi baada ya elimu kujitegemea, lakini sasa wanafunzi hawa pia bado ni ngumu sana kujitegemea moja kwa moja kwa sababu; elimu ya msingi umri wa mwanafunzi kuanza shule ni miaka saba na miaka sita. Mwanafunzi anamaliza elimu ya msingi akiwa na miaka aidha 12 au 13, ni uongo hata kama tutampa hizi stadi mwanafunzi wa miaka kumi mbili atakayemaliza darasa la saba na mfumo ukamuacha akawa amefeli yupo nyumbani, bado hawezikufanya chochote huyu bado ni mtoto mdogo mnoo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sasa, niishauri Serikali elimu msingi iwe ni kuanzia darasa la kwanza mpaka kidato cha nne, angalau sasa huyu mwanafunzi wa darasa la kwanza mpaka kidato cha nne; tukimpa sasa hizo *skills* anaweza baada ya hapo akitoka akaenda kukaanga *chips*, anaweza akawa bodaboda, anaweza akaenda kwenye ufgajji, anaweza kwenda kwenye kilimo, lakini sio mwanafunzi wa miaka 12 au 13 ambaye mfumo umemwacha, hataweza kufanya chochote. Matokeo yeke ndio hizo ajira za watoto wanachukuliwa kwenda kufanya kazi za ndani, kuuza karanga, tunaona watoto wengi stendi, majumbani, wapo watoto wadogo sana wamemaliza darasa la saba hawakupata bahati ya kuendelea, aidha anafanya kazi za ndani au anaiza karanga stendi au anaiza mayai ni watoto wadogo mno. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sasa, naona ipo haja ya kufanya maboresho kwenye mtaala, lakini pia kuangalia elimu msingi iwe ni kuanzia shule ya msingi mpaka *form four*, angalau mtoto huyu atamaliza *form four* akiwa aidha na miaka 16 au 17 angalau tutakuwa tumenvuta...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. MWANTUMU M. ZODO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Mwantumu Zodo. Mheshimiwa Mbunge wa Mpwapwa George Malima atafuatana na Mheshimiwa Mhe. Santiel Kirumba.

MHE. GEORGE N. MALIMA: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hotuba ya Wizara hii ya Elimu. Niwapongeze sana kwa kazi nzuri ambayo wanayoendelea kuifanya katika wizara hii. Napenda nichangie katika eneo la miundombinu. Sera yetu ya elimu bila malipo imepelekea kuwa na ongezeko kubwa

sana la wanafunzi wanaojiunga darasa la kwanza, lakini hata wale wanaojiunga kidato cha kwanza. Kwa hiyo utaona kwamba miundombinu haitoshi kwa sababu ya wingi wa wanafunzi. Kwa hiyo, naishauri sana Serikali kuititia Wizara hii ya elimu iangalie eneo hili kwa jicho la karibu sana kwa sababu uwiano wa watoto wanaojiunga shule na uwiano wa miundombinu inayojengwa haufanani kabisa.

Mheshimiwa Spika, niongelee hasa hapa kwenye madawati. Naamini kabisa *catalyst* ya kufaulu watoto ni mazingira mazuri ya kusomea. Mtoto anayesoma amekaa chini au amesimama hawezi kufaulu sawa na yule anayekaa kwenye viti. Hata hivyo, ninachokiona, mara nydingi msisitizo wa kutengeneza madawati unafanyika mwezi Januari, wanapojinga darasa la kwanza na kidato cha kwanza ndipo matamko yanatoka kwamba kufika tarehe Fulani madawati yaweshakamilika, watoto waanze shule. Baada ya hayo hakuna kitu kinaendelea na mimi katika Jimbo langu la Mpwapwa, watoto wameathirika, wapo waliosubiri madawati yatengenezwe ndipo wajunge na shule wakati wengine walishaanza tayari kusoma; wao wanasubiri madawati yatengenezwe.

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa naomba nishauri Serikali tuwe na Mpango endelevu wa kutengeneza madawati. Kwani kuna ubaya gani ikifika Januari tuna madawati *store*, lazima tuwe na utaratibu wa kutengeneza madawati kwa kutumia halmashauri zetu. Madawati yatengenezwe mwaka mzima ili tuwe na madawati ya kutosha, yawekwe *stote*. Tunapofungua shule mwezi Januari basi wanafunzi wapate mahali pa kusomea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni walimu, walimu kama tunavyojuua wote hawatoshi na mimi ningeshauri Wizara ijitätahidi sana kupata vibali kwa ajili ya kuajiri walimu. Lakini kuna tatizo moja dogo. Katika Jimbo langu nime-*experience*, walimu wanapangiwa vituo, wanaripoti halafu wakiondoka hawarudi tena. Hiyo sielewi kwa sababu unahesabika kama shule il eina walimu saba kumbe ina walimu sita au watano. Walimu wawili waliripoti halafu hawakurudi tena kwenye kazi,

ni kwasababu ya mazingira ya namna hiyo. Sasa Wizara lazima ije na Mpango na ikiwezekana ikomeshe tabia hii ya walimu ambao wanaajiriwa na kupangiwa vituo halafu wanaondoka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia vijana wetu wengi wanaomaliza elimu ya vyuo vikuu hawarudi makwao, wanakaa mjini. Kwenye miji kama Dodoma, Dar es Salaam, Arusha na mahali pengine wamejazana na kila siku utakutana nao wana bahasha za kaki wakitafuta kazi za kuajiriwa. Ni kwasababu elimu waliyoisoma hawawezi kui-*apply* kule walikotoka. Hawawezi kui-*apply* kwenye mashamba, kwenye *entrepreneurship* kwasababu hawakujifunza hayo. Kwa hiyo, nataka nitoe wito kwa Wizara, Mheshimiwa rais katika hotuba yake juzi alizungumza habari ya kuboresha mitaala ili iendane na mazingira ya nchi yet una iendane na soko la ajira. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kilimo ndiyo sekta inayotoa ajira kwa wingi kuliko sekta nyingine yoyote lakini kwa bahati mbaya sana haifundishwi sasa shulen. Kwa hiyo unategemea vijana wote ambao watamaliza shule hawawezi kwenda kufanya kilimo kwasababu hawajajifunza. Sasa tunapoiangalia mitaala hii kwa upya lazima iendane na mazingira yetu. Tuwafundishe katika sekta ambayo wataenda kufanya ajira, wanaenda kupata ajira ya kutosha. Wataenda kujajiri wenyewe na ndiyo lengo letu. Elimu yetu i-focus kwenye kujajiri wenyewe. Vijana wetu wajiajiri wenyewe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda niwapongeze wamezungumza habari ya ukarabati wa vyuo vyetu vya ualimu. Ni muhimu sana walimu wetu wakafundishwa, wale wanaokuja kufundisha watoto wetu wakasoma katika mazingira mazuri katika Jimbo langu la Mpwapwa chuo chetu kinasaidika katika utaratibu huu. Bajeti inayoisha mwaka huu tulipata shilingi bilioni 2.1 kwa ajili ya ujenzi wa miradi mipyä pale chuoni. Kuna ujenzi wa bwalo, kuna ujenzi wa jengo la ghorofa moja kwa ajili ya *computer* lakini kuna

ujenzi wa nyumba za watumishi ambao iko katika mtindo wa *two in one*. Lakini kinachonisikitisha ujenzi umesimama...

SPIKA: Tayari, muda umekwisha Mheshimiwa.

MHE. GEORGE N. MALIMA: Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iangalie ili ujenzi huu uanze mapema. Naunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana. Ahsante sana. Mheshimiwa Santiel Kirumba, atafuatiwa na Mheshimiwa Thea Ntara. Mheshimiwa Santiel.

MHE. SANTIEL E. KIRUMBA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote ningependa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Ningependa kumpongeza Waziri wa Elimu kwa jinsi anavyofanya kazi yake vizuri, ni mama ambaye anajitoa sana kwenye hii kazi na hata ukimuita kwenye Kamati yoyote ni mwepesi kuhudhuria. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini matatizo yanayowakabili wanafunzi hayana tofauti sana na matatizo ambayo yanawakabili walimu. Walimu unakuta kwa mfano natokea Jimbo la Msalala, Kata ya Bulyankulu walimu ni wachache. Walimu wana changamoto nyingi, wakitoka kazini wanaenda kuchota maji, kule unaweza ukakuta walimu wale labda wakang'atwa na nyoka. Kingine napenda kusema kwamba walimu hawa wamekuwa wakipitia changamoto nyingi sana *apart from* sisi Wabunge kuwasemea na watu wengine kuwasemea, walimu hawa wana chama chao. Chama chao hiki kimetuwa sio msaada kwa walimu kabisa, walimu wanakatwa asilimia mbili katika mishahara yao kila mwezi lakini mwalimu hata akipata ajali hawezikusaidia na chama chake. Zaidi kwamba anaonekana atatibiwa na Bima ya Afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, walimu hawa nimechukua tu kwa *ratio* ya kawida, walimu 5,000 Tanzania hii ambao wanakatwa shilingi 25,000 kwa mwezi wabachangia milioni 125,000. Kwa mwaka chama cha UWT kwa walimu 5,000

kipanata bilioni 1.5 lakini mwalimu anapostaafu chama hiki kinampa mabati. Kweli kwa miaka yote anayochangia ni kweli anastahili mwalimu kupewa mabati? Tufike mahali sisi wenyeWE tunawafanya hawa walimu wanashindwa ku-perform katika kazi zao vizuri. Chama hiki wanalazimishwa automatically kijiunga lakini katika ya CWT inamwambia kwamba mwalimu kijiunga ni hiari yake lakini automatically wanashirikiana na utumishi kuwafanya walimu hawa kuingia na kuwakata hiyo asilimia mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninachoomba Serikali chini ya Wizara ya Elimu, walimu wasilazimishwe kijiunga na hiki chama kwasababu sio msaada kwao. Walimu wana changamoto nyingi lakini CWT haiwasemei chochote zaidi ya kukusanya. CWT ina mabenki, lakini walimu hawanufaiki. Wana kila hela wanazochukua, mahesabu yao hayako wazi. Sijawahi kusikia CWT inatoa mwongozo wowote kwamba mapato na matumizi yaliyotumika mwaka huu yako hivi.

Mheshimiwa Spika, naomba *the way CAG anavyopambana* na watu wengine naomba sasahivi akaifanyie kazi CWT. Kwasababu haiwezekani walimu wanateseka kiasi hiki, CWT iko kimya! Kuna walimu wamefukuzwa vyeti feki, CWT ni chama tu kilitakiwa kiwape hata washirika wake pesa zozote hata kile kifuta jasho kwa ambao wamefukuzwa lakini CWT imekaa kimya! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kwa kweli Waziri wa Elimu hiki chama kifutwe kwasababu walimu wengi wanakuambia hakina manufaa, wanalamika. Elfu 25,000 kwa mwalimu mmoja kwa mwaka ni 200,000. Mimi kule ninapotoka chumba mwalimu ni shilingi 10,000 kwa hiyo hii kodi ya karibu mwaka mzima.

SPIKA: Mheshimiwa Santiel, kwa hiyo unataka walimu wasiwe na chama.

MHE. SANTIEL E. KIRUMBA: Mheshimiwa Spika, wajunge kwa hiari lakini sio kwa kulazimisha kwasababu walimu nao wana changamoto. Nakupa mfano kuna mwalimu

Shinyanga alipata ajali, chama kama chama anachangia, kweli leo ukistaafu upewe bati mbili na shughuli zote hizi unazowafanya wananchi wako? *Bundle* mbili za bati kweli ni sawa? Tuongee kwa hali halisi. Mwalimu anachangia, ni walimu wangapi wamechangia? Kwa nini hiki chama hakiko wazi? Waache watu wajiunge kwa hiari sio kuwalazimisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, walimu nao wana haki sidhani hapa kama sisi Wabunge tungelazimishwa kuchangia hela...

SPIKA: Mheshimiwa Santiel kuna mambo mengi inabidi ujifunze bado. (*Kicheko*)

MHE. SANTIEL E. KIRUMBA: Mheshimiwa Spika, sijakataa lakini naangalia. Nimechukua changamoto ambazo walimu wanapitia...

SPIKA: Nafikiri hilo siku moja ulinyanyue kwenye Kamati ya Chama upate elimu kidogo ya mambo haya yakoje na nini. Kuna haja ya ku-*improve* kama kuna *improvements* lakini ukisema kufuta sasa wabakie *empty* ndiyo watakuwa wamekwenda, wamerudi nyuma hatua 100? Lakini kama kuna *areas of improvement*, ndiyo kazi yetu Wabunge lakini kwamba kundi la wafanyakazi wasiwe na, yaani *does it...* ila kama kuna mapungufu ni *areas* za ku-*improve*.

MHE. SANTIEL E. KIRUMBA: Mheshimiwa Spika, samahani... hoja yangu ilikuwa...

SPIKA: Mheshimiwa waziri ulisimama, Waziri wa Nchi.

TAARIFA

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Spika, nilikuwa tu nataka kusaidia kwenye eneo hilo kwamba sisi ni wanachama wa Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) na tumesharidhia mikataba na katika mikataba tuliyoridhia iko mikataba ambayo inatutaka tutoe uhuru wa majadiliano kwa

wafanyakazi. Uhuru wa majadiliano ndiyo unaojenga uwepo wa vyama vya wafanyakazi kwenye maeneo ya kazi. Na wajibu wa vyama vya wafanyakazi ni kuhakikisha kwamba wao wanakuwa ni daraja la mahusiano kati ya mwajiri na wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, sasa nilichokuwa nataka kukisema hapa ni kwamba CWT iko kwa mujibu wa sheria na taratibu za vyama vya wafanyakazi nchini. Kwa hiyo, kama kuna walimu wanaona kuna matatizo kwa kuzingatia Katiba waliyonayo na miongozo inayoongoza uwepo wa vyama vya wafanyakasi wana fursa na nafasi ya kufanya majadiliano kwa kuititia utaratibu ambaa umewekwa kisheria na wakafikia muafaka na vyama hivyo vikaendelea kuwepo. Uwepo wa vyama vya wafanyakazi ni muhimu sana kwenye maeneo ya ajira kuliko kitu kingine chochote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni ushauri tu kama Taarifa. Niseme kwamba, kama yako matatizo iko fursa ya majadiliano na huo ndiyo msingi wa kisheria na sheria za kazi na ajira zinaweka msingi huo wa majadiliano ya pamoja.

SPIKA: Ndiyo maana nikasema Mheshimiwa Santiel kwamba bado kuna mengi ya kujifunza kwa sababu hawa wako kila Wilaya. Kila jimbo mlipo wapo CWT na wanafanya kazi pale na Mkurugenzi ambaye ndiyo mwajiri wa walimu katika wilaya ile. Ule uonevu wote n.k wanafanya kazi huko huko kimya kimya.

Mkitaka hicho chama kiwe ni cha kupiga kelele mtatoka jasho hasa ninyi Chama Tawala. Kumbuka kundi la walimu ndiyo kundi kubwa kuliko kundi lolote lile la wafanyakazi. Kwa hiyo, hawa watu wanaofanya kazi kubwa ambayo ninyi wengine hamujui mkafikiri kwamba zawadi yao ni kupigwa tu humu ndani n.k ndiyo maana nikasema *there is a lot to learn sometimes*. Bado una dakika mbili au ziliisha? Wanasema moja lakini nakuongeza ya pilii.

MHE. SANTIEL E. KIRUMBA: Mheshimiwa Spika, kikubwa nilichokuwa naomba kwasababu kuna Tume ya Utumishi wa

Walimu, lakini ninachoomba walimu kwenye chama hiki wasilazimishwe kujiunga. Wajiunge kwa hiari kwasababu Katiba yao inawaambia kwamba watumishi hawa wajiunge kwa hiari na sio kama hivi inavyopitia kwa utumishi kwamba automatically anakuwa amejiunga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimepitia kuwauliza walimu wengi, ni kweli wanakwambia hawajawahi kuandika barua yoyote ya kujiunga kwa hiyo inaenda automatically, kwasababu Katiba ipo...

SPIKA: Si umeshaambiwa ni sheria?

MHE. SANTIEL E. KIRUMBA: ... mimi naomba kwamba...

SPIKA: Sasa kaa chini!

Uwe unaelewa. Uctiona unakwenda mahali unatafuta kaa na Waheshimiwa Mawaziri n.k upate elimu Mheshimiwa Santiel. Usije na *pressure* tu. Upate elimu kidogo, wanaweza kuwa watu wanafanya kazi nzuri sana lakini kwasababu huna upande wa pili unawa-*destroy* bila sababu za msingi sana. Kuna Taarifa, basi nakuruhusu tu angalau maana ulisema.

Mheshimiwa Musukuma.

T A R I F A

MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *Concern* ya Mbunge anajaribu kuwatetea walimu. Ni kweli kwamba kwenye majimbo yetu walimu wanalamika kwamba wanachanga miaka 20 halafu ile miaka 20 yake akija kustaafu anapewa *bundle* mbili za mabati.

Kwa hiyo, alichokuwa anataka kusema kama walimu wanalamika kwa Wabunge ni wajibu wetu sisi Wabunge kumwambia Waziri aone namna ya kukaa na Chama Cha Walimu. (*Makofi*)

SPIKA: Sasa hujanielewa na wewe Musukuma ndiyo maana wenzio wanakutania wanasema darasa la saba. (*Kicheko*)

Jamani mtani wangu huyu! (*Kicheko*)

Katika *organization* yoyote panaweza pakawa na malalamiko lakini kama *conclusion* ni kufuta, ni kuua, ile huwa ni *ultimate* ni hukumu ya mwisho kwamba sasa badala ya mabati sjui mangapi wanayotoa watoe mara tano ya yale ni hoja nzuri. Ninachosemea kufuta, ufanye mwingine ajunge mwingine ambaye hataki. Sasa utakuwa ni umoja gani? Utakuwa tayari umeshawasambaratisha hawa walimu na kadhalika.

Kwa hiyo, ni mjadala kidogo mpana. *Angle* yangu mimi ile ya kufuta ndiyo kidogo inaleta shida. Lakini nakuahidi Mheshimiwa Santiel kwenye kikao chochote kile cha *caucus* wewe nyanyua hii hoja halafu utapata maelezo mazuri zaidi ya kuhusu jambo hili.

Mheshimiwa Thea Ntara nilikutaja. Atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Kikoyo Ishengoma.

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nami nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa waziri wa Elimu ambaye ni mwalimu wangu wa *Research Methodology* ingawa ulinibania bania sana.

SPIKA: Mchoyo wa *marks* eeh!

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Mheshimiwa Spika, nianze kwa neno moja halafu niendelee. Hilo neno atanisaidia kutafsiri baadaye Mheshimiwa Mwantumu Dau, linasema *lqra*. Nami niseme kama walivyosema wenzangu. Mitaala yetu ya elimu ni mizuri, sio mibaya. Tatizo mitaala yetu ya elimu ni mikubwa (*loaded*) mno. Kwa hiyo, cha kufanya nimshauri tu Mheshimiwa Waziri aunde timu, wafanye *in depth review* ya *program* zote na hasa vyo vikuu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, unakuta leo hii ukianzisha chuo chochote kikuu, mtu anayazoa ma-*program* ya Chuo Kikuu fulani yote anayaweka kwenye chuo chake. Kwa hiyo, ni *copy and paste*. Kwa hiyo, tunakuwa na ma-*program* mengi. Mengine wakati mwingine ndiyo hayo ambayo mtoto akimaliza anakosa ajira. Kwa hiyo, hapa Mheshimiwa waziri ana kazi nzito. Watu wameongea sana kuhusu elimu. Inaonekana tayari kuna tatizo na wakati huu uliopo. Kwa hiyo, waka echini wa-*review program* ya elimu iwe *reviewed in depth* ili waje na zile *special program* ambazo tunazihitaji kwa wakati huu na wakati ujao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nililizungumza lakini leo nzungumze kuhusu ku-*post* au kupata wahadhiri kutoka nje. Yaani tunatakiwa sasa tubadilike. Vyuo vikuu vyetu wahadhiri ni wale wa hapa Tanzania, hatukatai lakini tunatakiwa tuwe na angalau asillimia tano ya *professors* kutoka nje. Tukiwa na mchanganyiko wa *professors* wengine wakapata kibali cha kutangaza *Internationally* halafu tukapata wahadhiri kutoka nje kwanza itaongeza hadhi ya vyuo vyetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni jukumu sasa nimuombe Waziri watangaze kazi *Internationally* ili tupate maprofesa waweze kusaidiana na hao waliopo na hiyo itasaidia kuongeza *exchange programs*, itasaidia kuleta *projects* lakini pia hivi vyuo vyetu vitapanda hadhi. Tukiendelea tu kuwa wenyewe, *local, local* tu, laizma tufanye sisi wenyewe vile ambavyo leo kuna Watanzania Maprofesa wanaenda kufundisha South Africa, wengine wanaenda kufundisha Rwanda somo la Kiswahili. Kwa hiyo, na sisi lazima tujipange tuwe na wahadhiri kutoka nje. Na hapo ndiyo tutaleta maana ya neno *University*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna hili suala la Sheria za *Extension*. Pale Chuo Kikuu ukichelewa kumaliza *program* za *master's* au *PHD* unapewa *extension* na unalipa *fine* zaidi ya milioni moja. Sasa niombe, wanafunzi wanalalamika sana. Anayesababisha hawa wanafunzi mara nyingi kuchelewa ni yule *supervisor*. Kwa hiyo, kinachotakiwa hapa ile *fine*

igawanywe. Mwanafunzi alipe nusu na yule *supervisor* nusu. Kwa kufanya hivyo, hawa ma-*supervisor* watakuwa wanatosoma kazi za wanafunzi, wanamaliza kwa wakati, hakutakuwa na *extension fine*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wakishamaliza mwanafunzi yule anajulikana *details* zake zote. Siku anamaliza ana-*graduate* kupata cheti anaambiwa rudi Songea, au nenda Kagera uje baada ya wiki mbili. Hiyo nayo imekuwa inasumbua sana wanafunzi. Mheshimiwa Waziri asimamie. Akimaliza chuo, anapata cheti chake anaondoka. Lakini imekuwa ni usumbu mno. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho niwaombe sana Wizara pamoja na halmashauri tumekuwa tukilalamika vyuo vikuu hawafanyi utafiti...

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Ntara.

MHE. DKT. THEA M. NTARA: ... aaah! Hivi ni kweli?

SPIKA: Haya, nakupa dakika mbili au tatu umalizie. (*Kicheko*)

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, sasa niwaombe sana Wizara na halmashauri tutumie vyuo vyetu kufanya kazi ndani ya halmashauri na wizara. Mfano mzuri ni Mheshimiwa Sajin alipokuwa RASSimiyu. Alichukua wale wanafunzi kutoka ardhi Tabora kwenda kupima viwanja vyote kule Simiyu, wakammalizia kazi tena kwa bei ya chini.

Kwa hiyo, tutumie vyuo vyetu. Tutumie *TIA, IFM, Ardhi, University of Dar es Salaam, UDOM*. Tuwatumie wakafanye kazi zetu. Ahsante sana. (*Makof*)

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Spika, Taarifa!

SPIKA: Mheshimiwa Thea Ntara, kuna Taarifa unapewa. Endelea nimekuruhusu.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Spika, Taarifa,

SPIKA: Nimekuruhusu, jitambulisse tu.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Spika, naitwa Cosato Chumi...

SPIKA: Cosato Chumi, nimekuona sasa.

TAARIFA

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Spika, naomba kumpa Taarifa Mheshimiwa Mbunge anayezungumza kwamba hata sisi Halmashauri ya Mji wa Mafinga tumetengeneza *Master Plan* kwa kutumia wanafunzi wa Chuo cha Ardhi kwa hiyo hoja yake ni ya msingi sana. (*Makofi*)

SPIKA: Unaipokea hiyo hoja Mheshimiwa Ntara?

MHE. DKT. THEA M. NTARA: Mheshimiwa Spika, nimeipokea halafu nawapongeza sana. Hiyo ndiyo namna tutakuza hawa watoto wetu waonekane wanafanya kazil.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nikushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Jamani mnamuona mwanafunzi wa Profesa Ndalichako? Ubora wa mwalimu unauona kupitia wanafunzi wake. Hongera Profesa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, kama kuna mtu ambaye nimemsahau kwa vyovyote vile katika orodha ya leo mnijulishe tu, lakini bado tunaye Mheshimiwa Dkt. Kikoyo Ishengoma. Endelea sasa Mheshimiwa Dkt. Kikoyo.

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupewa nafasi hii kuchangia Wizara yetu muhimu ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nipeleke salamu kwa Waziri, Wilaya ya Muleba inakupenda na inakupongeza sana, kuna shule yako inaitwa Profesa Ndalichako; wamenituma nikuambie usiwasahau. (*Makofi*)

SPIKA: Imekuwa ya ngapi kwenye matokeo? (*Kicheko*)

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Spika, anajua mwenyewe Waziri wa Elimu. (*Kicheko*)

SPIKA: Endelea Mheshimiwa. (*Kicheko*)

MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO: Mheshimiwa Spika, lakini hizo salamu ni kwamba bado wanamhitaji sana na wanahitaji ulezi wake wa kimama na wa kiuwaziri.

Mheshimiwa Spika, nitajikita kwenye COSTECH. Jana kwenye mjadala hapa liliibuka suala la gongo na konyagi kwamba hao watu wanaotengeneza gongo na konyagi mara nydingi wanakimbizana na polisi kwamba ile ni bidhaa ambayo haitakiwi.

Mheshimiwa Spika, tunao vijana wengi wa Kitanzania ambao wamevumbua vitu vingi. Miaka mitatu iliyopita tulikuwa na maneno hapa, kuna vijana ambao walivumbua helikopta, sijui wako wapi leo? Kuna vijana ambao walivumbua magari, wako wapi leo? Serikali yetu kuititia Wizara hii imewapa msaada gani? Tumewaacha hawa vijana wanahangaika wao kwa wao, wanatumia pesa yao na muda wao na ile *end product*, kama Serikali, hatui-own. Tunawaacha tu na haya mambo yanapotea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kuna kipindi nilisoma siku za nyuma Mwalimu Nyerere alikuwa na wazo la kuanzisha vijiji vyaa sayansi ambavyo vingewasaidia vijana ambao wana

ubunifu wa aina yake waende kwenye vijiji vile wakapate muongozo na ku-*shape* yale mawazo yao tuweze kupata wabunifu ambaو wanaweza kutengeneza vitu. Tunavyoviona vinaelea Ulaya; ndege tunaziona zinatembea na magari, yalibuniwa na kuasiwi na vijana ambaو walikuwa na ubunifu kwenye miyo yao. Huu ubunifu haufundishwi vyuoni wala shulen, ila ni mtu anazaliwa ni mbunifu hajjalishi amesoma kiwango gani, ana elimu kiasi gani, lakini anao ubunifu ule. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sasa kazi yetu kupitia Wizara ya Elimu, hasa ile Taasisi ya *COSTECH* nadhani ndio kazi yake hiyo. Mwalimu alikuja na wazo la vijiji vyia sayansi tukaja na *COSTECH*, lakini sasa ukiangalia pesa wanayopewa *COSTECH* hawawezi kuendeleza ubunifu ambaو mbele ya safari ungeweza kusaidia Taifa hili. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, narudi kwenye jimbo langu. Tunayo kazi kubwa mbele yetu. Nilikuwa naangalia maoteo kwenye jimbo langu tu, mwaka huu vijana ambaو wamesajiliwa kidato cha kwanza walikuwa 9,041. Mwaka 2023 watakuwa 21,159, mwaka 2024 tutakuwa na vijana 30,025, lakini ukiangalia miundombinu ya shule tulizonazo ni ileile. Naomba Wizara ijpange, vinginevyo kufika mwaka 2025 tutafukuzana kwa sababu wanafunzi walio kwenye shule za msingi ambaو tunatarajia waingie kidato cha kwanza ni zaidi ya mara tatu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu ihakikisha kwamba mikoa ambayo iko pembezoni mwa nchi kama Kagera na mikoa mingine waiangalie kwa jicho la pekee. Ukienda kwenye mikoa mingi ya pembezoni walimu hawapo, unakuta shule ya msingi au shule ya sekondari ina wanafunzi 1,200 ina walimu sita halafu tunaongelea ubora wa elimu, tunajidanganya. Naomba Wizara ya Elimu tujipange kuhakikisha kwamba mikoa ya pembezoni tunaipatia kipaumbele na kuhakikisha ina nyumba za walimu otherwise walimu wote wanaopelekwa kule wanakimbia kwa sababu ya mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, lakini nipayendekeze, kwa mikoa ambayo iko pembezoni mwa nchi tuangalie kuwapatia motisha au *allowance*, ile wanaita *hardship allowance* iweze kuwa-*sustain* kule kwenye mazingira magumu ambako hakuna umeme, wakati mwingine hakuna barabara na ukienda kule kwa kweli wengi wanakataa kwenda maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, naunga hoja mkono na nawapongeza Mawaziri wetu kwa kazi kubwa wanayoifanya, ila Mheshimiwa Waziri asisahau *Ndalichako Secondary School*. Nashukuru sana. (*Makofii*)

SPIKA: Huyo ni Mheshimiwa Dkt. Kikoyo Ishengoma ndiye alichukua nafasi ya Profesa Anna Tibaijuka. Kwa hiyo, kule Muleba ametoka Profesa ameingia Daktari, unajua tena *nshomile* hawaa. Ahsante sana. (*Kicheko/Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa leo upande wa wachangiaji tuishie hapo, lakini nilikuwa nimeombwa na Mbunge wa Jimbo la Mbarali, Mheshimiwa Francis Leonard Mtega kwamba ana Maelezo ya Mbunge ambayo angependa kutoa. Nadhani dakika hizi zinamtosha kuweza kutoa maelezo hayo, Mheshimiwa Mtega karibu.

MAELEZO BINAFSI YA MBUNGE

MHE. FRANCIS L. MTEGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nasimama kwa Kanuni ya 57(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na kutuwezesha kukutana hapa na kuendelea na Mkutano wetu wa Bunge la Bajeti. Aidha, nitumie nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kuliongoza Bunge hili kwa umahiri mkubwa. Kupitia uongozi wako sauti za wananchi wetu zinasikika humu Bungeni na hivyo dhana ya kuwawakilisha wananchi wetu inatimizwa kikamilifu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa siku ya tarehe 23 Aprili, 2021 katika Kijiji cha Nyeregete, Kata ya Rujewa, Jimbo la Mbarali yalitokea mauaji ya wananchi watatu yaliyotekelizwa na wanaodhaniwa kuwa ni Askari wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, *TANAPA*. Majina ya wananchi hawa ni haya yafuatayo, wa kwanza ni Ndugu William Nundu mwenye umri wa miaka 39, wa pili Ndugu Sandu Masanja umri miaka 29 na wa tatu Ndugu Ngusa Salawa miaka 14. Aidha, kuna wananchi watatu wengine hadi muda huu naongea hawajapati kana na hawajulikani walipo na walikuwa pamoja katika tukio hilo. Kwa hiyo, inahofiya kuwa na wenyewe waliuwawa. Kwa kweli, hii imezua taharuki kubwa kwa wananchi maeneo yale. Hawa amba o hawajuliani walipo wa kwanza ni Ndugu Abdallah Daimon, wa pili Ndugu Mussa Ndikwega, watatu ni Abeid Stephen Obama.

Mheshimiwa Spika, wananchi waliuwawa kikatili walienda kujitafutia kipato kwa kuvua samaki katika korongo moja linaitwa Langenda na Mto unaitwa Angasada ambayo yote hiyo inapeleka maji Mto Ruaha, lakini iko mbali sana na Mto Ruaha, ni zaidi ya kilometra 20 hivi. Hawa watu hawakuwa na silaha walikuwa na ndoana tu na nyavu na wanavua samaki wenyewe kambale kwa ajili ya kitoweo. Kwa masikitiko makubwa wameuwawa na wawili inasemekana walinyongwa shingo baada ya mateso makali na mmoja ambaye kilipati kana kichwa chake tu kiwiliwili hakipo, yeye inadhaniwa alipigwa risasi kichwani. Ingekuwa ni majangili wana *AK47 that could be reasonable*, lakini hawana silaha yoyote wanauwawa kikatili.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa mgogoro huu baina ya wananchi na Hifadhi ya *TANAPA*, kwa ufupi sana, ilianzia wakati wa upimaji wa mpaka wa tatu, *G/Namba 28*. Mpaka wa awali ulikuwa unaeleweka vizuri lakini mpaka wa pili wananchi walishirikishwa, wakaelimishwa, wakakubali, mali zikathaminishwa, wakalipwa fidia, mojawapo Kijiji cha Ikoga na Kijiji cha Msangaji, walihama vizuri. Huo ndiyo mpaka wa *TANAPA* uliokuwa unaeleweka.

Mheshimiwa Spika, lakini ilifika wakati mpaka ukaja kuongezwa bila taarifa yoyote, wamekuja na *GPS*, wamepima *coordinates*, wananchi hawana taarifa. *TANAPA* wakaanza kuwanyanya wa wananchi kwa kuwaambia kwamba wapo ndani ya hifadhi, wananchi wale wanashangaa, miaka yote tunaishi huku, waliokuwa ndani ya *TANAPA* wameshalipwa fidia yao wamehamishwa inakuwaje sisi tuwe ndani ya *TANAPA*?

Mheshimiwa Spika, hivyo basi baada ya kuteswa na kunyanyasika mwaka 2016 tukaomba mipaka ile iainishwe ardhini ili tujue sasa hii *GN Namba 28* inaishia wapi? Kweli mawe yaliwekwa, cha ajabu ikaonesha vijiji zaidi ya 30 vimo ndani ya hifadhi. Kuna Kijiji cha Malosongwe jiwe liko katikati ya kijiji na vijiji vyote hivyo wananchi wanaishi wanafanya shughuli za kawaida, lakini ndio hivyo iko ndani ya hifadhi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mchakato ulianza pale kuanzia *Ward C, DCC, RCC* walishirikishwa mpaka ukafika huku taifani. Hayati aliyejewa Rais wakati ule, aliunde Tume ya Mawaziri na kiongozi mkuu alikuwa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Lukuvi kati ya wale Mawaziri nane; ikaonesha kwamba Mheshimiwa Rais amesema wananchi muendelee na shughuli zenu kama kawaida wakati suala hili linafanyiwa kazi na *TANAPA* walikuwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, licha ya kutoa ujumbe huo kutoka kwa Mheshimiwa Rais, mkuu wa nchi, bado Mkuu wa Mkoa wa wakati huo alikuja kufanya mkuutano mkubwa akawaambia wananchi msiwe na wasiwasi endeleeni kufanya shughuli zenu mpaka hapo Serikali itakavyoamua vinginevyo, *TANAPA* walikuwepo. Mwananchi mmoja akseliza, je, twende tukang'oe yale mawe? Mkuu wa mkoa akajibu kwamba, hapana msing'oe, utaratibu unafanyika. Cha kushangaza wenzetu *TANAPA* wanaendelea, kwanza walikuwa wanachukua ng'ombe wanaofugwa kule walikoruhusiwa wanapeleka ndani ya hifadhi.

SPIKA: Sasa kwa sababu ya muda, endelea na hatua gani ambazo unashauri zichukuliwe na Serikali.

MHE. FRANCIS L. MTEGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Japo inaniuma sana, napendekeza, Serikali ifanye mambo yafuatayo:-

(i) Serikali ifanye uchunguzi wa haraka na kuwachukulia hatua kali za kisheria wale askari wote waliohusika na mauaji haya ili iwe mfano kwa wengine. (*Makofii*)

(ii) Serikali itoe kifuta machozi na fidia kwa familia zilizopatwa na msiba huo kutokana na kwamba kuna wategemezi na watu kama hao. (*Makofii*)

(iii) Serikali igharamie mazishi ya wananchi wale waliofariki kutokana na ukatili huo. (*Makofii*)

(vi) Serikali itoe karipio kali kwa Mamlaka za Hifadhi, hasa wale askari wanaodhuru wananchi kwa sababu tembo wakiingia kule wanawaswaga salama salmini hakuna hata tembo anayejeruhiwa mguu, lakini wananchi wanaovua samaki ndiyo hao wanauwawa. (*Makofii*)

(v) Serikali ishirikiane na wananchi wa Mbarali kuwatafuta wananchi hawa watatu ambao bado hawajapatikana hadi sasa. Nimeshawataja pale mwanzo. (*Makofii*)

(vi) Serikali ikamilishe uainishaji wa mpaka mpya, hiyo ndiyo *GN Namba 28* niliyosema. Ni pale ambapo mpaka mpya utapimwa na kuainishwa kwamba sasa huku ni *TANAPA* huku ni wananchi, hakutakuwa na usumbufu, itakuwa mwisho wa matatizo haya vinginevyo wananchi wale wataendelea kuteseka. (*Makofii*)

(vii) Waziri wa Maliasili na Utalii afanye ziara katika eneo lile la mauaji, ili akawafariji wananchi na akasikilize malalamiko yao zaidi na pengine kumaliza kabisa mgogoro huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na mengi ya kusema, lakini kutokana na muda basi kwa masikito makubwa baada ya kusema hayo, naomba kukushukuru tena na naomba kuwasilisha. Ahsante sana. (*Makof*)

SPIKA: Ahsante Mheshimiwa Francis Leonard Mtega, Mbunge wa Mbarali kwa maelezo yako. Kwa Kanuni zetu maelezo haya hayafungui mjadala wowote, naona Mheshimiwa Godwin Kunambi anataka kusimama hapa na Mheshimiwa Zeno Mngungusi na Waheshimiwa wengine naweza nikawataja hapa ambao kwa maelezo haya walitaka kutoa machozi, lakini ni kulitaarifu Bunge ndiyo utaratibu wetu huu.

Sasa kwa vile jambo hili lina *borderline* ya kwenye ulinzi na usalama, nadhani nilipeleke kwenye Kamati ya Mheshimiwa Zungu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, watakutana na Serikali huko, watanong'ona halafu watanishauri. Nami tutashauriana na *Chief Whip* na Serikali hapa tutaona namna gani ya kuli-*handle* jambo hili kwa salama. *Otherwise* sisi kama Bunge tunawapa pole wananchi wa huko, Mheshimiwa Mbunge utufikishie salamu za pole kwa haya yaliyotokea, ahsante.

Kwa vile muda wetu sasa unaisha, niseme tu kwamba mjadala wetu wa Wizara ya Elimu kutwa nzima ya leo umekuwa mzuri sana. Naamini pia kesho utakuwa ni mjadala mzuri kabisa na kesho tutampa nafasi Mtoa Hoja Mheshimiwa Profesa Ndalichako aweze kuhitimisha hoja yake, lakini tunaomba sana hoja za Wabunge mztazame, mztile nguvu, mztile maanani ili turekebishe mambo. Mimi kesho sitakuwepo hapa, atakuwepo Naibu, nimalizie kwa kupigia mstari tena watu wa Ubora wanaohusika na uandikishaji wa shule zinazoanza; shule inaanza inafika darasa la nne, la sita, haijaandikishwa, tafsiri yake nini? Walimu 6,000 tunaowaajiri watakapopangwa na TAMISEMI moja kwa moja TAMISEMI haina hizo shule ambazo hazijaandikishwa. Kwa hiyo, wanakosa walimu moja kwa moja, Mkurugenzi hawezi kumhamisha mwalimu kumpeleka kwenye shule ile kwa sababu haijaandikishwa. (*Makof*)

Asubuhi nimeeleza mambo mengine kwa sababu shule ile hajaandikishwa haiwezi kupata fedha za *capitation*. Madhara ni makubwa, inakuwaje ninyi watu wa Ubora, yaani ninyi ni watu wa elimu halafu hamuelewi haya mambo? Mnategemea Wabunge ndiyo wawaambie? Mnawahukumu hawa viumbwe wa Mungu hawa, darasa la kwanza, chekechea, hamuwaandikishi mnawakosesha fursa zote hizo, kwa sababu gani? (*Makof*)

Watu wa Ubora yaani wao ni kama *ma-inspector* fulani hivi, wana-*inspect* tu yaani wao hawahusiki, *they are not part of the whole team*. Pia hawaambiagi wakasikia na wenyewe kama wale nilisemaga wale wa siku ile wale, *NEMC*. Wakishikilia hatuandikishi, hata waambiwe na nani, labda Mheshimiwa Ndalichako awaambie, hawafanyi hivyo, sasa wabadilike wawe ni sehemu ya Serikali. TAMISEMI hata ikiwaambia hawasikii kwa sababu wao wako Wizara ya Elimu na ndiyo maana hata hawaendi kukagua shule maana hata kwenda kuomba TAMISEMI bwana tupatiensi gari tukague shule wanaona tabu wanataka Katibu Mkuu Wizara ya Elimu ndiyo awape magari, ndio awape nini, yaani wako pemberipembeni. Ndiyo maana huwa kunatokea wito hapa kwamba hawa wa Ubora wa Elimu wahamishiwe TAMISEMI labda shida hii itaisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Profesa hawa watu ni kero, nimelibeba mwenyewe hili ili mjue, ni kero hawa watu wabadilike, *mentality*yao ina matatizo. Wao ni kama kitu fulani hivi wako pembeni. Nilitamani hata nihoji Bunge, waende TAMISEMI wasiende, ungesikia majibu hapa. (*Kicheko/Makof*)

Vinginevyo Mheshimiwa Waziri tunawapongeza, Serikali tuko pamoja. Kwa kuwa, sasa tunaelekeea kwenye mambo mazuri mazuri kule kwenye *Iftar*, basi Waheshimiwa Wabunge mniruhusu niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

(*Saa 12.05 Jioni Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 5 Mei, 2021 Saa Tatu Asubuhi*)